

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA NNE

Kikao cha Pili – Tarehe 4 Desemba, 2013

(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua

MASWALI NA MAJIBU

Na. 16

Uhalali wa Baadhi ya vyama vyaya Siasa Nchini

MHE. MARIAM R. KASEMBE (K.n.y. MHE. PROF. DAVID H. MWAKYUSA) aliuliza:-

Matamanio ya kila Chama cha Siasa ni kupata uungwaji mkono kwa idadi kubwa ya wananchi ili siku moja kishike dola na kuongoza nchi, kati ya vyama kumi na nane (18) vyaya siasa vyenye usajili wa kudumu nchini baadhi yake havijaweza kushinda hata uongozi wa kitongoji katika chaguzi mbalimbali zilizopita:-

Je, vyama hivyo vinapata uhalali kutoka kipengele gani cha sheria kinachoviwezesha kubakia katika daftari la usajili wa vyama vyaya siasa?

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Profesa David Homeli Mwakyusa, liloulizwa hapa na Mheshimiwa Kasembe, Mbunge wa Masasi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hadi sasa vyama vyaa siasa vyenye usajili wa kudumu ni ishirini na moja (21) na siyo (18) kama ilivyoulizwa na Mheshimiwa Mbunge. Aidha, ni kweli kwamba baadhi ya vyama vyaa siasa vyenye usajili wa kudumu havijawahi kushinda uongozi katika chaguzi wa Serikali za Mitaa au Uchaguzi Mkuu.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Vyama vyaa Siasa Namba 5 ya mwaka 1992 haitoi mamlaka kwa msajili kuvifutia usajili vyama vyaa siasa ambavyo havijashiriki au kushindwa katika uchaguzi mbaalimbali za kisasa. Kwa mujibu wa kifungu cha 19 cha Sheria hiyo, chama cha siasa kinaweza kufutwa iwapo kimekiuka masharti ya usajili.

MHE. MARIAM R. KASEMBE: Ahsante sana Mheshimiwa Spika kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa katika majibu ya Mheshimiwa Waziri amesema kwamba Sheria tuliyonayo kwa hivi sasa hairuhusu kufutiwa usajili wa vyama kwa sababu ya kukosa nafasi katika uchaguzi.

Je, Serikali iko tayari kuleta Sheria hiyo ili tuweze kuifanya marekebisho?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE: Mheshimiwa Spika, Ofisi yangu sasa hivi inafanya mapitio ya Sheria hii na sasa tuko kwenye zoezi la kushirikisha wadau. Kwa kadiri mchakato utakavyoendelea kwa vyovyote vile tutakuwa tayari kuleta marekebisho muhimu ya Sheria hii hapa Bungeni.

SPIKA: Naomba tuendelee na swali linalofuata Mheshimiwa Salum Khalfan Barwany, kwa niaba yake Mheshimiwa Rajab ndiyo.

Na. 17

Mikopo Benki ya Dunia

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED (K.n.y. MHE.
SALUM K. BARWANY) aliuliza:-**

Benki ya Dunia inatoa mikopo kwa Halmashauri kadhaa hapa nchini kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya barabara:-

(a) Je, kwa nini miundombinu hiyo inaharibika bila matengenezo?

(b) Je, taa za barabarani za mtaa wa Buguruni Malapa zimekwenda wapi?

(c) Je, uharibifu kama huu unaotokea Dar es Salaam utakuwa vipi kwa Manispaa ya Lindi inayopewa mgao wa kata 13 badala ya 18 zilizopo?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) alijibu:- Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Salum Khalfan Barwany, Mbunge wa Lindi Mjini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, miundombinu hii imeharibika ndani ya kipindi kifupi baada ya kumalizika kwa ujenzi kutokana na kukithiri kwa matumizi ya barabara yasiyozingatia usalama, wizi wa vifaa vya barabarani na uwingu wa magari yanayotumia barabara hizi.

(b) Mheshimiwa Spika, mradi wa *Community Infrastructure Upgrading Programme (CIUP)* katika mitaa ya Madenge na Malapa ilihuisha uwekaji wa taa barabarani 91, kujenga barabara ya Lami ya Mnyamani na mifereji ya mvua yenye urefu wa kilometra 3.23 na kampuni ya *M/S Estim Construction Ltd.* kwa gharama ya shilingi bilioni 1.6 ambazo

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA
NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)

zilikuwa ni mkopo kutoka Benki ya Dunia. Baadhi ya taa na nguzo za barabarani katika mtaa wa Buguruni Malapa zimeibiwa na wananchi wasio waaminifu na zingine kugongwa na magari na kuanguka na kesi moja ipo Mahakamani.

(c)Mheshimiwa Spika, suala la mgao wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mpango wa *ULGSP* unazingatia idadi ya watu walio kwenye Manispaa na Miji. Miradi hiyo haipangwi kwa kuzingatia maeneo ya Kata.

Hivyo, Manispaa ya Lindi ni kati ya Halmashauri 18 nchini zinazonufaika na mradi wa huo utakaotekelawa kwa kipindi cha miaka mitano kuanzia mwaka 2013/2014 na imepangiwa dola za kimarekani milioni 5.6 sawa na shilingi billioni 9 kwa kipindi chote cha mradi.

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED: Ahsante nakushukuru Mheshimiwa Spika. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri nilikuwa na maswali mawili madogo ya nyongeza.

Kwanza ni kwamba Mheshimiwa Waziri wakati anajibu swali hili la msingi anasema kwamba kuharibika kwa barabara hizi zimetokana na uwingu wa magari yanayotumia barabara hizi. Nataka kumwuliza Mheshimiwa Waziri hivyo ni kusema kwamba kabla ya huu mradi hakukufanyika *feasibility study*, ili kukajulikana magari ambayo yatakuwa yanatumia barabara hizi?

Lakini la pili, ni kwamba hivi karibuni tu wafadhili wetu ambaao wanafadhili *Local Government Reform Programme* ambayo sasa hivi anataka kuingia katika *program* namba mbili walitishia kusitisha fedha zao kwa sababu ya ubadhirifu, wizi na ujisadi uliofanywa na TAMISEMI.

Je, Mheshimiwa Waziri Wizara yako imejipangaje katika huu mradi mkubwa wa *ULGSP*? (*Makof!*)

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, feasibility study imefanyika. Lakini mara nyingi barabara ikiwa mbovu magari mengi yana kawaida ya kutoipenda hiyo barabara kuipita na mara inapotengezwa idadi ya magari yanaongezeka na pia katika barabara zetu nyingi za mitaani hatuna mizani ya kuweza kuzuia magari ambayo yanazidisha uzito.

Kuhusu suala la pili la wafadhili kutishia katika mradi wa *Local Government Reform* ni kweli kwamba wakati wafadhili walivyofanya uhakiki au walivyofanya *audit ukaguzi* wa mradi huu wa *Reform* kwa mwaka 2009/2010, na 2010/2011 waligundua kuwepo kwa ubadhirifu na mimi kama Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu niliingia kati.

Wale ambao walikuwa wanasimamia huo mradi tulisimamisha mkataba wao kwa sababu walikuwa wameajiriwa kwa mkataba. Tukateua watu wengine na pia *gratuity* yao ambayo walipaswa kupata tuliizua na pia tumewapeleka katika vyombo ya Sheria ili waweze kuchukliwa hatua.

MHE. MUSSA Z. AZZAN: Nakushukuru Mheshimiwa Spika. Mradi huu wa *ULGSP* uko katika Mkoa wa Dar es Salaam katika Wilaya ya Ilala na Wilaya ya Ilala iko jumla kilomita 26 za lami. Lakini cha kushangaza Mheshimiwa Spika, TAMISEMI ililetta maagizo, wanavyosema Watendaji wetu.

Inawezekana si kweli. Katika kilomita 26 hizi Jimbo la Ilala imepewa kilometra 2 tu na ndiyo *Centre* ya uchumi wa nchi yetu na Jimbo la Ukonga walipata kilomita zingine waligawana kilomita 24.

Je, Serikali iko tayari sasa ku-*revisit* mpango huu na kuzigawia kilomita nane nane kila Jimbo katika Wilaya ya Ilala?

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, kwa kweli Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI haikuhusika katika kupanga kilometa ngapi ziende katika Jimbo gani.

Sisi kama TAMISEMI tulichofanya tuliwapelekea *manual* ambao wao wenyewe walikuwa na uwezo wa kuchagua wanataka kutekeleza miradi ya aina gani kwa sababu inahusu utengenezaji wa barabara za lami za changarawe, uwekezaji wa taa za barabarani. Ujengaji wa mifereji ya maji ya mvua.

Kwa hiyo, Halmashauri yenyewe husika ndiyo inayohusika kuchagua wanatekeleza miradi gani na maeneo gani. Lakini kwa vile yapo malalamiko, nitawaagiza wataalam wangu wafuatilie kuona kama kweli hayo mambo yamefanyika kwa kisingizio kwamba sisi tumewaaagiza.

Lakini napenda nikuhakikishie Mheshemiwa Mbunge, ni Wilaya yenyewe ya llala ambayo imechagua maeneo gani iende. Lakini nakuahidi kwamba tutafuatilia na kama itabidi basi tutaingilia kati. (*Makofi*)

SPIKA: Naomba tuendelee na swali linalofuata. Mheshimiwa Felix Mkosamali.

Na. 18

Mapato Yatokanayo na Minara ya Simu

MHE. FELIX F. MKOSAMALI aliuliza:-

Ipo minara ya simu kwenye maeneo mbalimbali ya Kibondo Mjini:-

(a) Je, ni utaratibu gani unaotumika kuilipa fedha Serikali ya Kijiji cha Kibondo Mjini kutokana na minara hiyo?

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. FELIX F. MKOSAMALI]

(b) Je, Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo imekusanya fedha kiasi gani mwaka 2003 hadi 2013 na kiasi gani Kijiji cha Kibondo kimepata kat i ya hizo?

(c)Je, utaratibu gani wa mapato unatumika kwa mtu aliyetoa kiwanja, Serikali ya Kijiji na Halmashauri kwa ajili ya minara?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swal i la Mheshimiwa Felix Francis Mkosamali, Mbunge wa Jimbo la Muhamwe, lenye kipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, hakuna utaratibu wowote wa kulipa fedha Serikali ya Kijiji cha Kibondo Mjini.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Kijiji ya Kibondo Mjini haina eneo la ardhi inayomiliki kwa mujibu wa Tangazo la Serikali Na. 176 la tarehe 9 Agosti, 1996, ambalo lilitangaza kuwa maeneo ya Kibondo Mjini na Kifura yaliyopo katika Wilaya ya sasa ya Kibondo kuwa ni maeneo ya Mipango Miji. Kwa mujibu wa Tangazo hilo la Serikali na Sheria za Ardhi katika maeneo ya Kibondo Mjini na Kifura inasimamiwa na Kamishna wa Ardhi.

Hivyo ardhi ya kijiji hicho inatawaliwa na Sheria ya Ardhi Na. 4 ya mwaka 1994 na siyo Sheria ya Ardhi Na. 5 ya mwaka 1999. Kwa hiyo, Serikali ya Kijiji cha Kibondo Mjini hakina Mamlaka ya kugawa ardhi.

(b)Mheshimiwa Spika, kutokana na kutokuwepo kwa utaratibu wa kulipa Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo na Kijiji cha Kibondo Mjini hakuna fedha yoyote iliyokusanya wa kat i ya mwaka 2002 hadi 2013.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)]

Hata hivyo, upo mkataba wa kupanga eneo la Kumwerulo kwa ajili ya mnara wa *Vodacom* ambao umefanyika katika Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo na Kampuni ya Simu za Mkononi ya *Voda*. Mapato yanayotarajiwa kupatikana kutokana na mnara huo kwa Halmashauri ya Wilaya Kibondo ni shilingi milioni 6 kwa mwaka baada ya ujenzi wa mnara huo kukamilika na kuanza kufanya kazi. Hata hivyo, Serikali ya Kijiji Kibondo Mjini itafaidika kwa kupata asilimia 20 ya mapato ya Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo ambayo hupelekwa kwenye ngazi za chini ya Serikali za Mitaa.

(c) Hakuna utaratibu wa kisheria uliokwishawekwa kupata mapato ya mtu aliyetoa kiwanja chake anachomiliki kwa ajili ya ujenzi wa mnara kwa kampuni ya simu.

MHE. FELIX F. MKOSAMALI: Nakushukuru kwa kunipa fursa ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza kwenye kipengele (b) cha swali la msingi nimehoji kwamba ni fedha kiasi gani minara ya simu iliyopo kwenye eneo la Kibondo Mjini fedha kiasi gani wamechangia *whether* kwenye Halmashauri au kwenye Halmashauri au kwenye Kijiji. Serikali imesema hawajatoa pesa yoyote.

Sasa nataka majibu kwa nini vijiji vingine vyote vilivyoko Kibondo na maeneo mengine wamekuwa wanatoa fedha kwa ajili ya minara ya simu. Lakini eneo hili la Kibondo Mjini makampuni ya simu hayajalipa kitu chochote kile toka mwaka 2003 mpaka leo kwa nini tofauti na huu mnara mmoja ambao umezungumza ambao haujakamilika?

Swali la pili, kuna mkanganyiko kama Kibondo Mjini ni mji au siyo mji. Kwa mujibu wa Tangazo la Vijiji la mwaka 2009 Kibondo ni Kijiji na *confusion* hii imeendelea mpaka Serikali ya Kijiji hiki imejiuzulu kwa sababu haina ardhi, wala haina mapato wala mali yoyote. Wewe kama Waziri wa TAMISEMI, kwa nini usiye kutatua tatizo hili ambalo limeendelea kuleta mgogoro baina ya Halmashauri na Serikali ya Kijiji mpaka sasa hivi hakuna Serikali ya Kijiji pale? (*Makofii*)

SPIKA: Haya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, majibu.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, tofauti na kijiji cha Kibondo na vijiji vingine Kibondo ni eneo la Mipango Miji na eneo lolote likiwa ni eneo la Mipango Miji ardhi ile inakuwa si ardhi ya mali ya kijiji na ardhi ile inamiliikiwa na Kamishna wa Ardhi.

Kwa hiyo, usilinganishe Kibondo na Kijiji kingine nje ya mji huo. Kutokana na hiyo, ndio maana unakuta Kibondo hawapati pesa hiyo wanayopata vijiji vingine. Si Halmashauri ya Mji lakini ni eneo la Mipango Miji.

SPIKA: Ile ya kwanza ya minara na fedha sijui.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, hawawezi wakapata pesa kama kijiji kwa sababu ardhi ile iliyopo Kibondo si mali ya Kijiji cha Kibondo. Ile ardhi iko chini ya Kamishna wa Ardhi.

Kwa hiyo, kwa maana ya kijiji cha Kibondo hakuna eneo wanadolimiki ambalo wanaweza wakadai kwamba hili ni eneo letu tunaomba tupate tofauti na vijiji vingine.

MHE. MOSE J. MACHALI: Mheshimiwa Spika nakushukuru kwa kunipa fursa nimwulize swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri katika majibu yake amekiri kwamba Kibondo Mjini ni tofauti na maeneo ya vijijini na kwamba ardhi inamiliikiwa na Kamishna wa Ardhi na kwa kuwa maeneo yote ambayo ni ya Mipango Miji kunastahili kuwa na Afisa Mipango Miji. Ni sababu gani ambazo zinapelekea sasa makampuni haya ya simu yasilazimike kuweza kulipa fedha kwa Halmashauri ya Mji whether ni ya Mji lakini ni Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo na Halmashauri ya Mji haipo pale Kibondo, wala Mamlaka ya Mji sijui mji mdogo haieleweki.

Hii ni Nakala ya Mtaandeo (Online Document)

[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)]

Kwa nini Serikali isiingilie kati kuhakikisha kwamba makampuni haya yanalipa tozo zote zile ambazo ni za msingi kama *Service Levy* na kadhalika. Kuna tatizo gani? (*Makof!*)

SPIKA: Sijui wenyewe makampuni wenye hawapo.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, kwa maana ya *Service Levy* Halmashauri inaruhusiwa kutoza kama Sheria mnayo. Lakini kwa maana ya pango la ardhi, Kibondo haiwezi kupata kwa sababu hawana ardhi.

Kwa hiyo, naziomba Halmashauri zote kuwa na sheria ya huduma ambayo itawawezesha kutoza minara ya simu katika maeneo yao. Kwa sababu Halmashauri nyingine wanatoza.

Na. 19

Lango Kuu Bandari ya Dar es Salaam Kufukiwa na Mchanga

MHE. JUMA SURURU JUMA aliuliza:-

Inasekana kuwa lango kuu la kuingilia na kutoka kwa vyombo vya baharini katika Bandari ya Dar es Salaam, inajifukia kwa mchanga kadiri siku zinavyozidi kusogea:-

(a)Je, Serikali inalielewa jambo hili?

(b)Je, ni muda gani umepita tokea kuchimbwa eneo hilo?

(c)Je, kuna mpango gani endelevu wa kulihifadhi eneo hilo ili kuondoa kazi ya kuchimba kila mara?

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Juma Sururu Juma, Mbunge wa Bububu, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali inauelewa wa kina wa suala la kujaa mchanga katika lango kuu la Bandari ya Dar es Salaam. Utafiti wa kisayansi umedhihirisha kuwa kiwango cha kujaa mchanga sehemu hiyo ni sentimita 10-15 kwa mwaka yaani *annual siltation rate of between 10-15 centimeters*.

(b) Mheshimiwa Spika, lango kuu la kuingilia na kutoka vyombo vya baharini katika bandari ya Dar es Salaam lilichimbwa kwa mara ya mwisho mwaka 1998, hilayo ni takribani miaka 15 tangia kuchimbwa kwa eneo hilo.

(c) Mheshimiwa Spika, kazi ya kuondoa mchanga unaojifukia kwenye lango kuu la kuingilia na kutoka vyombo baharini ni kazi endelevu inayotakiwa kufanyika kila baada ya miaka 10.

Kwa sasa, Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania ina mpango wa kufanya kazi ya kuongeza kina cha lango kuu kutoka mita 12 za sasa hadi mita 14 na kazi hii itafanhyika sambamba na kazi kubwa ya ukarabati wa magati na 1-7 na ujenzi wa gati namba 13 na 14 inayotarajiwa kuanza hivi karibuni baada ya kukamilisha taratibu za mikataba.

MHE. JUMA SURURU JUMA: Mheshimiwa Spika, ahsante.

Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali ninaomba kuuliza maswali mawili kama hivi ifuatavyo:-

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. JUMA SURURU JUMA]

Swali la kwanza, kwa kuwa kazi ya uchimbaji na uondoaji mchanga ni endelevu, na amesema inaendelea miaka hadi miaka. Je, katika utekelezaji wa kazi hii, wanashirikiana na Taasisi za Mazingira? Wasije wakauliza mji wetu wa Kigamboni kule.

Swali la pili, kwa kuwa amesema wanaongeza kina cha maji katika Bandari (Gati Na. 1 - 7 na 13 – 14).

Je, Serikali haioni kufanya mpango mbadala wa kujenga Bandari mpya katika maeneo ya asili kama Mkoa wa Lindi kule ambako kuna kina kikubwa cha Bandari? (Makof)

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Juma Sururu Juma, kama hivi ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, suala la kuchimbua huo mchanga ili kurejesha kina, au tu hata pale inapotakiwa kuongeza kina cha Bandari zetu linafanyika kwa kuzingatia taratibu zote za Mazingira.

Wote wanaohusika na kutoa tathmini na kadhalika huhushisha kabla ya suala hilo kufanyika. Hii inalenga kulinda mazingira ya maeneo yanayofanyiwa utaatibu huo. Kwamba kazi hii ya kuongeza kina katika gati na. 1 na 7 na ujenzi wa Gati Na.13 na 14 isifanyike Dar es Salaam iende sehemu zingine.

Mheshimiwa Spika, ni kwamba hata hayo maeneo aliyoyataja iko mipango ya kujenga Bandari huko. Kwamba ujenzi wa Bandari ya Mtwara na Lindi, jana nilieleza hapa Rushungi na kwingineko, Bagamoyo na kule Tanga inaendelea sambamba na ujenzi na upanuzi wa Bandari yetu ya Dar es Salaam.

MHE. ALPHAXARD K.N. LUGOLA: Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa kunipa fursa ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)

[MHE. ALPHAXARD K.N. LUGOLA]

Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amekiri kwamba kina cha maji kilichopo pale ni mita 12. Kwa nini uongozi wa Bandari, mwaka huu uliruhusu Meli yenye urefu wa mita 250 ikiwa na uwezo wa *draft* yaani kina cha kwenda chini mita 13 ambayo ni zaidi ya mita 12, hali ambayo ingeliweza kusababisha meli ile izame pale, na uwezekano wa kuiondoa ni zaidi ya miaka 100 na hivyo kupelekea Bandari ile kujifunga.

Kwa nini waliruhusu jambo hili, na wakatokea kwenye vyombo vyaa habari, wakisherehekeea kwa mara ya kwanza wameweza kuingiza meli kubwa.

Mheshimiwa Spika, ninamtaka Waziri anipe jibu.

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swalii la Mheshimiwa Alphaxard K.N. Lugola, kama hivi ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, *draft* inayokuwa imetwajwa kwenye meli, kwanza hutegemea mambo mengi yaani meli ikaaingia kwa wakati gani katika Bandari.

'Kwa mfano maji yakiwa yamekupwa. Meli hata yenye *draft* ndogo yaani yenye uzito mdogo, haiwezi kuingia kwenye Meli. Lakini maji yakiwa yamejaa, meli hiyo inaweza kuingia kwenye Bandari. Kwa hivyo hapa pia kuna suala la mzigo kiasi gani meli imebeba.

Meli kama imebeba mzigo kidogo hahitaji kina kirefu kuingia katika Bandari. Meli kama ina mzigo mkubwa *maximum load* ndiyo inakuwa sasa na *limitation* ya hiyo *draft* ambayo imejengwa nayo. Kwa hivyo ile meli ya mita 250 iliporuhusiwa kuingia pale. *Draft* ya mita 13 inahitajika pale inapokuwa imebeba mzigo mzito kabisa inaoweza kubeba. Lakini kama imebeba mzigo kidogo, hata kama *draft* ya mita 10 meli ya namna hiyo inaweza kuingia.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

MHE. PETER J. SERUKAMBA: Mheshimiwa Spika, nina swali dogo la nyongeza. Toka nimeingia Bungeni hili Wizara hii imekuwa inasema itajenga Bandari ya Tanga, Bandari ya Dar es Salaam na Bandari ya Mtwara. Huu ni mwaka wa nane.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeliomba Naibu Waziri leo atuambie, na aliambie Bunge hili. Hii lugha ya tutajenga, wakati hatujengi itaisha lini? (*Makofii*)

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Peter Serukamba, kama hivi ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, kujenga ni *process*, ni mchakato. Kwa hivyo na ndani ya mchakato huu, yako mambo mengi sana ambayo inabidi yazingatiwe. Wakati fulani jambo linaanza, mnafika katika hatua fulani linajitokeza jambo ambalo haliwezi kuwaruhusu kuendelea kujenga. Kwa hiyo hamuwezi tu kulazimisha kuendelea ili hali mkijua mtafanya vibaya. Kwa hivyo, haya yote tunayoyasema Tanga, Dar es Salaam, Bagamoyo na Mtwara, yanazo hatua zake mbali mbali. Kwa mfano, Bandari ya Mtwara sasa hivi wamemaliza *evaluation* ya wale walionyesha nia ya kuwekeza pale, tunasubiria *request for proposals* wakileta watapewa *contract* za kuanza kujenga.

Bagamoyo, mazungumzo yanaendelea, kulikuwa kuna tofauti ya mambo karibia 17 mpaka 22, tumepunguza tofauti zetu na wale wanotaka kuwekeza zimebaki tano (5) na wenyewe tunaendelea kujadiliana nao, tukizimaliza zile watakabidhiwa kazi waendelee kujenga.

Dar es Salaam, kumekuwa na mkanyiko wa Kampuni ambayo mwanzo ilitarajiwa kujenga. Wachina wakaleta Kampuni nyingine. Kampuni hiyo ikaja na uwawakilishi tofauti wawili, kwa hiyo kulikuwa na suala la kisheria la *ku-sort out* ni nani anapaswa kihalali kuwawakilisha Kampuni inayotarajiwa kujenga. Sasa haya mambo ndiyo yanayosababisha ucheweshaji wa ujenzi kwa kweli.

Na. 20

Uuzaji na Uendelezaji wa Viwanda

MHE. RITA E. KABATI (K.n.y. ZARINA S. MADABIDA)
aliuliza:-

Serikali imekuwa ikipima viwanja na kuviuza, huku wananchi wamiliki wa ardhi wakipewa fidia ndogo sana hali hiyo huchangia kuleta umaskini na migogoro ya ardhi:-

(a) Je, kwa nini uuzwaji au uendelezaji wa viwanja vilivyopimwa au kuendelezwa usifanywe kwa ubia katika Serikali na wamiliki wa ardhi?

(b) Je, Serikali ipo tayari kuleta Muswada wa Sheria ya kulinda Ardhi na Maslahi ya wananchi hasa wa vijijini?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO
YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Zarina Shamte Madabida, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kwanza, napenda kumpongeza Mheshimiwa Madabida kwa jithada kubwa anazofanya kutetea haki za wananchi wazawa.

Pili, napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa mawazo mazuri ya Mheshimiwa Mbunge yenye nia ya kuwezesha wananchi waonaomiliki ardhi vijijini kutumia ardhi hiyo kama mtaji yalikwisha fanyiwa kazi na Serikali.

Naamini kuwa Waheshimiwa Wabunge wote wanaelewa maelekezo ya Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ya mwaka 2004 ambayo katika aya ya 4.9.2 inatamka kwamba "*Serikali itatumia ardhi kama njia muhimu ya kuwawezesha wananchi wake kushiriki kikamilifu kiuchumi.*

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI]

Aidha lengo ni kusaldia wananchi watumie ardhi waliyo nayo ama kwa kujipatia hisa katika shughuli za uwekezaji huo au pato lenye kuwanufaisha kushiriki kikamilifu katika shughuli nyingine za kiuchumi."

Ili kulipa nguvu tamko hilo Serikali ilitoa Sera ya kukuza ubia baina ya Sekta za Umma na za Binafsi ya mwaka 2010 yaani (*The Public Private Partnership Policy*) na Bunge lako Tukufu lilitunga Sheria ya kukuza Ubia baina ya Sekta za Umma na Binafsi (*The Public Private Partnership Act*) Na. 18 ya Mwaka 2010 ambayo imerasimisha uanzishaji ubia baina ya taasisi za umma na za binafsi katika uwekezaji ili kukuza uchumi.

Vile vile Serikali kupitia Wizara yangu imekwisha andaa rasimu ya Sera ya Ardhi ni Mtaji, yaani "*Land for Equity Policy*" yenye lengo la kuhakisha kuwa wawekezaji wote wa ndani na nje watakaogawiwa ardhi kwa ajili ya uwekezaji wanatoa hisa zisizopungua asilimia ishirini na tano (25%) ya thamani ya rasimali za kampuni au mradi utakaoanzishwa kwa wamiliki wa ardhi ikiwa ni pamoja na watu binafsi, serikali za vijiji au wilaya na Serikali kuu. Hivi sasa rasimu ya sera hiyo inasubiri kuwasilishwa Baraza la Mawaziri kwa ajili ya kuidhinishwa.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa sasa Serikali haijapanga kutunga Sheria anayopendekeza Mheshimiwa Mbunge kwa sababu inaamini kuwa Sheria ya Ardhi ya Vijiji Na. 5 ya Mwaka 1999 inakidhi dhamira iliyoelezwa nayo. Changamoto iliyo mbele yetu ni kusimamia kikamilifu utekelezaji wa Sera na Sheria, nilizozitaja ili kulinda haki na wamiliki wa ardhi vijijini ikiwa ni pamona na watu binafsi na mamlaka ya Serikali za vijiji.

Aidha napenda kutoa wito kwa watu wote bila kujali nyadhifa zao kuwa waheshimiwa mamlaka za Seriakli za vijiji katika usimamizi wa ardhi ili kuepusha migogoro baina ya makundi mbalimbali katika jamii kwani husababisha muda wa kushiriki katika shughli za maendeleo kupotea bure na wakati mwingine hueweza kugharimu maisha ya watu. (Makof)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, wenzio wanakupigia makofi, wanasema majibu ya maswali ni marefu.

MHE. RITA E. KABATI: Mheshimiwa Soika, ahsante kwa kunipa nafasi kuuliza maswali madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa majibu yako katika swali hili.

(a) Kwa kuwa ardhi katika miji na vijiji ndiyo rasilimali pekee ya urithi katika familia zetu za Kitanzania. Kwa nini Serikali isiweke utaratibu wa kugawa viwanja kwa wana familia, badala ya sasa unapogawa wanagawa kiwanja kimoja tu? (*Makofi*)

(b) Kwa kuwa hati za kumiliki ardhi za kimila hazitambuliki katika baadhi ya Taasisi za fedha?

(c) Je, Serikali inasema nini kuhusiana na suala hilo kwa ajili ya kuwasaidia wananchi ili ardhi iweze kuwasaidia?

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Rita E. Kabati, kama hivi ifuatavyo:-

(a) Kwamba kwa nini Serikali inapogawa ardhi, isiwigawie wanafamilia viwanja badala ya kugawa kiwanja kimoja tu. Nadhani kama nimemwelewa vizuri katika swali hili alimanisha ni kwamba kwa nini familia ile kila mtu asipewe kiwanja, nadhani hiyo ndiyo maana yake, badala ya kila familia kupewa kiwanja kimoja. (*Makofi*)

(b) Mheshimiwa Spika, kama ambavyo nimejibu katika swali la Msingi, tumesema kwamba tunakamilisha Sera ya Ardhi ni Mtaji yaani (*Land for Equity Policy*), ambapo badala ya mtu kuja na kutwaa ardhi ya wana kijiji na kuchukua na kuwalipa fedha ambazo haziwatoshii hata kwa wiki moja.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI]

Mwananchi yule atatakiwa kuwa mbia kwenye mradi utakaoanzishwa pale, ili manufaa yatakayotokana na uwekezaji huo, afaidike yeye aliyepo sasa watoto wake na wajukuu. Huo ndio mpango wa Serikali.

Kwa hiyo, kwanza hilo la kusema labda Halmashauri inakuja inapima viwanja. Tumekwishatoa maelekezo kwa Halmashauri. Kwamba wanapotaka kupanga eneo lazima wananchi washirikishwe na wananchi waeleweshwe kwamba watanufaika vipi na kile kinachofanyika pale.

Huu utaratibu ambao Halmashauri zimekuwa zikienda zinatoa ardhi. Zinapima na kuuza kwanza ndipo zije ziwalipe wananchi hilo tumesema hapa. Wakae nao waelezwe kinachofanyika. Wananchi wakisharithia kile kitakachofanyika pale waamue ya kwamba wanashiriki vipi. Si lazima Halmashauri itwae ardhi. Halmashauri inapashwa iandae mchoro. Wananchi wakishakubaliana nao, sasa wananchi wanaamua, kwamba mimi kama hapa mnataka kujenga shule, nitajenga mimi.

Lakini chini ya sheria ya mipango miji yule mwananchi ambaye ataamua kuendeleza eneo lake mwenyewe, atapashwa kuchangia tunachoita *betterment fee*, kwa ajili ya miundombinu na huduma nyingine zitakazotolewa pale.

Suala la pili, madai ya kwamba hatimiliki za kimila hazitambuliwi. Ninaomba nifafanue hapa, kwamba Hati Miliki za Kimila zina nguvu sawa na hati inayotolewa chini ya ardhi ya ujumla. Ni ile tu kwamba baadhi ya taasisi za fedha, bado hazijatambua hilo tunalolisema.

Faida kubwa ya Hati miliki za Kimila, tofauti na zile hati za ardhi ya ujumla ni kwamba haina ukomo. Haina ukomo kama ile ilivyo ya miaka 33, 66 na 99. Yenyewe unayo ni *parpeture* mpaka mwisho wa maisha yako. Kwa hivyo ina nguvu sawa. Ninatoa wito kwa Mabenki yote kwamba watambue hadhi ya Hati Miliki za Kimila na Washirikiane na wananchi kuwapa mikopo. (*Makof*)

Na. 21

Matumizi ya Mbolea ya Minjingu

MHE. RICHARD M NDASSA (K.n.y. MHE. GODFREY W. ZAMBI) aliuliza:-

Ni kwa nini Serikali inaendelea kuwapelekea Wakulima Mbolea ya Minjingu chini ya utaratibu wa ruzuku kwa ajili ya kupandia mahindi wakati iliwishakataliwa kwa sababu haina tija katika uzalishaji wa mahindi?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA
aliuju:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Godfrey W. Zambi, kama hivi ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, matumizi ya mbolea ya Minjingu (*NPS+*) katika mfumo wa mbolea za ruzuku yamezingatia ushauri wa kitaalam na kisanyansi uliiotokana na utafiti kuhusu matumizi endlevu ya mbolea hiyo. Uwepo wa *CaCO₃* katika udongo unafanya virutubisho vingine hususan vya Nitrogen asilimia 10, *Posphate* asilimia 20, *Sulphur* asilimi 5, *Magnesium* (*MgO*) asilimia 1.5, *Zinc* na asilimi 0.5 kuweza kutumika kikamilifu na mmea hasa kwenye ardhi zenye upotevu wa virutubisho kutokana na mvua nyingi ambapo kitaalam inaitwa (*Leaching*) hali ambayo ikichukuliwa na matumizi ya muda mrefu ya mbolea hususan kama zile zilizokuwa zinatumika za (*Suplate of Ammonia*) (*SA*) undongo katika maeneo hayo unabakiwa na kiasi kikubwa cha tindikali.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kwenye baadhi ya maeneo ya nchi yetu, mbolea ya Minjingu (*NPS+*) imekuwa haikufanya vizuri licha ya matokeo mazuri ya awali ya utafiti. Tathmini imebaini kuwa matumizi yasiyo sahihi ya mbolea hiyo katika maeneo hayo ndiyo imekuwa sababu kuu ya kutotoa matokeo mazuri.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA]

Mheshimiwa Spika, matumizi sasa ya mbolea ya Minjingu hiyo (*NPS+*) yameweza kuongezeka ka uzalishauji wa Mahindi Mpunga na alizeti katika maeneo mbali mbali nchini ikiwemo Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini. Changamoto kubwa kwa hivi sasa ni elimu juu ya matumizi sahihi ya mbolea ya Minjingu kwa wakulima kupitia kwa Makampuni ya Mbolea, mawakala ya Maafisa Ugani.

Mheshimiwa Spika, Serikali imefanya maamuzi ya makusudi ya kutumia mbolea ya Minjingu (*NPS+*) katika mfumo wa ruzuku kwa kuzingatia ushauri huo wa kitaalam na Kisayansi ikiwa ni pamoja na kuzingatia maslahi mengine ya kiuchumi na kijamii, ambayo yanahusisha matumizi na maslahi mapana ya mbolea hiyo.

MHE. RICHARD M. NDASSA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na maelezo mazuri sana ya Mheshimiwa Waziri. Kwa sababu mbolea ya Minjingu, Serikali inatoa ruzuku, na malalamiko yamekuwa mengi ya kwamba mbolea hii ya Minjingu, haifanyi kazi inayotakiwa, tatizo lililopo ni Maafisa Ugani kutopata elimu ya kutosha. Ni lini Serikali kwa dhati kabisa, itawagiza Maasifa Ugani kabla ya kupeleka hiyo mbolea ili Maasfisa Ugani hawa wapate elimu ya kutosha kwa wakulima?

Swali la pili, mbali ya mbolea hiyo ya Minjingu, Mbegu ya Pamba kutoka Kampuni ya *Quton* nayo inapata Ruzuku. Lakini kuna baadhi ya maeneo mbegu hizi zimekwishanza kugawiwa, lakini hazioti. Hata zisipoota mpaka sasa baadhi ya maeneo kwenye Jiombo la Sumve, mbegu hizi hazijapelekwa. Ninaomba kuiuliza Serikali, ni lini mbegu hizo zitapelekwa?

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Spika, naomba nijibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Richard M. Ndassa, kama hivi ifuatavyo.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA]

Mheshimiwa Spika, hili la kwanza la kwamba Serikali imetoa ruzuku kwenye (*NPS+*) ni kweli. Kwa sababu (*NPS+*) ilikuja nia yake ilikuwa kuwa mbadala wa mbole yta *DAP*, ambayo ilikuwa mbolea iliyokuwa inaagizwa kutoka nje na ilikuwa ina gharama kubwa sana.

Kwa hiyo ile mbolea ya Minjingu ya awali wa zamani (*MRP*) tukawaelekeza Minjungu, Serikali na watafiti wengine ya kwamba wakae wajaribu kuboresha mbolea ile ili kupata mbadala wa (*DAP*). Ikapatikana hii (*NPS+*) ambayo ni mbolea iliyoboreshwa, kama alivyoeleza Waziri Mkuu, wakati anajihitimisha Bunge liliopita. Sasa ni kweli naomba nikiri kwamba inaonekana kwamba Maafisa Ugani wetu wameshindwa kupeleka matumizi sahihi ya mbolea hiyo.

Kwa hiyo kuna baadhi ya maeneo ambayo mbolea hiyo halfanyi vizuri sana lakini maeneo ambayo ushauri umekwenda vizuri, maeneo ambayo ushauri umekwenda vizuri, zao hilo limeongezeka mara mbili.

Baadhi ya maeneo ya Ruvuma, Mbeya na Rukwa. Kwa hiyo, hili suala la *extension* kwa maana ya Maafisa Ugani tunalifanyia kazi kama nilivyosema kwenye jibu la awali kwamba itahusu Serikali, Mawakala lakini pia na Maafisa Ugani kwa pamoja ili tupate ufumbuzi wa matumizi bora ya mbolea hii na mbolea zote.

Mheshimiwa Spika, hili la pili la mbegu za *Quton*, ni kweli, mbegu za Kyutoni zimekuja *hybrid*, zile ni mbegu za *hybrid* za *UK 91* kwa maana ya Ukiliguru 91 zinatakiwa zitoe matokeo mazuri sana kuliko mbegu za kawaida na zimeonyesha matokeo mazuri kwenye *field trials*.

Sasa inaonekana pia kwamba kwa sababu ya haya matatizo ya ugani, lakini pia inaonekana kama ilivyokuwa kwenye mbolea ya Minjingu kuna mambo ya ubinafsi binafsi kidogo ya Mawakala na wafanyabiashara. Mbegu hii inakuwa imepata msukumo tofauti kwa wakulima.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA]

Kwa hiyo, tutakwenda kule na tumejipanga ili Wagani na sisi wenyewe kama Wizara, lakini pia na Mawakala wenyewe watoe elimu inayofaa ili mbegu hii ipate matumizi sahihi. (*Makof*)

MHE. DAVID E. SILINDE: Mheshimiwa Spika, ahsante. Nimemsikiliza sana Mheshimiwa Waziri, lakini pia suala la Mheshimiwa Zambi ni swali ambalo katika kikao cha *RCC* yaani Kikao cha Mashauriano ya Mkoa wa Mbeya mwezi Mei, tulikataa mbolea ya Minjingu hususani kwa Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi kwa sababu imeshindwa kuleta matokeo.

Lakini siyo hivyo tu, katika kikao kile Halmashauri ya Wilaya ya Chunya ilirudisha pembejeo za mbegu ya Mahindi ya *OPV*, zote kama zilivyo lakini mwaka huu ukisoma *circular* ya kilimo au waraka wa kilimo ulioletwa umerudisha pembejeo za mbegu ya *OPV* ya Mahindi katika Halmashauri ya Chunya, imerudisha vivyo hivyo pembejeo za ruzuku ya Minjingu mazao yaani *NPS Plus* katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi. Vile vile ukipitia huo waraka, katika Mkoa wa Ruvuma wamepewa *option* kati ya Minjingu ama *DIP*.

Kwa nini uamuzi huu ambao Wizara ilichukua wasingeufanya kwa Mkoa wa Mbeya kuweka *option* kati ya Minjingu au *DIP* kama ambavyo tulikuwa tumeshauru na huu ushauri ultolewa na Maafisa Kilimo wa Mkoa na Mkuu wa Mkoa naye alishangaa kwa nini watu wa Wizara mnatoa maamuzi tofauti na ambayo tumeamua sisi wadau, vikao vyta mashauriano ya Mkoa na Maafisa wa Kilimo wa Mkoa.

SPIKA: Hilo ni swali la nyongeza, isiwe hotuba! Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu!

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika naomba njibui maswali maswali mawili ya David Silinde kama ifuatavyo.

Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)

[NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA]

Mheshimiwa Spika, naomba nimfahamishe tu Mheshimiwa David Silinde kwamba Wilaya yake ya Mbozi na Mombasa kwa pamoja jana zilizalisha tani kama 200,000 lakini mwaka huu wamezalisha.....

SPIKA: Ni tani za kitu gani?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:
Mheshimiwa Spika, ni Tani za Mahindi.

Sasa baada ya kuvuja zile taarifa niliyoipata leo asubuhi kwa wataalam wa Halmashauri yake ni kwamba uzalishaji wa Mbozi umeongezeka na uzalishaji wa Mombasa umeongezeka, leo asubuhi!

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi nataka tu kusema kwamba kweli inawezekana kwamba hapo katikati bado tunakiri kwamba kwenye matumizi yaliyozoleka ya DAPkwa watu kwa makusudi wamekwenda kwa wakulima na kuwatolea maelekezo ambayo yanafanya matumizi ya NPS Plus yasiwe sawa sawa.

Mheshimiwa Spika, naomba kwa ruhusa yako niseme kwamba mwaka juzi (2011) mbolea ya DAP hiyo ambayo tulikuwa tunaagiza nje na tunalipa kwenye mfumo wa ruzuku ilikuwa kwa wastani ni shilingi 85,000/= mpaka 90,000/= lakini mwaka huu wameshusha mpaka 70,000/=, tukiuliza huko nje hakuna ushahidi wowote unaoonyesha kwamba bei imeshuka. Ina maana kwamba mkulima na Serikali walikuwa wanaumizwa kwa wastani wa shilingi 20,000/= kwa kila mfuko.

Kwa hiyo, baada ya kuonekana wamepata mshindani wote wameshuka sasa wana-*quote* shilingi 70,000/= . Sasa hiyo ni maslahi kwa mkulima na maslahi kwa Serikali kwa sababu tuna mbolea nydingi zaidi ya kusambaza.

Lakini ushauri wa kitaalam na *report* niliyokuwa nayo ya *Integrated Research* ya Wataalam wote wa Tanzania

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA]
inasema kwamba mbolea ya Minjingu haina matatizo. *NPS Plus* isipokuwa tuna tatizo la *application*. Ndiyo maana nikamjibu Mheshimiwa Ndassa kwamba tatizo tulilokwu nalo ni la wagani kufikisha elimu ya matumizi sahihi.

Mheshimiwa Spika, hii ya *OPV*niseme tu kwamba hizi mbegu za *OPV* za Mahindi zinazosemwa ni kweli, kwamba hapa katikati kumekuwa na biashara ya mambo ndivyo sivyo ambapo watu wanachukua mbolea wanaweka kama ni *label* ya *OPV* na kwamba ni mbegu *Hybrid* lakini ni mbegu feki, ndiyo maana tuliomba kwenye Bajeti na tulipewa pesa kidogo za ziada ya kwamba hizi taasisi zinazodhibiti mbolea, mbegu na madawa ziongezewe pesa ili ziweze kufika kwa wakulima na kudhibiti kwamba hizi ni mbegu sahihi zinazotolewa na kazi hiyo inaendelea.

Na. 22

Utafiti wa Zao la Mzeituni (*Olive*)

**MHE. MASOUD ABDALLA SALIM (K.n.y. MHE.
MUHAMMAD IBRAHIM SANYA)** aliuliza:-

Tanzania ni nchi kubwa yenye rutuba kutegemeana na maeneo na hali ya hewa ya Mkoa hutofautiana kijigrafia na mafuta yatokanayo na zao la Mzeituni yana ubora na bei nzuri duniani.

- (a) Je, Serikali imewahi kufanya utafiti wa zao hili?
- (b) Kama ndiyo. Je, ni maeneo gani ya Tanzania yanaweza kustawi zao hili?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA
alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Muhammad Ibrahim Sanya, Mbunge wa Mji Mkongwe, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA]

Mheshimiwa Spika, zao la Mizeituni (*Olive*) linalimwa kwa wingi duniani katika maeneo yenye hali ya hewa ya asili ya Ki-Mediterranean climate (Asilimia 95) na katika maeneo ya *sub-tropical* (Asilimia 5). Kwa Afrika nchi zinazolima kibiashara zao hilo ni Morocco, Tunisia, Misri, Algeria na Libya.

Kwa hiyo, utaona kwamba mazao haya yapo kwenye kanda ya *Mediterranean*. Asilimia 90 ya zao hilo huzalishwa kwa ajili ya mafuta ya kula, matunda na mashudu ambayo yanapatikana baada ya kukamua mafuta hutumika kama chakula cha mifugo.

Mheshimiwa Spika, mafuta ya kula ya Mzeituni yana ubora wa kipekee. Kiafya mafuta haya yanahusishwa na kupunguza ugonjwa wa moyo na Kansa na magonjwa mengine na hivyo kufanya mafuta hayo kununuliwa na walaji kwa bei ya juu. Utafiti wa kina wa zao la Mizeituni haujawahi kufanyika kufanyika hapa nchini kutokana na vipaumbele vya utafiti.

Aidha, kwa uangalizi wa awali, vituo vya utafiti nchini vimeshaingiza *germplasm collection* za aina mbalimbali ya miche ya Mizeituni na kuhifadhiwa katika benki ya nasaba za mimea (*Gene Bank*) katika kituo cha utafiti wa Mboga, Matunda na Maua HORTI Tengeru Arusha, Mlingano (Kituo cha Amani), ARI Kizimbani Zanzibar na Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine.

Mheshimiwa Spika, nchi ya Tanzania ina maeneo yenye ekolojia kama vile ukanda wa baridi (*temperate*), ukanda wa hali ya hewa ya kati (*sub-tropical*) na ukanda wa hali ya joto (*tropical*). Wawekezaji binafsi wanafanya uwekezaji wa mazao ambayo yanastawi katika mazingira ya *sub-tropical* baada ya kuzingatia viashiria vingine vinavyochangia ustawi bora wa zao la mizeituni, hivyo hakuna sababu ya kutoamini kwamba zao la Mizeituni haliwezi kuendelezwa katika ukanda wa hali ya hewa ya kati wa Tanzania.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA]
Aidha, Wizara ifashirikiana na taasisi za utafiti na wawekezaji katika nchi zinazolima zao hilo ili kuweza kuanzishwa utafiti wa zao hili hapa nchini kubaini kustawi kwa zao hilo na upatikanaji wa mbegu kabla ya kuhamasisha uzalishaji kamili.

MHE. MASOUD ABDALLA SALIM: Mheshimiwa Spika, nakushukuru lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Kwanza, kwa kuwa Serikali imekiri kwamba mti wa Mzeituni una ubora kipekee wa afya ambao unapunguza magonjwa ya Moyo na kukabiliana na magonjwa ya Kansa na Serikali imesema kwamba utafiti wa kina wa mti wa Mzeituni haujafanyika.

Je, Serikali ina sababu gani za msingi madhubuti za kucheleweshwa kwa utafiti wa mti wa Mzeituni ili kuweza kuyakabili magonjwa ya Moyo na Kansa kwa Watanzania? Au, Serikali haina mpango mzuri wa kuweza kuwasaidia Watanzania kuweza kuyakabili magonjwa haya?

Pili, kwa kuwa, Serikali imekiri kwamba moja ya mazingira yanayoweza kustawi kwa mti huu ni ile ya hali ya hewa ya kat i yaani *Sub-tropical*.

Je, ni sababu zipi za msingi zilizopelekea Serikali ambapo mnaelewa kwamba Tanzania ina hali ya hewa ya *sub-tropical* lakini hadi leo zao hili hamjatafuta wawekezaji wa kuweza kulima zao hili. Tatizo ni nini kwa Serikali ya Tanzania kuweza kuwasaidia Watanzania ambao magonjwa haya yanaendelea kuwasaidia siku hadi siku, vifo vinaongezeka lakini Serikali haitaki kulishughulikia jambo hili?

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana.

SPIKA: Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri na wewe usitupige *lecture!*

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:

Mheshimiwa Spika, naomba kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika nijibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, kwanza nimekiri kwamba utafiti wa kina haujafanyika lakini kimsingi ni kwa sababu ya *commercial viability*. *Olives* nyingi zinazolimwa duniani zinalimwa kwenye ukanda wa *Mediterranean* na *Olives* zina *varieties* tofauti. Zile *varieties* zenyе ubora kabisa ambao unapata soko kwenye dunia zinalimwa kwenye baadhi ya nchi chache tu lakini kama Algeria na kadhalika ambao ni *Mediterranean Countries* nao wanalima lakini asilimia 45 ya *Olives* zote duniani zinalimwa nchi moja tu yaani Spain, nyingine kama kumi na ngapi zinalimwa *Italy* na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kabla hatujahamasisha kilimo cha Mizeituni ni lazima tuangalie kwamba wale wakulima tunaowahamasisha wanaweza kwenda kuingia sokoni na zao hilo na wakapata manufaa?

Sasa kwa sababu ya hali hii ni na utafiti huu, utafiti wa minazi tu mpaka leo tuna miaka 30 bado hatujakamilisha kwa sababu ya ugumu wa masuala ya utafiti. Utafiti tangu *Olives* zilivyoingia mwaka 1946 mpaka leo bado hatujaweza ku-determine kama itapata *commercial viability*. Kwa hiyo, hili ni suala la *varieties* na *qualityya* *Olives* zenyewe na kuingia kwenye soko ndiyo maana ni ngumu kuingia huko.

Mheshimiwa Spika, hili la pili la kwamba tuna *climate* ya *sub-tropical* nimelijibu na swalı la kwanza ni kweli tuna ekolojia ya *sub-tropical* lakini kabla hujapanda au hujazingatia siyo ekolojia tu, bado kuna masuala mengine mengi kama hayo ya soko, *varieties*, *breeding*, na *plant breeding* na kadhalika, ambayo yanafanya kwamba suala hili kidogo lina utata. Lakini tunaendelea kufanya utafiti na kuangalia huenda tukabaini mbegu au *variety* ambayo itakuwa bora kwa Watanzania kuzalisha. (*Makofı*)

Kutenga Ardhi Inayofaa kwa Kilimo

MHE. BETTY E. MACHANGU (K.n.y. MHE. NAMELOK E. SOKOINE) aliuliza:-

Nchi nyingi duniani hutenga ardhi inayofaa kwa kilimo na kulindwa kwa mujibu wa sheria na Tanzania hususani Mkoa wa Arusha unayo ardhi inayofaa kwa kilimo kama vile mashamba ya Burka, Lakilaki, Manyara, Gomba na kadhalika ambayo yamebadilishwa matumizi kuwa viwanja.

Je, Serikali iko tayari kutunga sheria ya kulinda ardhi ya kilimo kama nchi nyingine duniani wanavyofanya?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA
aliujibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Namelok Edward Sokoine, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kwamba bila ya kutenga, kulinda na kuendeleza ardhi ya kilimo, ni vigumu kwa nchi inayoendelea kama Tanzania kupiga hatua kubwa ya maendeleo katika kilimo kwa kuzingatia kuwa kilimo cha kisasa kinategemea upatikanaji wa ardhi inayofaa kwa kilimo.

Mheshimiwa Spika, hivyo basi, kwa kutambua kuwa ardhi inayofaa kwa ajili ya kilimo inapaungua kutokana na kuongezeka kwa shughuli mbalimbali za kiuchumi na kijamii ikiwemo makazi, Wizara kwa kushirikiana na wadau wenzetu katika suala hili imeanza maandalizi ya mfumo wa kisheria wa kulinda ardhi ya kilimo.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU WAZIRI WA KILIMO CHAKULA NA USHIRIKA]
Mheshimiwa Spika, inapendekezwa pia kuwa kwa kuzingatia umuhimu wa ardhi ya kilimo, kama ilivyo kwa ardhi zitumikazo kwa ajili ya barabara, maliasili na hifadhi ya ardhi ya kilimo itambuliwe kama ardhi mionganoni mwa ardhi za hifadhi (*reserved land*) chini ya Sheria ya Ardhi na Sheria ya Ardhi ya Vijiji.

Mheshimiwa Spika, mapendelekezo ya sheria hiyo ya matumizi bora ya ardhi (*Agricultural Land Management Act*) yanategemewa kuimarisha mfumo wa usimamizi wa kilimo na matumizi endelevu ya raslimali za kilimo ikiwemo raslimali ardhi yenye, maji, uoto wa asili na mazingira pamoja na kutambua maeneo yanayofaa kwa kilimo mahsus.

Aidha, sheria hiyo pia itaweka kanuni zitakazotumika kuitambua, kuainisha, kupima, kutenga, kusajili na kuitambua kitaaluma madaraja, uwezo na sifa za kila daraja la ardhi la kilimo.

Pia kuweka taratibu za kusimamia uendelezaji wa ardhi ya kilimo, kuainisha majukumku ya mmiliki ikiwa ni pamoja na kuweka mfumo wa kuwataka wawekezaji na wanaomiliki ardhi ya kilimo kutumia ardhi wanayomiliki kwa shughuli zilizoainishwa kisheria ambazo zitazingatia kilimo matumizi bora na endelevu.

MHE. BETTY E. MACHANGU: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Spika, naomba kuuliza kuhusu mradi wa Rubada wa Kilimo ambapo tunaambiwa Bonde la Mto Rufiji limekuwa na nafasi kubwa ya kuweza kugawa maeneo na hususani kwa vijana niliona hata mfano kuna vijana wa Rufiji waligawiwa maeneo.

Sasa naomba kuuliza, katika mikoa mingine kwa vile tunaongelea mambo ya *big results now*, katika mikoa mingine.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. BETTY E. MACHANGU]

Je, ni maeneo gani yametengwa kwa ajili ya vijana kwa ajili ya kilimo?

Pili, tunaongea kuhusu *big results now* katika kilimo na maeneo mengine, lakini napenda kujua kwamba Serikali ina mpango gani sasa wa kuanzisha kilimo cha umwagiliaji kwa sababu maeneo mengi yamekuwa na ukame hususani mikoa ya Kanda ya Kaskazini.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza mabwawa kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji kwa ajili ya kupata hizo *big results now?*

SPIKA: Mheshimiwa Betty Machangu unatenda haki kwa swali hili? Hujatenda haki kabisa kabisa maana *big results* hakuna chochote alichouliza hapo. Waziri kwa sababu unajua *big results* jibu lakini, lakini Mheshimiwa Betty hukutenda haki.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Betty Machangu, kama ifuaavyo.

Kwanza, hili la Rubada na vijana wa Rufiji, Rubada wana kituo cha kuendelea, sasa kilichotokea ni kwamba Halmashauri yenyewe ya Rufiji, Mkuu wa Wilaya Mheshimiwa Nurdin, alikaa na na vijana akasema basi watatenga eneo na wametenga eneo kama ekari 50 ambazo vijana wanakwenda kujifunza mbinu bora za kilimo, hili hata Igunga limefanyika.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hili naomba nilisisitiza kwamba suala la kugawa matumizi ya ardhi kwa ajili ya vijana na kadhalika lipo kwenye Halmashauri na sisi kwenye Wizara tutatoa msukumo wa kitaalamu ili vijana hawa wapate kuona kama kilimo ni sehemu ya ajira mbadala.

Mheshimiwa Spika, hili la pili la kilimo cha umwagiliaji cha *BRN* mikakati iliyokuwepo kwenye *BRN* ni kuhakikisha kwamba uwekezaji uliofanyika kwenye *scheme* za sasa hivi

Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)

[NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA]
kwanza utoe tija kabla hujingia kwenye *scheme* mpya
vinginevyo tutakuwa hatufanyi uwekezaji ulio makini.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba niseme kwamba kuna miradi imetambuliwa kwenye *BRN* ambayo italeta matokeo ya haraka lakini inatambuliwa ile miradi ambayo tayari imeshaanza kufanyiwa kazi. Tumalize hiyo halafu ndiyo twende kwenye miradi mipya.

MHE. DAVID Z. KAFULILA: Mheshimiwa Spika, nchi za wenzetu ambazo zimepiga hatua kila kitu kinakuwa kimekwisha kufanyiwa tafiti ikiwa ni pamoja na matumizi ya ardhi.

Lakini leo Tanzania nzima ardhi iliyopimwa kwa ajili ya matumizi mbalimbali ni 12% tu, sasa kama miaka 50 Serikali imepima ardhi kwa matumizi mbalimbali 12% itachukua miaka mia ngapi Serikali hii kukamilisha upimaji wa matumizi ya ardhi ili kusudi tufike mahali tujue Tanzania tuna ekari kiasi fulani ambazo zinatafaa kwa kilimo fulani, tuna ekari kiasi fulani ambazo zinatafaa zao fulani. Mtachukua miaka mia ngapi?

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kafulila kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kiasi cha ardhi iliyopimwa hadi sasa hivi ni kidogo na hiyo inatokana na uwezo mdogo wa Serikali kutekeleza mpango wake uliopo wa sasa hivi kwa sababu ya mahitaji katika sekta nyingine.

Mwaka 2013 mwezi August, Serikali kwa maana ya Baraza la Mawaziri ilidhinisha mpango yaani *program* ya matumizi bora ya ardhi ambao utatekelezwa kwa muda wa miaka 20 yaani *the land use plan framework*.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAE, YA MAKAZI]
Matarajio yetu ni kwamba kuanzia mwaka huu unaokuja wa fedha Tume ya Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi itatengewa fedha za kutosha kwa ajili ya kutekeleza mpango huo.

Lakini pia tulikwishatoa wito kwamba Halmashauri zote za Wilaya na Miji zitenge fedha kwenye Bajeti zao ili zishirikiane na Tume ya Matumizi ya Ardhi kupanga matumizi ya ardhi katika maeneo yao na hivyo kuharakisha utekelezaji wa *program* hiyo kwa madhumuni ya kuwezesha ardhi kupimwa na kumilikishwa watumiaji mbalimbali na hii itapunguza migogoro ya makundi mbalimbali ikiwemo ile ya wafugaji na wakulima.

Na. 24

Ukarabati wa Miundombinu ya Maji Mufindi Kusini

MHE. MENDRAD L. KIGOLA alijibu:-

Kwa miaka mingi sasa kumekuwa na tatizo kubwa la kukosefu wa maji kwa wananchi wa Mufindi Kusini linatokana na kuharibika kwa miundombinu ya maji iliyojengwa mwaka 1970, kwenye matenki ya maji kumi (10) katika vijiji vya Sawala, Kibao, Igowole, Kisanga, Ihomasa, Nyololo, Maduma, Mukangwa, Ikangamwani na Nyigo, lakini miundombinu yake haijafanyiwa ukarabati wowote:-

Je, Serikali ina mikakati gani ya kukarabati miundombinu hiyo ili kuwapatia maji safi na salama wananchi wa Jimbo la Mufindi Kusini?

NAIBU WAZIRI WA MAJI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mendrad Lutengano Kigola, Mbunge wa Mufindi Kusini, kama ifuatavyo:-

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU WAZIRI WA MAJI]

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua tatizo kubwa la ukosefu wa maji kwa wananchi wa Jimbo la Mufindi Kusini, kutokana na kuharibika kwa miundombinu ya maji iliyojengwa miaka ya 1970. Kwa sasa Serikali inaendelea na utekelezaji wa mradi wa Vijiji (10) katika vijiji vya Sawala, Kibao, Ikimilinzowo, Kiponda, Luhunga, Mkonge, Lufuna, Mtwango na Igoda. Ujenzi wa miundombinu ya maji kwa Vijiji vya Ikimilinzowo na Kiponda upo katika hatua ya kuanza baada ya wakandarasi kupatikana. Vijiji vya Sawala, Kibao, Luhunga, Mkonge, Lufuna, Mtwango na Igoda vipo katika hatua ya kutangaza zabuni za kuwapata wakandarasi wa ujenzi wa miradi ya maji.

Mheshimiwa Spika, Serikali ina mkakati wa kukarabati miundombinu ya maji katika vijiji vya Igowole, Kasanga, Ihomasa, Nyololo, Maduma, Mukangwa, Ikangamwani na Nyigo. Kazi hii imepangwa kufanyika katika awamu ya pili ya utekelezaji ya Programu Maji na Usafi wa Mazinigra Vijijini itakayoanzia mwaka 2014/2015.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa wito kwa Halmashauri zote nchini kuhakikisha kwamba miradi yote iliyojengwa na Serikali ama Wafadhili inakuwa na vyombo vya kusimamia (*COWSOs*) na Halmashauri zifuatilie kwa karibu ili miradi hiyo iwe endelevu.

MHE. MENDRAD L. KIGOLA: Mheshimiwa Spika, kwanza nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali kwamba hatua zimeanza kufanyika katika Jimbo langu la Mufindi Kusini hasa kwa kijiji cha Kiponda utekelezaji umeanza. Lakini katika vijiji vya Sawala, Igoda, Ikimilinzowo, Kibao, Luhunga, Mkonge, Lufuna, Mtwango na Igoda na fedha inaonekana ipo. Sasa je, utekelezaji wa kumpata mzabuni inachukua muda gani?

kwa kuwa vijiji vya Sawala vilishachangia fedha yao kwa muda miaka mitatu sasa imepita na watu hawana maji kabisa. Je, Serikali haiwezi kuchukua hatua za dharura ili kuhakikisha miradi hii inanza mapema?

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, lakini kwanza nampongeza kwa namna ya pekee anavyofuatilia miradi ya maji ya Jimbo lake.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji unafuata ngazi mbalimbali. Jambo la msingi kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi kwamba ile miradi imekwishatangazwa akipatikana mkandarasi ndiyo unasainiwa Mkataba wa yeze kuanza kujenga hiyo miradi ya maji. Miradi hii ya vijiji 10 iliyo mingi inachukua kati ya miezi sita mpaka mwaka mmoja inategemea ni teknolojia inayotumika, lakini iliyo mingi ni miezi sita.

Kwa hiyo, tunategemea kwamba miradi ni kati ya ile miradi ambayo itawapatia wananchi maji kabla ya mwezi Juni, mwaka kesho ya vijiji 10.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya pili, kwamba vijiji vilichangia fedha tutafuate hatua za dharura ili viweze kupata maji. Kwanza nataka kumwambia Mheshimiwa Mbunge kwamba fedha walizochangia wananchi wa vijiji hivi hazitumiki kwenye ujenzi, fedha hizi watazitumia kuendeshea mradi utakapokuwa umekamilika.

Mheshimiwa Spika, nadhani Serikali imeishachukua hatua ya dharura kwa sababu vijiji 10 ilikuwa vitekelezwe kuanzia 2014 viliivyo vingi, viliivyo kuwa vinabakia 5, lakini baada ya kuanza Mpango wa kutekeleza sasa kwa Matokeo Makubwa tumevuta vile vijiji vitano na tumeanza kuvitekeleza katika mwaka huu wa fedha ambapo fedha zimeishatengwa na zimeishaanza kuingizwa kwenye Halmashauri mbalimbali ili ujenzi uanze mara moja.

MHE. JOSEPHINE J. NGENZABUKE: Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa kuniona, nina swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa, Wilaya ya Kasulu imejaliwa kuwa vyanzo vingi vya maji ikiwa pamoja na mito midogo midogo pamoja na mito mikubwa, ikiwa ni pamoja na mito mkubwa

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. JOSEPHINE J. NGENZABUKE]

kabisa wa Mto Malangarasi. Lakini vipo vijiji ambavyo vimepakana kabisa na mto huo havina maji. Mfano kijiji cha Makere, Nyarungusu na Herusingu.

Je, Serikali ipo tayari sasa kuweza kutumia maji ya kutoka Mto Malangarasi na kuyasambaza katika vijiji hivyo nilivyovitaja na vingine ambavyo vinazunguka mto Malangarasi?

SPIKA: Mheshimiwa Nganzebuке hata wewe ni swali jipya kabisa, hili linatakiwa lisimame peke yake siyo mradi ikisemwa maji kila mtu anaweza kuuliza maji tu. Mradi Naibu Waziri kwa sababu unajua hebu jibu tu, lakini ni swali jipya.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, Serikali inatekeleza miradi ya maji vijiji na kwa kuanzia tumeanza na vijiji 10 kila Halmashauri. Nataka nimirikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba ili kuwapelekea wananchi maji tunaangalia teknolojia mbalimbali ikiwemo kutumika mito iliyo maeneo hayo, kuchimba visima kama hakuna mito, ikiwemo kujenga mabwawa maeneo yanayohusika.

Kwa hiyo, vijiji alivyovitaja kama havipo kwenye vile vijiji 10 tutaviingga katika awamu ya pili ambayo inaanza mwezi Juni, 2014 ambapo tumeagiza kila Halmashauri ilete vijiji 20 mpaka 30 na tumwaomba Mheshimiwa Mbunge ashirikiane na Mkurugenzi na Mhandisi wa Wilaya kuona kama vile vijiji vinaingizwa ili viweze kuanza kupewa maji kwa teknolojia itakayokuwa imetathiminiwa na wataalam kwamba ipi inafaa.

Na. 25

Ongezeko la Bajeti ya Wizara ya Maji - 2013/2014

MHE. AZZA HILLAL HAMAD aliuliza:-

Katika mwaka wa fedha 2013/2014 kumekuwepo na ongezeko la fedha kwenye Bajeti ya Wizara ya Maji:-

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. AZZA HILLAL HAMAD]

(a) Je, ni fedha kiasi gani zimetengwa kwa ajili ya kutatua tatizo la maji lililopo katika Halmashauri ya Shinyanga?

(b) Je, ni vijiji vingapi vitanufaika na ongezeko hilo la fedha na vijiji vipi?

NAIBU WAZIRI WA MAJI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Azza Hillal Hamad, Mbunge Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ili kutatua tatizo la maji lililopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga katika mwaka wa Fedha 2013/2014, Serikali imetenga kiasi cha milioni 580.5 kupitia mfuko wa pamoja (*Basket Fund*) na kiasi cha milioni 358.7 kupitia mgao wa ongezeko la fedha za ndani kiasi cha bilioni 184.5 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maji vijijini.

(b) Mheshimiwa Spika, katika Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, Serikali inatekeleza mradi wa maji wa vijiji (10) katika vijiji kumi na tano (15). Vijiji vinavyonufalka na ongezeko la fedha zilizotengwa mwaka 2013/2014 ni vijiji kumi (10) vya Sayu, Bunonga, Kazuni, Mishepo, Didia, Mendo, Nyashimbi, Manyanda, Mwamadilanha na Mwakitolyo ambavyo viro katika hatua mbalimbali za utekelezaji na tayari vijiji vya Sayu na Bunonga vimekamilika. Vijiji vitano (5) viliv yokosa maji vya Lyamidati, Jomu, Ibingo, Ikonda na Bugogo Halmashauri imeanza zoezi la kuvitafutia vyanzo vingine vya maji.

MHE. AZZA HILLAL HAMAD: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. AZZA HILLAL HAMAD]

Kwa kuwa, fedha iliyotengwa katika miradi hii ni kidogo kuliko thamani halisi ya miradi yenyewe na fedha hiyo kidogo haijafika katika Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Spika, naomba nimwulize Mheshimiwa Naibu Waziri maswali mawili.

La kwanza, je, ni lini Serikali itapeleka fedha hizo kwa wakati katika kijiji cha Mendo, Nyashimbi na Manyanda ambako tayari walishatangaza zabuni na fedha hiyo haijafika?

Katika vijiji ambavyo vilikosa maji katika miradi 10, vijiji vitano vilikosa maji kikiwemo kijiji cha Jomu aliyekuwa Naibu Waziri wa Maji Mheshimiwa Lwenge alifika katika kijiji cha Jomu na kuahidi kujenga tenki kubwa katika kisima cha Mwakisu ambacho kina maji mengi na kinahudumia zaidli ya vijiji vitano na ahadi hiyo mpaka leo haijatimia. Naibu Waziri ananiambia nini kuhusu kisima cha Mwakisu hapo juu?

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, Iakini kwanza nampongeza kwa ufuatiliaji wa miradi ya maji na nimeduwa akitufuatalia mara kwa mara ili kuona kama miradi inatekelezwa.

Mheshimiwa Spika, siyo kweli kwamba fedha ni kidogo, naomba nitumie nafasi hii kutoa taarifa kwamba katika Wilaya ambayo ina bahati ya kuwa na miradi mingi ni Shinyanga, kwa sababu Shinyanga sasa hivi kwanza tulipeleka maji katika vijiji 20 katika Mradi wa Kahama - Shinyanga na sasa hivi tumepanga vilevile kwenye bajeti kuvipatia vijiji maji vijiji 46 ambavyo tayari utekelezaji wake umeanza na tunaanza na vijiji 10.

Kwa hiyo, mradi ule wa kutoa Maji Ziwa Victoria mpaka Shinyanga ukikamilika vijiji 46 vitapata maji kati ya vijiji 100 katika ule Mradi mzima.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU WAZIRI WA MAJI]

Kwa hiyo, Serikali imefanya kazi kubwa katika Wilaya hii. Lakini mwezi Oktoba, mwaka huu tumepeleka fedha milioni 600 ambazo Mhandisi na Mkurugenzi wamekiri nilipoongea nao kama wamezipata kwa ajili ya utekelezaji wa vijiji 10 na tunaendelea kupeleka nyingine ambazo zitakwenda awamu hii ya pili.

Kwa hiyo, ningewomba Mheshimiwa Mbunge awasiliane na Mhandisi na Mkurugenzi ili apate hizo taarifa ambazo ni sahihi kwamba fedha zimeishapelekwa na wana fedha nyingi ambazo wamepangija na ambazo nimezisema kwenye swali langu la msingi.

Mheshimiwa Spika, vijiji vilikosa maji ni pamoja na Jomu, kama nilivyosema katika jibu langu la msingi kwamba vijiji vilikosa maji tunafanya utafiti vipate maji na kama hiyo sehemu aliyosema ina maji ahadi hii tutaitekeleza kwa sababu katika vile vijiji vikikamilika 66 vijiji vinavyofuata vilivybaki maana Wilaya hii ina vijiji 117, tutahakikisha na Jomu inapata maji. Nataka nimhakikishie kwamba na hili tutalishughulikia.

MHE. JUMA A. NJWAYO: Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini uzoefu umeonyesha kuwa ahadi nyingi ya hizi fedha hazifiki kwa wakati kwenye maeneo yetu, ninayo mifano ya kule Tandahimba, Newala, Mtwara Vijiivini hata jirani yangu hapa moja ya mambo aliyokuwa analalamika ni hiyo hiyo kwamba fedha hazifiki kwa wakati.

Je, Serikali inafanya nini ili kuhakikisha fedha zinatifa kwa wakati kwa hiyo miradi hii isichelewe kutekelezwa?

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, kwanza, ninakubaliana naye kwamba ni kweli fedha hazifiki kwa wakati. Lakini hii inatokana na mchakato wa wale wanaohusika kuzipeleka fedha. Kwa mfano, hizi fedha za mgao wa robo ya kwanza tumezigawa sisi Wizarani mwezi Oktoba, lakini mpaka sasa hivi baadhi ya maeneo hawajazipata.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU WAZIRI WA MAJI]

Kwa hiyo, tutakazofanya sasa hivi nimeongea na mwenzangu kwamba ile orodha ya mgao utaileta kwa Wabunge ili nylie pia mtusaidie kufuatilia na kuona kama zile fedha zinafika. Nawaagiza wale watendaji wote wanaohusika kwenye mlolongo wote wa kuhakikisha fedha za maji zinafika kwa wahusika basi yale mafaili ya maji wayape kipaumbele ili fedha ziwafikie walengwa kwa mara moja.

Na. 26

Hitaji la Minara ya Simu Wilayani Kilombero

MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE (K.n.y. MHE. ABDUL RAJAB MTEKETA) aliuliza:-

Pamoja na kujaza fomu za kuomba minara na ahadi ya Waziri hapa Bungeni mwaka jana (2012) kuhusu upelekaji wa minara ya simu Tanganyika, Mwagati na Uchindile Wilayani Kilombero:-

Je, ni lini ahadi hiyo itatekelezwa?

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Abdul Rajab Mteketa Mbunge wa Kilombero, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua uwepo wa matatizo ya mawasiliano katika Kata mbalimbali za Wilaya ya Kilombero. Aidha, Serikali imeanzisha Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (*UCSAF*) kwa lengo la kufikisha huduma za mawasiliano hususan kwenye maeneo yasiyo na mvuto kibashara. Serikali kupitia Mfuko huo inaendelea na hatua mbalimbali kuhakikisha kwamba ahadi alioitoa Mheshimiwa Waziri Bungeni mwaka jana ya kufikisha mawasiliano ya simu inatimizwa haraka iwezekanavyo.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA]

Kwa kuzingatia ahadi hiyo, tayari Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa wote (*UCAF*) inayaainisha maeneo mbalimbali yanayohitaji mawasiliano kwa kuangalia idadi ya wakazi, ukubwa wa eneo na kiwango kilichopo cha mawasiliano na ruzuku inayofaa kwa kila Kata. Kata za Mwagati na Uchindile zimejumuishwa katika maandalizi ya orodha ya Kata zitakazoingia katika zabuni ya Awamu ya pili (*WB Phase 2*), inayotajaraiwa kutangazwa katika mwaka ujao wa fedha yaani 2014/2015.

MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mteketa naomba nimwulize Mheshimiwa Naibu Waziri maswali mawili madogo ya nyongeza.

Moja, kwa kuwa mwaka fedha aliyoahidi Mheshimiwa Waziri umepita bila mradi huu kutekelezwa.

Je, Naibu Waziri anawambia nini wananchi wa Jimbo la Kilombero na lini sasa mradi huu utatekelezwa ili kuondoa kero kubwa inayowakabili wananchi wa Jimbo la Kilombero?

Pili, kwa kuwa, majibu ya aina hii yamekuwa yakitolewa mara nyingi, *phase one, phase two*, Mheshimiwa Naibu Waziri anaweza kuliambia Bunge hili, *phase one* ni wapi wananchi wamepata mawasiliano ili tuweze kuamini *phase two* mradi huu utatekelezwa?

SPIKA: Ahsante kwa kuwa mwaminifu. Naibu Waziri majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Spika, kwanza nimhakikishie mwaka nilioutaja haujaisha, tunao, tunaendelea nao, tupo katikati ya mwaka huo, nina uhakika kwamba zabuni zikitangazwa mwezi Januari, 2014 bado tupo ndani ya mwaka huu na nina uhakika kwamba zabuni hizo zitatangazwa.

Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)

[NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA]

Mheshimiwa Spika, majibu ya *phase one, phase two* ni kweli tumekuwa tukisema majibu ya *phase one, phase two*, lakini kufanya hivyo, tulikuwa tukifanya kwa sababu hatukuwa na fedha za kutosha.

Sasa hivi Serikali inafanya majadiliano na Serikali ya India ili kupata fedha nyingi zaidi ili tuweze kutangaza vijiji vyote kwa wakati mmoja bila kujali wapi kuna matatizo au wapi kuna mapungufu zaidi.

MHE. LUHAGA J. MPINA: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa katika miradi ya *phase one* inayosemwa sasa hivi, Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano alitupa barua wahusika wa maeneo hayo nikiwemo mimi ya kutwambia kwamba Serikali inazo fedha na itatekeleza mradi mara moja kuanzia mwezi Julai, lakini hadi sasa ni Desemba, 2013 hakuna kinachoendelea.

Mfano, Jimboni kwangu mimi katika Kata ya Mwasengela na Kata ya Lindeka zote zilipewa *dollar* Marekani 144, 000 na akasema kwamba mzabuni amepatikana wa Kampuni ya Tigo, sasa nini sababu inayopelekea mpaka sasa hivi miradi hiyo isianzishwe na isitekelezwe? (*Makof!*)

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Spika, naomba tu nimfahamishe Mheshimiwa Mpina kwamba utekelezaji tayari unaendelea, tayari wazabuni wameishapewa Mikataba na wazabuni sasa hivi wapo katika mchakato wa kuhakikisha kwamba wanaweka minara, hii ikiwa pamoja na kuhakikisha kwamba wanaweka minara, hii ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kwamba wanaangalia sehemu ambazo zinafaa kuweka minara hiyo na ni sehemu mbalimbali.

Kwa hivyo, nimhakikishie tu kwamba wakandarasi wapo *site*, lakini kulingana na mchakato wa kuhakikisha kwamba minara inasimikwa ni lazima wafuate Sheria na taratibu na Kanuni ambazo sote kwa pamoja tunazifahamu.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Na. 27

Ulipaji wa "Dependant Visa" kwa Raia wa Nchi Wanachama wa Afrika Mashariki

MHE. HUSSEIN MUSSA MZEE (K.n.y. MHE. MUHAMMED AMOUR CHOMBOH) aliuliza:-

Raia wa nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki hawalipi Visa wanapotembelea nchi wanachama:-

Je, kwa nini raia hao hulipishwa ada ya "Dependant Visa" dollar mia tano Hamsini (\$550) kama wanavyolipishwa raia wa nchi nyingine?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Muhammed Amour Chomboh, Mbunge wa Magomeni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba raia wa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki hawalipi Visa wanapotembelea nchi wanachama. Hata hivyo, napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kuwa hakuna kibali kinachoitwa *Dependant Visa*.

Mheshimiwa kibali kinachotolewa na Serikali kwa Mujibu wa Kanuni ya 9, ya Kanuni za Uhamiaji wa mwaka 1997, ni kibali kinachoitwa Hati ya Mfuasi yaani *Dependant Pass*. Kibali hiki hutolewa kwa mgeni yejote ambaye ni Mfuasi wa Mgeni Mkaazi au Mwanamke raia wa kigeni aliyeolewa na mwanamme raia wa Tanzania ili kumwezesha Mfuasi huyo kuishi nchini na mwenyeji wake au mumewe kwa mujibu wa Sheria.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI]

Wageni wanaopewa kibali cha aina hii ni kama vile Mke na watoto. Ada ya kibali hiki kwa mujibu wa tangazo la Gazeti la Serikali Namba 186 la mwaka 2011 jedwali la pili, ni *dollar* za Kimarekani 500.

Mheshimiwa Spika ada iliotajwa hupaswa kulipwa pamoja na ada ya *dollar* za kimarekani 500 za kibali cha kumuezesha Mfuasi huyo, kuweza kuingia na kutoka Nchini yani *re-entry pass*, kulingana na kibali cha mwenyeji wake. Ada hii hutozwa kwa mujibu wa kanuni ya kumi na nne ya kanuni za uhamiaji ya mwaka 1997. Utaratibu huu pia upo katika Nchi zote Wanachama wa jumuiya ya Afrika Mashariki. Vile vile utaratibu unatambua na itifaki ya soko la pamoja la Jumuiya hiyo.

SPIKA: Mheshimiwa Mzee, maswali ya nyongeza.

MHE. HUSSEIN M. MZEE: nimeelezwa kwamba tuzo hii hutozwa kwa Nchi zote za Afrika Mashariki.

(i) Je, kima chetu cha dola mia tano na hamsini kinaungana vipi na Nchi nyingine?

(ii) Ni muda gani Mfuasi anaeweza kuishi Nchini kwa *visa* ya kawaida?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ndani wa Mambo ya Nchi, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mzee kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ada ya dola mia tano tunayotoza Sisi inachukua miaka miwili mpaka mitatu, kulingana na kibali cha mwenyeji wa Mfuasi. Ada hii kwa wenzetu kama Kenya, wanatoza dola mia sita na tisini. Uganda wanatoza dola mia mbili. Rwanda wako chini kidogo hata hivyo hawa Kenya na Uganda wanatoza kwa kila mwaka. Sisi tunatoza kwa miaka miwili ambapo kile kibali kitakuwa kimemalizika.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI]

Mheshimiwa Spika, kuhusu visa ya kawaida, visa ya mtembezi ya Afrika Mashariki inatakiwa iwe miezi sita na baada ya hapo analazimika au aondoke au abadilishe *status* yake kulingana na mipango aliyo nayo.

SPIKA: Mheshimiwa Yusuph Hussein swali la nyongeza.

MHE. YUSSUF HUSSEIN: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Naomba nimwulize Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba baada ya *independent pass* kupewa, ama mwanamke, ama mwanaume kumfuata huyo mwenza wake na kuwepo hapa ndani ya Nchi kwa miaka miwili kwa kumfuata mwenza wake.

Je, visa hiyo inamruhusu mwenza huyo kuwa nayo ni hati ya kufanya kazi katika Nchi yetu? *Au work permit?*

SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Waziri majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ndani wa Mambo ya Nchi, napenda kujibu swali moja la Mheshimiwa Yussuf kama ifuatavyo.

Dependent pass, au hati ya Mfuasi wanapewa wale ambaa ni Wafuasi wa mtu mwingine pengine anaefanya kazi. Kisheria hawatakiwi wafanye kazi na ndio maana wakawa Wafuasi siku watakayoamua kufanya kazi watalazimika *kubadilisha* na wapate kibali kingine cha ukazi.

SPIKA: Naomba tuendelee na swali linalofuata la Mheshimiwa Asha Omari kwa niaba yake Mheshimiwa Mtutura uliza swali. Basi uliza mwenyewe tafadhali. Mheshimiwa Malocha hebu kaa kwanza. (*Makofii/Kicheko*)

Mheshimiwa naomba kwanza ukae. Swali hili la Mheshimiwa Asha Mohammed Omari kwa niaba yake nilishamwita Mheshimiwa Mtutura, naomba aulize.

MHE. MTUTURA A. MTUTURA: Mheshimiwa Spika, niwie radhi nilisimama kwa ajili ya swali la Mheshimiwa Mchungaji Getrude Rwakatare.

SPIKA: Basi Mheshimiwa Malocha uliza swali hilo.
(Makofi)

Na. 28

Mpango wa Maboresho wa Jeshi la Polisi

MHE. IGNAS A. MALOCHA (K.n.y. ASHA M. OMARI
aliuliza:-

Mpango wa Maboresho wa Jeshi la Polisi nchini
ulizinduliwa mwaka 2010/2011:-

- (a) Je, ni nini mafanikio ya utekelezaji wa mpango
huu?
- (b) Je, ni zipi changamoto zake?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Spika kwa niaba ya Waziri wa mambo
ya Ndani ya Nchi napenda kujibu swali la Mheshimiwa Asha
Mohamed Omari, Viti Maalum lenye sehemu A na B kwa
pamoja kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, Sera ya Maboresho katika Jeshi la
Polisi inatokana na Uongozi wa Jeshi la Polisi, Serikali na
Wananchi kwa jumla kutambua ulazima wa kuwepo
mabadiliko ya mifumo ya utendaji ndani ya Jeshi hilo. Lengo
kuu la maboresho ni kuongeza kasi na uwezo wa Jeshi hili
kukabiliana na changamoto za usalama wa raia na mali
zao hususan uhalifu. Mihimili Mikuu ya Programu ya Maboresho
ya Jeshi la Polisi ni Usasa, Weledi na Polisi Jamii.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI]

Mheshimiwa Spika, mafanikio yaliyopatikana tangu kurasimishwa kwa programu hii ni ya kuridhisha. Mafanikio hayo ni pamoja na kuongezeka kwa ushirikiano kati ya Jeshi la Polisi na Wananchi katika kupambana na Wahalifu nchini na kuimarika kwa mifumo ya kubaini kuzuia na kutanzua matukio ya Uhalifu.

Mafanikio mengine ni kurekebishiwa kwa Sheria, kanuni na taratibu za kazi, kuongezeka kwa matumizi ya TEHAMA, kuimarika kwa mifumo ya usimamizi wa rasilimali, kuboreshwa kwa maslahi na ustawi wa Serikali na kuongezeka kwa idadi ya Serikali nyumba na vituo vyta polisi nchini.

Mheshimiwa Spika, changamoto ziliopo katika utekelezaji wa programu ya Maboresho ya Jeshi la Polisi, ni pamoja na upungufu wa rasilimali fedha, rasilimali watu na vitendea kazi kwa ajili ya kutekeleza Mpango Kazi wa Maboresho, katika kufikia shabaha na malengo yaliyowekwa ifikapo Mwaka 2015.

SPIKA: Mheshimiwa Malocha, maswali ya nyongeza.

MHE. IGNAS A. MALOCHA: Mheshimiwa Spika, Nashukuru. Pamoja na maboresho ambayo Mheshimiwa Waziri amekiri kwamba yameanza kufanyika na yanaendelea kuboreshwa, lakini bado lipo tatizo kubwa la askari waliopo ndani ya Makao Makuu ya Wilaya kukosa vyombo vyta usafiri na hatimaye kushindwa kufika kwenye tukio mara wanapopewa Taarifa.

Je, Serikali imejipangaje kutoa vyombo vyta usafiri katika maeneo hayo hasa ya Vijijini?

Huko Zanzibar, matukio yamekuwa yakijitokeza kwa watu kumwagiwa tindikali. Je, Serikali inaweza kutuambia kwamba ni hatua gani zimechukuliwa na imejipangaji kupambana na tatizo hilo?

SPIKA: Ahsante, Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa mambo ya Ndani ya Nchi napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Malocha, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu vyombo vya usafiri nakiri kwamba tuna tatizo kubwa na kila mtu anajua hilo. Hata hivyo Serikali ipo mbioni kutaka kuhakikisha kwamba vyombo vya usafiri vinapatikana hasa kwa askari walio vijijini.

Mpango huu wa Maboresho lengo lake kubwa, ambalo halijatimia kama nilivyosema ni kuhakikisha kwamba vitendea kazi vinaongezeka. Maboresho ni kwa maana ya Ubunifu juu ya Bajeti. Kwa hiyo, tunajitahidi kuhakikisha kwamba lengo hili linatimia na vyombo vya usafiri miongoni mwa vifaa ambavyo vinahitajika vipatikane. Juzi tu kumezinduliwa Mfuko kwa ajili ya Wananchi pamoja na Wafanyabiashara na watu wengine wadau kuchangia.

Kwa hiyo, tunatakiwa nah ii ndio maana ya Maboresho tuchangie pale ambapo Serikali hajafikia tuweze kukamilisha kinachoitajika.

Kuhusu tindikali Zanzibar, ni kweli kumetokea matukio mengi ya tindikali Zanzibar na katika ya matukio haya upelelezi unaendelea. Kuna baadhi ya matukio wahusika wameshakamatwa na wamekabidhiwa kwa Mwanasheria Mkuu kwa ajili ya kuwapeleka Mahakamani. Kuna wengine walishafika Mahakamani, wengine upelelezi bado uko unaendelea.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mpango wakulitatua tatizo hili, tatizo la tindikali hasa linatokana na urahisi wa kuipti tindikali, kuichukua na kuitumia utakavyo. Sheria zilipo za usambazaji, uingizaji nchini bado kuna walakini. Huko ndiko ambapo pamoja na Elimu ya watu kwamba usalama ni muhimu tunaendelea ku-zero / in kwenye hilo hasa kwa kupitia wakemia wakuu wa Bara na visiwani ili kuweka *guideline* ambazo tutajua nani anahusika ku-handle hizi tindikali, ili zisitumike vibaya.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

SPIKA: Ahsante, Mheshimiwa Kombo.

MHE. KOMBO H. KOMBO: Mheshimiwa Spika, nashukuru. Hasa kwanza kwa kutizama wenzangu na ndio kunipa Mimi nafasi. Mheshimiwa Spika, Mimi namwomba Mheshimiwa Naibu Waziri atusaidie, ni sababu gani Wizara yake ikawa haina imani na kodi za Wananchi wetu, ambazo zinatoa kwa nchi, mpaka leo wakaweka magari yao pale Mkoa Kusini Pemba, yanaharibika, hayauzwi, hayafanyi chochote ili Wananchi hawa ile kodi yao wakapata angalau kidogo ikasaidia maendeleo.

SPIKA: Umelielewa hilo swali, haya naomba ujibu.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa mambo ya Ndani ya Nchi napenda kujibu swali la nyongeza ya Mheshimiwa Kombo, kama ifuatavyo:-

Kwanza nimwambie kwamba Wizara ya Mambo ya Ndani ni moja katika Taasisi za Serikali inayothamini sana kodi za Serikali. Shida tulizozisema hizi na nikasema sana kwamba hatuzitimizi, hatuwezi tukazitimiza kama kodi hii tutaidharau.

Kwa hiyo, narudia kwamba tunathamini sana kodi za wananchi, na tunawaomba kwa dhati kabisa waendelee kutimiza wajibu wao. (*Makofii*)

Kuhusu magari ambayo amesema Mheshimiwa kwamba yamekaa pale na hayauzwi, kwanza Polisi ina magari mengi sana ambayo ni mabovu au makuukuu. Lakini ni magari haya haya wakati mwengine tunayafanya Sabaganga yaweze kutumika kwenye matukio mbalimbali. Kwa hiyo, kuna magari ambayo tunajaribu kuyatafutia fedha kuyafufua na yale ambayo hayawezekani kuititia taratibu za kawaida za *disposal/ya property* za Serikali tutachukua hatua haraka iwezekanavyo.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

SPIKA: Sabaganga ndio nini? Naheshimu muda angalieni, twende Wizara ya Nishati na Madini, Mheshimiwa Mchungaji Getrude Rwakatare kwa niaba yake Mheshimiwa Mtutura.

Na. 29

Gawio Litokanalo na Vyanzo vyat Umeme Kihansi na Kidatu.

MHE. MTUTURA A. MTUTURA (K.n.y. MHE. DKT. GETRUDE RWAKATARE) aliuliza:-

Tanzania inafidiwa madeni yake na nchi za nje. Migodi ya Kihansi na Kidatu inayozalisha umeme wa maji ipo katika Wilaya ya Kilombero.

Je, Serikali ina mpango gani wa kutoa gawio litokanalo na vyanzo hivyo katika Wilaya hiyo?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mchungaji Dkt. Getrude Lwakatare, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kutoa gawio kwa migodi ya uzalishaji wa umeme haupo kwa sasa. Kama ilivyo katika Migodi ya Madini ambapo hutolewa kwa kuzingatia kuwa Madini yanaukomu yaani *non renewable*. Migodi ya kuzalisha umeme wa Maji ni rasilimali endelevu yaani renewable ambayo inamilikiwa na Serikali kwa asilimia mia moja. Hivyo ni mali ya Watanzania wote kwa ujumla bila kujali eneo wanilotoka.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI]
Mheshimiwa Spika kwakuwa sio Sera ya Serikali na sio busara kutoa gawio kwa Wananchi wa maeneo jirani pekee, Serikali haina Mpango la kutoa gawio kwa Wananchi wanaoishi karibu na Migodi ambayo inazalisha umeme.

SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Mtutura, swali la nyongeza.

MHE. MTUTURA A. MTUTURA: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Kwa kuwa kwenye jibu la msingi Serikali imesema kwamba gawio ni Sera ya Serikali, na kwa kuwa kumekuwa na Sera ya Serikali ya kutoa gawio kwenye Migodi ambayo ni *non renewable*.

Je, Serikali ipo tayari kuleta Sera hiyo hapa Bungeni ili tuifanyie mabadiliko, ili na wale ambao wanaishi katika Migodi ambayo ni *renewable* waweze kupata gawio hilo?

Swali la pili, wakati tunasubiri Sera hiyo ibadilishwe. Je, Serikali haioni busara kuishauri *TANESCO* watenge kiasi cha fedha na kuwapa Halmashauri zinazozungukwa na Migodi hiyo, ili kuleta mawasiliano mazuri kati ya wananchi hao ambao ni walinzi wa kwanza wa rasilimali hizi za Taifa?

SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE) : Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mtutura, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, zipo *concept* mbili hapa, ipo *concept* ya gawio kwa maana ya kodi. Lakini ipo *concept*

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI]
ya *corporate social responsibility* kwa maana ya mchango wa makumpuni kwa jamii zinazozunguka.

Kwa hiyo, tukijua tofauti hizi unaweza ukaona ile ya kwanza niliyojibu kwenye jibu langu la msingi, ambayo ndio inajibu swali la kwanza la Mheshimiwa Mtutura, ni ile ya gawio ambayo tunasema kwa sasa hatuna Sera hapo itakapobidi basi tutaleta hiyo Sera, hapo itakapobidi.

Mheshimiwa Spika, lakini hii ya *corporate social responsibility* hii ipo, hii ipo na wamekuwa *TANESCO* wakifanya na tukumbuke tu *TANESCO* Kwa muda sasa wanapata hasara kubwa katika kuzalisha umeme. Kwa hivyo, *corporate social responsibility spirit* yake ni pale wanapokuwa hiyo kampuni hiyo iwe ya umma au binafsi inapata faida.

Sasa katika mazingira haya ni vigumu sana kwa *TANESCO* kuweza kufanya hivyo ingawa utaratibu na Sera hii ipo na inaruhusiwa kabisa pale inapowezekana na kwa mujibu wa *corporate social responsibility policy* wakaweza Halmashauri hizi kupata gawio. Ni suala la mahusiano tu lakini hii inaruhusiwa. (*Makofii*).

SPIKA: Mheshimiwa Christina Lissu.

MHE. CHRISTINA L. MUGHWAI: Mheshimiwa Spika, Ahsante sana. Katika jitihada za kutatua tatizo la umeme nchini, Serikali kwa kushirikiana na *NBC* na *TANESCO*, walianzisha mradi wa umeme wa upepo katika Mkoa wa Singida.

Je, hatua za utekelezaji wa Mradi huo wa umeme katika Mkoa wa Singida zipo katika hatua ipi?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE): Mheshimiwa Spika kwa niaba ya Waziri

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI]
wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Christina Lissu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, umeme wa Singida mradi ule unaendelea zipo kampuni mbili, ambazo zote zinakusudia kuzalisha umeme wa upepo. Michakato inaendelea na tumesaidia sana Sisi Wizara kuhakikisha kwamba wanaingia katika Mikataba kwa raha kati ya makampuni haya na TANESCO na hatua hiyo naamini itakuwa imefikia hatua nzuri. Nimwombe tu Mheshimiwa Mbunge avute subira ili tuweze kufanya mawasiliano na Makampuni haya, tujue wamefikia *so far wapi* kwa sababu ile biashara ni ya *private sector* na Sisi tunapopata Taarifa basi tutaweza kuzitoa kwamba tumefikia wapi wakati wowote.

Nichukue nafasi hii, nilikuwa nimewaagiza kwamba tarehe 9 waje hapa Dodoma, Makampuni pamoja na TANESCO, tuone wamefikia wapi kwa hivyo, Mheshimiwa Mbunge baada ya tarehe 9 ukiniuliza nitakuwa na jibu zuri zaidi.

SPIKA: Mheshimiwa Mbunge, muda umekwisha bahati nzuri maswali pia yameisha. Niwatambue wageni tulionao, tunao wageni 34 kutoka Mkoa wa Tabora ambao ni viongozi wa vikundi mbalimbali vya wafugaji nyuki kutoka Mkoa wa Tabora. Wapo katika ziara ya mafunzo hapa Bungeni, mafunzo ya ufugaji nyuki kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba wageni wetu wasimiamme walipo tuweze kuwatambua. Ahsanteni sana karibu. Nadhani mnawungu Mheshimiwa Waziri Mkuu katika ufugaji nyuki na asali hutakiwa duniani kote. Ahsanteni sana.

Matangazo mengine, kuna Mheshimiwa Rajabu Mohammed, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya hesabu za Serikali za Mitaa, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba, leo tarehe nne saa tano asubuhi, baada ya kipindi cha maswali na majibu kutakuwa na kikao cha kujadili Taarifa, kikao hicho kitafanyika katika ukumbi wa Msekwa B, watu wanaokutana saa tano lazima waombe

Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)

[SPIKA]

ruhusa kwa spika lakini nakuruhusu. Kwa hiyo, Kamati hiyo ikutane saa tano asubuhi katika Ukumbi wa Msekwa B.

Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, Mheshimiwa Saidi Mkumba, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati.

Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji Mheshimiwa Said Nkumba, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba leo saa 7.00 mchana kutakuwa na kikao, kikao cha Kamati hiyo ambayo kitafanyika katika Ukumbi Na. 227.

Ninalo tangazo la Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala. Mwenyekiti yeye anaomba leo saa 7.00 mchana Mheshimiwa Pindi Chana, katika Ukumbi Na. 231 ghorofa ya pili. Wabunge wote wanaokusudia kuwasilisha majedwali ya marekebisho kwenye Muswada wa Sheria ya Kura za Maoni wanaombwa kufika na kuyawasilisha mbele ya Kamati. Sasa hili tangazo naomba nieleze kwa mujibu wa Kanuni zetu huwezi kama una marekebisho yako ukaenda moja kwa moja kwenye Kamati. Unatakiwa kwanza kuyawakilisha kwa Katibu wa Bunge.

Sasa baada ya kuwasilisha kwa Katibu wa Bunge mimi ndiye nitakayeweza kusema kwamba kwa sababu haya marekebisho ni mengi na tusianze kulumbana hapa na hasa Muswada wenye ni muhimu sana. Ni vizuri ukapata nafasi ya kutafakariwa katika kiwango cha Kamati. Sasa kama kuna watu wenye marekebisho haya, naomba sana wawe wamepeleka kwa Katibu wa Bunge. Tuweze kufahamu kabisa ni marekebisho mangapi yako wapi. Sababu yenye ni kwamba huwezi kuzuka tu na marekebisho mahali popote. Ni lazima na upande wa pili wa Serikali wawe nayo na Wabunge wengine waweze kushiriki kwamba ni kitu gani na umuhimu wa Muswada huu ni vizuri tukawa makini sana katika kuleta marekebisho.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[SPIKA] Ndiyo maana Mwenyekiti wa Kamati hii angependa na sisi wote tungependa hivyo marekebisho yakajadiliwa kwa uwazi kwenye Kamati na ikishirikisha watalaan mnawenza mkabishana mkaona umuhimu wake. Kwa sababu tukifika hapa mabishano huwa hayawi mazuri kwa sababu tuna kanuni za kuzungumza. Unazungumza mara moja halafu ukae basi. Sasa na wengine nao bahati mbaya tena marekebisho mengine yanazukia humu humu ndani. Sasa wewe huungi mkono watu wanaanza kuunga vyama vyao na watu waliosema. Tunaunga mkono kama hoja ni ya msingi.

Kwa hiyo, ni kweli kwamba kama yapo ama kama kuna watu wanakusudia kufanya hivyo, basi waende wakasikilize kwenye Kamati halafu walete kwa utaratibu unaostahili iweze kupata kibali.

Kwa hiyo, Mwenyekiti wa Kamati hii anasema kama kuna watu wanaokusudia kufanya marekebisho wangependa kuwasikiliza. Jambo ambalo ninafikiri ni jema. Kwa hiyo, wao watakutana saa 7.00 mchana katika Ukumbi Na. 231. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge baada ya kusema hili tunaendelea na hoja nyingine. Katibu tuendelee.

MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

Muswada wa Sheria ya Kura ya

Maoni wa mwaka 2013 (*The Referendum Bill, 2013*)

(Kusomwa Mara ya Pili)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, mbona mmechelewa kusimama? Haya mimi sikubali mmechelewa. Haya mmoja akae. Mheshimiwa Mkosamali.

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. FELIX F. MKOSAMALI: Nakushukuru Mheshimiwa Spika, nimesimama hapa kuomba mwongozo kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7) kuhusu majibu ambayo nimejibiwa kwenye swali langu leo. Haya majibu Mheshimiwa Spika haya, siyo majibu ya kuleta Bungeni hapa na imekuwa ni mara nydingi tunasimama kuomba maswali ambayo yanajibiwa hovyo hovyo yaletwe tena.

Lakini sijawahi kuona swali ambalo linaletwa hapa. Kwanza swali langu la nyongeza la pili waziri hakulijibu kabisa. Sasa mimi nimesimama kuomba mwongozo. Kwa sababu hili ni Bunge ni Bunge Tukufu siyo la kuleta majibu rahisi rahisi na mwepesi mwepesi.

Kwanza nimemwomba Waziri aje atatue huu mgogoro ulioko Kibondo. Hajajibu kama atatatua au hatatatua. Lakini niombe aje ajibu tena, maana hakuna kitu hapa. Hii ni blaa blaa tu. Naomba mwongozo wako kuhusu jambo hili.

MHE. DAVID Z. KAFULILA: Mheshimiwa Spika, mimi nimesimama kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7) kwa ajili ya kuomba mwongozo wako kwa kuzingatia kwamba Mheshimiwa Spika hili ni Bunge ambalo linafanya kazi lenye mamlaka ya kuisimamia Serikali kwa mujibu wa Katiba.

Lakini Mheshimiwa Spika, wewe utakuwa shahidi kwamba tumekuwa tukishuhudia majibu ya chini ya viwango kwa muda mrefu. Leo ikiwa ni moja ya siku ambapo Mawaziri kadhaa wametoa majibu ya chini ya viwango kabisa na wewe unaona. Sasa tatizo hili katika namna nyginginwe

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. FELIX F. MKOSAMALI]

tunaye Waziri Mkuu ambaye katika namna nyingine angeweza kuwa ana-enter vine kusaidia Bunge kupata usahihi wa majibu ya kutosha. (*Makof!*)

Lakini upande mwingine tumekuwa na Mawaziri hapa, Naibu Waziri siku swali lake linaulizwa Waziri hayupo, Naibu hayupo, anapewa Waziri mwingine ambaye anakuja kujibu majibu ambayo yeye mwenyewe hayupo *well informed*. Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako. Unalisa diaje Bunge hili Tukufu kwa niaba ya wananchi lipate majibu yenye viwango siku zote? (*Makof!*)

SPIKA: Ni vizuri kila tunachozungumza hapa kiko kwenye *Hansard*. Juzi Mheshimiwa Kombo aliuliza hivyo hivyo kutokuridhika na majibu yaliyotolewa. Nikamwambia tunao utaratibu. Utaratibu ule kama nyinyi mngeandika ingekuwa ni rahisi kwetu sisi kusema una-quote na jibu lake lile na unachukua na *Hansard*yako unatuletea hapa kweli kwamba mimi sikuridhika kwa sababu hivi na hivi.

Mimi Spika ningechukua hatua. Kwa sababu kusema majibu hayaridhishi ama hayajaridhisha ni *relative*, *ni relative*. Kwa hiyo, ndiyo maana tukasema utaratibu wake wewe unaandika malalamiko yako kuhusu lile jibu halafu sisi tutaliweka kadiri inavyostahili. Lakini kwa kusema hivi mwongozo wangu ni kwamba nendeni mkaniandikie malalamiko yenu kuhusu majibu hayo. (*Makof!*)

Tunaendelea, halafu ya pili, ingawa Lusinde umekaa hapa. Kwa kweli Waheshimiwa Wabunge bado mnavuruga. Mheshimiwa Waziri Mkuu yuko hapa kwa ajili ya kazi. Ndiyo hicho anacho sema watu. Waziri Mkuu hasikilizi mambo akasikiliza mmoja mmoja akikaa hapo wengine wanakaa wanahamia kabisa. Jamani nawaombeni Waziri Mkuu kama yupo basi akakae Ofisini aweze kuwasikiliza vizuri. Akakae Ofisini halafu muende huko kwa *appointment*.

Lakini akiwa hapa inatutia kidogo, maana unawakuta kabisa Waziri anajibu huku kuna neno lakini Waziri Mkuu yuko na watu wanazungumza hapa. Tunaomba kama ikibidi Waziri Mkuu ukae Ofisini waende wanaotaka kwenda. (*Makof!*)

Kwa hiyo, tunaendelea⁵⁶ Mtoha hoja, Mheshimiwa mtoha hoja. (*Makof!*)

SPECIAL BILL SUPPLEMENT

No. 1

5th November, 2013

*to the Gazette of the United Republic of Tanzania No. 1
Vol. 94 dated 5th November, 2013*

Printed by the Government Printer, Dodoma by Order of
the Government

THE REFERENDUM ACT, 2013

ARRANGEMENT OF SECTIONS

Sections

Title

PART I

PRELIMINARY PROVISIONS

1. Short title and commencement.
2. Application.
3. Interpretation.

PART II

CONDUCT OF REFERENDUM

4. Power to initiate a referendum.
5. Notice of holding referendum.
6. Responsibilities of the Commission.
7. Returning officers.
8. Appointment of other officers.
9. Right to vote at referendum.
10. Polling areas and polling stations.
11. Use of public facilities.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

PART III REFERENDUM COMMITTEES

12. Establishment of referendum committees.
13. Registration of referendum committees.
14. Register of agents.
15. Appointment of agents at a polling area.
16. Referendum question campaign.
17. Referendum campaign expenses.

PART IV VOTING IN A REFERENDUM

18. Voting procedure.
19. Equipment of polling stations.
20. Admission to polling stations.
21. Keeping order at the polling station.
22. Postponement and extention of polling.
23. Communication with voters at polling station.
24. Sealing of ballot boxes.
25. Ballot papers.
26. General voting procedures.
27. Assisted voters.
28. Procedure on close of polling station.
29. Voters to be counted at the polling station.
30. Recount.
31. Rejected ballot papers.
32. Sealing of ballot papers.
33. Constituency results.
34. Announcement and publication of referendum results.
35. Referendum results.

PART V GENERAL PROVISIONS

36. Procedure for conduct of referendum.
37. Voting under High circumstances.
38. Accreditation of observers.
39. Attendance of agents.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

40. General Powers of the Commission.
41. Cost of referendum.
42. Person not required to state how he voted.
43. Challenging referendum results.
44. Deposit of Security for costs.
45. Determination of petition by the court.
46. Appeal.
47. Prohibition of incitement of public disorder at a referendum .
48. Offences and penalties.
49. Regulations.
50. Power to amend or replace Schedules.
51. Application of other laws.
52. Promulgation of the Constitution.

SCHEDULES

NOTICE

This Bill to be submitted to the National Assembly was published as Bill Supplement No 4 of 7th June, 2013 and was First Read in the National Assembly on the 28th day of June, 2013. This Bill is now re-published for purposes of Second Reading and Third Reading.

Dar es Salaam,
3rd November, 2013

OMBENI Y. SEFUE
Secretary to the Cabinet

A BILL

for

An Act to provide for legal and institutional framework for the conduct of referendum with a view of making decision by the people on the proposed Constitution, and for other related matters.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

PART I PRELIMINARY PROVISIONS

Short title
and commen-
cement

1.- This Act may be cited as the Referendum Act, 2013 and shall come into operation on the date to be appointed by the Minister by order published in the *Gazette*.

Application

2. This Act shall apply to Mainland Tanzania and Tanzania Zanzibar in relation to a referendum for approval of the proposed Constitution.

Inter-
pretation

3. In this Act, unless the context requires otherwise-

"agent" means a person duly appointed by a referendum committee and registered by the Commission to act both as a counting agent and a polling agent for the purposes of this Act;

"Attorney General" means the Attorney General of the United Republic or as the case may be the Attorney General of Zanzibar;

"Commission" means the National Electoral Commission and the Zanzibar Electoral Commission;

"Constitution" means the Constitution of the United Republic of Tanzania 1977;

"constituency" means a constituency for the purposes of elections of the member of the National Assembly or the House of Representative;

"deputy referendum officer" means the person appointed under section 7(2);

"deputy referendum returning officer" means the person appointed under sections 7(1);

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

"Director" has a meaning ascribed to it under the National Elections Act and the Zanzibar Elections Acts;

"High Court" means the High Court of Tanzania and the High Court of Zanzibar and their respective registries shall be construed accordingly;

"Minister" means the Minister responsible for electoral affairs;

"polling station" means any room, place, vehicle or vessel set apart and equipped for the casting of votes by a voter at a referendum;

"President" means the President of the United Republic;

"proposed Constitution" means the constitution passed by the Constituent Assembly which is the subject of the referendum;

"referendum" means a public vote or a poll cast in accordance with the provisions of this Act for the purpose of attaining people's decision on the proposed constitution;

"referendum committee" means the committee established under section 12;

"referendum officer" means a person appointed under section 7(2) for the purpose of conducting the referendum at a polling station;

"referendum returning officer" means a person appointed under section 7(1);

"referendum campaign period" means the period specified as such by the Commission;"referendum coordinator" mean a person appointed under section 8(1);

"voter's card" means a card issued to a voter by the Commission as an evidence of the person's registration in the register of voters;

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

"voter" means a person qualified to vote at an election in accordance with the law governing election for Presidential or a Member of the Parliament or House of Representatives.

PART II CONDUCT OF REFERENDUM

Power to initiate a referendum

- 4.-**(1) The President in Consultation with the President of Zanzibar shall, within fourteen days from the date of receiving the proposed Constitution, by Order published in the *Gazette*, direct the Commission to conduct a referendum on the proposed Constitution.
- (2) An Order for a referendum shall be in the format set out in Form No. 1 of the Schedule to this Act, and shall-
- (a) specify the proposed Constitution to be determined;
 - (b) specify the period within which the referendum campaign shall be conducted; and
 - (c) specify the period within which a referendum shall be held.
- (3) For the purpose of subsection (2), the Commission shall, within seven days after the publication of the proposed Constitution, frame and publish in the *Gazette* the question to be determined by the referendum.
- (4) The question to be asked to the referendum shall require the voter to indicate whether the voter approves or does not approve the proposed Constitution and shall be so framed in the manner which requires the voter to answer "YES" or "NO".

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Notice of holding referendum

5.-(1) The Commission shall, within fourteen days after publication of the referendum question in the *Gazette*, specify-

- (a) the day on which the referendum is to be held;
- (b) the polling time of the referendum; and
- (c) the period for sensitization and public awareness on the referendum on the proposed Constitution.

(2) Every referendum returning officer shall, within twenty one days from publication of the notice by the Commission, notify the public in his respective constituency about the procedure for the conduct of the referendum.

(3) For the purposes of sensitization and public awareness on the referendum for the proposed Constitution, the Commission shall provide civic education on the proposed Constitution for the period of sixty days from the date of publication of the proposed Constitution in the *Gazette*.

(4) Without prejudice the provision subsection (3) the commission may allow civil societies and non-governmental organizations which are interested in disseminating civic education or carrying awareness campaign on the proposed constitution to disseminate the education and carry on the campaign for a period of not more than thirty days prior to the voting date.

6.-(1) The Commission shall be responsible for-

- (a) supervision of the general conduct of a referendum; and

- (b) promotion and regulation of voters' education for the referendum.
- (2) During the conduct of a referendum, the Commission shall not be subject to the direction or control of any person or authority.
- (3) The Commission shall organize, conduct and supervise the conduct of poll during the referendum.
- Referendum Returning officer
- 7.**-(1) The Commission shall appoint a referendum returning officer for each constituency and may appoint such deputy referendum returning officers for the constituency as it may consider necessary.
- (2) The referendum returning officer shall appoint referendum officers and deputy referendum officers to preside at a polling station.
- (3) A deputy referendum returning officer shall, subject to the general direction and control of the referendum returning officer, have all the powers and may perform all the duties of the referendum returning officer under this Act.
- (4) A deputy referendum officer may, upon the direction and control of the referendum officer, perform any act which the referendum officer is required or authorized to perform under this Act; except that such officer shall not have power to order the arrest of any person or the exclusion or removal of any person from a polling station.
- (5) Every appointment of a referendum returning officer and a referendum deputy returning officer under this section shall be published in such manner as the Commission may deem necessary.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Appoint-
ment of
other officers

- 8.-**(1) The Commission may, during a referendum, appoint by office or by name in respect of every region, a regional referendum coordinator to coordinate information, the availability of material resources and other matters necessary for the efficient conduct of referendum in constituencies within the Region.
- (2) The Commission may appoint such other staff as it deems necessary to assist in the conduct of the referendum and such staff may, subject to the general or specific directions of the Commission, exercise any or all of the duties and powers conferred or imposed upon the Commission under this Act or any other written law.
- (3) The officers appointed under section 7 and this section shall take such oath or affirmation of office.
- (4) The referendum officers shall be impartial in performing their duties.

Right to
vote at
referendum
Cap.343
Act No.11
of 1984

(3) Kwa madhumuni ya kuelimisha na kuhamasisha wananchi kuhusu kura ya maoni Tume, itatoa elimu ya uraia juu ya Katiba inayopendekezwa kwa kipindi cha siku sitini kuanzia tarehe ya kuchapishwa katika *Gazeti* la serikali kwa Katiba inayopendekezwa.

(4) Bila ya kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (3), Tume inaweza kutoa ruhusa kwa asasi za kiraia na asasi zisizo za kiserikali zinazopendelea kutoa elimu ya uraia na kuendesha uhamasishaji juu ya katiba inayopendekezwa kutoa elimu na kuhamasisha juu ya katiba hiyo kwa kipindi kisichozidi siku thelathini kabla ya upigaji kura.

Wajibu
wa Tume

6.-(1) Tume itakuwa na wajibu wa-

(a) kusimamia kwa ujumla uendeshaji wa kura ya maoni; na

(b) kuhamasisha na kusimamia elimu ya mpiga kura kwa ajili ya kura ya maoni.

(2) Wakati wa kuendesha kura ya maoni, Tume haitapokea maelekezo au kuwa chini ya udhibiti wa mtu au mamlaka yoyote.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Msimamizi
wa Kura
ya Maoni

(3) Tume itaandaa, kuendesha na kusimamia upigaji wa kura wakati wa kura ya maoni.

7.-(1) Tume itateua msimamizi wa kura ya maoni wa kila jimbo na inaweza kuteua naibu wasimamizi wa kura ya maoni kwa majimbo kama itaonekana ni lazima.

(2) Msimamizi wa kura ya maoni, atateua maafisa wa kura ya maoni na naibu maafisa wa kura ya maoni kusimamia upigaji kura katika kituo cha kupigia kura.

(3) Naibu msimamizi wa kura maoni, kwa kuzingatia maelekezo ya jumla na udhibiti wa Msimamizi wa kura ya maoni ana mamlaka yote na anaweza kufanya kazi zote za msimamizi wa kura ya maoni zilizoainishwa chini ya sheria hii.

(4) Naibu Afisa wa Kura ya maoni anaweza, kwa maelekezo na udhibiti wa afisa wa kura ya maoni kufanya kitu chochote ambacho Afisa wa Kura ya Maoni anatakiwa au ameidhinishwa kufanya chini ya sheria hii, isipokuwa kwamba afisa huyo hatakuwa na mamlaka ya kuamrisha kukamatwa kwa mtu ye yeyote au kuondoshwa kwa mtu ye yeyote kutoka kituo cha kupigia kura.

(5) Kila uteuzi wa msimamizi wa kura ya maoni na naibu msimamizi wa kura ya maoni chini ya kifungu hiki, utatangazwa katika namna ambayo Tume itaona ni lazima.

Uteuzi
wa
Maafisa
wengine

8.-(1) Tume wakati wa kura ya maoni kwa kuzingatia kila mkoa inaweza kumteua kwa ofisi au kwa jina, mratibu wa kura ya maoni wa mkoa kuratibu taarifa, upatikanaji wa vifaa na masuala mengine ya lazima kwa ajili

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

ya kufanikisha uendeshaji wa kura ya maoni katika majimbo ndani ya mkoa.

(2) Tume inaweza kumteua mtumishi yejote mwingine kama itaona ni lazima kwa ajili ya kusaidia katika uendeshaji wa kura ya maoni na mtumishi huyo anaweza, kwa kuzingatia maelekezo ya jumla au mahususi ya Tume, kutekeleza jukumu lolote au majukumu yote na kutumia mamlaka ya Tume yaliliyotolewa na Sheria hii au Sheria nyingine yoyote.

(3) Maafisa walioteuliwa chini ya kifungu cha 7 na kifungu hiki wataapa au kuthibitisha kiapo cha Ofisi.

(4) Maafisa wa kura ya maoni watatenda kazi zao bila upendeleo.

Haki ya
kupiga
kura
katika
kura
ya maoni

9.-(1) Daftari la wapiga kura lilioanzishwa chini ya Sheria ya Taifa ya Uchaguzi na Sheria ya Uchaguzi ya Zanzibar atakuwa ni daftari la wapiga kura kwa madhumuni ya kura ya maoni.

(2) Mtu ambaye jina lake limeingizwa katika Daftari la Wapiga Kura lilioanzishwa chini ya Sheria ya Taifa ya Uchaguzi au Sheria ya Uchaguzi ya Zanzibar atakuwa na haki ya kupiga kura ya maoni, isipokuwa kama mtu huyo amezuiwa kupiga kura na sheria nyingine yoyote.

(3) Afisa wa kura ya maoni atamtaka mtu anayeomba karatasi ya kupigia kura kutoa kadi ya mpiga kura iliyotolewa na Tume kama uthibitisho wa utambulisho wa mtu anayedai kuwa anaruhusiwa kupiga kura.

(4) Pale ambapo mtu yejote aliyesajiliwa kama mpiga kura na taarifa zake zipo

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

kwenye daftari la wapiga kura ila amepoteza kitambulisho cha kupigia kura, Afisa wa kura ya maoni atamtaka mtu huyo kuonyesha kitambulisho kingine chochote kinachomtambulisha na atamruhusu mtu huyo kupiga kura baada ya kujaza fomu maalum ya kiapo.

Maeneo
ya kupigia
kura na
vituo vy
kupigia kura

10.-(1) Tume-

(a) itagawanya kila jimbo ambamo kura ya maoni inafanyika kuwa maeneo ya kupigia kura au kutangaza jimbo lolote husika kuwa eneo pekee la kupigia kura;

(b) itatoa kwa kila eneo la kupigia kura namba ya kipekee au herufi au vyote kwa pamoja namba na herufi;

(c) itateua kituo au vituo vy kupigia kura kwa kila eneo la kupigia kura; na

(d) itatangaza katika *Gazeti* la Serikali taarifa itakayoelezea:

(i) eneo la kupigia kura kwa kila jimbo; na

(ii) namba ya kipekee au herufi, au mchanganyiko wake, zilizotolewa kwa kila eneo la kupigia kura;

(2) Katika kuamua mipaka ya eneo lolote la kupigia kura, Tume itazingatia:

(a) vituo vy kupiga kura viliviyopo katika jimbo la uchaguzi;

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

- (b) mazingira ya kijiografia;
- (c) idadi ya watu; na
- (d) sababu nyingine yoyote inayoathiri mawasiliano katika maeneo mbalimbali ndani ya eneo la kupigia kura.

Matumizi
ya vifaa
vya
umma

11.-(1) Tume inaweza, bila malipo yoyote, kutumia eneo lolote la umma kama kituo cha kupigia kura.

(2) Tume inaweza pale ambapo kutakuwa na haja, kutumia jengo au eneo binafsi baada ya kupata ridhaa ya mmiliki wa eneo au jengo hilo.

SEHEMU YA TATU

KUANZISHWA KWA KAMATI ZA KURA YA MAONI

Uanzishwaji
wa
kamati
za kura
ya maoni

12. (1) Zinaanzishwa kamati mbili za kura ya maoni katika ngazi ya taifa na Kamati mbili za Kura ya maoni katika ngazi ya jimbo.

(2) Kamati zilizoanzishwa chini ya kifungu kidogo cha (1) zitaundwa na makundi ya watu, vyama vya siasa, taasisi za kiraia au asasi zinazokusudia kuunga mkono au kupinga swali la kura ya maoni katika kipindi cha kura ya maoni.

Usajili
wa kamati
za kura
ya maoni

13.-(1) Kamati ya kura ya maoni, ndani ya siku ishirini na moja kabla ya kipindi cha kura ya maoni, itaomba usajili kwa Tume au kwa Msimamizi wa kura ya maoni kwa madhumuni ya kuendesha kampeni za kura ya maoni.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

(2) Kila kamati ya kura ya maoni ambayo inakusudia kuomba usajili kabla ya kuwasilisha maombi yake itateua kiongozi.

(3) Kiongozi aliyeeteuliwa chini ya kifungu kidogo cha (2) atawajibika kwa-

(a) masuala yote ya kamati ya kura ya maoni iliyosajiliwa;

(b) uteuzi wa mawakala wa kamati ya kura ya maoni; na

(c) kutoa sampuli za saini za mawakala kwa Tume.

(4) Maombi chini ya kifungu hiki yataambatana na taarifa na matamko yanayoonesha kwamba muombaji anawakilisha wale wanaopiga kampeni ya kuunga mkono au kupinga swali la kura ya maoni.

(5) Ombi la usajili litasainiwa na kiongozi wa kamati ya kura ya maoni na lita-

(a) onyesha-

(i) jina kamili la kamati;

(ii) jina kamili, anuani na nambari za simu za kiongozi wa kamati ya kura ya maoni;

(iii) jina, anuani na nambari ya simu na cheo cha kila mjumbe wa kamati;

(iv) anuani na nambari ya simu ya ofisi ya kamati

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

ambayo mawasiliano
yanaweza kupelekwa;

(v) jina, anuani na nambari
ya simu ya mawakala;

(b) onesha vyanzo vya mapato;

(c) onyesha maeneo ambayo kamati
inataka kuunga mkono au kupinga
swali la kura ya maoni; na

(d) ambatana na taarifa iliyosainiwa
na kiongozi kwamba wakala
amekubali uteuzi kama wakala.

(6) Baada ya kupokea maombi kwa ajili ya
usajili wa kamati ya kura ya maoni, Tume
itatolea maamuzi maombi na inaweza
kumsajili muombaji au kukataa maombi na
itamtaarifu mwombaji ipasavyo, ikielezea
sababu za kukataa.

(7) Kamati ya kura ya maoni haitasajiliwa
iwapo-

(a) jina la kamati linafanana na jina
la kamati ya kura ya maoni iliyosajiliwa
awali kwamba kamati inaweza
kuchanganywa na kamati iliyosajiliwa
awali; au

(b) Tume haitaridhishwa kuwa
muombaji anawawakilisha vya
kutosha wale wanaofanya kampeni
kwa ajili ya matokeo fulani;

(8) Usajili wa kamati ya kura ya maoni kwa
madhumuni ya kura ya maoni utakuwa ni
halali tu kwa kura ya maoni hayo.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Daftari
la
mawakala

Uteuzi
wa
mawakala
katika
eneo la
kupigia
kura

Kipindi
cha kampeni
za kura
ya maoni

14. Tume itatunza daftari la mawakala wa kamati za kura ya maoni zilizosajiliwa ambamo yataingizwa majina, anuani na nambari za simu za mawakala wa kila kamati.

15.-(1) Viongozi wa kamati zote za kura ya maoni watateua mawakala wasiozidi wawili wa kura ya maoni watakaokuwepo mahali ambapo kura zinapigwa katika kila eneo la kupigia kura.

(2) Kila mtu aliyeuleuliwa kama wakala kwa mujibu wa kifungu hiki atateuliwa kwa maandishi na atapewa kitambulisho kabla ya kujihusisha na shughuli zozote za kura ya maoni na ataapa kama Tume itakavyoolekeza.

16.-(1) Kamati ya kura ya maoni inayounga mkono au inayopinga swali la kura ya maoni inaweza kufanya kampeni za kuunga mkono au kupinga swali la kura ya maoni kwa kipindi cha kisichozidi siku thelathini katika kipindi cha kura ya maoni.

(2) Kamati za kura ya maoni hazitaanza kampeni chini ya kifungu kidogo cha (1) hadi pale Tume itakapotangaza tarehe rasmi ya kuanza kwa kampeni.

(3) Kampeni zote zilizorejewa katika kifungu kidogo cha (1) zitakoma saa ishirini na nne kabla ya kuanza kupiga kura.

(4) Taarifa ya kufanya kampeni katika kura ya maoni itakuwa kama ilivyoweka katika fomu itakayoandalisha na Tume.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Gharama
za
Kampeni
na
kura ya
maoni
kubebwa
na kamati

- 17.-**(1) Kamati ya Kura ya maoni itaendesha na kugharimia kampeni zake za kura ya maoni.
- (2) Kamati ya Kura ya maoni italazimika kutoa taarifa ya vyanzo vyake nya mapato kwa Tume.
- (3) Taarifa ya vyanzo nya mapato itakayotolewa chini ya kifungu hiki itakuwa ya siri na itatolewa pale tu taarifa hiyo inahusika kwenye malalamiko yaliyowasilishwa na mtu yejote, Mkurugenzi au upelelezi ulioanzishwa na Mkurugenzi, au inahusika kwenye kesi yoyote iliyoko mahakamani.
- (4) Kwa ajili ya utekelezaji wa kifungu hiki, Waziri, kwa amri iliyochapishwa kwenye *Gazeti la Serikali*, ataainisha kiwango cha chini cha gharama zitakazotumiwa na Kamati ya kura ya maoni kulingana na ukubwa wa jimbo.
- (5) Tume itaweka utaratibu wa kutoa taarifa ya vyanzo nya mapato ya Kamati za kura ya maoni na ukaguzi wa mahesabu ya gharama ambazo kamati ya kura ya maoni imezitumia kwa ajili ya kuendesha kampeni za kura ya maoni.

SEHEMU YA NNE

UPIGAJI WA KURA KATIKA KURA YA MAONI

Upigaji
kura ya
maoni

- 18.-**(1) Upigaji kura katika kura ya maoni utakuwa kwa kura ya siri na utafanyika kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii.
- (2) Isipokuwa kwa watu waliotajwa katika kifungu cha 36, hakuna mtu atakayepiga

kura katika eneo, tofauti na lile ambalo ameandikishwa kama mpiga kura.

(3) Mtu yejete hatopiga zaidi ya kura moja katika kura ya maoni.

(4) Bila ya kujali masharti mengine yoyote ya Sheria hii, endapo mpiga kura aliyeandikishwa katika eneo la uchaguzi ameajiriwa kama Afisa wa kura ya maoni, msimamizi wa kituo, afisa wa polisi au katika wadhifa wowote rasmi katika kituo cha kupigia kura katika eneo la uchaguzi mbali na kituo cha kupigia kura alichandikishwa, Mkurugenzi au mtu mwingine yejete aliyeidhinishwa na Mkurugenzi anaweza, kwa hati alioisaini, kumuidhinisha mpiga kura huyo kupigia kura katika kituo kingine chochote cha kupigia kura katika eneo hilo la uchaguzi na kituo hicho kwa madhumuni ya Sheria hii kitahesabika kuwa ni kituo cha kupigia kura alichandikishwa mpiga kura huyo.

Vifaa
vya
kituo cha
kupigia
kura

19.-(1) Msimamizi wa kura ya maoni atatoa kwa kila afisa wa kura ya maoni, idadi ya masanduku ya kura na karatasi ya kupigia kura, kulingana na mahitaji ya maeneo, kwa utekelezaji bora wa masharti ya Sheria hii.

(2) Kila sanduku la kura litatengenezwa-

(a) na kiupenyo chenye ukubwa wa kutosha kuitisha karatasi ya kupigia kura lakini ambacho si kikubwa sana;

(b) ili kuweza kufungwa kiasi kwamba karatasi za kura hayataweza

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

kutolewa ndani ya sanduku pale ambapo lakiri haijavunjwa; na

(c) ili liweze kuwekewa namba zinazofuatana za vituo vyta kupigia kura ambazo zitabandikwa katika sehemu ya wazi kwa kila kituo cha kupigia kura.

(3) Msimamizi wa kura ya maoni atatoa kwa kila kituo cha kupigia kura-

(a) vifaa ili kuwawezesha wapiga kura kuweka alama katika karatasi ya kupigia kura pale alama inapohitajika;

(b) vifaa vyta kugongea alama rasmi katika karatasi za kupigia kura;

(c) lakiri ya Tume inayofaa kwa dhumuni hilo;

(d) chupa au chombo kilicho na wino usiyofutika unaofaa kwa madhumuni hayo;

(e) nakala ya daftari la wapiga kura au sehemu yake iliyo na majina ya wapiga kura wanaostahili kupiga kura katika kituo cha kupigia kura;

(f) idadi ya kutosha ya vyumba vyta kupigia kura kuwawezesha wapiga kura kupiga kura kwa usiri; na

(g) kifaa kingine chochote cha kupigia kura kitakachoidhinishwa na Tume kwa ajili ya kupiga kura katika kituo cha kupigia kura.

Kuingia
katika
kituo cha
kupigia kura

20.-(1) Afisa wa kura ya maoni atasimamia idadi ya wapiga kura watakaoingia katika kituo cha kupigia kura kwa wakati mmoja na atazuia watu wengi wote isipokuwa-

- (a) makamishna au maafisa wa Tume;
- (b) maafisa wa polisi au mtu mwingine mwenye jukumu la ulinzi;
- (c) watu wanaohitajika kwa ajili ya kuwasaidia wapiga kura wasioona au wasiyojiweza;
- (d) mawakala waliosajiliwa na Tume; na
- (e) waangalizi wanaotambulika na wawakilishi wa vyombo vya habari vinavyochapisha habari na vya kielektroniki vilivyoidhinishwa au kutambuliwa na Tume;

(2) Mtu yeote ambaye hajaandikishwa kama mpiga kura, hatoruhusiwa kuingia katika kituo chochote cha kupiga kura.

Utulivu
katika
kituo
cha
kupigia
kura

21.-(1) Itakuwa ni jukumu la Afisa wa kura ya maoni kuhakikisha utulivu katika kituo cha kupigia kura.

- (2) Afisa wa kura ya maoni anaweza kuamuru kutawanyika kwa mkusanyiko wa watu ambao unaonekana kwa msimamizi huyo kuwa utazuia uingiaji au utokejia kwa uhuru katika kituo cha kupigia kura au kutuo au kuingilia wapiga kura, na amri hiyo itakuwa ni mamlaka tosha kwa ofisa wa polisi au mtu mwingine

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

yeyote aliyeidhinishwa kwa amri hiyo
kutekeleza utawanyishaji wa
mkusanyiko.

(3) Mamlaka aliyopewa Afisa wa kura ya maoni na ofisa wa polisi kwa mujibu wa kifungu hiki hayatakuwa na ukomo katika eneo ambalo kituo cha kupigia kura kipo pekee, isipokuwa yatajumuisha eneo la umbali wa mita miambili kutoka katika kituo cha kupigia kura.

(4) Iwapo mtu yeyote atafanya fujo katika kituo cha kupigia kura, au kutotii maelekezo au amri halali ya Afisa wa kura ya maoni, mtu huyo anaweza kuondolewa mara moja, kwa amri ya Afisa wa kura ya maoni au ofisa wa polisi, na mtu huyo aliyeondolewa hataingia tena katika kituo cha kupigia kura wakati upigaji kura ukiendelea bila ya ruhusa ya Afisa wa kura ya maoni.

Kuahirishwa
na
kuongeza
muda wa
upigaji
kura

22.-(1) Bila kujali masharti ya taarifa yoyote iliyotolewa chini ya Sheria hii, Afisa wa kura ya maoni anaweza kuahirisha zoezi la kupiga kura ya maoni katika kituo cha kupigia kura iwapo utaingiliwa na vurugu, janga la asili, upungufu wa vifaa au sababu nyingine, isipokuwa zoezi litaruhusiwa kuendelea haraka iwezekanavyo.

(2) Mamlaka ya Afisa wa kura ya maoni yatajumuisha mamlaka ya kuhamisha zoezi la kupiga kura kwenda katika kituo kingine cha kupigia kura katika jimbo hilo hilo, na katika hali kama hiyo-

(a) Afisa wa kura ya maoni atatoa taarifa ya jambo hilo baada ya kushauriana na kamati za kura ya

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

maoni, kwa namna yoyote atakayoona inafaa kufikisha taarifa hiyo, kwa wapiga kura; na

(b) eneo la kupigia kura la kituo cha kura ambacho zoezi la kupiga kura linahamishiwa kwa madhumuni hayo litachukuliwa kuwa ni sehemu ya eneo la kupigia kura na kituo cha kupigia kura ambacho zoezi la kupiga kura linahamishiwa.

(3) Afisa wa kura ya maoni anaweza kuongeza muda katika kituo cha kupigia kura pale ambapo upigaji kura umeingiliwa au kwa sababu nyingine ya msingi, na ataongeza muda wa kupiga kura ili kufidia muda wowote uliopotea pale ambapo upigaji kura katika kituo umecheleweshwa.

Mawasiliano
na wapiga
kura katika
kituo cha
kupigia kura

23.-(1) Hakuna mtu isipokuwa msimamizi wa Kura ya maoni au Afisa wa kura ya maoni aliyeko zamu, isipokuwa kwa mamlaka ya Afisa wa kura ya maoni, atakayewasiliana na mpiga kura ambaye yuko ndani ya eneo la kituo cha kupigia kura kwa madhumuni ya kupiga kura.

(2) Kifungu kidogo cha (1) hakitatafsiriwa kuwa kinamzuia msaidizi wa mtu aliye na ulemavu wa kuona au asiyejiweza kuwasiliana na mpiga kura huyo.

Kufungwa
kwa
sanduku
la kupiga
kura

24.-(1) Mara tu kabla ya kuanza kwa upigaji kura, Afisa wa kura ya maoni ataonyesha sanduku la kupigia kura au masanduku ya kupigia kura kwa mawakala ili kuhakikisha kuwa sanduku hilo au masanduku hayo ni matupu, na baada ya hapo atalifunga sanduku au masanduku kiasi kwamba

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

hayataweza kufunguliwa pasipo kuvunja lakiri.

(2) Baada ya sanduku la kupigia kura kufungwa na lakiri, Afisa wa kura ya maoni ataelekeza liwekwe katika kituo cha kupigia kura kiasi kwamba katika kipindi chote litawenza kuonekana na Afisa wa kura ya maoni, naibu afisa wa kura ya maoni na mawakala waliopo.

(3) Wakati wa kuahirishwa kwa zoezi la kupiga kura ya maoni katika kituo cha kupigia kura kwa siku nyingine, au kwa kufungwa kwa kituo kimoja kwa lengo la kuhamisha sanduku la kupigia kura kwenda kituo kingine, na katika muda mwengine wowote pale ambapo sanduku la kupigia kura halitumiki, Afisa wa kura ya maoni atafunga kiupenyo kilichotumika kuingizia karatasi za kupigia kura katika sanduku na kuweka lakiri rasmi juu yake kwa namna itakayozuia uingizaji wa makaratasi ya kupigia kura pasipo kuvunja lakiri.

(4) Baada ya sanduku la kupigia kura kufungwa kwa lakiri, lakiri haitavunjwa au kiupenyo kufunguliwa hadi hapo lakiri itakapovujwa na kufunguliwa mbele ya watu ambao wako kihalali katika kituo cha kupigia kura katika muda ambao upigaji kura unaanza tena.

(5) Afisa wa kura ya maoni atawaruhusu Mawakala wa kura ya maoni waliopo katika kituo cha kupigia kura kukagua karatasi ya kupigia kura yaliyotolewa kwa matumizi katika kituo cha kupigia kura na kunakili namba zilizo katika mfululizo, kabla ya upigaji kura kuanza.

Karatasi
za Kura

25.-(1) Tume itakuwa na wajibu wa kuandaa Karatasi ya kupigia kura kwa ajili ya kutumika wakati wa kura ya maoni.

(2) karatasi za kupigia kura-

(a) itakuwa na swali linalopigiwa kura katika lugha ya Kiswahili;

(b) itaweza kukunjika, kuwa na namba au muunganisho wa herufi na namba, vilivyochapishwa kwa mbele;

(c) itaambatana na kishina kilicho na namba zile zile au muunganisho wa herufi na namba vilivyochapishwa kwa mbele; na

(d) itakuwa na alama tofauti na ya kipekee kwa kila jibu la swali linalopigiwa kura.

(3) karatasi ya kupigia kura ya maoni itaelezea swali linalotakiwa kujibiwa na wapiga kura kwa mfumo wa jibu la "NDIYO" au "HAPANA".

Taratibu
za jumla
za kupiga
kura

26.-(1) Afisa wa kura ya maoni, kabla ya kumpatia mpiga kura karatasi ya kupigia kura atahakikisha kwamba-

(a) sehemu ya nyuma ya karatasi ya kupigia kura inapigwa mhuri wenye alama maalum ya Tume;

(b) namba na jina la mpiga kura kama lilivyoainishwa katika nakala ya daftari linatajwa;

(c) jina la mpiga kura linawekewa alama na namba ya mpiga kura

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

inabakizwa kama ushahidi kuwa karatasi ya kupigia kura imetolewa kwake.

(2) Mpiga kura-

(a) baada ya kupokea karatasi ya kupigia kura -

(i) ataenda mara moja katika moja ya vyumba vya kupigia kura na wakati akiwa hapo kwa siri ataweka alama katika karatasi ya kupigia kura katika kiboksi na safu iliyotolewa pembedi ya alama katika upande ambao mpiga kura anataka kupigia kura;

(ii) ataikunja kiasi cha kuficha kura na kuiweka karatasi ya kupigia kura katika sanduku la kupigia kura mbele afisa wa kura ya maoni, huku akiwa anaonekana kikamilifu na watu waliopo hapo kihalali;

(b) atapakwa wino usiofutika katika kidole chake kidogo cha kushoto iwapo hana kidole hicho atapakwa wino katika sehemu yoyote ya mwili ambayo wino huo hautofutika kwa kipindi chote cha kura ya maoni;

(c) mara baada ya kupiga kura ataondoka katika kituo cha kupigia kura.

(3) Hakuna mtu, isipokuwa mtu anayefanya kazi kwa mujibu wa masharti ya kifungu cha 19, atakaye kuwepo katika chumba cha

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

kupigia kura cha kituo cha kupigia kura wakati mpiga kura yuko ndani ya chumba hicho kwa madhumuni ya kuweka alama katika karatasi ya kupigia kura.

(4) Mtu ambaye, akiwa na ufahamu kamili, atashindwa kuweka karatasi ya kupigia kura iliyotolewa kwake, mbali na karatasi ya kupigia kura iliyoharibika, katika sanduku la kupigia kura kabla ya kuondoka katika eneo ambalo sanduku la kupigia kura lipo, anatenda kosa, na atakapotiwa hatiani, atawajibika kulipa faini isiyozidi shilingi laki tano au kutumikia kifungo kwa kipindi kisichozidi miezi mitatu au vyote.

(5) Afisa wa kura ya maoni ambaye kwa makusudi atakataa kuweka alama au mhuri katika karatasi yoyote ya kupigia kura, anatenda kosa na atakapotiwa hatiani, atawajibika kulipa faini isiyozidi shilingi laki tano au kutumikia kifungo kwa kipindi kisichozidi miezi mitatu au vyote.

Wapiga
kura
wanaohitaji
msaada

27.-(1) Afisa wa Kura ya Maoni, kutokana na ombi la mpiga kura ambaye anatamka kuwa hana uwezo wa kusoma au kuandika, au ambaye anashindwa kupiga kura kutokana na ulemavu wa kuona au sababu nyingine ya kimaumbile kwa namna ilioainishwa chini ya Sheria hii, atamruhusiwa mpiga kura huyo kusaidiwa na mtu ambaye mpiga kura huyo atamchagua.

(2) Mtu yejote ambaye si mtu aliyechanguliwa na mpiga kura hataruhusiwa kuingia katika chumba cha kupigia kura wakati mpiga kura anapiga kura yake.

(3) Mtu ambaye atamsaidia mpiga kura -

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

(a) atamsaidia mpiga kura mmoja tu lakini ikiwa katika familia kuna watu zaidi ya mmoja ambao wanahitaji msaada chini ya aya hii, itakuwa halali kwa familia kumchagua mmoja wao kuwa saidia wapiga kura hao; na

(b) atazamisha au kuchovya kidole chake cha kushoto au sehemu yoyote ya mwili katika wino uliyo na rangi ya kipekee ambao, kwa kadri itakavyowezekana, utakuwa haufutiki kiasi cha kuacha alama kwa kipindi chote cha upigaji wa kura ya maoni.

(4) Afisa wa kura ya maoni anaweza kufanya uchunguzi kama ambavyo inafaa ili kujiridhisha kuwa mpiga kura na msaidizi wake wanafuata masharti ya sheria hii.

(5) Afisa wa kura ya maoni anaweza, pale ambapo mpiga kura hana msaidizi, na kutohakana na ombi la mpiga kura, kuwezesha kura ya mpiga kura kupigwa kwa niaba ya mpiga kura huyo.

(6) Pale ambapo afisa wa kura ya maoni anakubali ombi la mpiga kura chini ya kifungu hiki, afisa wa kura ya maoni atanakili kwenye nakala ya daftari, pembeni mwa jina la mpiga kura kama ushahidi kwamba mpiga kura huyo alisaidiwa na sababu ya kusaidiwa huko.

(7) Mtu ambaye atatoa maelezo ya uongo kuhusiana na kutokuwa na uwezo, pamoja na afisa mwengine au wakala ambaye anafahamu, anaruhusu au anamsaidia mtu huyo kusaidiwa anatenda kosa.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Utaratibu
wa
kufunga
kituo
cha
kupigia
kura

(8) Mtu ambaye atakiuka masharti ya kifungu hiki anatenda kosa na atawajibika, atapakotiya hatiani, kulipa faini islyozidi shilingi milioni mbili au kutumikia kifungo kwa kipindi kisichozidi miezi mitatu au vyote.

28.-(1) Mara baada ya kufungwa kwa kituo cha kupiga kura, afisa wa kura ya maoni ataandaa taarifa ya maandishi yenye idadi ya:

(a) karatasi za kupigia kura zilizotolewa kwa afisa wa kura ya maoni;

(b) karatasi za kura yaliyotumika;

(c) kura zilizoharibika; na

(d) karatasi za kura ambayo yaliyosalia bila kutumika.

(2) Mara baada ya kukamilika kwa maelezo katika kifungu kidogo cha (1), afisa wa kura ya maoni, mbele ya mawakala atatenga katika bahasa tofauti inayojumuisha-

(a) kura zilizoharibika, kama zipo;

(b) nakala ya daftari lilitlowekwa alama;

(c) vishina vya makaratasi ya kupigia kura yaliyotumika; na

(d) maelezo yaliyotolewa katika kifungu kidogo cha (1), na atafunga kila pakiti kwa muhuri rasmi wa Tume.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Kura
zitahesabiwa
katika
kituo
cha kupigia
kura

29.-(1) Afisa wa kura ya maoni mara baada ya zoezi la kupiga kura kukamilika mbele ya mawakala, atahesabu kura za kituo hicho cha kupigia kura.

(2) Hakuna wakala atakayechukuliwa kuwa ni wakala wa kuhesabu kura isipokuwa angalau saa thelathini na sita kabla ya kufungwa kwa kupiga kura katika kura ya maoni, jina na anuani ya wakala na barua yake ya uteuzi na kamati ya kura ya maoni iliyosajiliwa imewasilishwa kwa Afisa wa kura ya maoni na Afisa wa kura ya maoni hataruhusu mtu ambaye uthibitisho wake haujawsilishwa kuhudhuria kuhesabu kura.

(3) Bila kujali masharti ya kifungu hiki, Afisa wa kura ya maoni hatapokea zaidi ya mawakala wawili wa kuhesabu kura katika kituo cha kupigia kura.

(4) Afisa wa kura ya maoni atawaruhusu wafuatao kuwa katika kituo cha kuhesabu kura-

(a) Makamishna au maafisa wa Tume;(b)
maafisa wa polisi au mtu mwengine mwenye jukumu la ulinzi;

(c) Mawakala waliosajiliwa na Tume;
na

(d) waangalizi walioruhusiwa na Tume.

(5) Iwapo gari au chombo kimetumika kama kituo cha kupigia kura na kumetokea hali ya hewa inayoweza kuathiri kuhesabu kura, mara baada ya Afisa wa kura ya

Kuhesabu
kura
kwa mara
nyingine

Karatasi
za kupiga
kura
zilizokataliwa

maoni kutekeleza masharti ya kifungu cha 21, afisa wa kura ya maoni anaweza, kwa kushirikiana na mawakala, kuruhusu gari au chombo kuhamishiwa sehemu ambapo kura zinaweza kuhesabiwa.

30. Wakala wa kura ya maoni anaweza, baada ya kukamilika kwa kuhesabu kura na pale ambapo hajaridhika na kuhesabiwa kwa kura, atamtaka Afisa wa kura ya maoni kuhesabu kura kwa mara nyingine au Afisa wa kura ya maoni anaweza, kwa matakwa yake mwenyewe kuhesabu kura kwa mara nyingine, isipokuwa kwamba kuhesabu kura kwa mara nyingine hakutafanyika zaidi ya mara mbili.

31.-(1) Kila karatasi ya kupigia kura iliyokataliwa itawekwa alama yenye neno "imekataliwa" na Afisa wa kura ya maoni na, iwapo pingamizi la kukataliwa limetolewa na mtu au kundi la watu lenye maslahi katika matokeo ya kura ya maoni, Afisa wa kura ya maoni ataongeza maneno "kukataliwa kumepingwa".

(2) Afisa wa kura ya maoni ataweka alama katika kila karatasi ya kupigia kura iliyohesabiwa ambayo uhalali wake unapingwa au unabishaniwa na mtu au kundi la watu lenye maslahi katika matokeo ya kura ya maoni kwa neno "imepingwa".

(3) Pale ambapo kuhesabu kura kumefikia tamati afisa wa kura ya maoni ataandaa maelezo yanayoonesha idadi ya karatasi za kupiga kura yzilizokataliwa kwa kuzingatia sababu zifuatazo-(a)
hitaji la alama rasmi;

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

(b) kupiga kura kwa vyote viwili, kuunga mkono na kwa kupinga swalii la kura ya maoni;

(c) maandishi yasiyoidhinishwa au alama ambayo kutokana nayo mpiga kura anawenza kutambulika; na

(d) haijawekwa alama au ni batili kwa kutoeleweka.

(4) Mtu au kundi la watu lenye maslahi katika matokeo ya kura ya maoni watastahili kupewa nakala ya maelezo hayo.

Kufungwa
kwa
karatasi
za kupigia
kura

32.-(1) Baada ya kukamilika kwa zoezi la kuhesabu kura, afisa wa kura ya maoni atafunga katika pakiti tofauti-

(a) kura zilizohesabiwa ambazo hazibishaniwi;

(b) kura zilizokataliwa pamoja na maelezo kuhusiana nazo; na

(c) kura zinazobishaniwa.

(2) Afisa wa kura ya maoni ata-

(a) ziweka bahasha tatu zilizotajwa chini ya kifungu kidogo cha (1) pamoja na maelezo yaliyotengenezwa chini ya kifungu cha 27;

(b) tangaza matokeo;

(c) ataonesha wazi kwa wapiga kura, waangalizi waliokubalika na mawakala wowote waliokuwepo, kwamba boksi la kupigia kura liko tupu;

Matokeo
ya jimbo

- (d) funga sanduku la kupigia kura kwa lakiri ya Tume;
- (e) ruhusu mawakala waliopo au yeyote kati yao kuweka lakiri zao katika sanduku la kupigia kura endapo watapenda; na
- (f) haraka iwezekanavyo atawasilisha kwa msimamizi wa kura ya maoni sanduku la kupigia kura lenye vitu vilivyoorodheshwa chini ya kifungu kidogo cha (2).

33.-(1) Mara baada ya matokeo ya kura kwa vituo vyote vya kupigia kura katika jimbo kupokelewa na msimamizi wa kura ya maoni, msimamizi wa kura ya maoni, katika uwepo wa wajumbe au maafisa wa Tume, askari ama mtu yeyote anayeshughulikia usalama, wakala, waangalizi na waandishi habari waliothibitishwa na Tume na kiongozi wa kamati ya kura ya maoni-

(a) atachunguza makaratasi ya kupigia kura yaliyowekewa alama ya "imekataliwa" "kukataliwa kumepingwa" na "inabishaniwa" na kuthibitisha au kutofautiana na maamuzi ya maafisa wa kura ya maoni kwa kuzingatia uhalali wa makaratasi hayo ya kupigia kura;

(b) atatangaza wazi kwa watu waliopo idadi ya jumla ya kura halali zilizopigwa kwa kila upande katika kura ya maoni;

(c) atatamka wazi kwa watu waliopo upande ambao umepata idadi kubwa ya kura halali zilizopigwa

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

katika kura ya maoni na hivyo ndiyo upande ulioshinda;

(d) atakamilisha fomu ambamo atatamka:

(i) jina la jimbo;

(ii) idadi ya jumla ya wapiga kura waliosajiliwa;

(iii) kura halali zilizopigwa ambazo zinaunga mkono au kupinga swali la kura ya maoni;

(iv) idadi ya kura zilizokataliwa zilizopigwa kuunga mkono au kupinga swali la kura ya maoni katika kila kituo cha kupigia kura;

(v) idadi ya kura zote zilizopigwa katika jimbo; na

(vi) idadi nzima ya kura zote zilizokataliwa; na

(e) atasaini na kuweka tarehe katika fomu na-

(i) kutoa nakala ya fomu kwa mawakala waliosajiliwa wa kamati ya kura ya maoni; na

(ii) kuwasiliisha nakala halisi ya fomu kwa Tume.

(2) Matokeo katika jimbo yatakuwa katika fomu itakayoandalisha na Tume na yatazingatia uthibitisho wa Tume baada ya

kuhesabiwa kwa kura zote zilizopigwa katika kura ya maoni.

(3) Uamuzi wa msimamizi wa kura ya maoni juu ya uhalali au vinginevyo wa makaratasi ya kupigia kura au kura chini ya kifungu hiki, kwa kuzingatia uthibitisho wa Tume, utakuwa ni wa mwisho isipokuwa, pale ambapo kwa maoni itakuwa imepingwa mahakamani.

Kutangazwa
na
kuchapishwa
matokeo
ya kura
ya maoni

34.-(1) Tume, baada ya kupokea matokeo ya kura ya maoni kutoka katika majimbo yote na ndani ya saa sabini na mbili toka kufungwa kwa upigaji kura wa mwisho katika kura ya maoni:

- (a) itatangaza kwa umma idadi ya jumla ya kura halali zilizopigwa kuunga mkono au kupinga swali la kura ya maoni kama iliyowekwa katika Jedwali la Pili la Sheria hii;
- (b) itatamka iwapo au la jambo linalojadiliwa la kura ya maoni imekubaliwa na zaidi ya asilimia hamsini ya kura halali zilizopigwa kwa Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar;
- (c) itachapisha tangazo katika *Gazeti* la Serikali kuonesha matokeo ya kura ya maoni katika kila jimbo; na
- (d) itachapisha katika *Gazeti* la Serikali cheti katika fomu itakayoandaliwa na Tume ikitangaza matokeo ya kura ya maoni na kuthibitisha iwapo au la jambo linalotakiwa kuamuliwa limekubaliwa kwa mujibu wa masharti ya Sheria.

(2) Kwa madhumuni ya kifungu kidogo cha (1)(b), kura zitakazo hesabiwa kwa Tanzania Zanzibar zitajumuisha:

(a)kura za watu walioandikishwa katika daftari la wapiga kura la Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar; na

(b) kura za watu wanaoishi Zanzibar na walioandikishwa chini ya daftari la kura la Tume ya Taifa ya Uchaguzi.

(3) Kwa madhumuni yote ya kura ya maoni, matokeo yaliyochapishwa katika *Gazeti* la Serikali yatakuwa ni matokeo rasmi ya kura ya maoni.

Matokeo
ya kura
ya maoni

35.-(1) Matokeo ya kura ya maoni yataamuliwa kwa msingi wa kuungwa mkono kwa asilimia inayozidi hamsini ya jumla ya kura halali zote zilizopigwa kutoka Tanzania Bara na zaidi ya asilimia hamsini ya kura halali zote za maoni zilizopigwa Tanzania Zanzibar.

(2) Wingi wa kura ya halali zilizopigwa katika kura ya maoni zitaamua juu ya matokeo ya swali litakalopigiwa kura ya maoni na matokeo ya kura ya maoni yatakayotangazwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi yataheshimiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

(3) Pale ambapo kura zilizopigwa za "NDIYO" ya swali la kura ya maoni hazijazidi asilimia hamsini ya jumla ya kura halali zote zilizopigwa Tanzania Bara au Tanzania Zanzibar, Tume kwa taarifa itakayotangazwa katika *Gazeti* la Serikali, itateua siku nyingine ya kupiga kura ndani ya siku sitini baada ya

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

kutangazwa matokeo, na itarudia utaratibu wa kupiga kura ya maoni ambao utaanza upya.

(4) Bila ya kujali masharti ya kifungu kidogo cha (3), Tume pale ambapo mazingira yatahitaji, inaweza:

(a) kutoa muda wa kutosha kwa ajili ya uhamasishaji na kutoa elimujuu ya kura ya maoni ya Katiba inayopendekezwa; au

(b) kutoa muda unaofaa kwa Rais, kwa kukubaliana na Rais wa Zanzibar kuitisha upya Bunge la Katiba kwa dhumuni la kuangalia upya vifungu vyta Katiba inayopendekezwa.

(5) Pale ambapo wingi wa kura halali zilizopigwa kwenye kura ya maoni zitakuwa ni "HAPANA", Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, itaendelea kutumika.

SEHEMU YA TANO

MASHARTI YA JUMLA

Utaratibu
wa
kuendesha
kura ya
maoni
Sura ya 343
na 292
Sheria Na.11
ya1984

36. Utaratibu wa uendeshaji wa Uchaguzi Mkuu chini ya Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sheria ya Uchaguzi ya Zanzibar na Sheria ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa pamoja na marekebisho yanayofaa, utatumika kuendesha kura ya maoni chini ya sehemu hii.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Kupiga
kura
katika
mazingira
maalum

37.-(1) Tume inaweza kuweka masharti maalum kwa ajili ya upigaji kura ya maoni kwa raia wa Tanzania ambao wanaishi nje ya Jamhuri ya Muungano au ambao hawataweza kupiga kura siku ya kupiga kura kutokana na majukumu muhimu, kwa sababu za kijamii na kiuchumi, wagonjwa walioko hospitalini, watu wanaishi katika nyumba za kutunzia wazee na taasisi zinazofanana na hizo, watu wanaishi maisha ya kuhama hama kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa, watu wenye ulemavu na wakina mama wajawazito:

Isipokuwa, mtu hataruhusiwa kupiga kura mpaka awe amesajiliwa kama mpiga kura katika daftari la mpiga kura.

(2) Tume, kwa madhumuni ya kura ya maoni, itaweka utaratibu wa kuandikisha raia wa Jamhuri ya Muungano ambao wanaishi nje ya Jamhuri ya Muungano na ambao hawajasajiliwa kama wapiga kura katika daftari la mpiga kura.

Uthibitishaji
wa
waangalizi

38.-(1) Mtu ye yeyote au chama, taasisi au asasi, inayotaka kuwa mwangalizi, italazimika kuomba katika Tume kwa ajili ya kuthibitishwa kwa muda usiozidi miezi miwili kabla ya tarehe ya kura ya maoni.

(2) Tume inaweza kuwathibitisha watu, au maafisa wa chama, taasisi au asasi ambazo si wanachama wa chama chochote cha siasa kuwa waangalizi wa kura ya maoni.

(3) Tume itatoa miongozo kwa ajili ya waangalizi wa kura ya maoni, ambao itafuatwa na waangalizi wa kura za maoni waliothibitishwa.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mahudhurio
ya
mawakala

Mamlaka
ya jumla
ya Tume

Gharama
za
uendeshaji
kura
ya
maoni

(4) Tume inaweza kufuta uthibitisho ilioutoa kwa mwangalizi yeote wa kura ya maoni, iwapo itajiridhisha kwamba muangalizi wa kura ya maoni ni mwanachama anayeegemea upande mmoja.

(5) Waangalizi wote wa kura ya maoni waliothibitishwa watawasilisha kwa Tume taarifa ya maandishi kuhusu maoni yao binafsi au ya kikundi si zaidi ya siku kumi na nne baada ya tarehe ya kutangazwa kwa matokeo ya kura ya maoni kuhusiana na uangalizi wa kura ya maoni.

39. Pale ambapo katika sheria hii yametumikwa maneno ambayo yanahitaji, yanaidhinisha au kuonyesha kwamba kitendo chochote au kitu kinatakiwa kufanywa mbele ya mpiga kura au wakala wa kuhesabu kura, maneno hayo yatachukuliwa kama hivyo na kutokuwepo kwa wakala yeote katika muda na mahali hapo na kama kitendo au kitu chochote kimefanywa kihalali haktabatilisha kitendo au kitu hicho.

40. Hakuna kitu chochote katika Sheria hii kitakachotafsiriwa kuizua Tume kuchukua hatua zaidi za kiutawala au kutoa miongozo ya kisera na kanuni kuhakikisha utekelezaji sahihi wa uendeshaji wa kura ya maoni.

41. Gharama zitakazotumika katika uendeshaji wa kura ya maoni zitachukuliwa kutoka katika Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mtu
hatatakiwa
kueleza
jinsi alivyopiga
kura

Kupinga
matokeo
ya Kura
ya maoni

42. Mtu ambaye amepiga kura katika kura ya maoni hatahitajika katika mwenendo wowote ambao umeletwa chini ya sheria hii au vinginevyo, kueleza jinsi alivyopiga kura.

43.-(1) Pingamizi ya kamati ya kura ya maoni dhidi ya matokeo ya Kura ya maoni ni juu ya Katiba inayopendekezwa itawasilishwa mbele ya Mahakama Kuu itakayokaa chini ya jopo la Majaji watano.

(2) Kamati ya kura ya maoni itaruhusiwa tu kuwasilisha ombi la kupinga matokeo ya kura ya maoni mbele ya Mahakama Kuu baada tu ya kupata si chini ya asilimia kumi ya saini za idadi yote ya wapiga kura waliosajiliwa kutoka katika majimbo matano ya kila upande wa muungano.

(3) Ombi litakuwa kama ilivyoelezwa katika fomu iliyowekwa katika Jedwali la Tatu la Sheria hii, na litawasilishwa katika Masjala ya Mahakama Kuu ndani ya siku kumi na nne baada ya kutangazwa kwa matokeo ya kura ya maoni.

(4) Kwa madhumuni ya kifungu kidogo cha (2), Kamati ya kura ya maoni haitajumuisha katika ombi lake jina la mtu bila idhini yake au jina la mtu ambaye alifariki kabla ya tarehe ya ombi.

(5) Mtu ambaye anadai kuwa jina lake limejumuuhishwa katika ombi bila idhini yake, au kwamba ombi limejumuisha jina la mtu aliyefariki kabla ya tarehe ya kufanyika kwa ombi, atawasilisha pingamizi katika Mahakama Maalum, katika fomu iliyowekwa katika Jedwali la Nne la Sheria hii.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Sura ya 343
na Sheria
Na. 11
ya 1984 (Z)

Uwekaji
wa
dhamana

Uamuzi
wa
malalamiko
wa
Mahakama

(6) Mtu anayekiuka kifungu kidogo cha (4) anatenda kosa, na atawajibika, iwapo atatiwa hatiani, kulipa faini ya shilingi milioni kumi au kifungo kwa kipindi cha miaka saba au vyote viwili.

(7) Kamati ya kura ya maoni inaweza kupinga matokeo ya kura ya maoni ya walioshindwa kufuata Sheria hii au Sheria ya Taifa ya Uchaguzi na Sheria ya Uchaguzi ya Zanzibar, iwapo kutofuata huko kumeathiri kwa kiasi kikubwa matokeo ya kura ya maoni.

44.-(1) Msajili wa Mahakama Kuu hatapanga tarehe ya kusikilizwa kwa maombi yoyote ya kupinga matokeo ya kura ya maoni isipokuwa kama mpinga matokeo amelipa kwa mahakama na kama dhamana ya gharama kiasi ambacho hakitazidi shilingi milioni tano.

(2) Kiasi cha fedha kilicholipwa kama dhamana za gharama chini ya kifungu kidogo cha (1), zitarejeshwa kwa mleta maombi ya kupinga matokeo ya Kuara ya maoni pale ambapo mpinga matokeo anashinda kesi au baada ya rufaa, na iwapo hakuna amri ya kulipa gharama imetolewa dhidi yake.

45.-(1) Mahakama Kuu itakuwa na mamlaka ya kusikiliza na kutolea uamuzi malalamiko ya kura ya maoni.

(2) Mahakama Kuu itawasikiliza na kutoa uamuzijuu ya pingamizi la kura ya maoni ndani ya kipindi cha siku kumi na nne tangu lalamiko lillipowasilishwa mahakamani.

(3) Baada ya kulisikiliza lalamiko la kura ya maoni, Mahakama Kuu inaweza, ama-

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

- (a) kuondoa maombi;
 - (b) kutangaza matokeo kuwa si sahihi na kutangaza matokeo sahihi;
 - (c) kuiamuru Tume kurudia kupiga kura ya maoni katika eneo lolote maalum au maeneo yoyote maalum; au
 - (d) kutengua matokeo ya kura na kuamuru kura ya maoni kupigwa upya.
- (4) Bila kuathiri kifungu kidogo cha (3), Mahakama Kuu inaweza, kabla ya kufanya uamuzi, kuamuru kura zilizopigwa zihesabiwe upya.
- (5) Hakuna katika kifungu hiki kitakachoipa Mahakama Kuu mamlaka ya kumtia mtu hatiani kwa kosa la jinai wakati wa kusikiliza lalamiko chini ya kifungu hiki.
- (6) Pale inapotokea kwa Mahakama Kuu, wakati wa kusikilizwa kwa lalamiko chini ya kifungu hiki, kwamba maelezo yaliyotolewa kabla ya kubainisha kwamba kosa la jinai linaweza kuwa limetendeka, itapeleka taarifa kuhusu jambo hilo kwa Mkurugenzi wa Mashtaka kwa ajili ya kuchukua hatua stahiki na itataja katika taarifa hiyo jina la mtu huyo.
- Rufaa **46.-(1)** Upande wowote usioridhishwa na uamuzi wa Mahakama Kuu uliofanywa chini ya kifungu cha (44) atakata rufaa katika Mahakama ya Rufaa ndani ya siku saba kutoka tarehe aliyo pata nakala ya hukumu na mwenendo wa shauri.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Zuio la
kuchocha
vurugu
wakati
wa kura
ya maoni

Makosa
na
adhabu
Sura 343

Kanuni

(2) Mahakama Kuu itatoa nakala ya hukumu na mwenendo wa shauri kwa muombaji ndani ya siku tano kutoka tarehe ya kutolewa uamuzi.

(3) Mahakama ya Rufaa, itakayokaa chini ya jopo la Majaji saba, itaamua rufaa ndani ya siku saba kutoka tarehe ya kuwasilishwa kwa ombi la rufaa.

47.-(1) Mtu, yejote wakati wa zoezi la kura ya maoni hatatumia lugha inayodhalilisha au inayochocha uvunjifu wa amani ya umma, chuki au vurugu.

(2) Mtu ambaye anakiuka kifungu kidogo cha (1), anatenda kosa na atawajibika, atakapotiwa hatiani, kulipa faini isiyopungua shilingi milioni mbili au kutumikia kifungo kwa kipindi kisichopungua miezi sita au vyote viwili.

48. Mtu yejote ambaye anakiuka masharti yoyote ya Sheria hii ambayo kwayo adhabu haijatolewa, anatenda kosa na atawajibika, kulipa faini ya shilingi milioni moja au kutumikia kifungo cha miezi sita.

49.-(1) Tume inaweza, pale itakapohitajika, kutunga kanuni kwa ajili ya utekelezaji bora wa masharti ya Sheria hii.

(2) Bila kuathiri ujumla wa kifungu kidogo cha (1), Tume inaweza kutunga kanuni kwa ajili ya mambo yafuatayo:

(a) uanzishwaji wa vituo vya kupigia kura;

(b) namna na utaratibu wa kupiga kura katika kura ya maoni;

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

(c) namna ya kuhakikisha utambuzi wa watu walio na nia ya kupiga kura katika kura ya maoni, na kama watu hao wanazo sifa za kupiga kura;

(d) namna ambayo watu waliyo na ulemavu wanavyoweza kupiga kura katika kura ya maoni;

(e) upigaji kura kwa watu walio kazini katika siku ya kupiga kura ya maoni;

(f) utunzaji wa usiri katika kura ya maoni;

(g) usitishaji au kuongezwa kwa muda kwa ajili ya kupiga kura iwapo kunatokea fujo au vurugu katika kura ya maoni;

(h) viapo au uapishwaji wa maafisa kuhusiana na masuala ambayo yameainishwa;

(i) utaratibu utakaofuatwa katika kuhitimisha upigaji kura katika kura ya maoni;

(j) utaratibu wa kuhesabu na kujumlisha kura katika kura ya maoni kwa Tanzania Bara na kwa Zanzibar na mazingira ambayo kura inaweza kukataliwa na msimamizi wa kura ya maoni kama ni batili;

(k) utangazaji, utoaji taarifa na uchapishaji wa matokeo ya kura ya maoni;

(l) utunzaji na kuharibu karatasi a kupigia kura, kumbukumbu, nyaraka

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

au vitu vingine vinavyohusiana na uendeshaji wa kura ya maoni;

(m) fomu na kumbukumbu zitakazotumika kwa madhumuni yoyote la sheria hii;

(n) jambo jingine lolote ambalo Tume itaona inafaa kwa madhumuni ya Sheria hii.

(3) Kanuni chini ya Sheria hii zitachapishwa katika *Gazeti* la Serikali.

Mamlaka
ya
kurekebisha
au kubadilisha
Jedwali

50. Waziri anaweza baada ya kushauriana na Waziri mwenye dhamana na masuala ya Uchaguzi wa Tanzania Zanzibar kwa taarifa iliyochapishwa katika *Gazeti* la Serikali, kurekebisha, kutofautisha au kuondoa Jedwali lote au sehemu ya Jedwali chini ya Sheria hii.

Kutumika
kwa
Sheria
nyingine
Sura za 343

51.-(1) Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, na Sheria ya Uchaguzi Zanzibar pale ambapo hakuna vifungu vinavyoelezewa chini ya Sheria hizi zitatumika katika uendeshaji wa kura ya maoni, ikiwa na marekebisho muhimu.

(2) Inapotokea mgongano kati ya Sheria hii na masharti yoyote ya Sheria za Uchaguzi, Sheria hii itatumika.

Utangazaji
wa
Katiba

52. Mara baada ya kutangazwa kwa Katiba Mpya, Sheria hii haitatumika na haitakuwa na nguvu yoyote kisheria.

MAJEDWALI

JEDWALI

(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 4(2))

AMRI YA KUITISHA KURA YA MAONI

Mimi.....Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, nina iamuru Tume kuendesha kura ya maoni ili kupata uamuzi wa watu kuhusu Katiba inayopendekezwa, iliyotangazwa

Maoni ya watu kuhusu Katiba inayopendekezwa ya tatangazwa si zaidi ya siku sabini tangu tarehe ya kutolewa kwa amri hii.

Imetolewa tarehe..... Mwaka 20.....

.....
Rais

MADHUMUNI NA SABABU

Muswada huu unapendekeza kutungwa kwa Sheria ya Kura ya Maoni ya mwaka, 2013.

Madhumuni ya jumla ya Muswada ni kutoa hoja ya kutungwa kwa Sheria ya Kura ya Maoni kuongoza mchakato wa kupata uamuzi wa wananchi wa Jamhuri ya Muungano juu Katiba inayopendekezwa. Kwa hiyo, Muswada huu, unatarajia kuweka utaratibu wa kisheria na kitaasisi kwa ajili ya uendeshaji wa kura ya maoni kama ilivoyeleza hapo juu. Muswada huu umegawanyika katika Sehemu Tano.

Sehemu ya Kwanza ya Muswada inahusu mambo ya utangulizi, kama vile jina fupi la Sheria, matumizi na tafsiri ya maneno mbalimbali yaliyotumika katika Muswada.

Sehemu ya Pili inaweka masharti ya uendeshaji wa kura ya maoni. Katika Sehemu hii, Rais baada ya kushauriana na Rais wa Zanzibar, amepewa mamlaka ya kuielekeza Tume kuendesha kura ya maoni kwa ajili ya kupata uamuzi wa wananchi kuhusu Katiba inayopendekezwa. Sehemu hii pia Tume imepewa mamlaka ya kuendesha elimu ya kura ya maoni na elimu ya wapiga kura kwa kura ya maoni. Sehemu hii pia inazitambua sheria nyingine zinazohusiana na mchakato wa uchaguzi Rais na Srikali za Mitaa.

Sehemu ya Tatu ya Muswada inahusu uanzishwaji wa Kamati za Kura ya Maoni. Kamati hizi zimepewa kazi za kusimamia vikundi vyta watu ambavyo vinaunga mkono au vinaptinga swali la kura ya maoni. Kamati hizi zinatakiwa kusajiliwa na Tume kwa madhumuni ya kuendesha Kampeni za ya kura ya maoni. Mbali na hilo, Sehemu hii inatoa mamlaka kwa kamati za kura ya maoni kuwateua

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

mawakala wanaotakiwa kuwepo katika kila kituo cha kupigia kura na kuhesabu kura. Vile vile inaelezea juu ya kipindi cha kuendesha kampeni za kura ya maoni.

Sehemu ya nne inatoa utaratibu wa kupiga kura katika kura ya maoni. Sehemu hii pia inaelezea vifaa vitakavyotumika katika kura ya maoni, kuruhusu wapiga kura kuingia kati8ka vituo vya kura, utaratibu wa kuwasaidia wate wenyewe ulemavu kupiga kura, ufungaji wa vituo vya kupigia kura, kuhesabu kura, utangazaji na uchapishaji wa matokeo ya kura ya maoni.

Sura ya Tano inahusu masharti ya jumla ambapo inaeleza masharti ya upigaji kura ya maoni kwa watu walio katika mazingira maalum. Sehemu hii pia inaruhusu wagonjwa walio hospitali, wazee wanaoishi katika nyumba za kutunzia wazee, watu wenye ulemavu na watu wanaoishi maisha ya kuhama hama. Aidha sehemu hii inaweka utaratibu wa kupinga matokeo ya kura ya maoni, Mahakama yenye uwezo wa kusikiliza malalamiko yanayohusiana na kura ya maoni na Utaratibu wa kukata rufaa. Sehemu hii pia, ina vifungu vivyokataza kuchochaea vitendo vya fuja na vurugu katika kura ya maoni, offences and penalties, na inatoa uwezo kwa Waziri kwa kushauriana Waziri mweny dhamana ya Uchaguzi Zanzibar kutunga Kanuni na kurekebisha au kubadilisha Jedwali katika Sheria hii. Mwisho kabisa, hesemu hii inaelezea vifungu vinavyohusiana kutangazwa kwa Katiba mpya.

Dar es Salaam,

MIZENGO P. K. PINDA

Juni, 2013

Waziri Mkuu

Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kutoa Hoja kwa Mujibu wa Kanuni ya 86(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2013 kwamba, Muswada wa Sheria ya Kura ya Maoni [*The Referendum Act, 2013*], kama ulivyochapishwa upya sasa usomwe mara ya pili.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kukushukuru wewe binafsi, kwa kazi kubwa ya kusimamia Bunge na pia namshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Pindi Hazara Chana, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Katiba, Sheria na Utawala, Naibu wake, Mheshimiwa Ngeleja na Wajumbe wote wa Kamati pamoja na Waziri Kivuli wa Kamati hiyo wa Wizara hiyo kwa ushirikiano wao walionipa katika kuchambua Muswada huu kwa kina na kutoa mapendekezo na ushauri ambao umetusaidia sana katika kuboresha Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Balozi Seif Ali Idd, Mbunge Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, pamoja na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa ujumla, kwa maoni na ushauri wao waliomletea Mheshimiwa Mizengo Peter Pinda, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhusu Muswada huu pamoja na maoni ambayo wameyaleta na leo.

Baadhi ya masuala ambayo SMZ wameshauri ni pamoja na umuhimu wa Muswada kuandikwa kwa Kiswahili na Kiingereza ili kuwapa uelewa na ufahamu mkubwa Watanzania wote, ulazima wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi [NEC] kusimamia kura ya maoni kwa upande wa Tanzania Bara tu na Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar [ZEC] kusimamia Tanzania Zanzibar.

Vile vile nawapongeza sana kwa kuongeza na kuboresha tafsiri na maneno mbalimbali kama vile Tume, NEC, ZEC, Jimbo, kura ya maoni na mengineyo.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE]

Nawashukuru sana na kwa ujumla, maoni yao yalikuwa mazuri sana na Kamati pamoja na Serikali tumeyazingatia.

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Mathias Menrad Chikawe – Waziri wa Katiba na Sheria na Naibu Waziri wa Katiba na Sheria Mheshimiwa Kariuki. Aidha namshukuru Mheshimiwa Abubakar Khamis Bakari - Waziri wa Katiba na Sheria wa SMZ na Naibu yaani Naibu Waziri wa Katiba na Sheria wa SMZ pamoja na Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Muungano pamoja na Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kwa ushiriki wao mzuri na msaada mkubwa katika kuandaan hadi kufikia leo Muswada huu.

Nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote Maafisa wa Serikali na wananchi kwa michango yao illyoisaidia sana kuboresha Muswada huu kupitia Kamati ya Bunge na wadau wengine mbalimbali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 21 (2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, inampa kila mwananchi haki ya kushiriki kikamilifu katika kufikia uamuzi kuhusu mambo yanayomhusu yeye mwenyewe, maisha yake au yanayolihsu Taifa. Katika kutekeleza masharti hayo ya Kikatiba, nchi yetu imekuwa ikitumia njia tofauti za kukusanya na kutambua maoni ya wananchi kabla ya kufikia uamuzi mkubwa unaohusu mustakabali wa nchi yetu.

Njia hizo ni pamoja na; kutumia utaratibu wa Waraka Maalum (*White Paper*); kuteua Kamati au Tume ya kupata maoni hayo; kufuatilia maoni ya watu na vyombo vyaa habari na kadhalika. Utaratibu wa kufikia uamuzi kwa njia ya kupiga kura ya maoni haujawahi kutumika Tanzania Bara.

Utaratibu huu ambao unatumika Tanzania Bara kwa mara ya kwanza, unawawezesha wananchi kupigia kura suala lenye maslahi ya Taifa baada ya kuandika swala ama maswala yanayoongoza kupata uamuzi kwa wananchi wakati wa kupiga kura. Kwa uhakika, utaratibu wa kufikia

Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)

[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE]
uamuzi wa njia ya kura ya maoni unaimarisha mamlaka ya wananchi katika kutoa uamuzi kidemokrasia na hivyo kukuza utawala bora.

Mheshimiwa Spika, uzoefu wa nchi nyingine zilizowahi kupata uamuzi wa wananchi kupertia kura ya maoni unaonesha kwamba utaratibu unaotumika ni wa kuwa na Sheria inayojitegemea ya kura ya maoni. Mfano wa nchi za Afrika zilizoendesha kura ya maoni kwa kuwa na Sheria mahsus ya kura ya maoni ni Jamhuri ya Kenya, Zimbabwe, Msambiji, Afrika Kusini na Malawi. Aidha, Zanzibar ilipoamua kupata uamuzi wa wananchi kwa njia ya kura ya maoni kuhusu Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuwa ya mfumo wa Umoja wa Kitaifa ilitunga Sheria ya Kura ya Maoni.

Mheshimiwa Spika, kwa kutumia uzoefu wa nchi nyingine na ili kuepuka mkanganyiko unaoweza kujitokeza iwapo Sheria za uchaguzi zilizopo zitatumika kusimamia uendeshaji wa kura ya maoni, Serikali imeona umuhimu wa kutunga Sheria ya Kura ya Maoni itakayotumika kwa ajili ya mchakato wa kutupatia Katiba Mpya unaoendelea hivi sasa.

Sheria hii si ya kudumu na itafikia ukomo wake mara tu baada ya Katiba Mpya kupatikana. Hili ndilo dhununi kuu la kupendekeza kutungwa kwa sheria hii ya Kura ya Maoni.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi, sasa ninaomba kuelezea kuhusu sehemu zilizomo kwenye Muswada wa Sheria ya Kura ya Maoni ambao umelenga kuweka muundo wa kisheria na kitaasisi wa uendeshaji wa kura ya maoni kama inavyoelezwa kwenye jina refu la Muswada.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu umegawanyika katika sehemu kuu Tano. Sehemu ya kwanza ina Ibara ya kwanza ya pili na ya tatu zenye masharti ya utangulizi yanayohusu Jina la Sheria inayopendekezwa, matumizi ya Sheria inayopendekezwa na kutoa tafsiri ya misamiati na

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE]

maneno yaliyotumika katika Muswada huu. Aidha, Sehemu hii inaeleza Kwa mujibu wa Ibara ya 2 kwamba Sheria ya Kura ya Maoni itatumika Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar kuhusiana na kura ya maoni kwa ajili ya kuthibitisha Katiba inayopendekezwa.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya Pili inaweka masharti kuhusu uendeshaji wa Kura ya Maoni. Muswada unapendekeza kwamba Rais kwa kushauriana na Rais wa Zanzibar kwa amri itakayochapishwa kwenye Gazeti la Serikali, ataaelekeza Tume, Tume kwa tafsiri hapa ataaelekeza Tume, Tume kwa tafsiri hapa ni Tume zote mbili kuendesha kura ya Maoni kuhusiana na Katiba inayopendekezwa. Swali la Kura ya Maoni litaandalisha na Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwa kushirikiana na Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar katika swali litakalohitaji jibu la **ndiyo** au **hapana**. Aidha, sehemu hii inapendekeza kuwa Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwa kushirikiana na Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar zipewe wajibu wa kusimamia uendeshaji wa kura ya maoni na kusimamia elimu ya wapiga kura katika kura hii ya maoni.

Masharti mengine yaliyomo katika sehemu hii yanahusu uteuzi wa wasimamizi wa kura ya maoni ambayo inapendekezwa katika Ibara ya 7 na 8 kwamba Tume ziteue Wasimamizi wa Kura ya Maoni kwa kila jimbo kusimamia uendeshaji wa Kura ya Maoni. Aidha, kila Msimamizi wa Kura ya Maoni kwa kushirikiana na Tume hizi mbili atateua Maafisa wa Kura ya Maoni na Naibu Maafisa wa Kura ya Maoni kwa ajili ya kusimamia vituo vya kupigia kura ya maoni.

Mheshimiwa Spika, Mpiga kura aliyesajiliwa katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura la Tume ya Taifa ya Uchaguzi au Daftari la Kudumu la Tume ya Uchaguzi Zanzibar atakuwa na haki ya kupiga kura katika Kura ya Maoni. Aidha, Muswada unapendekeza kuwa kwa watu walioandikishwa kama wapiga kura na taarifa zao zipo kwenye Daftari la NEC na ZEC ila wamepoteza kitambulisho cha kupigia kura lakini wameandikwa katika Daftari la

Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)

[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE]

Mpiga Kura, watajaza fomu maalum na kuruhusiwa kupiga kura. Hii itamwezesha kila mwananchi aliyejiandikisha katika Daftari la NEC au ZEC kupiga kura ya maoni.

Urekebishaji wa daftari la wapiga kura Zanzibar uko katika hatua za mwisho hivi sasa na kwa upande wa Tanzania Bara uboreshaji utaanza mwakani mwezi wa kwanza. Lakini zoezi hili la Kura ya Maoni halitafanyika mpaka uboreshaji wa Daftari hili ukamilike. Masharti mengine yanayopendekezwa katika sehemu hii yanahusiana na maeneo na vituo vya kupigia kura [lbara ya 10] pamoja na matumizi ya vifaa vya umma [lbara ya 11].

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya tatu ya Muswada yenyewe lbara ya 12, 13, 14, 15, 16 na 17 inaweka masharti kuhusiana na uanzishwaji wa Kamati za kura ya maoni kwa kila jimbo. Kamati hizo zitaundwa na makundi ya watu, vyama siasa na asasi za kiraia zinazokusudia kuunga mkono au kupinga swali la kura ya maoni kama inavyoelezwa kwenye lbara ya 12. Aidha, sehemu hii inaainisha masharti kuhusiana na: Usajili wa Kamati za kura ya maoni kwenye Tume ya Taifa ya Uchaguzi na Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar [lbara ya 13]; daftari la mawakala wa Kamati za kura ya maoni [lbara ya 14]; uteuzi wa mawakala wa Kamati za kura ya maoni watakauwepo katika kila kituo cha kupigia kura ya maoni [lbara ya 15]; kipindi cha kampeni cha kura ya maoni [lbara ya 16] na gharama za Kampeni na kura ya maoni kubebwa na Kamati [lbara ya 17].

Masharti haya yanalenga kuweka mfumo wa uwazi kwa utendaji kazi wa Kamati za kura ya maoni katika kutoa elimu kwa wananchi kuhusu suala linalohitaji kuthibitishwa.

Vile vile masharti hayo yanaainisha usimamizi na utaratibu wa Kamati hizo ili kuепusha mgongano unaoweza kutokea iwapo kila Kamati itaruhusiwa kuendesha kazi ya kuelimisha wananchi pasipo kuongozwa na chombo chochote.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE]

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Nne ya Muswada huu yenye Ibara za 18, 19, 20, 21, 22, 23, 24, 25, 26, 27, 28, 29, 30, 31, 32, 33, 34 na 35 inazungumzia mambo yafuatayo:-

- Utaratibu wa Kupiga Kura katika Vituo vyatupigia Kura ambao ki-msingi hautofautiani sana na utaratibu wa kupiga kura katika uchaguzi wa sasa;
- Vifaa vyatupigia kura;
- Utaratibu wa kuingia katika vituo vyatupigia kura;
- Utulivu katika kituo cha kupigia kura;
- Utaratibu wa Kuainisha au kusimamisha upigaji wa kura kutakapokuwa na umuhimu wa kufanya hivyo;
- Mawasiliano na wapiga kura katika kituo cha kupigia kura;
- Utaratibu wa kufunga masanduku ya kupigia kura;
- Makaratasi ya kura;
- Utaratibu wa jumla wa kupiga kura;
- Utaratibu utakaotumika kwa Wapiga kura wanaohitaji msaada;

Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)

[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE]

- Utaratibu wa kufungwa kwa kituo cha kupigia kura;
- Kura kuhesabiwa katika kituo cha kupigia kura;
- Utaratibu wa kurudia kuhesabu kura;
- Utaratibu kuhusu karatasi za kupigia kura zilizokataliwa;
- Utaratibu kuhusu kufungwa kwa karatasi za kupigia kura;
- Utaratibu kuhusu Matokeo ya Jimbo;
- Utaratibu wa Kutangazwa na kuchapishwa matokeo ya kura ya maoni; na mwisho
- Matokeo ya kura ya maoni.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Tano inaanzia Ibara ya 36 hadi Ibara ya 52 ambazo kwa ujumla zinaelezea masuala ya utaratibu wa kuendesha kura ya maoni, upigaji kura katika mazingira maalum, kuthibitishwa kwa waangalizi, mahudhurio ya mawakala, mamlaka ya jumla ya Tume zetu mbili za Uchaguzi, gharama za kura ya maoni, upingaji wa matokeo ya kura ya maoni, uwekaji dhamana ya gharama, uamuzi wa malalamiko wa Mahakama, rufaa, zuio la kuchochea vurugu wakati wa kura ya maoni, makosa na adhabu. Aidha, mamlaka ya Tume zetu mbili katika kutengeneza Kanuni kwa ajili ya utekelezaji wa sheria hii, mamlaka ya Waziri katika kurekebisha jedwali [Schedule]

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE]

na matumizi ya Sheria nyingine za Uchaguzi vimeainishwa katika sehemu hii.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, ninaliomba Bunge lako Tukufu liujadili Muswada huu wa Kura ya Maoni kama nilivyosema utaratibu wa Kupiga Kura kwa mujibu wa Sheria hii, hautofautiani sana tofauti kubwa ni kwamba Uchaguzi mwingine wowote tunapigia watu, tunapigia vyama na watu wanaoonekana, Uchaguzi wa Kura ya Maoni tutakuwa tunapigia swalii kwa kuandika unakubaliana na rasimu hiyo **Ndiyo** au hukubaliani **Hapana**. Hakuna mtu atakayeonekana wala chama kitakachoonekana.

Campaign zitafanywa na makundi yaliyosajiliwa ya taasisi kama sheria zilivyoainisha. Hiyo ndiyo tofauti kubwa. Lakini taratibu zingine za Uchaguzi zinafanana sana na ndiyo usimamizi utafanywa na Tume hizi za Uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ninaliomba Bunge lako Tukufu liujadili Muswada wa Kura ya Maoni na kutoa ridhaa kwa Muswada huo kusomwa Bungeni kwa mara ya tatu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofii*)

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:
Mheshimiwa Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

**MHE. PINDI H. CHANA - MWENYEKITI KAMATI YA KATIBA,
SHERIA NA UTAWALA:** Mheshimiwa Spika, kwa idhini yako naomba kutoa maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge kuhusu Muswada wa Sheria ya Kura ya Maoni mwaka 2013 (*The Referendum Act, 2013*).

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa kanuni ya 86 (5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Aprili, 2013, naomba kuwasilisha Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu Muswada wa Sheria ya Kura ya Maoni, 2013 (*The Referendum Act, 2013*).

Mheshimiwa Spika, Kamati ilikutana na Mheshimiwa William V. Lukuvi - Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Uratibu na Bunge) pamoja na Mheshimiwa Jaji Frederick M. Werema - Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa mara ya kwanza ili kupokea maelezo kuhusu Muswada husika mnamo tarehe 05 Agosti, 2013 katika Ofisi Ndogo ya Bunge, Dar es Salaam.

Katika maelezo yake, Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Uratibu na Bunge) alifieleza Kamati kuwa Muswada wa Sheria ya Kura ya Maoni, 2013 unakusudia kuweka muundo wa kisheria na kitaasisi kwa ajili ya uendeshajii wa Kura ya Maoni, kuweka masuala ambayo maoni ya wananchi yatahakikiwa kuitia Kura ya Maoni na kuweka masuala mengine yanayohusiana.

Mheshimiwa Spika, baada ya kupokea maelezo ya Waziri wa Nchi, Kamati ilialika wadau mbalimbali kwa mujibu wa kanuni ya 84 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Aprili, 2013 ili kupata maoni yao kuhusu mapendekezo ya Muswada katika ibara mbalimbali kwa lengo la kuisaidia Kamati katika uchambuzi.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru wadau wote ambao waliwasilisha maoni yao mbele ya Kamati kwa mdomo na kwa maandishi wakiwemo Chama Cha Wanasheria Tanganyika (*TLS*), *Tanzania Women Lawyers Association (TAWLA)*, Vyama vya Siasa, Taasisi za Dini,

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. PINDI H. CHANA - MWENYEKITI KAMATI YA
KATIBA, SHERIA NA UTAWALAJ]

Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Chuo Kikuu Huria na wengine. Maoni, michango na maelezo ya ufanuzi yaliyotolewa mbele ya Kamati yamesaidia kwa kiasi kikubwa kuuboresha Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, Wajumbe wa Kamati walipata nafasi ya kuujadili na kuuchambua Muswada huu katika ibara zote pamoja na majedwali yake. Kipekee napenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati kwa umakini mkubwa, uvumilivu na weledi wa hali ya juu katika kutoa maoni yao kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, awali, madhumuni ya jumla kuhusu Muswada huu yalikuwa ni kutoa hoja ya kutungwa kwa Sheria ya Kura ya Maoni kwa ajili ya kuongoza mchakato wa kupata na kuhakikisha maoni ya wananchi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania juu ya masuala mbalimbali yenye maslahi kwa umma yanachukuliwa kila inapohitajika kama njia mahsusii ya kuwashirikisha watu.

Hata hivyo, kwa kuzingatia ukweli kwamba, suala la kutunga Sheria ya Kura ya Maoni lilianzia wakati mchakato wa kutungwa kwa Sheria ya Mabadiliko ya Katiba na kisha kuwekwa katika Sheria hiyo kama nyenzo ya kuhalalisha Katiba inayopendekezwa, Kamati iliishauri Serikali kubadilisha madhumuni na sababu za Muswada unaopendekezwa ili ujikite katika suala la kukusanya maoni kuhusu Katiba Mpya peke yake, na siyo masuala mengine yanayohitaji Kura ya Maoni kama Muswada ulivyopendekeza awali.

Mheshimiwa Spika, ushauri huu wa Kamati ultokana na sababu mbalimbali, zikiwemo sababu za ugumu wa utekelezaji endapo Muswada ungepitishwa kuwa sheria. Kamati imeona kuwa kwa kuwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar inayo Sheria yake kuhusu Kura ya Maoni, ni vyema Muswada huu ukajikita katika uhalalishwaji wa Katiba inayopendekezwa tu.

Mheshimiwa, napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba Serikali imelifanyia kazi pendeleko la Kamati na

Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)

[MHE. PINDI H. CHANA - MWENYEKITI KAMATI YA
KATIBA, SHERIA NA UTAWALA]

imefanya marekebisho makubwa katika Muswada huu kwa kuuchapa upya ili kukidhi maudhui yaliyopendekezwa na Kamati. Hivyo, Jina Refu la Muswada limebadilika kuendana na madhumuni ya Muswada. Kwa sababu hiyo, Ibara ya (3) inayohusu Matumizi pia imebadilika ili kuweka sharti la kwamba Sheria inayopendekezwa itatumika Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar kuhusiana na Kura ya Maoni kwa ajili ya kuhalalisha Katiba Inayoependekezwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati imechambua kwa kina ibara kwa ibara katika Muswada wa Sheria ya Kura ya Maoni (*The Referendum Act, 2013*) na kubaini kwamba baadhi ya ibara hazina matatizo yoyote. Katika uchambuzi na maoni ya Kamati baadhi ya ibara hazitajitokeza, bali Kamati itajikita zaidi kuchambua na kushauri katika Ibara zile zinazohitaji kuziboresha zaidi. Ibara hizo ambazo hazitajitokeza katika uchambuzi wa maoni ya Kamati ni kama zifuatazo:- 1, 2, 5, 8, 11, 12, 13, 14, 16, 17, 21, 25, 29, 30, 31, 37, 38, 39, 41, 42, 43, 47, 49 na 51.

Mheshimiwa Spika, ibara ya 3 inatoa Tafsiri katika maneno mbalimbali ambayo yametumika katika Muswada. Kamati ilimshauri Waziri wa Nchi, kuongeza baadhi ya maneno ambayo awali hayakuwa yametolewa tafsiri pamoja na kufanya marekebisho ya msingi katika baadhi ya maneno ili kuondoa utata katika matumizi yake.

Aidha, katika eneo la tafsiri, kulikuwa na mjadala mrefu kuhusiana na tafsiri ya maneno "Kura ya Maoni". Hata hivyo, baada ya Wajumbe kulitafakari suala hili kwa kina, walikubaliana kwamba tafsiri iliyotumika katika Muswada kama ulivyochapwa upya inajitosheleza kwa madhumuni ya utekelezaji wa Sheria inayopendekezwa.

Mheshimiwa Spika, tafsiri ya neno "Tume" kama ambavyo limetumika katika ibara hii na Muswada kwa ujumla, linamaanisha "Tume ya Taifa ya Uchaguzi na Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar". Kamati ilitafakari pendekezo hilo, na ikaamua kwamba, neno "Tume" kama ambavyo tafsiri inavyosomeka, libaki kama liliyvo kwa sababu neno hilo

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. PINDI H. CHANA - MWENYEKITI KAMATI YA
KATIBA, SHERIA NA UTAWALA]

linajumuisha Tume mbili zilizoundwa kwa masharti ya Katiba na Sheria zilizopo hivyo matumizi yanayopendekezwa hayatakuwa halisi kwa msingi huo.

Mheshimiwa Spika, ibara ya (4) ya Muswada inazungumzia kuhusu Mamlaka ya kuitisha Kura ya Maoni ambapo awali Muswada ulipendekeza kwamba Rais, pale anapoona inafaa, anaweza kuielekeza Tume kuendesha Kura ya Maoni kuhusu swalilolote kwa amri itakayochapishwa katika *Gazeti la Serikali*.

Katika Ibara hii ya (4), kulikuwa na maoni mbalimbali. Baada ya Wajumbe wa Kamati kulitafakari pendekezo hili kwa kuzingatia pia maoni yaliyotolewa, Kamati iliishauri Serikali kwamba Mamlaka ya kuitisha Kura ya Maoni yabaki kwa Rais isipokuwa, yasiwe katika suala lolote bali kwa madhumuni yanayopendekezwa katika Muswada huu, iwe katika Kura ya Maoni kuhusu Katiba Mpya.

Mheshimiwa Spika, napenda kulitaarifu Bunge lako kuwa pendekezo hilo limefanyiwa kazi na Serikali kwa kuweka sharti jipya kwamba Mheshimiwa Rais, baada ya kushauriana na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na baada ya kupokea Katiba inayopendekezwa, kwa amri itakayochapishwa katika *Gazeti la Serikali*, ataielekeza Tume kuendesha Kura ya Maoni kuhusiana na Katiba Inayopendekezwa.

Mheshimiwa Spika, katika ibara ya (7) Kamati inashauri kuwa Wasimamizi wanaotajwa hapa wajulikane kama "Wasimamizi wa Kura ya Maoni" badala ya "Wasimamizi wa Uchaguzi" kama ilivyo sasa ili kuondoa mkanganyiko unaoweza kujitokeza. Marekebisho haya yafanyike katika ibara zote za Muswada ambazo watu hawa wametajwa.

Aidha, Kamati ilipendekeza kuwa sifa za watu hawa watakaoteuliwa na Tume ziwekwe bayana kwa madhumuni ya uteuzi huo. Serikali imeahidi kulitekeleza suala hilo kwa Tume kuandaa Kanuni ambazo pendekezo hilo la Kamati litashughulikiwa kikamilifu.

Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)

[MHE. PINDI H. CHANA - MWENYEKITI KAMATI YA
KATIBA, SHERIA NA UTAWALA]

Mheshimiwa Spika, ibara ya (9) ya Muswada inazungumzia haki ya kupiga kura na ushahidi wa utambulisho. Katika eneo hili kulikuwa na mjadala mpana hasa kuhusu suala zima la maboresho ya Daftari la Wapiga Kura. Kimsingi, Kamati inaishauri Serikali iboreshe Daftari hilo kwa haraka iwezekanavyo ili kuweza kuwajumuisha Watanzania wote wenye haki ya kupiga kura kushiriki zoezi la Kura ya Maoni.

Mheshimiwa Spika, katika ibara ya 10 inayohusu maeneo ya kupigia kura na vituo vya kupigia kura, Kamati inashauri kuwa Muswada uweke masharti kwamba Majimbo yaliyokuwa yametangazwa na kutumika katika Uchaguzi Mkuu uliofanyika kabla ya Kura ya Maoni kupigwa yawe ndiyo Majimbo ya Uchaguzi kwa ajili ya Kura ya Maoni na kwamba, vituo vipya vitakavyokuwa vimetangazwa na vituo viliviyokuwa vimetangazwa na kutumika katika Uchaguzi Mkuu uliofanyika kabla ya Kura ya Maoni kupigwa ndiyo viwe Vituo vya Uchaguzi kwa ajili ya Kura ya Maoni.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapendekeza kuwa katika ibara ya 15 (2), baada ya neno "ataapa" yaongezwe maneno "au atathibitisha" ili kujumuisha watu wanaoamini dini ya Kiislam.

Mheshimiwa Spika, katika ibara ya 18 inayohusu vifaa vya Vituo vya Kupigia Kura ya Maoni, Kamati ilipendekeza kuwa, Msimamizi anayetajwa atatekeleza masharti ya ibara ya 18 (1) kwa kadri ya mahitaji ya eneo linalohusika na siyo kwa kadri atakavyoona inafaa ili kutoruhusu matumizi mabaya ya madaraka. Serikali ililichukua suala hili na kilifanya kazi kama ambavyo Muswada uliochapwa upya unavyoonesha.

Mheshimiwa Spika, ibara ya 19 inahusu masharti ya kuingia katika Vituo vya Kupigia Kura ambapo inampa Afisa wa Kura ya Maoni mamlaka ya kusimamia idadi ya wapiga kura watakaoingia katika Kituo cha Kupigia Kura kwa wakati mmoja au kuzuia watu wengine wote, isipokuwa wale waliokuja wametajwa katika ibara ndogo ya (1). Kamati

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. PINDI H. CHANA - MWENYEKITI KAMATI YA
KATIBA, SHERIA NA UTAWALAJ]

ilipendekeza kuwa baada ya neno "maafisa" yaongezwe maneno "wa Tume" ili iainishe kuwa ni Makamishna na Maafisa wa Tume ambao ni mionganini mwa watu ambao hawatazuiwa kuingia katika Kituo cha Kupigia Kura. Pendekazo hili pia limefanyiwa kazi na Serikali.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 20 inaweka utaratibu wa udhibiti wa fujo katika vituo vya kupigia kura katika mchakato mzima wa upigaji wa Kura ya Maoni.

Ibara ya 20(2) inampa mamlaka Afisa wa Kura ya Maoni kutoa amri ya kutawanyika kwa kundi la watu ambalo kwa maoni ya Afisa wa Kura ya Maoni, kundi hilo linazua uingiaji kirahisi wa wapiga kura katika Kituo cha Kupigia Kura au kutoka au kinawatisha wapiga kura ili kuhakikisha kuwa wapiga kura wanakuwa huru wakati wa zoezi hilo. Kamati inaipongeza Serikali kwa kutambua kuwa kunaweza kujitokeza mazingira ya kuhatarisha uendeshaji wa zoezi la upigaji wa Kura ya Maoni, hivyo ni muhimu yaweze kudhibitiwa kwa masharti yaliyowekwa katika ibara hii ya 20.

Mheshimiwa Spika, katika ibara ya 22 Kamati ina maoni kwamba ibara ndogo (2) isomeke kama ifuatavyo:-

"kifungu kidogo cha (1) hakitatafsiriwa kuwa kinamzuia mtu anayemsindikiza mtu asiemeona au mtu asijejua kusoma na kuandika ."

Mheshimiwa Spika, katika ibara ya 23 inayohusu kufungwa kwa sanduku za kupigia kura, kamati inapendekeza katika ibara ndogo ya (5) kuwa watakaohusika na zoezi hili wave ni Mawakala waliosajiliwa na Tume ili kuepuka fujo na mtafaruku wakati wa kukagua karatasi kwa mujibu wa ibara hii.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 24 ya Muswada inahu uandaaji wa karatasi za kupigia kura kwa kuonesha muundo, alama zitakavyokuwa nazo na jinsi zitakavyoonekana. Ibara ndogo ya (4) inapendekeza kuwa wakati wa uandaaji wa Swali la kuwaauliza wananchi kama wanaikubali au

Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)

[MHE. PINDI H. CHANA - MWENYEKITI KAMATI YA
KATIBA, SHERIA NA UTAWALA]

wanaikataa Katiba inayopendekezwa, Tume ya Taifa ya Uchaguzi na Tume ya Uchaguzi Zanzibar zishauriane na Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Kamati imetafakari kwa makini sharti hili na kuona kuwa suala la uandaaji wa swali liachwe kwa Tume ili kulinda dhana ya uhuru wa Tume Katika utekelezaji wa majukumu yake. Endapo kifungu hiki kitabaki kama kilivyo, kinaweza kuondoa dhana ya Uhuru wa Tume na kuleta hisia kwa baadhi ya makundi ya Kijamii kuwa Serikali inaiingilia Tume na hivyo kuondoa imani kwa Tume juu ya Mchakato mzima wa uhalalishaji wa Katiba inayopendekezwa.

Aidha, kamati inashauri kwamba, kwa kuwa maoni ya wananchi juu ya kuikubali au kuikataa Katiba inayopendekezwa ndiyo uamuzi wa mwisho, neno "kuhahakikiwa" katika ibara ndogo ya (4) ni vyema likaondolewa na badala yake liwekwe neno "kuamuliwa".

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 26 inaweka taratibu za kufuatwa kwa wapiga kura wanaohitaji msaada. Uwepo wa Ibara hii ni muhimu sana kwani umezingatia mahitaji ya watu wenye mahitaji maalumu na ambao kwa namna moja au nydingine wanaweza kuhitaji msaada wakati wa upigaji wa kura kama walemavu wa aina mbalimbali. Pamoja na umuhimu mkubwa wa kifungu hiki, Kamati inapendekeza kufutwa kwa ibara ndogo ya (3) kwani inaweka sharti kwamba mpiga kura anayehitaji msaada ni lazima asaidiwe na mtu aliyefikia umri wa utu uzima.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaona kwamba mpiga kura mwenye uhitaji wa kusaidiwa aachiwe achague mtu anayemwamini kwani kwa mazingira ya sasa mtoto wa umri kuanzia miaka kumi anaweza kutoa msaada unaohitajika kwa minajili ya ibara hii. Kufutwa ibara hii kunafanya uwepo wa ibara ndogo ya (5) kutokuwa na umuhimu wowote kwani uwepo wake ulikuwa unategemea uwepo wa ibara ya (3) hivyo Kamati inashauri kifungu hiki nacho kifutwe na vifungu vilivyobaki vipangiliwe upya.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. PINDI H. CHANA - MWENYEKITI KAMATI YA
KATIBA, SHERIA NA UTAWALAJ]

Mheshimiwa Spika, ibara ya 27 ya Muswada inaweka utaratibu wa kufuatwa na kuzingatiwa na Afisa wa Kura ya Maoni wakati wa kufungwa kwa Kituo cha Kupigia Kura. Ibara ya 27(1) (c) inamtaka Afisa wa Kura ya Maoni kuandika maelezo kuhusu idadi ya kura zilizoharibika. Kwa kuwa ushirikishaji wa mawakala unafanyika kwa lengo la kuhakikisha kwamba utaratibu mzima wa ufungwaji wa Kituo cha Kupigia Kura unafuatwa, ni vyema ushuhudiaji wa kutengwa kwa kura zilizoharibika, nakala ya daftari liliowekwa alama, vishina vya karatasi za kupigia kura zilizotumika ukafanyika kabla ya Afisa wa Kura ya Maoni hajatoa maelezo kuhusu mambo yaliyopo katika ibara ya 27(1) ili kutoa nafasi kwa mawakala kushuhudia zoezi lote la ufungwaji wa Kituo na kisha uandikaji wa maelezo ukafuatia.

Mheshimiwa Spika, Katika Ibara ya 28(4) Kamati inashauri kufutwa kwa maneno "itawapokea" yaliyopo katikati ya maneno "Tume" na "Waangalizi" na pia kufutwa kwa maneno "na wawakilishi wa vyombo vya habari" na badala yake kukiandika upya ili kisomeke "Tume itawaruhusu waangalizi waliodhinishwa au kutambulika na Tume kuhudhuria mwenendo wa kuhesabu kura." Kamati inaona ibara hii ikiandikwa kwa namna ambayo Kamati imeshauri kitasomeka vizuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 32 inaweka utaratibu wa kutoa matokeo ya Kura ya Maoni katika ngazi ya Majimbo. Utaratibu huu umeelezwa kwamba matokeo katika ngazi yatatatangazwa na Msimazizi wa Uchaguzi ngazi ya Jimbo na yatajazwa katika Fomu Namba 6 na 7 zilizoko katika Jedwali la kwanza la kanuni.

Katika ibara hii Kamati inashauri kwamba neno "Msimamizi wa Uchaguzi" lifutwe na badala yake liwekwe neno "Msimamizi wa Kura ya Maoni". Aidha, Kamati inashauri kufutwa kwa maneno "kukataliwa" "zinazounga mkono" na "zinazopinga" yaliyoko kwenye jedwali na badala yake yawekwe maneno kura ya "Ndiyo" au "Hapana" ili kuondoa mkanganyiko wa kutumika kwa maneno ya aina nyingi yanayomaanisha jambo la aina moja.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. PINDI H. CHANA - MWENYEKITI KAMATI YA
KATIBA, SHERIA NA UTAWALA]

Mheshimiwa Spika, ibara ya 33(2) ya Muswada inaweka masharti ya uhesabuji wa kura zilizopigwa katika Kura ya Maoni. Muswada unapendekeza kuwa kura zitangazwe ndani ya masaa 72 toka kufungwa kwa Vituo vya Kupigia Kura. Kamati ina maoni kwamba masharti haya ni mazuri kwa kuwa yatawezesha wananchi kujuua mapema matokeo ya tukio lao kubwa la kidemokrasia la kuamua kuhusu hatima ya Katiba yao mpya ya nchi.

Mheshimiwa Spika, kutokana na umuhimu wa kupata matokeo mapema ndani ya masaa 72, Kamati inaishauri Serikali kuandaa vifaa vya kisasa na kuwajengea uwezo Watendaji wa Tume zote mbili ili waweze kumudu usimamizi wa mchakato wa upigaji wa Kura ya Maoni kwa weledi na umahiri wa hali ya juu na pia kwa kutambua kuwa nchi yetu kijografia ni kubwa, hivyo masaa yaliyotajwa yanahitaji kufanyiwa kazi kwa juhudi ya hali ya juu.

Mheshimiwa Spika, ibara ya 34 ya Muswada inatoa masharti kuhusiana na matokeo ya Kura ya Maoni. Kwa mujibu wa ibara hii, matokeo ya Kura ya Maoni yataamuliwa kwa kigezo cha asilimia 50 ya kura halali zilizopigwa za kuunga mkono.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swalii la Kura ya Maoni kwa pande zote mbili za Muungano; ibara ya 34(2) inaweka sharti kwamba wingi wa kura halali zilizopigwa katika swalii la Kura ya Maoni ndiyo utakaoamua kuhusu kukubalika au kutokubalika kwa Katiba inayopendekezwa. Aidha, matokeo ya Kura ya Maoni yataheshimiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Kamati inaunga mkono masharti haya kwa kuwa maamuzi ya wananchi ndiyo maamuzi ya mwisho kuhusu jambo kubwa na nyeti kama la Katiba na ni mojawapo ya misingi wa demokrasia kuheshimu jambo ambalo wananchi wamelitolea maamuzi kuititia upigaji kura.

Mheshimiwa Spika, ibara ya 35 inaweka sharti la kutumika kwa Daftari la Kudumu la Mpiga kura Tanzania Bara

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

*[MHE. PINDI H. CHANA - MWENYEKITI KAMATI YA
KATIBA, SHERIA NA UTAWALA]*

na Daftari la Kudumu la Mpiga kura Zanzibar katika zoezi la upigaji wa Kura ya Maoni baada ya kufanyiwa maboresho muhimu. Aidha, Kamati imefahamishwa kwamba Daftari la Kudumu la Mpiga kura Zanzibar limekwishaanza kuboreshwa na uboreshaji huo unakaribia kwisha. Kamati inashauri Kwamba Daftari la Kudumu la Mpiga kura Tanzania Bara nalo lianzesha kuboreshwa kwani kuna vijana wengi waliofikisha umri wa kupiga kura lakini bado hawajaandikishwa. Pia wapo waliofariki au kuhama, hivyo ni bora likaboreshwa ili kuwapa fursa watu wote wenye sifa na haki ya kupiga kura.

Mheshimiwa Spika, katika ibara ya 36 inaweka masharti maalum kwa ajili ya upigaji wa Kura ya Maoni katika mazingira maalum. Kamati inaona kwamba, katika mazingira ya Raia wa Tanzania walioko nje ya nchi, utekelezaji wa masharti yanayopatikana katika ibara hii utakuwa mgumu kwa sababu hiyo masharti kuhusu raia hao yafutwe.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu wa suala hili nyeti la upigaji wa Kura ya Maoni, Muswada umeweka masharti ya kuruhusu uwepo wa waangalizi wa zoezi la Kura ya Maoni. Sharti hili limebainishwa katika Ibara ya 37 ya Muswada huu. Waangalizi hawa wanapaswa kujianidikisha katika Tume ili waweze kutambuliwa. Lengo la kujianidikisha ni kuwatambua na kuhakikisha kuwa hawaegemei upande wowote, bali wanatimiza wajibu wao wa kuangalia zoezi zima la upigaji wa Kura ya Maoni kama limefuata sheria, kanuni na taratibu zilizopo.

Mheshimiwa Spika, ibara ya 40 ya Muswada inahu su Fedha za kugharamia zoezi la Kura ya Maoni na pia kwamba zitataki katika Mfuko Mkuu wa Hazina. Kamati inashauri kwamba fedha hizo zitolewe mapema kwa Tume za Uchaguzi ili kuziwezesha kufanya maandalizi mapema na hatimaye kufanikisha zoezi la Kura ya Maoni.

Mheshimiwa Spika, katika ibara ya 44 inahu su uamu ziwa malalamiko ya Mahakama, Kamati inapendekeza kwamba ibara ndogo ya (1) ifanyiwe marekebisho ili malalamiko haya yawasilishwe katika Mahakama Kuu

Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)

[MHE. PINDI H. CHANA - MWENYEKITI KAMATI YA
KATIBA, SHERIA NA UTAWALA]

badala ya Mahakama Maalum kama Muswada unavyopendekeza.

Mheshimwa Spika, ibara ya 45 inaweka masharti kwa Kamati ya Kura ya Maoni ambayo haikuridhika na maamuzi ya Mahakama ya chini, kuwasilisha rufaa yake ndani ya siku tano toka tarehe iliyopata nakala ya hukumu. Kamati inashauri kwamba, muda wa kukata rufaa uwe siku saba badala ya siku tano zilizopendekezwa katika Muswada.

Mheshimiwa Spika, katika ibara ya 46, kwa madhumuni ya kifasihi, Kamati inapendekeza katika ibara ndogo ya (2) mstari wa kwanza, baada ya maneno "kifungu kidogo cha (1)" lionezwe neno "atakuwa". Kamati imeshauri hivyo ili kuifanya ibara hii isomeke vizuri na kueleweka kirahisi.

Mheshimiwa Spika, ibara ya 50 ya Muswada inahusu Matumizi ya Sheria nyingine. Katika ibara ndogo ya (2) ambayo inaweka sharti kwamba Sheria ya Kura ya Maoni itatumika endapo kutatokea mgongano na Sheria ya Uchaguzi, Kamati ina maoni kwamba, badala ya kutumika maneno "Sheria ya Uchaguzi" yatumike maneno "Sheria za Uchaguzi" ili kutambua matumizi ya Sheria zote mbili yaani Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 342 na Sheria ya Uchaguzi Zanzibar, Sura ya 278.

Mheshimiwa Spika, katika Muswada huu, kuna majedwali mbalimbali ambayo yatakuwa sehemu ya Sheria inayopendekezwa. Kamati inashauri kwamba majedwali yote yanayoambatana na Muswada huu, yawekwe katika Kanuni zitakazotungwa na Waziri mwenye dhamana kwa madhumuni ya utekelezaji wa Sheria inayopendekezwa.

Mheshimiwa Spika, hitimisho. Nachukua fursa hii kuipongeza Serikali kwa kuja na Muswada huu ambao unajenga msingi wa kupata maoni ya wananchi katika kuamua mustakabali wa masuala yanayowahusu wananchi kuititia Katiba inayopendekezwa. Kipekee namshukuru Waziri Mkuu - Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda; Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Uratibu na Bunge) -

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. PINDI H. CHANA - MWENYEKITI KAMATI YA
KATIBA, SHERIA NA UTAWALA]

Mheshimiwa William V. Lukuvi akishirikiana kwa karibu na Mwanasheria Mkuu wa Serikali - Mheshimiwa Jaji Frederick Mwita Werema (Mb) pamoja na watendaji wote wa Ofisi ya Waziri Mkuu na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kwa kazi kubwa ya kuandaa Muswada huu pamoja na marekebisho kwa maelekezo ya Kamati yangu ya Katiba, Sheria na Utawala. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii vilevile, kuwashukuru sana Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala kwa kuchambua kikamilifu maoni yaliyowasilishwa na wadau kuhusu Muswada huu na kuchambua Muswada wenyewe ibara kwa ibara pamoja na maudhui yake kikamilifu. Nawashukuru kwa ushirikiano wao na maoni yao ambayo yamefanikisha kuuboresha Muswada huu pamoja na taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, kwa heshima na taadhima, naomba kuwatambua Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Pindi Hazara Chana - Mwenyezekiti Mheshimiwa William Mganga Ngeleja, - Makamu Mwenyezekiti, Mheshimiwa Gosbert Begumisa Blandes, Mheshimiwa Abbas Zuberi Mtemu, Mheshimiwa Nimrod Elirehema Mkono, Mheshimiwa Felix Francis Mkosamali, Mheshimiwa Nyambari Chacha Mariba Nyangwine, Mheshimiwa Fakharia Shomari Khamis, Mheshimiwa Rukia Kassim Ahmed, Mheshimiwa Jaku Hashim Ayoub, Mheshimiwa Mustapha Boay Akunaay, Mheshimiwa Ramadhan Haji Saleh, Mheshimiwa Jasson Samson Rwekiza, Mheshimiwa Tundu Antiphas Mughway Lissu, Mheshimiwa Deogratias Aloyce Ntukamazina, Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mheshimiwa Mariam Reuben Kasembe, Mheshimiwa Abdallah Sharia Ameir, Mheshimiwa Halima James Mdee na Mheshimiwa Zahra Ali Hamad. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mwisho lakini si kwa umuhimu, niwashukuru sana Watendaji wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi wa Katibu wa Bunge, Dkt. Thomas D. Kashilillah, kwa

Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)

[MHE. PINDI H. CHANA - MWENYEKITI KAMATI YA
KATIBA, SHERIA NA UTAWALA]

kuihudumia Kamati kikamilifu hadi kuandaliwa kwa taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana. Nilikuwa nimepata hofu kwamba Kiongozi wa Kambi ya Upinzani simwoni na saa zinapita, lakini sasa nimemwona, naomba utoe maoni ya Kambi ya Upinzani.

MHE. TUNDU A. M. LISSU - MSEMAJI WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA SHERIA NA KATIBA: Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru kwa kunipa fursa kwa mara nyine tena kuwasilisha maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu Wizara ya Sheria na Katiba juu ya Muswada wa Sheria ya Kura ya Maoni ya mwaka 2013 na ninaomba kufanya hivyo kwa mujibu wa Kanuni ya 86(6) ya Kanuni za Kudumu za Bunge lako Tukufu za mwaka 2003.

Mheshimiwa Spika, Muswada wa Sheria ya Kura ya Maoni (*The Referendum Act*), 2013, ulichapishwa katika *Gazeti la Serikal* la tarehe 7 Juni, 2013 na kusomwa kwa mara ya kwanza katika Mkutano wa Kumi na Moja wa Bunge lako Tukufu. Endapo Bunge lako Tukufu litaupitisha Muswada huu kuwa sheria, itakuwa ni mara ya kwanza kwa nchi yetu kuwa na utaratibu wa Kura ya Maoni katika sheria zetu za Muungano. Hii ni kwa sababu, Zanzibar siyo tu ina Katiba inayotambua Kura ya Maoni kama mojawapo ya njia rasmi za kufanya maamuzi makubwa ya kikatiba, bali pia inayo Sheria ya Kura ya Maoni inayoweka utaratibu wa namna ya kuendesha na kusimamia kura hiyo. Kwa sababu hiyo, Muswada huu ni wa kihistoria; na pengine kwa sababu hiyo, Muswada huu una mapendekezo mengi yenye kuibua masuala mazito ya kikatiba na ya kisheria.

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala yameonyesha, Muswada huu umejadiliwa kwa kirefu na Kamati, Serikali na wadau mbalimbali wa nje ya Serikali na

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. TUNDU A. M. LISSU - MSEMAJI WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA SHERIA NA KATIBAJ]

Bunge. Kwa sababu ya majadiliano hayo, Muswada umefanyiwa marekebisho makubwa na muhimu. Kwanza, aya ya 4(1) na (2) ya Muswada wa mwanzo ilikuwa inapendekeza Rais apewe mamlaka ya kuitisha Kura ya Maoni juu ya jambo lolote ikiwa ni pamoja na Mambo ya Muungano. Mapendekezo hayo yalikuwa yanazua maswali mengi na magumu ya kikatiba.

Sasa, kufuatia majadiliano kati ya Kamati, Serikali na wadau, aya mpya ya 4(1) inapendekeza kwamba Muswada huu utahusu Kura ya Maoni kwa ajili ya kuhalalisha Katiba Mpya peke yake. Kwa sababu ya marekebisho haya, hata tafsiri ya 'Kura ya Maoni' imebadilika kuwa "kura iliyopigwa kwa madhumuni ya kupata uamuzi wa wananchi juu ya Katiba inayopendekezwa." Tafsiri ya mwanzo ilikuwa inatafsiri Kura ya Maoni kuwa ni kura inayopigwa ili "kuhakikisha maoni ya wananchi juu ya swali lolote au suala lolote."

Pili, Kura ya Maoni na mambo ya Muungano. Aya ya (2) ya Muswada ilikuwa inatamka kwamba Sheria hii "itatumika Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar kuhusu Mambo ya Muungano." Aidha, aya ya 4(2) ilikuwa inapendekeza masuala yanayohusiana na 'mambo ya Muungano' yathibitishwe kwa Kura ya Maoni. Kama mapendekezo haya yangepitishwa na kuwa sheria, yangeweza kusababisha mgogoro mkubwa wa kikatiba na wa kislasa kati ya Serikali Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa sababu yangekuwa yanakiuka sehemu kadhaa za Katiba ya Jamhuri ya Muungano na Hati za Muungano kwa vile 'Kura ya Maoni' siyo mojawapo ya Mambo ya Muungano.

Sasa, Muswada umeepuka uwezekano wa mgogoro huo kwa kuweka wazi kwamba "Sheria hii itatumika Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar kuhusiana na Kura ya Maoni kwa ajili ya kuthibitisha Katiba inayopendekezwa." Kwa vile 'Katiba ya Jamhuri ya Muungano' nijambo la kwanza katika Orodha ya Mambo ya Muungano yaliyoko kwenye Nyongeza ya Kwanza ya Katiba, marekebisho haya yako ndani ya matakwa ya ibara za 4(2) na (3), 64(2), (3) na (4), 102(1) na

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. TUNDU A. M. LISSU - MSEMAJI WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA SHERIA NA KATIBA]

106(1) za Katiba juu ya, pamoja na mambo mengine (*inter alia*), mamlaka ya Bunge lako Tukufu kutunga sheria kwa ajili ya mambo ya Muungano na yasiyo ya Muungano yanayohusu Zanzibar.

Kamati ilifaidika sana ushauri wa Profesa Gamaliel Mgongo Fimbo, mwanazuoni maarufu na wa siku nyingi wa Shule ya Sheria ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, wakati alipotoa maoni yake kwa Kamati juu ya jambo hili tarehe 11 Agosti, 2013. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaanmini kwamba Ukumbi huu wa Bunge lako Tukufu ni mahali pazuri pa kumpongeza na kumshukuru Profesa Mgongo Fimbo kwa ushauri wake huu kwa Bunge, na kwa utumishi wake uliotukuka kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, eneo la tatu ambalo limefanyiwa marekebisho na kuboreshwa zaldi linahusu tafsiri ya maneno 'Kura ya Maoni' ambayo ndio hasa yanautambulisha Muswada wenyewe. Kama tulivyoonyesha hapa juu, tafsiri iliyokuwa kwenye Muswada wa mwanzo ilikuwa inaashiria kwamba Kura ya Maoni kwa mujibu wa Sheria ni kura ya kuhakikisha maoni ya wananchi. Hii haikuwa sawasawa.

Katika matumizi yake ya kawaida, maneno 'Kura ya Maoni' yametafsiriwa kuwa ni kura ya moja kwa moja (*direct vote*) ambapo wapiga kura wote wanaulizwa kama wanakubali au wanakataa jambo fulani. Kura ya Maoni ni aina ya demokrasia ya moja kwa moja (*direct democracy*) ambapo wananchi wenyewe wanaamua juu ya jambo fulani linalotakiwa kuamuliwa badala ya kutumia Wawakilishi wa kuchaguliwa au Serikali yenye kufanya maamuzi.

Kwa mtazamo huu, jina sahihi la utaratibu huu wa kufanya maamuzi ni kura ya uamuzi na sio Kura ya Maoni. Ndio maana *Sheria ya Kura ya Maoni, 2010*, ya Zanzibar imetafsiri maneno 'Kura ya Maoni' kuwa ni "mchakato wa kupeleka jambo au suala kwa wapiga kura kwa ajili ya uamuzi." Kwa upande Kenya, pamoja na ukweli kwamba Sheria ya Mabadiliko ya Katiba ya Kenya ya 2008 haikutafsiri kabisa maneno hayo, Kanuni za Kura ya Maoni ya Mabadiliko

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. TUNDU A. M. LISSU - MSEMAJI WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA SHERIA NA KATIBA]

ya Katiba ya Kenya, 2010, zilizotengenezwa na iliyokuwa Tume Huru ya Mpito ya Uchaguzi ya nchi hiyo zilitafsiri maneno 'Kura ya Maoni' kuwa ni "mchakato wa kuridhia Katiba Mpya ya Kenya inayopendekezwa."

Kwa kubadilisha tafsiri ya 'Kura ya Maoni' kuwa ni kura ya *uamuzi* juu ya Katiba inayopendekezwa, Muswada huu sasa utaenda sambamba na maana ya kawaida na ya kisheria ya maneno hayo kama yanavyotumiwa katika nchi nyingine. Aidha, tafsiri hii mpya imeondoa mkanganyiko uliokuwepo kati yake na aya za 34(4) na (5) na 41(1) na (3) za Muswada wa mwanzo juu ya Serikali kufungwa na matokeo ya Kura ya Maoni. Kwa sababu ya tafsiri mpya na sahihi ya 'Kura ya Maoni', aya hizo sasa zimefutwa.

Mheshimiwa Spika, eneo la nne la Muswada ambalo limerekebishwa kufuatia majadiliano ya Kamati, Serikali na wadau linahusu Sehemu ya Tatu ya Muswada inayopendekeza kuundwa kwa Kamati za Kura ya Maoni. Kama ilivyokuwa mwanzoni, aya ya 12(1) na (2) inalazimu kuanzishwa kwa Kamati mbili za Kura ya Maoni kwa kila Jimbo ambazo zitaundwa na makundi ya watu, vyama (vyasiasa), asasi za kiraia au asasi (kidini) zinazokusudia kuunga mkono au kupinga maswali ya Kura ya Maoni katika kipindi cha Kura ya Maoni. Hata hivyo, tofauti na Muswada wa mwanzo, aya ya 13(1) ya Muswada huu inatoa mwanya kwa Kamati hizi kuomba usajili kwa Tume ya Uchaguzi au kwa Msimamizi wa Kura ya Maoni madhumuni ya kuendesha kampeni Kura ya Maoni.

Mapendekezo haya ni mazuri kwani yataondoa usumbufu na gharama zisizokuwa za lazima endapo masharti ya kusajili Kamati katika Makao Makuu ya Tume yangebaki kama yalivyokuwa mwanzo. Ili kwenda sambamba na *spirit* ya aya ya 13(1), Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapendekeza marekebisho madogo kwa kuongeza maneno 'na Msimamizi wa Kura ya Maoni' mbele ya neno 'Tume' katika aya za 13(3)(c), (6), (7)(b), 14 na 17(2) ambazo bado zinaitaja Tume peke yake.

Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)

[MHE. TUNDU A. M. LISSU - MSEMAJI WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA SHERIA NA KATIBAJ]

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, mapendekezo yanayohusu Kamati za Kura ya Maoni bado yana walakini. Kwa mujibu wa aya ya 13(6) ya Muswada, Tume inaweza kukubali au kukataa maombi ya usajili wa Kamati ya Kura maoni kwa sababu zilizotajwa katika aya ndogo ya (7), yaani kama jina la Kamati linafanana na Kamati iliyokwishesajiliwa awali, na kama "Tume haitaridhishwa kuwa mwombaji anawakilisha vya kutosha wale wanaofanya kampeni kwa ajili ya matokeo fulani."

Mapendekezo haya yanakinzana na mapendekezo ya kuwa na Kamati mbili katika kila Jimbo chini ya aya ya 12. Hii ni kwa sababu kama uamuzi wa Kura ya Maoni ni 'Ndiyo' au 'Hapana', Kamati zitakazotakiwa kusajiliwa ni Kamati za kukubali au kupinga swali la Kura ya Maoni. Hii maana yake ni kwamba wale wote wanaotaka kupinga swali hilo watasajiliwa katika Kamati ya 'Hapana', wakati wale wote wanaokubali swali la Kura ya Maoni watasajiliwa katika Kamati ya 'Ndiyo.' Kwa sababu hiyo, hakuna msingi wowote wa kukataa kusajili Kamati yoyote ya Kura ya Maoni.

Ili kurahisisha usajili na utendaji wa Kamati hizo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapendekeza kuwe na Masjala mbili au hata mafaili mawili. Masjala au faili la kwanza litatumika kusajili taasisi zote zinazotaka kuunga mkono swali la Kura ya Maoni, wakati masjala au faili la pili litatumika kusajili taasisi zote zinazotaka kupinga swali la Kura ya Maoni.

Baada ya taasisi hizi kusajiliwa na Tume na ili kurahisisha utendaji wao wa kazi, inapendekezwa kwamba taasisi ziunde Kamati ya pamoja ya Kura ya Maoni kwa kila upande wa swali la Kura ya Maoni. Kwa maana nyingine, taasisi zote zinazopinga swali la Kura ya Maoni, zitaungana katika Kamati moja na vivyo hivyo kwa taasisi zote zinazounga mkono swali la Kura ya Maoni. Kwa kufanya hivyo, hakutakuwa tena na sababu ya aya ya 13(7).

Mheshimiwa Spika, eneo la tano ambalo limefanyiwa ukarabati mkubwa linahusu muda wa kutoa elimu ya uraia na uhamasishaji kuhusu Katiba Mpya, na kipindi cha kampeni

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. TUNDU A. M. LISSU - MSEMAJI WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA SHERIA NA KATIBA]

za kuunga mkono au kupinga Katiba Mpya. Muswada wa mwanzo haukuainisha kipindi cha kampeni za Kura ya Maoni. Hata hivyo, kwa kuangalia tafsiri ya maneno 'kipindi cha Kura ya Maoni' kama kilivyokuwa kwenye Muswada huo na kukioanisha na zilizokuwa aya za 37(1) na 38(1) na (2), ni dhahiri kwamba kipindi cha Kura ya Maoni kilichokuwa kinapendekezwa mwanzoni kilikuwa angalau siku 45.

Zaidi ya hayo, Muswada ulikuwa unapendekeza muda wa ziada wa kampeni wa siku 60 endapo wapiga kura wataikataa Katiba inayopendekezwa. Tume ilikuwa inaweza pia kuongeza muda wa kutosha kwa ajili ya uhamasishaji na kutoa elimu juu ya Kura ya Maoni pale ambapo mazingira yatahitaji.

Muswada wa sasa unafanya mabadiliko makubwa katika mapendekezo ya muda wa kampeni za Kura ya Maoni na elimu ya uraia kuhusu Katiba Mpya. Hii ni kwa sababu, kwa kuangalia aya za 4(1) na (3), 5 na 16(1) za Muswada wa sasa, muda wa kutoa elimu ya uraia kuhusu Katiba Mpya na kufanya kampeni za kuunga mkono au kupinga swali la Kura ya Maoni unaweza kufikia siku 104 au miezi mitatu na nusu, kuanzia tarehe ambayo Rais anapokea Katiba inayopendekezwa. Muda huu ni nje ya muda wa nyongeza wa siku 60 na 'muda wa kutosha' mwingine endapo wananchi wataikataa Katiba inayopendekezwa katika Kura ya Maoni.

Mapendekezo haya mapya juu ya muda wa elimu ya uraia na kampeni ya Kura ya Maoni yanaendana na mapendekezo ya wadau wengi waliotha maoni kwa Kamati kwamba kuwe na muda wa kutosha wa kutoa elimu kwa wapiga kura na kampeni za Kura ya Maoni. Aidha, kama ilivyokuwa kwa Muswada wa mwanzo, mapendekezo ya aya mpya ya 35(3) juu ya kurudia Kura ya Maoni yanaenda sambamba na kuongezwa kwa muda wa uhamasishaji na kutoa elimu juu ya Kura ya Maoni, na kuitishwa upya kwa Bunge Maalum kwa lengo la kuangalia upya vifungu vya Katiba inayopendekezwa, chini ya aya ya 35(4). Kwa maneno mengine, Kura ya Maoni ya marudio, itafanyika baada ya

Hii ni Nakala ya Mtandoao (Online Document)

[MHE. TUNDU A. M. LISSU - MSEMADI WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA SHERIA NA KATIBA]

Bunge Maalum kukutana tena na *presumably*, kufanya marekebisho katika Katiba inayopendekezwa. Hii, kwa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, ni sawa sawa.

Mheshimiwa Spika, eneo la sita ambalo limefanyiwa marekebisho muhimu linahusu mamlaka ya kuandaan swali la Kura ya Maoni. Katika Muswada wa mwanzo, aya ya 37(1) na (2) ilikuwa imependekeza kuzipa Tume ya Uchaguzi na Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar kwa kushauriana na Mwanasheria Mkoo wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Mwanasheria Mkoo wa Zanzibar mamlaka ya kutayarisha na kuchapisha kwenye Gazeti la Serikali swali la Kura ya Maoni. Mapendekezo hayo yalikuwa na hatari ya kuiingiza Serikali katika mchakato wa usimamizi na uendeshaji wa Kura ya Maoni. Hii ni kwa sababu, Mwanasheria Mkoo wa Serikali iwe ya Jamhuri ya Muungano au ya Zanzibar ni Mteule wa Rais, na ni Mjumbe wa Baraza la Mawaziri kwa Jamhuri ya Muungano na Baraza la Mapinduzi la Zanzibar. Aidha, kwa majukumu yao ya Kikatiba, wote ni washauri wakuu wa kisheria wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa upande mwingine, Tume ya Uchaguzi na Tume ya Uchaguzi Zanzibar zinatakiwa kuwa vyombo huru vya Kikatiba. Kama inavyosema ibara ya 74(7) ya Katiba, "Tume ya Uchaguzi itakuwa ni Idara huru inayojitegemea" Aidha, Tume hizi zimekatazwa na Katiba zetu "kufuata amri au maagizo ya mtu ye yeyote au Idara yoyote ya Serikali, au maoni ya Chama chochote cha Siasa." Mapendekezo ya kuwaingiza Wanasheria Wakuu wa Serikali kama washauri wa Tume za Uchaguzi katika kutayarisha swali la Kura ya Maoni yangeingilia uhuru wa Tume hizo katika kuendesha na kusimamia Kura ya Maoni juu ya Katiba inayopendekezwa.

Mapendekezo hayo yalikuwa pia yanaenda kinyume na *regional best practices* kwa sababu Mwanasheria Mkoo wa Zanzibar hana mamlaka yoyote juu ya utayarishaji wa swali la Kura ya Maoni chini ya Sheria ya Kura ya Maoni ya Zanzibar. Nchini Kenya, ili kuhakikisha Serikali haiingilii

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. TUNDU A. M. LISSU - MSEMAJI WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA SHERIA NA KATIBAJ]

mchakato wa Kura ya Maoni, Kanuni za Kura ya Maoni za nchi hiyo ziliweka wazi kwamba Tume Huru ya Mpito ya Uchaguzi itatayarisha swalii la Kura ya Maoni kwa kushauriana na Kamati Teule ya Bunge. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaunga mkono marekebisho yaliyoko kwenye aya mpya ya 4(3) ya Muswada wa sasa, ambayo yatawaondoa Wanasheria Wakuu wa Serikali katika maandalizi ya swalii la Kura ya Maoni juu ya Katiba inayopendekezwa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mapendekezo ya maana ambayo tumeshayajadili hapa, kuna maeneo mengine kwenye Muswada huu yanayotatiza na yanahitaji tafakuri ya kina ya Bunge lako Tukufu. Ni muhimu kuzingatia kwamba, pamoja na ukweli kwamba Muswada huu unapendekeza utaratibu wa kuhalalisha Katiba Mpya kwa ajili ya nchi yetu, Sheria yoyote inayotungwa na Bunge lako Tukufu kwa ajili ya jambo lolote lille, sharti izingatie masharti ya Katiba iliyopo sasa. Kutunga Katiba Mpya siyo, na hajjawahi kuwa, leseni ya kukiuka Katiba iliyopo, ambayo sisi wote tulipo ndani ya Ukumbi huu tulipa kuihifadhi, kuilinda na kuitetea.

Eneo la kwanza linalotatiza ni mapendekezo ya kuipa Tume ya Uchaguzi ya Jamhuri ya Muungano wajibu wa usimamizi wa jumla wa uendeshaji wa Kura ya Maoni; kukuza na kusimamia elimu juu ya Kura ya Maoni, na kadhalika. Kama tumekwisha kuonyesha, 'Kura ya Maoni' ni aina ya uchaguzi. Hata hivyo, Katiba yetu sasa haitambui aina hii ya uchaguzi. Badala yake, Katiba inatambua na imeweka utaratibu wa uchaguzi wa kawaida wa kupata viongozi wa kuchaguliwa. Hata tafsiri ya Kikatiba ya neno 'uchaguzi' inaonyesha dhahiri kwamba Kura ya Maoni sio sehemu ya uchaguzi unaotambuliwa na Katiba. Kwa mujibu wa Ibara ya 151 ya Katiba, maneno 'Uchaguzi Mkuu' au 'uchaguzi unaofanywa na wananchi' maana yake ni "uchaguzi wa Rais na Wabunge wanaowakilisha Majimbo ya uchaguzi unaofanywa baada ya Bunge kuvunjwa."

Katiba pia imeikasimisha Tume ya Uchaguzi majukumu ya kusimamia na kuratibu uendeshaji wa uchaguzi.

Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)

[MHE. TUNDU A. M. LISSU - MSEMADI WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA SHERIA NA KATIBA]

Tunafahamu kwamba Tume ya Uchaguzi ina mamlaka ya kutekeleza majukumu mengine yoyote kwa mujibu wa Sheria iliyotungwa na Bunge kwa mujibu wa Ibara ya 74(6)(e).

Hata hivyo, kwa maoni yetu, maneno hayo hayaipi Tume ya Uchaguzi mamlaka ya kusimamia na kuendesha Kura ya Maoni. Kwa ufahamu wetu, Ibara ya 74(6)(e) inahusu majukumu ambayo ni *ejusdem generis* na Uchaguzi Mkuu, yaani majukumu yanayofanana na ya uchaguzi, kama vile gharama za uchaguzi, maadili ya uchaguzi, na kadhalika, ambayo yametungiwa Sheria mahsus na yanasi mamiwa na Tume ya Uchaguzi.

Kwa hulka yake, Kura ya Maoni na masharti yanayoishusu ni *sui generis*, yaani ni masuala ya kipekee, na yanatakiwa yatajwe wazi wazi kwenye Katiba. Ndio maana Katiba za Zanzibar, Kenya, Zimbabwe, Ghana na nchi nyiningine zinazotambua Kura ya Maoni zimeveka masharti mahsus kwa ajili hiyo katika Katiba za nchi zao. Kutokuwapo kwa mamlaka ya Kikatiba ya kutunga Sheria inayohusu Kura ya Maoni kunamaanisha kwamba, endapo utapitishwa kuwa Sheria, Muswada huu utakuwa umekiuka masharti ya Ibara ya 64(5) ya Katiba ya sasa na, kwa kiasi cha ukiukwaji huo, Sheria hiyo itakuwa batili na itatanguka.

Kama ambavyo tumependekeza siku za nyuma kuhusiana na mchakato wa Katiba Mpya, ni muhimu kwa Bunge lako Tukufu kutumia mamlaka yake ya Kikatiba ili kufanya marekebisho muafaka katika Katiba ya sasa ili kuweka masharti mapya yatakayotambua na kuruhusu Kura ya Maoni na kwa hiyo kuhalalisha Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, Katiba yetu inatambua na kuhifadhi uhuru wa kushiriki shughuli za umma. Kwa mujibu wa ibara ya 21(1): "Bila ya kuathiri masharti ya ibara ya 39, ya 47 na ya 67 ya Katiba hii na ya Sheria za nchi kuhusiana na masharti ya kuchagua na kuchaguliwa, au kuteua au kuteuliwa kushiriki katika shughuli za utawala wa nchi, kila raia wa Jamhuri ya Muungano anayo haki ya kushiriki katika shughuli za utawala wa nchi, ama moja kwa moja au kwa

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. TUNDU A. M. LISSU - MSEMAJI WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA SHERIA NA KATIBAJ]

kupitia wawakilishi waliochaguliwa na wananchi kwa hiari yao, kwa kuzingatia utaratibu uliowekwa na Sheria au kwa Mujibu wa Sheria.”

Ibara ndogo ya (2) inasema: “Kila raia anayo haki na uhuru wa kushiriki kwa ukamilifu katika kufikia uamuzi juu ya mambo yanayomhusu yeye, maisha yake au yanayolihusu Taifa.”

Swali la kujiuliza, na linalohitaji majibu ya Bunge lako Tukufu ni: Je, Ibara ya 21 ya Katiba inatoa msingi wa kuendesha Kura ya Maoni; na kwa hiyo, Muswada huu? Licha ya kutosema hivyo wazi wazi, Maelezo ya Waziri mbele ya Kamati yanaashiria kwamba Ibara ya 21(2) ndio msingi wa Muswada huu. Kwa maneno ya Mheshimiwa Waziri “Ibara ya 21(2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, inampa kila mwananchi haki ya kushiriki kwa ukamillifu katika kufikia uamuzi juu ya mambo yanayomhusu yeye mwenyewe, maisha yake au yanayolihusu Taifa.”

Aidha, mwakilishi wa Chama cha Mapinduzi (CCM) ameiambia Kamati kwamba kwa maoni ya CCM Ibara hiyo inahalalisha Muswada huu.

Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatofautiana na tafsiri hii pana ya Ibara ya 21. Kwanza, kama ambavyo Mahakama ya Rufani ya Tanzania imewahi kusema katika kesi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali dhidi ya Mchungaji Christopher Mtikila, haki ya kushiriki moja kwa moja katika mambo ya umma chini ya Ibara ya 21 imewekewa masharti na vizingiti vingi katika Katiba yetu. Mifano ya vizingiti hivyo ni pamoja na haki hiyo kutokuhalusu Watanzania wasiokuwa wanachama wa vyama vya siasa; au wasiotimiza masharti ya umri wa kugombea nafasi mbalimbali za uongozi kukatazwa kugombea nafasi hizo; au wasiokuwa raia wa kuzaliwa kutokuhala na haki ya kugombea urais; au Wabunge wa Viti Maalum kutokuhala na haki ya kuteuliwa Waziri Mkuu, na kadhalika. Kwa maana hiyo, Ibara ya 21 haiwezi kutumika kuhalalisha Kura ya Maoni ambayo hajatajwa mahali pengine popote katika Katiba.

Hii ni Nakala ya Mtandoao (Online Document)

[MHE. TUNDU A. M. LISSÙ - MSEMAJI WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA SHERIA NA KATIBAJ]

Pili, maneno yaliyotumika kwenye Ibara ya 21 yenewe yanathibitisha kwamba haki ya kushiriki shughuli za umma chini ya ibara hiyo ni finyu sana. Maneno 'bila kuathiri masharti ya Ibara ya 39, 49 na 67 na ya Sheria za nchi kuhusiana na masharti ya kuchagua na kuchaguliwa' yaliyoko kwenye Ibara ya 21 yanamaanisha kwamba haki ya kushiriki shughuli za umma haihusu masharti ya uchaguzi wa Rais, wala Makamu wake, wala Wabunge.

Aidha, haki hii haihusu masharti ya uchaguzi wa Wenyeviti wa Vitongoji, Vijiji na Madiwani kwa sababu wote hao wanatakiwa kuwa wanachama wa Vyama vya Siasa kwa mujibu wa Sheria husika za uchaguzi. Kupanua wigo wa haki hii finyu Kikatiba mpaka ifunike Kura ya Maoni ambayo hajatajwa mahali popote katika Katiba kunaifanya nchi yetu ionekane kama haina wataalamu wa Sheria wenye weledi wa kuishauri Serikali juu ya mambo haya.

Tatu, ibara ya 21 ya Katiba yetu inafanana na ibara ya 21(1) na (2) ya Katiba ya Zanzibar. Hata hivyo, licha ya kufanana huko, Katiba ya Zanzibar imetambua Kura ya Maoni kwa kuitaja rasmi katika Katiba na kuiwekea utaratibu katika Katiba yenewe na kwenye Sheria ya Kura ya Maoni. Kama Ibara ya 21(1) na (2) za Katiba ya Zanzibar zingekuwa zinajitosheleza kuhusiana na Kura ya Maoni, Zanzibar isingekuwa na haja ya kuweka masharti ya Kura ya Maoni katika Ibara ya 80(a) ya Katiba yake.

Mheshimiwa Spika, kwa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, Serikali hii ya CCM inaogopa kufungua mjadala wa marekebisho ya Katiba ili kuruhusu Kura ya Maoni kwa hofu kwamba mjadala huo utapanuliwa kwa kuhoji uhuru wa Tume ya Uchaguzi katika kuendesha na kusimamia uchaguzi. Kwa sababu hiyo, Bunge lako Tukufu linaombwa kufunika kombe ili wanaharamu wapite, yaani tupitishe Muswada huu hata kama kwa kufanya hivyo tutavunja Katiba.

Hata hivyo, hofu ya Serikali hii ya CCM haiwezi kukubaliwa kama sababu ya msingi kuruhusu Bunge lako

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. TUNDU A. M. LISSU - MSEMAJI WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA SHERIA NA KATIBAJ]

Tukufu kutunga Sheria zinazopingana na Katiba. Kufanya hivyo itakuwa sawa na kubariki ukiukwaji wa Katiba ambayo Wabunge wote tulipo ndani ya Ukumbi huu tulipa kuihifadhi, kuilinda na kuitetea.

Katika hotuba yake ya nyufa ya tarehe 13 Machi, 1995, Baba wa Taifa Mwalimu Julius K. Nyerere alisema yafuatayo kuhusu utamaduni aliouita wa 'Kupuuza na Kutojali Katiba', na ninaomba nimnukuu Mwalimu.

"Sasa hapa katikati, kumetokea kupuuza puuza Katiba. Hatuwezi kuendelea kupuuza Katiba, ndiyo Sheria ya msingi; Sheria nyingine zote zinatokana na Katiba. Haiwezi kupuuuzwa na hatuwezi kuendelea na utaratibu wa kupuuza Katiba ya nchi yetu au kuwa na Rais anayeonea haya kuitetea Katiba, naye amechaguliwa kwa mujibu wa Katiba, ameapa kuilinda Katiba hiyo halafu anaona haya hawezi kuitetea Katiba hiyo. Mtu ambaye hawezi kuitetea Katiba ya nchi yetu, hawezi kuilinda, hawezi kuisimamia baada ya kiapo, hatufai. Hafai! Aende akaendeshe shamba lake huko. Hawezi kuwa Rais wa nchi yetu. Tunamchagua kwa mujibu wa Katiba, tunamwapisha kuwa Katiba ailinde, aitetee kwa moyo kabisa kabisa bila uwoga. Hawezi, hatumtaki kuwa kiongozi wetu." Mwisho wa kumnukuu Mwalimu.

Pamoja na kwamba onyo hili la Baba wa Taifa lilikuwa linahusu wajibu wa Rais kuilinda na kuitetea Katiba, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaamini kwa sababu za wazi kabisa kwamba onyo hili pia linahusu Serikali hii ya CCM na linalihusu pia Bunge hili Tukufu. Kwa sababu hizi, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapendekeza kwamba Muswada huu uondolewe kwa Mujibu wa Kanuni ya 90 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, 2013, hadi hapo Bunge lako Tukufu litakapofanya marekebisho katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano kwa lengo la kuruhusu Kura ya Maoni na kuipa Tume ya Uchaguzi mamlaka ya kuisimamia na kuiendesha.

Mheshimiwa Spika, pendekezo la aya ya 4(1) ya Muswada kuhusu mamlaka ya Rais kuitisha Kura ya Maoni, lina utata pia. Pendekezo hili ni mwendelezo wa Urais wa

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. TUNDU A. M. LISSÙ - MSEMAJI WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA SHERIA NA KATIBAJ]

Kifalme ambayo ndio imekuwa nguzo kuu ya Kikatiba katika historia ya nchi yetu tangu Katiba ya Jamhuri ilipotungwa mwaka 1962. Urais wa Kifalme ndio ulikuwa msingi mkuu wa dola ya kiimla ya chama kimoja iliyodumu kwa karibu miongo mitatu. Urais wa Kifalme ndio umekuwa msingi mkuu wa utawala usiowajibika kwa wananchi wala kwa vyombo vya uwakilishi vya wananchi. Urais wa Kifalme ndio umekuwa mhimili mkuu wa ujisadi unaolitafuna Taifa letu.

Kwa Serikali hii ya CCM kupendekeza Rais awe ndio mwanzilishi wa mchakato wa Kura ya Maoni, kama inavyopendekezwa na aya ya (4) ya Muswada, ni kuthibitisha, kwa mara nyingine tena, jinsi ambavyo Serikali hii ya CCM haiko tayari kuruhusu mabadiliko ya kidemokrasia katika mfumo mzima wa utawala wa nchi yetu. Kwa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, pendekezo hili linaenda kinyume na wimbi la mabadiliko ya Kikatiba katika sehemu hii ya dunia. Kama ilivyokuwa kwa Sheria ya Haki za Binadamu mwaka 1984, Serikali hii ya CCM imepitwa tena na Zanzibar na nchi nyingine jirani katika kuweka utaratibu wa kidemokrasia wa kuendesha na kusimamia Kura ya Maoni.

Tutaanza na Zanzibar. Chini ya kifungu cha 3(1) cha Sheria ya Kura ya Maoni ya Zanzibar, mchakato wa Kura ya Maoni unaweza kuanzishwa kwa Azimio lillipitishwa na Baraza la Wawakilishi, au na Rais wa Zanzibar.

Kwa upande wa Kenya, kwa Mujibu wa Ibara za 256 na 257 za Katiba ya nchi hiyo, Rais hana mamlaka yoyote ya kuanzisha mchakato wa Kura ya Maoni, bali mamlaka hayo yamekasimiwa kwa Bunge na kwa wananchi wenyewe. Badala ya kuangalia mbele palipo na demokrasia pana na mamlaka ya wananchi na vyombo vyao vya uwakilishi yanazingatiwa na kuheshimiwa, Muswada huu unatutazamisha nyuma kwenye uimla wa Urais wa Kifalme, ukiritimba wa madaraka na utawala usiowajibika.

Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapendekeza masharti ya aya ya 4(1) yarekebishwe ili Muswada uonyeshe wazi kwamba mchakato wa Kura ya Maoni juu ya uhalalishaji

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. TUNDU A. M. LISSU - MSEMAJI WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA SHERIA NA KATIBA]

wa Katiba Mpya unaweza kuanzishwa na wananchi wenyewe, au kwa Azimio la Bunge au na Rais, kwa maana ya Serikali. Kufanya hivyo kutaiweka nchi yetu katika kundilila nchi zenyet utaratibu wa kidemokrasia wa Kura ya Maoni kama vile Kenya na hata Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, pengine eneo lenye utata mkubwa kuliko mengine katika Muswada huu ni suala la haki ya Watanzania wote wenyewe sifa ya kushiriki katika Kura ya Maoni kuhalalisha Katiba Mpya. Aya ya 43 ya Muswada wa mwanzo ilikuwa inayohusu kupiga kura katika mazingira maalum. Kwa mapendekezo hayo, kwa mara ya kwanza katika historia yetu, raia wa Tanzania waishio nje ya Jamhuri ya Muungano wangekuwa na haki ya kujandikisha katika Daftari la Wapiga Kura na kupiga Kura ya Maoni. Aidha, watu ambaao kwa sababu ya majukumu yao ya kikazi, au kwa sababu za kijamii na kiuchumi, nao wangekuwa na haki ya kupiga Kura ya Maoni.

Hii pia inawahu watu wasiojiweza kwa sababu ya ulemavu, au ugonjwa, au uzee, au ujauzito na watu wanaohamahama kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa. Kwa sababu ambazo hazijulikani, na ambazo Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali hii ya CCM kuzieleza mbele ya Bunge lako Tukufu, aya ya 43 ya Muswada wa mwanzo imeondolewa katika Muswada wa sasa. Badala yake, aya ya 9(1) ya Muswada wa sasa inapendekeza kwamba Daftari la wapiga kura lililoanzishwa chini ya Sheria ya Taifa ya Uchaguzi au Sheria ya Uchaguzi ya Zanzibar litakuwa ni daftari la wapiga kura kwa madhumuni ya Kura ya Maoni. Aidha, aya mpya ya 9(2) inapendekeza kwamba "mtu ambaye jina lake limeingizwa katika Daftari la Wapiga Kura lililoanzishwa chini ya Sheria ya Taifa ya Uchaguzi au Sheria ya Uchaguzi ya Zanzibar atakuwa na haki ya kupiga Kura ya Maoni, isipokuwa kama mtu huyo amezuiwa kupiga kura na sheria nyingine yoyote."

Kwa masharti haya, Muswada unapendekeza utaratibu wa kupiga kura katika Tanzania Bara na Zanzibar ambaao utakuwa chini ya sheria mbili tofauti. Kama hii haitoshi,

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. TUNDU A. M. LISSU - MSEMADI WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA SHERIA NA KATIBAJ]

aya ya 34(2) ya Muswada inapendekeza kwamba katika kutangaza matokeo ya Kura ya Maoni, "kura zitakazohesabiwa kwa Tanzania Zanzibar zitajumuisha kura za watu walioandikishwa katika daftari la wapiga kura la Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar na kura za watu wanaoishi Zanzibar na walioandikishwa chini ya daftari la wapiga kura la Tume ya Taifa ya Uchaguzi."

Mapendeleko haya yana utata mkubwa. Kwanza, kumekuwa na malalamiko mengi na ya muda mrefu kuhusu uandikishaji wa wapiga kura katika Daftari la Wapiga Kura la Zanzibar. Katika andiko lake *The State of Constitutionalism in Zanzibar*, mwanazuoni wa Kizanzibari na Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Mheshimiwa Mahadhi Juma Maalim ameелеza jinsi ambavyo Masheha wengi wao wakiwa makada wa CCM wametumiwa kuzuia uandikishaji wa wafuasi wa Vyama vya Upinzani katika Daftari la Wapiga Kura la Zanzibar. Naomba kumrukuu mwanazuoni huyu. Anasema "Kwa upande mwingine," anasema, "*masheha walihamasisha uandikishaji wa wafuasi wa Chama Tawala hata kama hawakuwa na sifa za kuandikishwa. Hii ilipelekea kuwepo kwa vurugu katika Vituo vya Kuandikishia Wapiga Kura.*" (*Makof!*)

Tatizo la pili linahusu masharti ya ukaazi yaliyoko kwenye Sheria ya Uchaguzi ya Zanzibar, 1984. Sheria hii imeweka sharti kwamba ili Mzanzibari awe na sifa ya kuandikishwa kwenye Daftari la Wapiga Kura la Zanzibar, anatakiwa awe mkazi wa Jimbo husika kwa kipindi cha miezi 36 mfululizo.

Kwa vile hakuna ushahidi wa maandishi unaotolewa na mamlaka yoyote kwa mtu anayehama kutoka Jimbo moja kwenda lingine, Wazanzibari wengi wamekataliwa kuandikishwa kwenye Daftari la Wapiga Kura kwa kushindwa kutimiza masharti haya ya ukaazi katika Majimbo walikohamia. Pale wanaporudi kwenye Majimbo yao ya zamani, wanakataliwa kuandikishwa pia kwa sababu hiyo hiyo ya ukaazi kwa vile walikwishahama kwenye Majimbo hayo. Kwa mujibu wa Mheshimiwa Mahadhi Maalim,

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. TUNDU A. M. LISSU - MSEMAJI WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA SHERIA NA KATIBAJ]

“matokeo ya masharti haya ni Wazanzibari wengi waliokuwa na haki ya kuandikishwa kuwa wapiga kura kunyimwa haki ya kupiga kura.”

Tatizo la tatu linahusu pia masharti ya ukaazi. Chini ya Sheria ya Uchaguzi ya Zanzibar, masharti haya hayawahuusu Askari wa vikosi vya majeshi ya Ulinzi na Usalama ya Jamhuri ya Muungano, na wa vikosi vya Idara Maalum za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar pamoja na watumishi wa umma na familia zao. Wote hawa wana haki ya kuandikishwa na kupiga kura mahali popote bila kujali wameishi hapo kwa muda gani. Kwa mujibu wa Mheshimiwa Mahadhi Maalim, utaratibu huu ‘umetumiwa vibaya’ kwa vile Askari wengi wamekuwa wakihamishiwa katika maeneo mbali mbali ya Zanzibar wakati wa uchaguzi ili kuongeza kura za Chama Tawala.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, ambayo ni Sheria ya Muungano, imeshindwa kabisa kutatua tatizo la haki ya Wazanzibari kupiga kura hata kwenye uchaguzi wa Muungano. Kifungu cha 12(1) cha Sheria hiyo kinaunda Daftari la Wapiga Kura kwa ajili ya Jamhuri ya Muungano. Daftari hili litawekwa, kutunzwa na kuboreshwa na Tume ya Uchaguzi. Hata hivyo, licha ya masharti haya, Sheria ya Uchaguzi imeikasimisha Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar mamlaka ya ‘uandikishwaji wa wapiga kura Tanzania Zanzibar.’

Kwa mujibu wa kifungu cha 12A(1): “Bila ya kujali masharti ya kifungu cha 12, kwa madhumuni ya kuendesha uchaguzi wa Wabunge na Rais Tanzania Zanzibar, Sheria inayohusu uandikishwaji wa wapiga kura na daftari la wapiga kura kwa ajili ya uchaguzi katika Baraza la Wawakilishi la Zanzibar, itatumika pamoja na mabadiliko yanayofaa kuwa Sheria ya uandikishwaji wa wapiga kura na daftari la wapiga kura kwa Tanzania Zanzibar kwa madhumuni ya Sheria hii.”

Mheshimiwa Spika, licha ya kifungu cha 12(a)(2) kuahidi kwamba “Tume itamwandikisha mtu yejote Tanzania Zanzibar ambaye anastahili kuandikishwa kuwa mpiga kura”,

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. TUNDU A. M. LISSU - MSEMADI WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA SHERIA NA KATIBA]

kwa kadri masharti ya uandikishwaji wapiga kura yanavyoendelea kutawaliwa na masharti ya Sheria ya Uchaguzi ya Zanzibar, basi masharti ya ukaazi chini ya Sheria hiyo yataendelea kuwanyima Wazanzibari wengi haki yao ya kupiga kura. Kwa sababu hiyo hiyo, Wazanzibari wengi hawatapata haki ya kuandikishwa na kupiga kura yoyote kwa mujibu wa Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, haki ya kupiga kura imehifadhiwa na Katiba zote mbili za nchi zetu. Hivyo basi, kwa mujibu wa ibara ya 5(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano, "kila raia wa Tanzania aliyetimiza umri wa miaka 18 anayo haki ya kupiga kura katika uchaguzi unaofanywa Tanzania na wananchi." Kwa upande wake, ibara ya 7(1) ya Katiba za Zanzibar imerudia msimamo huo huo: "Kila Mzanzibari aliyetimiza umri wa miaka 18 anayo haki ya kupiga kura katika uchaguzi unaofanywa Zanzibar na wananchi." Ibara ya 7(2) imeweka 'masharti yanayoweza kuzuia Mzanzibari asitumie haki ya kupiga kura' kuwa ni:-

- (a) Kuwa na uraia wa nchi nydingine;
- (b) Kuwa na ugonjwa wa akili;
- (c) Kutiwa hatiani na kuendelea kutumikia adhabu kwa kosa la jinai katika Chuo cha Mafunzo;
- (d) Kukosa au kushindwa kuthibitisha au kutoa kitambulisho cha umri, uraia au uandikishwaji kama mpiga kura.

Pamoja na masharti haya, ibara ya 7(3)(b) ya Katiba ya Zanzibar imeruhusu Baraza la Wawakilishi kutunga Sheria ya Uchaguzi inayoweka masharti ya ukaazi katika Jimbo la Uchaguzi kwa ajili ya kupiga kura. Vile vile, Sheria ya Kura ya Maoni ya Zanzibar nayo imetamka wazi kwamba: "mtu yejote ambaye wakati wa kipindi cha Kura ya Maoni ameandikishwa kama mpiga kura katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura la Zanzibar atakuwa na haki ya kupiga kura katika Kura ya Maoni." Kwa maneno mengine, utaratibu huu

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. TUNDU A. M. LISSU - MSEMAJI WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA SHERIA NA KATIBA]

wa kikatiba na kisheria ambao umesababisha Wazanzibari wengi kunyimwa haki ya kupiga kura ndiyo utakaotumika Zanzibar kwenye Kura za maoni kwa mujibu wa Muswada huu.

Ikumbukwe kwamba Katiba ya Jamhuri ya Muungano na Sheria ya Taifa ya Uchaguzi hazina masharti haya ya ukaazi katika Jimbo la Uchaguzi. Ni ajabu ilioje kwamba Mzanzibari anawenza kuandikishwa kuwa mpiga kura katika eneo lolote la Tanganyika bila kuhojiwa ameishi eneo hilo kwa muda gani, lakini hana haki ya kuandikishwa kuwa mpiga kura katika eneo lolote la nyumbani kwao Zanzibar mpaka athibitishé kwamba ameishi katika eneo hilo kwa miaka mitatu mfululizo.

Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapendekeza yafuatayo kuhusiana na haki ya kupiga Kura ya Maoni kwa mujibu wa Muswada huu:-

(a) Vifungu vyote vinavyoruhusu Daftari la Wapiga Kura la Zanzibar kutumika katika Kura ya Maoni kwa mujibu wa Muswada huu vifutwe na badala yake Muswada utamke wazi kwamba Daftari la Wapiga Kura litakalotumika ni lile liliandalialiwa kwa mujibu wa Sheria ya Taifa ya Uchaguzi;

(b) Kifungu cha 12(a) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi ambacho kimekasimisha mamlaka ya kutayarisha Daftari la Wapiga Kura la Jamhuri ya Muungano kwa upande wa Zanzibar kwa Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar ikitumia Sheria ya Uchaguzi ya Zanzibar kifutwe ili masuala yote yanayohusu uandikishwaji wa wapiga kura kwa ajili ya Kura ya Maoni yasimamiwe moja kwa moja na Tume ya Taifa ya Uchaguzi;

(c) Kwa vile kuna Wazanzibari wengi ambao wamenyimwa haki yao ya kupiga kura kwa sababu ya masharti ya ukaazi, na kwa vile Tume ya Uchaguzi haijaandikisha wapiga kura wapya tangu mwaka 2010, aya ya (9) irekebishwe ili kuweka masharti kwamba Tume ya Uchaguzi itaboresha Daftari la Kudumu la Wapiga Kura kabla ya kufanyika kwa Kura ya Maoni kwa mujibu wa Sheria hii;

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. TUNDU A. M. LISSU - MSEMAJI WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA SHERIA NA KATIBAJ]

(d) Kwa vile kuna Wazanzibari wengi wanaoishi Tanzania Bara na mahali pengine nje ya Zanzibar, Tume ya Taifa ya Uchaguzi iweke utaratibu maalum wa kuwaandikisha katika Daftari la Wapiga Kura na utaratibu utakaowawezesha kupiga Kura ya Maoni sawa na Wazanzibari waishio Zanzibar. Hii itakuwa na maana ya kuirudisha katika Muswada wa sasa iliyokuwa aya ya 43 ya Muswada wa mwanzo;

(e) Aya ya 34(2) irekebishwe kwa kuweka wazi kwamba kura zitakazohesabiwa Zanzibar ni pamoja na kura za Wazanzibari wote waishio ndani na nje ya Zanzibar katika Jamhuri ya Muungano, na nje ya Jamhuri ya Muungano; na

(f) Aya ya 34 irekebishwe kwa kuongeza aya ndogo mpya ya (4) itakayoweka wazi kwamba kura zitakazohesabiwa Tanzania Bara ni pamoja na kura za Watanganyika wote wanaoishi Tanzania Bara, Zanzibar na mahali pengine nje ya Jamhuri ya Muungano.

Mheshimiwa Spika, aya ya 9(3) ya Muswada wa sasa inatamka kwamba "Afisa wa Kura ya Maoni atamtaka mtu anayeomba karatasi ya kupigia kura kutoa kadi ya mpiga kura iliyotolewa na Tume kama uthibitisho wa utambulisho wa mtu anayedai kuwa anaruhusiwa kupiga kura." Kwa upande mwingine, aya mpya ya 9(4) inatamka wazi kwamba: "Pale ambapo mtu ye yote aliyesajiliwa kama mpiga kura na taarifa zake zipo kwenye daftari la wapiga kura ila amepoteza kitambulisho cha kupigia kura, Afisa wa Kura ya Maoni atamtaka mtu huyo kuonyesha kingine chochote kinachomtambulisha na atamruhusu mtu huyo kupiga kura baada ya kujaza fomu maalum ya kiapo."

Masharti haya ni muhimu sana. Kwa muda mrefu, wapiga kura wengi walioandikishwa katika Daftari la Wapiga Kura lakini ambao wamepoteza kadi zao za mpiga kura wamekataliwa kupiga kura. Licha ya Tume ya Uchaguzi kutengeneza Fomu Na. 17 kwa ajili ya wapiga kura wa aina hiyo, Tume hiyo hiyo imekuwa mstari wa mbele kuwanyima Watanzania hao haki ya kupiga kura kwa kutoa maelekezo kwa wasimamizi wa uchaguzi na wa vituo vyaa kupigia kura

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. TUNDU A. M. LISSU - MSEMAJI WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA SHERIA NA KATIBAJ]

ya kuwazuia wasiokuwa na kadi za mpiga kura hata kama majina na picha zao zipo kwenye Daftari la Wapiga Kura.

Mapendekezo ya aya ya 9(4) ya Muswada yatawezesha wapiga kura ambao, kwa sababu mbalimbali, hawana kadi zao za mpiga kura kupiga kura. Aidha, mapendekezo haya yataondoa kabisa uwezekano wa watu wanaotaka kufifisha demokrasia katika nchi yetu kununua kadi za wapiga kura ili kupunguza idadi wa wapiga kura wanaoweza kupiga kura zisizotakiwa na wanunuzi hao wa kadi za mpiga kura au mawakala wao. Muhimu zaidi, mapendekezo haya yataongeza idadi ya wapiga kura, na kwa hiyo uhalali wa kisia wa Katiba Mpya, kwani utaruhusu wapiga kura wote walioandikishwa kwenye Daftari la Wapiga Kura kupiga kura hata kama wamepoteza kadi zao za mpiga kura. Kwa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, hili ni jambo jema la kuungwa mkono.

Mheshimiwa Spika, Muswada wa mwanzo ulikuwa umependekeza utaratibu wa kupinga matokeo ya Kura ya Maoni. Kwa kiasi kikubwa, utaratibu huo ulikuwa hautekelezeki kwa sababu mbalimbali. Muswada mpya unapendekeza utaratibu wa kupinga matokeo ya Kura ya Maoni ambao, kwa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, hautekelezeki pia.

Kwanza, aya ya 43(2) ya Muswada wa sasa inatamka kwamba haki ya kupinga matokeo ya Kura ya Maoni itapatikana tu endapo Kamati ya Kura ya Maoni inayotaka kupinga matokeo hayo itapata si chini ya asilimia 10 ya saini za idadi yote ya wapiga kura waliosajiliwa kutoka katika Majimbo matano ya kila upande wa Muungano. Kwa mujibu wa aya mpya ya 43(3), ombi la kupinga matokeo ya Kura ya Maoni litawasilishwa katika Masjala ya Mahakama Kuu ndani ya siku kumi na nne baada ya kutangazwa matokeo ya Kura ya Maoni.

Baada ya pingamizi kufunguliwa, Mahakama Kuu ikikaa kama jopo la Majaji watano itawasikiliza (wadaawa) na kutoa uamuzi juu ya pingamizi la Kura ya Maoni ndani ya

Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)

[MHE. TUNDU A. M. LISSU - MSEMADI WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA SHERIA NA KATIBA]

Kipindi cha siku 14 tangu lalamiko lilipowasilishwa Mahakamani.

Kwa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, ukomo wa muda unaopendekezwa na Muswada huu unathibitisha kwamba lengo la mapendekezo haya siyo kuwawezesha wananchi kupinga matokeo ya Kura ya Maoni. Badala yake, inaelekea kwamba lengo halisi la mapendekezo haya ni kutengeneza kiini macho kwamba kuna haki ya kupinga matokeo ya Kura ya Maoni wakati haki hiyo haitekelezeki kivitendo katika hali halisi.

Hii ni kwa sababu, kwa ulinganisho tu, mlalamikaji anayepinga matokeo ya uchaguzi wa Mbunge hana haja ya kukusanya saini ya mpiga kura yejote lakini amepewa siku thelathini za kufungua mashauri kutoka tarehe ya kutangazwa matokeo ya uchaguzi anayoyapinda.

Katika hali halisi ya nchi yetu, itakuwa vigumu sana kwa Kamati ya Kura ya Maoni kukusanya saini za makumi ya maelfu ya wapiga kura katika Majimbo 10 ya uchaguzi ya pande zote za Muungano, kukusanya ushahidi wa makosa mbalimbali, kutafuta Mawakili na fedha za kuwalipa ili waandae kesi itakayofunguliwa ndani ya siku 14 tangu kutangazwa kwa matokeo ya Kura ya Maoni. Ndani ya kipindi hicho hicho, kamati ya Kura ya Maoni itatakiwa kutafuta na kupata fedha za kulipa dhamana ya gharama ya pingamizi kama inavyotakiwa na aya mpya ya Muswada wa sasa.

Aidha, Kamati inatakiwa ihakikishe kwamba orodha ya waungaji mkono haijumuishi wapiga kura ambao hawajatoa idhini zao, au waliokufa kabla malalamiko hayajafunguliwa, vinginevyo mlalamikaji atawajibika kulipa faini ya Shilingi milioni kumi au kifungo cha miaka saba au vyote viwili.

Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapendekeza kwamba muda wa kufungua malalamiko uwe siku 30 sawa na muda wa kufungua mashauri ya yanayohusu matokeo ya uchaguzi wa Wabunge chini ya Sheria ya Uchaguzi.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. TUNDU A. M. LISSU - MSEMAJI WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA SHERIA NA KATIBAJ]

Mheshimiwa Spika, muda wa kuendesha mashauri ya kupinga matokeo ya Kura ya Maoni unaopendekezwa na Muswada huu haujazingatia hali halisi ya nchi yetu. Ikiwa misingi ya kuendesha mashauri kwa haki itafuatwa, itabidi walalamikiwa wapatiwe fursa ya kujibu malalamiko dhidi yao. Baada ya hapo, ushahidi wa pande zote itabidi utolewe, mashahidi kama wapo wahojiwe, pande zote mbili ziwasilisho hoja za mwisho na Mahakama Kuu iandike hukumu na kuitoa kwa wadaawa. Yote haya yanatakiwa yafanyike ndani ya kipindi cha wiki mbili! Utaratibu wa rufaa ni *equally unrealistic*.

Aya mpya ya 46(1) inapendekeza, kwa mfano, kwamba upande ambao haujaridhika na uamuzi wa Mahakama Kuu utakata rufaa katika Mahakama ya Rufaa ndani ya siku saba kutoka tarehe aliyopata nakala ya hukumu na mwenendo wa shauri. Mahakama Kuu inatakiwa kutoa nakala hizo ndani ya siku tano kutoka tarehe ya uamuzi.

Aidha, Mahakama ya Rufaa ikiwa imekaa kama *Full Bench* inatakiwa kuamua rufaa hiyo "ndani ya siku saba kutoka tarehe ya kuwasilishwa kwa ombi la rufaa. Hii ina maana kuwa rufaa inatakiwa iwe imeshawasilishwa katika Mahakama ya Rufaa ndani ya siku kumi tangu tarehe ya uamuzi unaokatiwa rufaa, na kuamuliwa ndani ya siku saba baada ya hapo. Kwa ulinganisho tu, Kanuni za Mahakama ya Rufaa ya Tanzania zinataka rufaa iwasilishwe Mahakamani ndani ya siku 60 tangu mwomba rufaa kupatiwa nakala ya hukumu na mwenendo wa shauri. Baada ya hapo, mwomba rufaa anatakiwa kuwasilisha hoja za maandishi ndani ya siku nyingine 60, na zijiwi na mjibu rufaa ndani ya siku 30 tokea hapo.

Kwa vyovyote vile, kutakuwa na haja ya kutunga Kanuni nyingine za rufaa ili kuweka utaratibu wa rufaa kwa ajili ya Kura ya Maoni ili kutekeleza matakwa ya Muswada huu! Bila kufanya hivyo, mapendekezo haya hayatekelezeki na yanaonekana kuwa kiini macho zaidi.

Mheshimiwa Spika, kuna masuala mengine muhimu ambayo pengine hayahusiki na Muswada huu moja kwa

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. TUNDU A. M. LISSU - MSEMADI WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA SHERIA NA KATIBAJ]

moja, lakini yanahitaji kuzingatiwa katika mjadala wa Muswada huu. Kwanza, ni muhimu kuzingatia masharti ya Katiba ya Zanzibar kuhusu Kura ya Maoni juu ya Mambo ya Muungano. Kama tulivyoonyesha, Katiba hiyo imeweka masharti ya Kura ya Maoni ya Wazanzibari kuhusu vifungu vinavyohusu, *inter alia*, Mambo ya Muungano. Kwa mfano, masuala ya kama Zanzibar ni nchi au la pamoja na mipaka yake; Rais wa Zanzibar kama Mkuu wa Nchi na Kamanda Mkuu wa vikosi vya Idara Maalum za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar; na masuala ya Zanzibar kuwa na vikosi vyake vya kijeshi.

Yote haya ni masuala ya msingi ya Muungano yaliyotokana na Hati za Makubaliano ya Muungano na Sheria ya Muungano ya mwaka 1964. Kwa maneno mengine, kwa mujibu wa Katiba ya sasa ya Zanzibar, masuala ya kama Tanzania ni nchi moja au la, majeshi ya Ulinzi, Polisi, na kadhalika ambayo yamekuwa Mambo ya Muungano tangu mwaka 1964, sio mambo ya Muungano tena hadi hapo wananchi wa Zanzibar watakapoamua kwa Kura ya Maoni kuyarudisha kwa mamlaka ya Muungano.

Sasa Muswada huu unapendekeza yaamuliwe kwa Kura ya Maoni ya wananchi wa pande zote mbili za Muungano. Suala hili linahitaji kupatiwa ufumbuzi, vinginevyo litasababisha mgogoro mkubwa wa kikatiba katika kutekeleza matakwa ya Muswada huu.

Pili, Katiba ya Zanzibar imeweka masharti mengine ya ziada. Hivyo, kwa mfano, ibara ya 64(4) ya Katiba ya Muungano inayoweka utaratibu wa kutunga Sheria zitakazotumika katika pande zote mbili za Muungano, imewekewa masharti ya ziada na ibara za 132(2) na 133(2) vya Katiba ya Zanzibar. Masharti hayo ni kwamba hakuna sheria yoyote inayohusu mambo ya Muungano itatumika Zanzibar mpaka kwanza ipelekwe mbele ya Baraza la Wawakilishi na Waziri anayehusika. Masharti haya yanahusu Muswada huu moja kwa moja kwa sababu ya mapendekezo ya aya ya (2) na 4(2). Bunge hili Tukufu lijadili Muswada huu likijua kwamba endapo litaupitisha kama inavyopendekezwa

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. TUNDU A. M. LISSU - MSEMAJI WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA SHERIA NA KATIBAJ]

itabidi upelekwe mbele ya Baraza la Wawakilishi Zanzibar
kupata ridhaa ya Wazanzibari! (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, naomba hayo mengine vilevile
yaingie katika record ya *Hansard*. Nashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. (*Makof*)

SPIKA: Ahsante. Isipokuwa na wewe siku nyingine
ulete nakala kwa wenzako.

Tunaendelea Waheshimiwa Wabunge. Tungependa
hizi nakala zitoke kabla ya saa 7.00. Ninao wachangiaji wengi,
kwa hiyo, sasa hivi nitawaita wafuatao waanze kuchangia.
Mheshimiwa Betty Machangu namwona, Mheshimiwa Leticia
Nyerere na Mheshimiwa Khatib Said Haji. Hawa watatosha
kwa asubuhi, baadaye tutaangalia kama tutahitaji wengine.

Mheshimiwa Betty Machangu kwanza.

MHE. BETTY E. MACHANGU: Mheshimiwa Spika,
ahsante kwa kunipa nafasi ya kuwa mchangiaji wa kwanza.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu ni mfupi.
Nilikuwa napenda nichangie kwenye kipengele cha Tafsiri
ya Tume. Inatafsiriwa kuwa, "ni Tume ya Taifa ya Uchaguzi
na Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar." Kwa maana hiyo, kuna
Tume mbili ambazo zitakuwa zinafanya kazi kama
ilivyoainishwa kwenye sehemu ya pili, hasa vifungu vya (5),
(6), (7) na (8) ya Sheria hiyo.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, ingefaa viongezwe
vifungu kuonyesha namna ambavyo Tume hizi zitafanya kazi;
nani atakuwa Mwenyekiti wa Tume, tukikumbuka kwamba
tuna Tume mbili? Nani atakuwa Mkurugenzi? Kwa hiyo,
ningeshauri Sheria ingeweza kurekebishwa na kusema Rais
atamteua Mwenyekiti wa Tume kutoka mionganoni mwa
Wajumbe na kumtangaza moja kwa moja kama Mwenyekiti
wa Tume ya Uchaguzi ya Taifa, na inawezekana Mwenyekiti
yule wa Zanzibar pengine akawa ndiyo Makamu ili

Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)

[MHE. BETTY E. MACHANGU]

kuunganisha hizi Tume mbili tukiweka kifungu kitachoonyesha utawala itakuwa ni vizuri na itakuwa kiutawala wanatenda kazi zao vizuri zaidi na watawajibika.

Mheshimiwa Spika, niende kwenye kifungu cha 8(3) kinasema: "Maafisa wataapa," lakini hakisemi wataapa kwa nani? Ili kuondoa mkanganyiko ni vyema ikaelezwa kabisa kwamba wataapa mbele ya Hakimu au Jaji au Kamishna yeoyote mwingine mwenye uwezo wa kuapisha.

Mheshimiwa Spika nikiendelea kifungu cha 11, kinasema: "Tume inaweza kutumia eneo lolote la umma bila malipo, kama Kituo cha Kupiga Kura."

Mheshimiwa Spika, nadhani uwanja huu ni mpana sana. Sheria ingesema Tume baada ya kushauriana na viongozi husika wa eneo la umma, inawekana likatumika kama Kituo cha Kupiga Kura bila malipo.

Mheshimiwa Spika, mashauriano ni muhimu kwasababu huenda eneo hilo, likawa teyari lina mipango mingine au likawa halifai kwasababu kadhaa. Hivyo kushauriana naomba liwe ndiwe takwa la kisheria.

Mheshimiwa Spika, kuna kifungu cha 17 (4) kinasema: "Waziri ataainisha kiwango cha chini cha gharama, zitakazotumiwa na Kamati." Nadhani hapa kuna kasoro. Badala ya kutangaza gharama za chini, atangaze gharama za juu, na lengo liwe kuweka ukomo wa kiasi cha fedha kitakachotumika. Kiwango cha chini hakitakuwa na mantiki yoyote kwasababu kama Kamati inaweza kufanya kazi bila pesa kabisa, basi iruhusiwe kufanya hivyo kuepuka gharama kubwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 25 kinaweza kuboreshwa ili kuruhusu karatasi ya upigaji kura kutumia pia maandishi maalumu kwa ajili ya walemvu, maandishi ya nundu. (*Makof*)

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. BETTY E. MACHANGU]

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 27 kinatumia neno la Mpiga Kura kutamka kwamba hana uwezo. Neno tamka linaweza kutafsiriwa ni kuzungumza. Lakini tukumbuke kwamba tutakuwa na wapiga kura wengine bubu ambao hawawezi kuongea. Kwa hiyo, nashauri badala ya neno kutamka, Mpiga kura atakayeomba iwe kwa ishara, kwa maandishi, au kwa maneno. Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (*Makof*)

SPIKA:Ahsante, anayefuatia Mheshimiwa Leticia. Mheshimiwa Khatibu Said Haji jiandae.

MHE. LETICIA M. NYERERE: Ahsante sana Mheshimiwa Spika, kunipatia nafasi nami nichangie kwenye Muswada huu. Nikianza na ibara ya (5) pameainisha kwamba Tume ndani ya siku 14 baada ya kuchapishwa kwa swali la kura ya maoni katika Gazeti la Serikali, itayainisha yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, nilikuwa napendekeza baada ya (a) ambayo inasema kwamba: "Siku ambazo kura ya maoni itafanyika," ningeomba kuwekwe pia siku maalumu ya kura ya maoni itafanyika. Nasema hivyo kwanini? Wasimamizi ambao watasimamia Uchaguzi siku ya Uchuguzi wenyewe, wapatiwe nafasi ya kupiga kura. Kwa hiyo, kuna haja ya kuwa na siku ya kura maalum.

Mheshimiwa Spika, nikienda katika ibara ya 9 (4) ningependekeza kwa upande wa Kiingereza iondolewe hii sehemu inayosema: "*produce any identity which identifies him.*" Ningependekeza iwe *substituted* na kwamba "*fill his information on the affidavit*", kwa Kiswahili chake ni kwamba badala ya kuwataka hawa tena, wa *produce another identity*, ukizingatia kwamba wananchi wengi vijijini wanakuwa hawana *identity*mbali za hizi kadi za kupigia kura. Yaani vitambulisho vyta kupigia kura.

Mheshimiwa Spika, sasa mimi sioni kama kuna mantiki yoyote, baada ya wao kutokuwa na kile kitambulisho cha kupigia kura bado unawadai kitambulisho kingine. Kama mnavyojua mazingira ya kijijini, hawezি kuwa na kitambulisho

Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)

[MHE. LETICIA M. NYERERE]

zaidi ya hicho cha kupigia kura. Kwa hiyo, ningependekeza yale mahitaji ya kumtaka a-produce kitambulisho kingine ndio ajaze ile fomu ya maelezo yake ili aweze kuruhusiwa kupiga kura, yaondolewe hayo matakwa na badala yake hajaze tu zile fomu na aruhusiwe kupiga kura. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tukienda kwenye kifungu cha 11 (2), naomba niende sehemu ya Kiswahili, sehemu hiyo inazungumzia: "Tume inaweza bila malipo yoyote kutumia eneo lolote la umma kama Kituo cha Kupiga Kura. Kifungu cha pili, kinasema: "Tume inaweza pale ambapo kutakuwa na haja kutumia jengo au eneo binafsi baada ya kupata ridhaa ya mmiliki wa eneo au jengo hilo."

Ningependekeza kutolewe ufafanuzi kwamba eneo binafsi bure, siyo kwamba ibaki hivyo hivyo kwamba eneo binafsi haijullikani litalipiwa au hallipiwi. Kwa hiyo, ni lazima liwe *indicated* kwamba hilo eneo la kupigia kura ambalo litatolewa na mtu binafsi au kampuni binafsi, litatolewa bure.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba mabadiliko yafuatayo: "Tume inaweza pale ambapo kutakuwa na haja kutumia jengo au eneo binafsi bure, baada ya kupata ridhaa ya mmiliki wa eneo au jengo hilo."

Mheshimiwa Spika, nikienda kwenye ibara ya 37 naomba marekebisho yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, ibara hii imezungumzia utaratibu wa kuandikishwa kwa wapiga kura. Kwa kuzingatia kwamba ibara ya 43 iliyokuwa kwenye Muswada wa mwanzoni imeondolewa. Kwa maoni yangu sidhani kama ni sahihi kuondoa kipengele kinachomtaka Mtanzania ye yeyote aliye kujaa ya nchi kupiga kura.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nashauri kwasababu hicho kipengele cha 47 tayari kimeshaondolewa, ningeomba ufanyike utaratibu wa kuongeza maneno haya chini ya kipengele cha 37 baada ya kifungu cha pili; yaani kinapoishia kifungu cha pili yaongezwe maneno yafuatayo: "Raia wa

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. LETICIA M. NYERERE]

Tanzania waishio nje ya nchi wapewe siku zisizopungua 60 kujandikisha kupiga kura."

Mheshimiwa Spika, bado naona umuhimu wa Watanzania wanaoishi nje wakiwa kama Watanzania, wana haki ya kikatiba kuruhusiwa kushiriki katika zoezi hili muhimu. Kwa hiyo, ningeomba sasa yafanyike marekebisho maneno haya yaongezwe pale ili kutoa mwanya kwa Watanzania wote kupata nafasi ya kupiga kura.

Mheshimiwa Spika, ahsante. (*Makof*)

SPIKA: Ahsante. sasa namwita Mheshimiwa Khatibu Saidi Haji atafuatiwa na Mheshimiwa Yahaya Issa. Naona hayupo, basi Mheshimiwa Yahaya, halafu atafuatiwa na Mheshimiwa Mussa Haji Kombo.

MHE. YAHYA KASSIM ISSA: Mheshimiwa Spika, kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Natangulia kwa kusema kwamba naunga mkono moja kwa moja Sheria hii, iliyombele yetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, mimi sina mengi ya kusema lakini kuna mambo kidogo yamenichanganya na nina wajibu wa kuyaweka wazi katika Bunge hili.

Mheshimiwa Spika, Zanzibar ina Serikali yake na nchi yoyote ambayo ina Serikali yake, ina maana lazima itakuwa na Sheria zake, mahala popote pale. Kwa hiyo, Zanzibar ina Sheria zake na hata katika taratibu za Uchaguzi, tunajua kwamba kule kuna ZEC, kuna NEC na ZEC. Kwa hiyo, utaona kwamba pana tofauti. Sasa tuna wajibu wa kufuata Sheria zile, kuziheshimu Sheria za nchi moja kutokana na nchi nyingine, ni wajibu wetu kuziheshimu. (*Makof*)

Kwa hiyo, Sheria ambayo ipo Tanzania Bara haiwezi tena kuikinga Sheria iliyopo Zanzibar, wala Sheria ya Zanzibar haiwezi tena kuikinga Sheria iliyopo Tanzania Bara. Kwa hiyo, hili lazima kwanza tulijue na taratibu ambazo zinastahiki kufuatwa.

Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)

[MHE. YAHYA KASSIM ISSA]

Tunaelewa wazi kwamba katika shughuli zetu hizi za upigaji kura, Zanzibar kuna Sheria yake, kuna taratibu awe Mkazi na atimie muda wa miaka mitano. Hili tunalielewa. Sasa huwezi kuja mto a mtu ambaye unasema Mzanzibari kazaliwa Bara kwa muda wote, anaishi Bara kwa muda wote, halafu useme kwamba aje apige kura kule. Hili haliwezi kuwa. Hii haimkiniki kabisa!

Ujanja huu mara nyingi unapita; mimi siku moja nipo pale Bandarini kuna mtu anatoka Tabora lakini hata ile Zanzibar hajui. Mimi nikamwuliza, wewe kijana unakwenda wapi? Akaniambia Mimi wazee wangu wanatoka Zanzibar lakini umri huu unaoniona maisha yote nipo Tabora. Halafu mtu yule ukaseme akapige kura, haiwezi kumkinika. Kule kuna Sheria yake na tufuate Sheria.

Jambo lingine ambalo hapa linataka kuzuka, mimi nataka kuweka wazi kabisa. Kule kweli kuna Masheha lakini Masheha wale ni Masheha wa watu wote, wa kijiji chote ambacho Sheha yupo. Wala hawezikubagua kwamba huyu labda yupo fani fulani, yule ni kiongozi, ni kiongozi wa Serikali kama huku tunasema kiongozi wa vijiji. Kwa hiyo, hakuna Ubaguzi kwamba niweze kumzuia mtu kwamba labda asiende kupiga kura, kwamba labda yupo Chama fulani hapana. Kama inamkinika hivyo, basi yasingetokea matatizo, yasingetokea matokeo kwamba baadhi ya vijiji kwamba labda wanatokea Chama kingine.

Kwa hiyo, unaona kwamba wanatokea Chama kingine kwa sababu Ubaguzi, anastahiki mtu yoyote kupiga kura, wakati muda umefika akili zake timamu na hana matatizo. Kwa hiyo, hili alilizungumza kiongozi aliyepita, kabisa afute usemi wake, hakuna taratibu hizo. Sisi tunakwenda vizuri kabisa wala hakuna matatizo.

Mheshimiwa Spika, kubwa ilikuwa nataka kuweka wazi hayo ili yaeleweke kwa sababu yanaingia katika *Hansard* isije ikaonekana labda Masheha Zanzibar wanafanya Ubaguzi, hakuna Ubaguzi. Ni watu waliochaguliwa na Serikali, ni watu wa vijiji wanaendesha

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. YAHYA KASSIM ISSA]

shughuli zao, matatizo yanakuja na wala hajazuiwa mtu kwamba labda asipate kadi. Hajazuiwa mtu asipate kitambulisho, hajazuiliwa mtu kabisa. Kila anayetaka, anapata kitambulisho, wala hakuna Ubaguzi huo.

Kwa hiyo, hili napenda kuliweka sawa ili lieleweke. Mimi kwa kweli sina tatizo na Sheria hii, sina tatizo la Muswada huu, sina tatizo nao. Nau-support mia juu ya mia, tunangoja kazi ili tuhitimishe wajibu uliowekwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Haji Kombo, atafuatiwa na Mheshimiwa Riziki Omari Juma.

MHE. MUSSA HAJI KOMBO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kunipa nafasi ili kutoa mawazo na mchango wa Muswada huu.

Mheshimiwa Spika sitaki kujibu au kuendeleza maelezo ambayo Mheshimiwa amekaa kitako saa hivi. Yeye anatoka Zanzibar na mimi natoka Zanzibar na bahati nzuri ye ye anatoka CCM na Mimi natoka CUF. Sipendelei kupinga wazo la mtu ambalo mwenyewe analifikiria wengine watalifikiria ni sahihi. Kama anavyosema Masheha ni wa Serikali na ni watu wote, sasa angelitizama kwanza Sheha anapatikana vipi, nani anatoa pendekexo, nani anatoa maamuzi. (*Makofi*)

Sasa hapo nitamsaidia sana. Angetizama pia wale ambaao wanatoa uamuzi wa yule Sheha wanampa agizo gani, afanye kazi gani, ili aweze kuisaidia nchi yetu. Mambo mengine mazuri Sheha anafanya, anatoa vyeti vyaa ndoa, anatoa vyeti vyaa kulima na kadhalika. Lakini issueya uchaguzi Zanzibar ni uhasama na unaanzia hapo.

Mheshimiwa Spika, sasa mimi nakubaliana na Muswada huu. Nakubaliana sana kuwapa haki wananchi ya kuamua wanachokitaka. Lakini ninachosema, tutakwenda

Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)

[MHE. MUSSA HAJI KOMBO]

Kinyume sana kwasababu suala hili ni la Muungano. Tukitazama watu ambao wana haki ya kupiga kura ni Watanzania wote; ambaye amefika umri wa miaka ya 18 hakukoseshwa haki yake ya uraia, maana yake hana akili au yupo gerezani.

Sheria zetu zote zinasema, mtu yeyote atakayefika umri wa miaka 18 ana haki ya kupiga kura. Bahati mbaya sana Zanzibar huwezi kupiga kura au huwezi kuwa na kura mpaka uwe na kitambulisho cha ukaazi. Maana yake Katiba haikuwa na nguvu, kuliko kitambulisho cha ukaazi. (*Makof*)

Watu wengi wamekosa haki hiyo, na anayesababisha kukosa haki hiyo ni mtu mmoja; ni Sheha tu. Lakini pia nakubaliana naye Sheha kwasababu ya mtu aliyemwajiri kazi. Sasa tunazungumzia suala la Kura ya Maoni ya suala la Muungano. Bara au Muungano hakuna Sheria inayosema Mtanzania aliyeppita miaka 18 hatakuwa na haki ya kupiga kura kwasababu hana kitambulisho cha aina yeyote. (*Makof*)

Je, haki hii itakuwa sahihi, ikiwa Wazanzibari, Watanzania wengine hawatapiga kura kwasababu ya kukosa kitambulisho cha ukazi na kwa hivyo, hakuandikwa kwenye buku la kupiga kura.

Mheshimiwa Spika, naomba, napendekeza sana, kwa kuondoa utata uliopo, buku la Kupiga Kura la Zanzibar lifutwe, waandikishwe Watanzania wenyе umri zaidi ya 18 wenyе haki ya nchi yao ya Tanzania. Msitugawe kwa Ubaguzi, mambo ya Ubaguzi yasiletwe. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, haiwezekani kwenye kura hii anayetoka Tabora ataandikishwa bila kuulizwa lolote, lakini anayetoka Michweni hawezi kuandikishwa mpaka awe na kitambulisho cha ukazi kwenye Kura ya Maoni ya kuitaka Katiba mpya, haiwezekani¹ Tungojane kwenye Serikali zetu zitakavyokwenda kule. Tupigane, tuuane, atangazwe atakiwaye, lakini kwenye Katiba lazima twende sawa sawa pande zote mbili. (*Makof*)

Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)

[MHE. MUSSA HAJI KOMBO]

Mheshimiwa Spika, tumezoea kusema uwongo, tumezoea kuwa si wakweli na tunazoea kutaka kuficha. Mimi naomba kuwaambieni tu, vyama vyote hivi vilivyopo vimetoka ndani ya mfupa wa CCM, CHADEMA, CUF sijui NCCR Mageuzi, na vingine vyote. Tulikuwa viongozi wakubwa, sasa tunajua mbinu zote hizi ndiyo tukawaombeni wenzetu tusije tukafika mahali tukaona kwamba aah, hata Katiba leo yapelekwa kichama! Kwa nini nikasema hivyo? Yule mwenye uwezo wa kutoa kitambulisho cha ukazi wa Zanzibar ni Sheha. Anatoka wapi? Sasa anayemzuia, anayefanya lolote anampunguzia haki yake ya uraia. Naomba hilo lifikiriwe sana.

La pili, katika vituo ambavyo vitatumika kwa kupiga kura ambapo inaelezwa safi hapa. Kimoja ni gari. Kituo kimoja ambacho kitahusika kupiga kura ni gari. Sasa mimi sijui nimewahi kuona gari za *Ambulance* zinazochukua wagonjwa, maiti na kadhalika. Naona gari za abiria, gari ya Rais pia gari nyingine. Sasa naomba ufanuzi, ni gari gani hizi ambazo zitakuwa Vituo vya Kupiga Kura. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, sijakataa kwamba gari haiwezi kuwa kituo. Lakini itakuwa ni wapi pasipokuwa na Kituo gari ikawa ndiyo kituo? Je, kila apitae njiani ataitwa; wewe umepiga kura au hujapiga kura? Gari tayari itapiga kura. Nawaombeni sana Waheshimiwa nipate ufanuzi wa aina ya gari na aina ya kituo kitakachokuwa cha gari. Mimi wasiwasi wangu, hakutakuwa na utapeli ndani ya gari humo? (*Kicheko/Makof*)

Mheshimiwa Spika, alikuwa amesema Mjumbe mmoja hapa kwamba vituo vingine vilikuwa vina fujo na ghasia. Sasa hii gari ndiyo itakwenda kule kwenye vile vituo vyenye fujo na ghasia iondoe fujo? Naomba ufanuzi huo.

Mheshimiwa Spika, naomba kila la heri kura hii ya maoni watu waamue kwa mujibu watakavyoona nchi yao iende vipi.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru. (*Makof*)

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

SPIKA: Ahsante. Nilisema nitamwita Mheshimiwa Riziki Omar Juma, atafuatiwa na Mheshimiwa Peter Serukamba.

MHE. RIZIKI OMAR JUMA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii ili nami nichangie machache katika Muswada huu wa Sheria ya Kura ya Maoni ambao ndiyo utakaotupelekea kupata mustakabali wa Katiba wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kusema kwamba sina tatizo na huu Muswada, utatupeleka pazuri, ila kuna mambo madogo madogo nami naomba niyachangie. Naomba nianze na kwenye tafsiri.

Mheshimiwa Spika, tafsiri ya mwanzo ambayo nilitaka nianze nayo ni Kituo cha Kupigia Kura ambayo Mheshimiwa Mussa ameisema. Tumezoea sana kuona matatizo mbalimbali yanayojitokeza katika Vituo vya Kupigia Kura. Tunapokuja kusema kwamba gari ni Kituo cha Kupigia Kura ni utata mkubwa na ninaomba suala hili liondoke hapo mara moja, turekebishe kifungu hicho ili neno 'gari' tuondoe.

Mheshimiwa Spika, la pili tafiri ya "Waziri mwenye dhamana ya masuala ya Uchaguzi" naomba hapo isomeke kwamba: "Waziri mwenye dhamana ya masuala ya Uchaguzi kwa upande wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar."

Tatu, naomba niende kwenye tafsiri ya maana ya neno "Rais". Pale ametajwa tu "Rais wa Jamhuri ya Muungano." Lakini naomba tuweke "na Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar."

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 37(2) kinasema Tume kwa madhumuni ya Kura ya Maoni itaweka utaratibu wa kuandikisha raia wa Jamhuri ya Muungano ambao wanaishi nje ya Jamhuri ya Muungano na ambao hawajasajiliwa kama wapiga kura katika Daftari la Wapiga Kura.

Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)

[MHE. RIZIKI OMAR JUMA]

Mheshimiwa Spika, hapa naomba nipazungumzie kidogo kwamba wananchi hawa amba wapo nje ya nchi, watapewa fursa hii kwa kutumia utaratibu amba o utaanishwa au utawekwa na Tume. Lakini tukumbuke kwamba kuna Watanzania wengi au Wanzibari wengi amba wanaishi katika nchini hapa hapa lakini wamenyimwa hiyo fursa au haki ya kupiga kura kutokana na Sheria ya Uchaguzi ya Zanzibar ambayo inalazimisha kwamba mpiga kura au mtu anayeweza kupata haki ya kitambulisho cha Mzanzibari ili aweze kuwa mpiga kura lazima awe anaishi katika eneo ndani ya miaka mitatu. Lakini pia awe na cheti cha kuzaliwa.

Mheshimiwa Spika, kuna watu amba wana umri wa zaidi ya miaka 80 hawana cheti cha kuzaliwa, ni maskini, ni wanyonge, taratibu zinazoweza kumfanya apate cheti cha kuzaliwa ni ngumu zinahitaji fedha nyingi ambazo hana uwezo hata kupata mlo wake wa siku moja. Ananyimwa haki hiyo. Tunamfanyaje huyu? Tunamweka katika kifungu gani? Tunamnyima haki ya kuandika Katiba yake naye, kutoa mawazo ya kupata Katiba ya nchi yake?

Mheshimiwa Spika, zaidi ni kwamba Sheria ya Zanzibar ambayo inatunyima hii fursa na Wanzibar wengi amba pengine wako hapa Tanzania Bara katika kuhangaika kutafuta maisha, wengine wako pale pale Zanzibar, lakini ananyimwa hiyo fursa kutokana na kipengele hicho ambacho kinamlazimisha apate cheti cha kuzaliwa.

Mheshimiwa Spika, naomba nikwambie kwamba wenzenetu hawataki kuwa wakweli. Sheha ni kikwazo kikubwa, ni tatizo kubwa katika nchi yetu ya Zanzibar katika kupata watu haki zao. Siku moja nilimwambia Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mheshimiwa katika Kamati za Ulinzi na Usalama ukituvekea Sheha umemaliza nchi hii. Kamati ya Ulinzi na Usalama ikianzia katika eneo la Sheha sisi umetumaliza. Ibakie hapo hapo ngazi ya Wilaya. Mheshimiwa Jenista Mhagama muda mrefu alikuwa ananiita Sheha kwa tatizo hilo. Mheshimiwa Sheha ni tatizo! Ni kikwazo kikubwa kwetu Sheha! (Makof)

Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)

[MHE. RIZIKI OMAR JUMA]

Mheshimiwa Spika, mimi ni Katibu wa Wilaya katika wa Chama changu. Nina watu zaidi ya 10,000 hawana vitambulisho vya Mzanzibar na kwa maana hiyo hawana haki ya kupiga hiyo Kura ya Maoni. (*Makof!*)

Sheha anaitwa, mnaitwa kikao cha pamoja anaagizwa wapeni watu wajaze fomu hizo ili waweze kupata kitambulisho. Halafu anapitiwa kwa mlango wa nyuma, anaambiwa zuia, uzi ndiyo huo huo! Huo ndiyo ukweli! Wenzetu wapende wasipende huo ndiyo ukweli jamani. Njooni kwetu mwone hali halisi wa mambo yalivyo. Tuna tatizo! Sheha ni kikwazo! Watu wananyimwa fursa zao hivi hivi bure bure. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, lazima tutafute dawa ya kuhakikisha watu wanapata haki yao ya kupiga kura ya maoni. Vinginevyo tunalipeleka Taifa hili pabaya, Katiba hili itawekwa na watu wachache. Siku za mbele zinazokuja tunawaletea watoto wetu tatizo.

Mheshimiwa Spika, hili ni tatizo la muda mrefu. Hii ni Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Siku moja nilisema ndani ya Bunge hili, jamani pesa za uchaguzi ambazo zinatolewa na wenzetu wanaotusaidia kutufadhilli kuandaa Daftari la Wapiga Kura na mambo mengine, zinatumwi vibaya. Wananchi hawapati haki. Sasa basi, ikiwa wananchi walio wengi; nitoe mfano Kisiwa cha Kojani. Kojani iko katika Wilaya yangu ya Wete. Hawa hawajui utaratibu jinsi gani mtoto akizaliwa waende wakapate cheti cha kuzaliwa. Ni tatizo!

Sasa leo mtu anafika miaka 20 hana cheti za kuzaliwa, akienda wanamwambia aende akapate cheti cha kuzaliwa kwa kutumia *processya* Mahakama au aende akapate cheti Unguja. Cheti cha kuzaliwa, mtoto aliyezaliwa leo anafika mwaka hajapata hicho cheti.

Mheshimiwa Spika, hivi ninavyoongea kuna watu wako katika Ofisi ya Vitambulisho wanasubiri wapatiwe *Zan ID* ili waweze kuandikishwa katika Daftari la Wapiga Kura, wanapigwa dana dana. Akienda leo kama kajaaliwa

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. RIZIKI OMAR JUMA]

kwenda nacho kwanza anaambiwa kwamba hiki cheti kina makosa. Cheti katoa nani? Kama kina makosa! Nani katoa cheti? Ooh, cheti hiki sijui kimechorwa, sijui kimetiwa tarehe siyo. Nani katoa? Mkojani huko anaweza kuandika cheti, akaja nacho pale? Micheweni anaweza kuandika cheti akaja nacho pale? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tuna tatizo na hii Sheria tunayokwenda nayo sasa tunakwenda katika zoezi muhimu sana la kihistoria la nchi yetu, kama hatukuwa waangalifu, tutaharibu sana na hatimaye hatutaipata Katiba tunayoitaka kwa kufuata matakwa ya mtu au mawazo ya mtu mmoja. Nawaomba Mheshimiwa nyinyi Serikali naomba muwape watu haki zao. Msiangalie matakwa ya Vyama? (*Makofi*)

Kule Zanzibar Mheshimiwa Rais anasema, wapeni watu wote *Zan ID* kila anayestahili kupata *Zan ID* apewe ili aweze kupata haki ya kuandikishwa. Mlango wa nyuma unafunguliwa, anaambiwa, zuia! Usitoe! Sheha anayezuia kutoa fomu ndio anayepewa kipaumbele. Ndio Sheha anayesifiwa huyo! Huyo ndiyo Sheha anayasifiwa katika Serikali ya Zanzibar. Tusifichane, naomba sana Waheshimiwa twende tuhakikishe kwamba watu wanapata haki zao.

Mheshimiwa Spika, hili ni jambo ambalo tutalisema sana, tutalisema kwa vinywa vipana, bado kuna ukiritimba mkubwa, wananchi walio wengi hawana *Zan ID*. Mimi binafsi kama mtoto wangu sikumpeleka mimi mwenyewe kwa Sheha, nakuhakikisha angepigwa danadana, ni kwa sababu Sheha ananijua. Angepigwa danadana! Akienda mtu mwingine, atamwambia njoo kesho, njoo Ijumaa, njoo keshokutwa. Sasa hivi nasali, sasa hivi niko Msikitini. Ndizo hoja zinazotolewa za ajabu ajabu. Mkuu wa Wilaya ndio anachangia kwa kiasi kikubwa kumwambia Sheha, usitoe! (*Makofi*)

Mimi nafanya nao kazi kwa karibu, tunaambizana, tunazungumza. Lakini hatimaye ukiondoka mlango wa nyuma unafunguliwa anaambiwa Sheha, hatoi. Wa CCM mpaka wa miaka 12 wameshapewa *Zan ID*. Hawana mtu

Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)

[MHE. RIZIKI OMAR JUMA]

wao ambaye hana *Zan ID*, hawana kabisa! Njoo kwa watu wanaojulikana kama ni Vyama vyta Upinzani, hawana. Hili suala litatupeleka pabaya.

Naomba sana Serikali iliangalie kwa umakini ili watu wote waweze kupata haki yao ya kupiga kura ya maoni.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Peter Serukamba, atafuatiwa na Mheshimiwa Ali Khamisi Seif.

MHE. PETER J. SERUKAMBA: Mheshimiwa Spika, nami nikushukuru kwa kunipa nafasi nichangie Muswada huu muhimu. Kwanza nianze kwa kuunga mkono hoja ya Serikali. Jambo hili ni kubwa na kwa kweli katika nchi nyngi zilizotengeneza Katiba, ni nchi chache sana duniani zilizoamua kwenda kwenye Bunge la Katiba, kwenda na kwenye kura za maoni. Kwa hiyo, sisi tumechukua njia ambayo ni ya kidemokrasia zaidi. Naipongeza Serikali, ingawa ina *challenge* zake hii njia tulioamua kuchukua.

La pili, nilikuwa namsikiliza Msemaji wa Upinzani, alijaribu kujenga hoja ya kwamba hapa tunavunja Katiba. Nia yangu siyo kuitetea Serikali, lakini nataka labda kuweka rekodi sawa. Mimi naamini moja ya jukumu letu ni kutunga Sheria na kazi tunayoifanya hapa ni ya kutunga Sheria kwa ajili ya kura ya maoni. Nadhani Katiba hiyo inaturuhusu kutunga hii Sheria. Tungeamua kufanya kura za maoni bila kutunga sheria hii, hapo tungakuwa tunavunja Katiba. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, jambo langu la muhimu ni kuhusu kuandikisha Wapiga Kura ama kuboresha Daftari letu. Zanzibar wao wameanza kwa ajili ya kuboresha Daftari. Tanzania Bara hatujaanza. Lakini Tanzania Bara nchi ni kubwa. Mimi nangeomba watuhakikishie hasa watu wa Tume ya Uchaguzi kwamba kweli wataifanya kazi hii; tunaweza tukasema tutaenda haraka, lakini tukaacha

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. PETER J. SERUKAMBAJ]

watu wengi sana. Nia yetu tunataka zoezi hili ama Katiba hii kwa kweli iandikwe na wananchi. (*Makofii*)

Kwa hiyo ningeomba sana watu wa Tume ya Uchaguzi wapewe nyenzo, fedha na muda ili kazi hii tuhakikishe kila ambaye anatakiwa kuandikishwa apate nafasi ya kuandikishwa. Kwangu mimi hili ndiyo la muhimu sana ili tuweze kuifanya kazi hii vizuri.

La pili Mheshimiwa Spika, kwangu mimi ni elimu kwa Wapiga Kura. Kwenye kura ya maoni kwa Tanzania Bara ni jambo jipya. Sasa lazima suala la elimu lifanye kazi kubwa sana. Tusipotoa elimu nya kutosha, watu wengi hawataenda kupiga kura siku hiyo. Nyie ni mashahidi, tumekwenda kwenye chaguzi, mwaka 2010 zaidi ya watu asilimia 50 hawakupiga kura. Sasa hapa ndiyo wanapochagua Diwani wanayemfahamu, Mbunge na Rais.

Sasa kwa hili tusipofanya elimu, tutakosa mtu wa kuli-*own*, tutakosa mtu wa kusema hili tulifanye ama kulimiliki; natafuta Kiswahili kizuri; nani wa kumiliki mchakato huu? Kama kwenye chaguzi ya kawaida tumeona watu zaidi ya asilimia 50 hawaendi kupiga kura, tusipoendesha elimu vizuri na tukapata mtu wa kulimiliki zoezi hili, tutapitisha Katiba, wamepiga kura watu wachache hasa Wanaharakati na sisi Wanasiaya. (*Makofii*)

Kwa hiyo, mimi nasema, mimi ninapopata taabu ni hapa kwenye elimu, kwa sababu tunavyoendesha mambo yetu, tunaenda haraka haraka, ni mchaka mchaka. Jambo hili ni kubwa. Unaona jambo hili litasimamiwa na Tume ya Uchaguzi. Tume ya Uchaguzi ndiyo watafanya kila kitu, ndiyo watahesabu kura, ndiyo watafanya kila kitu pamoja na vyombo vya Ulinzi na Usalama. Kwa hiyo, ili tuweze kufanikiwa suala la elimu ni kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, lakini elimu tunaanza kuitoa lini? Muda wa kuitoa hiyo elimu ni muda gani? Maana tunakwenda kwenye Bunge la Katiba. Tutamaliza siku 70, tukimaliza tutaanza kuandika hiyo Katiba sasa ambayo

Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)

[MHE. PETER J. SERUKAMBAJ]

itakuwa imetungwa. Baada ya pale, kabla ya tarehe ya kupiga kura, tunahitaji muda gani wa kufanya hiyo elimu? Hapa ndipo panapotia wasiwasi tu. Tunaweza tukafanya, na muda wenyewe tumebakwa *almost* na mwaka mmoja, na wakati huo tunamaliza Bunge hilo tunakuja kwenye Bunge la Bajeti, ili tupate fedha zenyewe za kwenda kufanya hiyo kazi. Mimi shida yangu, ni muda gani tunautenga? Naomba wakati Serikali inajibu waeleze wanadhani ni muda gani wametenga kwa ajili ya elimu? Maana tusipowaelimisha watu vizuri, zoezi hili tutakuwa tumpoteza fedha bure. Tutatunga Katiba *yes*, lakini itakuwa imetungwa na watu wachache sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo mchakato unaoendelea sasa, tumejitahidi sana, Tume imekwenda nchi mzima, imefanya kazi mpaka wameomba waongezewe muda kwa sababu kazi ni kubwa. Sasa tunamaliza tutakuwa na kazi ya kuteua, tukimaliza tunaingia kwenye Bunge lenyewe. Kwa hiyo, hata muda wa wanasiisa kwenda kusakidia suala la elimu mimi siuoni hapa. Ndiyo maana nasema, nataka jibu. Kwangu mimi suala kubwa kwenye huu Muswada kwangu ni elimu, ili siku hiyo tuhakikishe Watanzania wengi wanakwenda kupiga kura ya maoni.

Kwa hiyo, mambo makubwa kwangu ilikuwa ni hili la kwanza, naamini hatujavunja Katiba, kwa sababu ndiyo maana tunatunga Sheria, na Katiba tulioapa inaturuhusu kutunga Sheria, na hii ni kazi yetu; lakini pia la kwangu ni tuharakishe Tume ya Uchaguzi ianze mchakato. Habari zilizo rasmi, wamechelewa kwa sababu walikuwa hawjapata fedha. Kwa hiyo, hata *Procurement* ya vifaa imetumia muda mrefu. Sasa tuulizane, kama tunaendelea hivi hivi na kesho kutwa tuna mahali tunakwenda, kama watakuwa hawajamaliza tutapata matatizo, tutafanya haraka haraka, tutakosa muda wa kuandikisha suala hili.

La mwisho, ni kwenye kuandaa hayo maswali. Tujitahidi tuwashirikishe watu wengi zaidi ili kuweza kupata maoni ya kuandaa hayo maswali ya kwenda kuuliza kwenye Kura ya Maoni. Kwa sababu tumeamua kwamba tunataka

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. PETER J. SERUKAMBA]

tutunge Katiba ambayo ni shirikishi, ndiyo maana unaweza ukaona tumepanua sana Bunge la Katiba ili waingie watu wengi sana kwenye hili Bunge, kwa maana ya kushirikisha jamii yetu yote. Sasa kama huko tumefanya vizuri, ni vizuri sasa na tufanye vizuri katika kuhakikisha tunawaandikisha watu wengi zaidi, watu wasikose nafasi.

Lakini namba mbili, tuhakikishe sasa tunafanya elimu na tupate watu ambao watausimamia huo mchakato wa kura ya maoni na ambao ndiyo watakuwa wanamiliki hili zoezi liweze kufanikliwa vizuri.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja hii. (*Makof*)

SPIKA: Ahsante, Mheshimiwa Ali Khamis Seif.

MHE. ALI KHAMIS SEIF: Mheshimiwa Spika, kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunijalia uhai na uzima kuweza kusimama katika Bunge lako Tukufu. Lakini la pili, nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Spika, tunaingia, au tunajadili Muswada wa Kura ya Maoni. Muswada ambao utaifikisha nchi yetu katika kuamua Katiba ambayo tunaihitaji.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu mkubwa ni suala zima la ushirikishaji wa wananchi katika suala hili la Kura ya Maoni. Ni kiasi gani Sheria hii, au Muswada huu tunaoujadili utawashirikisha wananchi wengi kwa kadri itakavyowezekana ili kuamua hatma ya nchi yetu? (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, ukiangalia Muswada huu, Kifungu au aya inayowashikirikisha au inayowataka wananchi washiriki, unakuta kiko katika Kifungu cha 9(1) na (2). Kifungu hiki kinatambua uwepo wa madaftari mawili, ambayo nakubali ndiyo msingi wa suala zima. Kuna Daftari ambalo liko chini ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi, na Daftari ambalo liko chini ya Tume ya Uchaguzi la Zanzibar.

Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)

[MHE. ALI KHAMIS SEIF]

Mheshimiwa Spika, vile vile katika Muswada huu, Kifungu cha 36 kinatambua au kimeipa mamlaka Tume, kuweza kuanzisha utaratibu wa kupata maoni au kuandikisha Watanzania ambao wako nje ya nchi. Ni jambo zuri ingawa lina matatizo yake.

Mheshimiwa Spika, Daftari la Tume ya Taifa ya Uchaguzi, naamini tatizo lake kubwa au changamoto kubwa ni kuliboresha, ambalo Waheshimiwa Wabunge wamelishazungumza. Daftari la Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar, tayari wanaliboresha, lakini ninachosema ni kuwa uboresha huu, bado Daftari hili lina matatizo makubwa. (Makof)

Mheshimiwa Spika, Daftari hili limewaacha Wapiga Kura, ambao waliwahi kupiga Kura mwaka 2000 na mwaka 2005. Nlnachokisema ni kuwa kuna Wanzibari ni wakazi, wamezaliwa Zanzibar, wanaishi Zanzibar, kama kutembea, basi ni kwenda kutembea sehemu za mbali. Lakini wanaishi katika maeneo hayo hayo, lakini hawamo katika Daftari hilo. (Makof)

Kwa hiyo, tukitegemea Daftari pekee la Zanzibar la Wapiga Kura, basi wako wananchi wengi tutawaacha ambao hawatapiga kura ya maoni, hili ni jambo ambalo siyo sahihi.

Mheshimiwa Spika, uzoefu wa nchi ya, kwa mfano Zimbabwe ambayo imewahi kupiga kura ya maoni. Wao walipokwenda katika Kura ya Maoni, hawakutegemea Daftari la Wapiga Kura, lile linalohusiana na Chaguzi la Viongozi, kwa sababu wenzetu wamepiga hatua katika Vitambulisho vya Uraia, ambapo kila mwananchi aliyefikisha umri wa miaka 16, basi anakipata kitambulisho hicho; wao waliruhusu vile vile wananchi wapige kura kwa kutumia Kitambulisho cha Uraia. Lengo lilikuwa, ili wananchi wengi washiriki. (Makof)

Mheshimiwa Spika, tatizo hili la Zanzibar kwa kweli nasema ni kubwa, hata Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar

Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)

[MHE. ALI KHAMIS SEIF]

wanatambua. Nina ushahidi huu hapa ambao nitauwasilisha kwako baadaye. (*Makofii*)

Tume ya Uchaguzi wa Zanzibar, wakati wanataka kuboresha Daftari la Wapiga Kura, wametoa kipeperushi hiki hapa, na wameeleza pia watu ambao wataandikishwa katika kuliboresha Daftari. Wametaja kama Kada aina sita. Lakini nitasoma hii ambayo itanisaidia sana katika maelezo yangu.

Wapiga kura wanaohusika kujiandikisha na uendelezaji wa Daftari la kudumu la Wapiga Kura, wametajwa hapa. Kwanza labda nianze. "Wale ambao mpaka wakati wa kazi ya kuandikishaji katika maeneo yao wametimiza miaka 18 na wametimiza masharti ya kuandikishwa kwa mujibu wa Sheria ya Uchaguzi wa mwaka 1984. Lakini wa pili, Wapiga Kura ambao awali wallandikishwa kuwa Wapiga Kura mwaka 2005, lakini kutokana na sababu mbalimbali hawakuwahi kubadilisha shahada zao za zamanii na kupigia kura katika kazi ya kuandikishaji iliyofanyika kati ya mwaka 2009 na 2010. Hii inaonesha kuwa wanakubali Tume ya Uchaguzi kuwa kuna wananchi ambao wameshiriki Uchaguzi wa mwaka 2005. Lakini hawakubadilishiwa, matokeo yake hawakushiriki katika Uchaguzi wa 2010. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hapa nina ushahidi, na nitauwasilisha kwako. Kuna mwananchi mmoja ana umri wa miaka 39, anaishi Uweleni Mkoani Pemba katika Jimbo langu. Huyu kashiriki uchaguzi wa mwaka 2000 na mwaka 2005. Kwa sababu ya kitambulisho cha Uzanzibari Ukaazi, na hana cheti cha kuzaliwa, Uchaguzi wa mwaka 2010 hakushiriki. Kwa hiyo, mwananchi huyu hatashiriki katika Kura ya Maoni, kwa sababu hayumo katika Dafatari la Wapiga Kura la Zanzibar. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mwananchi huyu anaitwa nani? Anaitwa Doto Haji Mohamed. Ni mkazi wa Uweleni, umri wake ni miaka 39 lakini nasema tena uchaguzi wa mwaka 2010 hakushiriki.

Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)

[MHE. ALI KHAMIS SEIF]

Vile vile mfano mwagine unahusiana na mwanamke, ni Asha Said Abeid, umri wake ni miaka 31 mkaazi wa Wambaa huyu. Huyu kashiriki uchaguzi wa 2005, lakini uchaguzi wa mwaka 2010 hakushiriki, kwa sababu hana Zanzibar *Identity Card*.

Mheshimiwa Spika, hili ni tatizo. Kama litafumbiwa macho na lifumbiwe, lakini hili tatizo lipo, na ushahidi ni huu. Haya yote nataka nikukabidhi wewe utajua pa kuyapeleka ili yafanyiwe kazi, lakini hili lipo, na linahitaji lichukuliwe hatua. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tunazungumzia Kura ya Maoni, hatuzungumzii Uchaguzi wa Zanzibar, kwa hiyo sheria hii inao uwezo kuweka Kifungu cha kuanzisha Daftari pengine lingine maalum kwa Wanzibari wanaoishi Zanzibar, ili wapate fursa hili. Wakishaipata, basi limekwisha. Chaguzi za Zanzibar tutakwenda hivyo tunavyokwenda, ndio inavyotakiwa.

Kwa hiyo, ninahisi Mheshimiwa hili lifanyike. Kufanyike marekebisho, Serikali ishauriane na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, waone ni kwa kiasi gani wananchi hawa; hawa wameshiriki katika chaguzi, kuna wengine wengi hawamo hata katika kushiriki na watakosa.

Kwa hiyo, tunaweza tukaamua Kura ya Maoni hiyo kwa wananchi ambao wengine watakuwa hawakupata fursa hii.

Mheshimiwa Spika, nadhani tukilichukulia hatua hilo, tunaweza tukaondoa tatizo kubwa katika Muswada huu. Ahsante sana. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Khatibu Said Haji.

MHE. KHATIB SAID HAJI: Mheshimiwa Spika, ahsante. Naashukuru kwa kunipa nafasi name niweze kuchangia mada hii muhimu yenye mustakabali nadhani utakuwa mwema kwa nchi yetu.

Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)

[MHE. KHATIB SAID HAJI]

Mheshimiwa Spika, nami nataka kuanza kwa kuipongeza Serikali, kwa kuona umuhimu wa jambo hili na kulikubali mpaka leo hii tuko kwenye hatua ya kujadili namna gani ya Kupiga Kura ya Maoni.

Mheshimiwa Spika, kwa sisi tunaotoka upande wa Zanzibar, tutakuwa, kwa bahati mbaya sana kuna neno linalojirudia, lakini tunaomba utuvumilie; kuhusu suala hili la Masheha. Nitalizungumza, lakini kwanza nataka nizungumzie suala la Kifungu cha 361, kinacho sema kwamba wale walioko nje, kama itakubalika, waandikishwe kwa mujibu wa Tume itakavyoona.

Mheshimiwa Spika, walioko ndani ya nchi, tunajua kwamba kuna Mawakala wa Vyama wanaokaa kudhibitisha wale wanaoandikishwa. Hili lilikubalika kama Tume itakavyoona: Je, hapa kwa upande wa uwakilishi wa Vyama atakayethibitisha ni nani? Naomba hili liwekwe wazi ili tuelewe. Kama ikiwekwa tu nje huko Ofisi au Ubalozi pale wanasmamia, tunataka tujue udhibiti hasa utakuwaje?

Suala lingine, tunapofikiria Watanzania walioko nje ya nchi kwamba wapate fursa hii ya kijiandikisha, lakini tunaacha kufikiria juu ya Wanzibari walioko ndani ya Zanzibar ambao wananyimwa haki hii muhimu na ya msingi. Hili ni tatizo kufikiria wa mbali, tunageuka kivuli cha mvumo, kinachostiri walioko mbali, wale walioko karibu wanapigwa na jua. Hiyo siyo tija. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, tuwfikirie wale walioko ndani ya nchi ya Tanzania, walioko Zanzibar. Hili ndiyo maana nasema tutalirudia sana, kwa sababu kule hawa Masheha wanajigeuza Miungu Watu.

Hili siyo bure, wanapewa amri na Watendaji Wakuu wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa, sijali wamo *CUF* wamo nani. Kama anahuksika na dhambi hii, wote itawatafunu; awe Makamu wa Kwanza wa Rais, awe Makamu wa Pili wa Rais, wote itawatafunu, kwa sabbau wananyima haki ya

Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)

[MHE. KHATIB SAID HAJI]

Wanzibari walioko ndani ya Zanzibar kupata haki yao.
(*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nataka nisema nia nzuri ya Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete, nia nzuri ya Serikali ya kuleta mabadiliko haya ili Watanzania waamue nini wanachokitaka juu ya hatma ya nchi yao, kinapatiwa matatizo kwa hofu iliyowatawala CCM wa Zanzibar. Hofu ni maradhi, mkiyaendekeza mtakufa siku siyo zenu. Ondoeni hofu, waacheni Wanzibari, Watanzania, kila mwenye haki juu ya maamuzi haya, wapate fursa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kuna ubaguzi, Masheha hawaruhusu watu kupata haki hii na hili tatalisema sana. Mimi binafsi Mbunge wa Jimbo la Konde, Sheha wangu alininyima karatasi ya kwenda kupata kitambulisho cha Uzanzibari. Kama ya Mbunge yamekuwa hayo raia wa kawalda yatakuwaje? Kama Kilemba kimelowa, utauliza magotini? (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, hili jambo litatuletea taabu katika maamuzi haya muhimu tunayoyafanya. Tuache kutumia Daftari la Wapiga Kura la Zanzibar. Lile siyo Daftari, lile ni uchochezi, litatuletea taabu sana! (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni zaidi ya miaka 20 na zaidi ya vyama vingi Tanzania, mwezi uliopita kwa mara ya kwanza chama cha CUF, kimefanya Mkutano katika Jimbo la Donge. Siyo kwa sababu ndivyo tulivyotaka, lakini angalau ndipo tulipopatiwa fursa hiyo. Siku zote watawala Wafalme walilokwepo kule walikuwa hawataki upinzani uingie Jimbo lile. Tumejua kwa nini walikuwa wanakataa, ni kwa sababu tutapata aibu nydingi sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nilihudhuria Mkutano ule, moja lililosemwa pale, alinyanyuka mwananchi wa Donge, bahati nzuri sana alikuwa amerudi *Al-Haj*, alikwenda kujitakasa na kuomba kwa Mungu wake. Alipanda juu ya jukwaa na akaeleza akasema Ndugu zangu mnisamehe, nilishikiri katika dhambi kubwa sana ambayo viongozi wa Chama cha

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. KHATIB SAID HAJI]

Mapinduzi walikuwa wakinituma niifanye. Nitaisex! Leo ninataka kukohoa, niteme niliyo nayo niyaseme. (*Kicheko/Makofii*)

Mheshimiwa Spika, aliwaomba radhi Wazanzibari, kwamba yeche aliwaomba ni Mpiga Kura wa Kijiji cha Bumbwini chini, lakini aliwaomba ana *Identity Card 10* za kupiga kura katika maeneo tofauti katika Zanzibar, na alitoa ushahidi kwenye jukwaa. Najua Kanuni zetu hapa zinamkataza mtu kusema uongo. Kama nasema uongo, Kanuni ichukue mkondo wake. (*Makofii*)

Alitangaza na akatoa ushahidi wa *ID 10* na alisema, yeche na wenziwe wengi waliokuwa katika mtindo huo. Leo hii tunakwenda kutumia Daftari hilo ambalo tayari hofu limewatawala, wengine wananyanya watu wazima wanasema uongo, kwamba kila anayetaka *ID* anapewa Zanzibar. Huo ni uongo! Aibu! (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tunachoomba kama nia hii nzuri ambayo Serikali inaonekana kuwa nayo, tuondoe hofu, na hofu kubwa inatawala baada ya matokeo ya Kura ya Maoni iliyo takwa kuleta Serikali ya Umoja wa Kitaifa Zanzibar, na tunatabiri matokeo yatakuwa yale yale ya kubaliana na mfumo wa Serikali tatu, hii ndiyo hofu iliyowatawala. Lakini apangalo Mungu, binadamu hawezi kulizuia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tunachosema, tunataka uwekwe utaratibu utakaowaruhusu Watanzania wote wapate haki yao ya kupiga kura katika maamuzi muhimu ambayo sisi tutayaacha na watakuja wengine watayakuta na kuyatumia hayo. (*Makofii*)

Hutakuwa tayari kukubali kuingia katika Daftari lile ambalo Tume ya Uchaguzi Zanzibar na Mwenyekiti wake wa

Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)

[MHE. KATIB SAID HAJI]

Tume ile ambaye tunamjua wenyewe jinsi alivyo na mapenzi makubwa katika hao walimteua na Wakuu wa Mikoa, wale ambao wanaamua kwa maslahi ya wakubwa waliowateua. Hatuko tayari!

Ninasema tuko tayari kuendeleza jambo hili kwa maslahi ya nchi yetu, lakini kikwazo hiki ambacho Wanzibar tunakutana nacho, mimi kwenye Jimbo langu sasa hivi nina watu zaidi ya 1,000 ambao wamekosa haki hii ya kupata vitambulisho vya Uzanzibar. Leo mnapowaleta tena kwenye kupiga Kura ya Maoni ambayo siyo uchaguzi wa Zanzibar, nyinyi tutabanana kule kwenye uchaguzi wa Zanzibar, lakini hili la Watanzania wote, tuachieni tupumue! Waachieni Wanzaibari wapumue! (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, naomba sana, leo nilitaka niliseme hili kwa mapana yake, kwamba tuko tayari kuwa pamoja na kurekebisha yale mabaya yote ambayo hayatatufikisha katika lengo, lakini hatutakuwa tayari kushiriki kwenye Kura ya Maoni tukiwaacha Watanzania wengine wa Zanzibar wakikosa haki yao hii ambayo ni ya Kikatiba na ya kimsingi.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makof*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, naomba tu angalizo. Kuna wengine wanaomba, halafu anasema atachangia kesho. Sasa watu wakiisha mimi niwasubiri wa kesho?

Kwa hiyo, yejote aliyeomba ajue ataitwa wakati wowote. Kwa hiyo, wale wanaoniambia kesho, mimi nitadharau hilo. (*Makof*)

(Saa 6.53 mchana Bunge lilisitishwa Mpaka Saa 11.00 jioni)

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

(Saa 11.00 jioni Bunge lilitrudia)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tulikuwa na wachangiaji lakini sikuwataja wakati naondoka, sasa nitamwita Mheshimiwa Masoud Abdalla Salim, atafuatiwa na Mheshimiwa Felix Mkosamali, atafuatiwa na Mheshimiwa Parecco.

MHE. MASOUD ABDALLA SALIM: Mheshimiwa Spika, nakushukuru na namshukuru Mwenyezi Mungu, *Subhana Wata'ala*, kwa kunijalia uzima na afya njema katika kuchangia Muswada huu wa Sheria ya Kura ya Maoni wa Mwaka 2013.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu ni muhimu sana juu ya hatima ya nchi yetu ya Tanzania sambamba na mchakato wa mabadiliko ya Katiba.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu wakati wa kutafuta wapiga kura au Wananchi wanaotakiwa kupiga kura kama Watanzania katika pande zote mbili za Muungano, yaani Tanzania Bara na Zanzibar, katika Visiwa vya Unguja na Pemba, wasiwasi wangu ni baadhi ya Wananchi kukosa haki yao ya Kikatiba, Ibara ya 5(1), ya kuweza kupiga kura.

Mheshimiwa Spika, hili limedhihirika, Wabunge wengi wameliongelea na mimi naendelea kuzidi kuliongelea au kulizungumza ili Serikali kwa namna moja ama nyiningine, ione basi Watanzania waliopo Tanzania Bara na waliopo Zanzibar, ambao wana haki ya Kikatiba kwa mujibu wa Ibara ya 5(1), waweze kupiga kura.

Mheshimiwa Spika, kinachonisukuma na kinachonifanya nipate wasiwasi, kuna Watanzania wengi na hasa upande ninaotoka mimi wa Zanzibar, ambao kutokana na uchaguzi uliopita wa mwaka 2010, walifikia 16,000 ambao hawakuwepo katika Daftari la Zanzibar (ZEC), walikuwepo kwenye Daftari za NEC na walipiga kura moja tu. Swali linakuja; Watanzania waliopo Zanzibar ambapo

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. MASOUD ABDALLA SALIM]

mnasema ZEC ni Wakala wa NEC wataweza kupiga kura kwa namna gani; haki yao ikoje?

Mheshimiwa Spika, hili ni vyema likapatiwa ufumbuzi na likaandaliwa mazingira yaliyo mazuri, angalau basi wale wote ambao wanaostahili kupiga kura, waliofikia umri wa kupiga kura na ambao hawapo katika Daftari za ZEC, Serikali ambayo imeleta Muswada huu wa Sheria ya Kura ya Maoni iandae mazingira ya kuhakikisha watu wale nao wanapiga kura. Vinginevyo, tunaandaa Katiba mpya lakini tunavunja Katiba tuliyonayo. Tunaandaa Katiba katika michakato yake, lakini tunavunja, kuna watu wana haki lakini hawatapata haki. Kwa hiyo, hapo itakuwa kidogo ni kichekesho.

Mheshimiwa Spika, naomba niendelee; katika kuchangia Muswada huu naenda moja kwa moja kwenye tafsiri. Ukurasa wa 39, tafrisi ya kituo cha kupigia kura maana yake chumba chochote, sehemu, gari au chombo kilichotengwa na kuwekewa vifaa kwa ajili ya upigaji kura katika kura ya maoni. Ninapata wasiwasi kwamba, gari nayo inaweza kutumika kama kituo cha kupigia; hii ni dalili na ishara ya wizi wa kura, haikubaliki! Udanganyifu hapa utatokea tu, huwezi kusema kwamba gari nayo ni sehemu ya kituo cha kupigia kura; kwenye mazingira haya ambayo tunakwenda nayo inakuwaje hapo gari nayo inakuwa na tafsiri ya kituo cha kupigia kura? Naomba gari liondolewe kwani haifai, inatatanisha na haikubaliki! (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine, Rais kwa mujibu wa tafsiri ya hapa maana yake ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tunasema Muswada huu wa Sheria ya Kura ya Maoni utafanya kazi kwa pande zote mbili za Muungano. Maeneo mengi yanapotajwa ukiambiwa Tume maana yake ni Tume ya Uchaguzi ya Taifa (NEC) na (ZEC). Rais mmemuweka peke yake wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mimi nadhani hapa Rais maana yake ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Naomba iwekwe wazi nayo vilevile. (*Makof!*)

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. MASOUD ABDALLA SALIM]

Mheshimiwa Spika, naomba niende kwenye Kifungu cha 5(4) kinachosema kwamba; bila kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (3), Tume inaweza kutoa ruhusa kwa asasi zote za kiraia na asasi zisizo za Kiserikali zinazopendelea kutoa elimu ya uraia na kuendesha uhamasishaji juu ya Katiba inayopendekezwa, kutoa elimu na kuhamasisha juu ya Katiba hiyo kwa kipindi kisichozidi siku 30 kabla ya upigaji kura.

Kwa kuwa mchakato huu, Vyama vya Siasa vina uwezo mkubwa na kwa uzoefu wa kule Zanzibar wakati wa kura ya maoni, Vyama vya Siasa vilichukua nafasi kubwa ya kuweza kutoa elimu kwa Wananchi; nasema ni vyema itamke wazi na ninapendekeza kwamba, hapa Vyama vya Siasa navyo vipewe nafasi ya kutoa elimu juu ya suala hili. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nikiendelea kwenye sehemu ya tano ya Muswada huu kuhusu masharti ya jumla na ninakwenda kwenye Ibara ya 37(2). Naomba ninukuu: "Tume, kwa madhumuni ya kura ya maoni, itaweka utaratibu wa kuandikisha raia wa Jamhuri ya Muungano ambao wanaishi nje ya Jamhuri ya Muungano na ambao hawajasajiliwa kama wapiga kura katika Daftari la Mpiga Kura."

Utaratibu wa kuandikisha raia wa Jamhuri ya Muungano ambao wanaishi nje ya Jamhuri ya Muungano; swali linakuja, naomba Mheshimiwa Waziri uwaeleze Watanzania ambao wako nje, utaratibu wa kuweza kuandikishwa kupiga kura ya maoni wataandikishwa wakiwa kulekule nje au wataandikishwa wakiwa ndani ya Tanzania na utaratibu huo ambao ninyi mnataka kuuanzisha Watanzania wenyewe waliopo ndani hamjawaandikisha mnataka kuwaandikisha waliopo nje kwa vipi?

Hamjakamilisha utaratibu wa kuwaandikisha Watanzania katika pande zote mbili za Muungano. Tanzania Bara na Zanzibar, kuna watu wengi bado

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. MASOUD ABDALLA SALIM]

hawajapata fursa ya kuandaa mchakato na kuanza kupiga kura ya maoni. Leo mnaandaa mazingira kwa Watanzania waliopo nje; je, mtawaandikisha wakiwa nje au wakiwa hapa na waliopo ndani mikakati yenu ni ipi?

Lazima muweke bayana, mtueleze na muwaeleze Watanzania ili waridhike na waridhie kuwa michakato yenu hii haitakuwa na tabia yoyote ambayo itakinzana na demokrasia ya kweli ambayo itachukuliwa. Tunataka tupate Katiba ya kweli, iliyo imara, ya miaka mingi na ambayo ndani yake haitakuwa na migogoro kama ilivyo katika nchi nyingine.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri kwa hili akubali atoe maelezo ya kina ambayo Watanzania wote walioko ndani na nje waridhike. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naendelea na ninafurahi sana mtoha hoja, Mheshimiwa Lukuvi, katulia kwelikweli leo!

Mheshimiwa Spika, katika hali hii tunayokwenda nayo, ninachoomba kwa Serikali na ninaloona ni vyema wakati huu ambao tupo katika mikakati hii kuna mambo mengi, kuna manung'uniko mengi na wengine wanaonekana labda watu wanashambuliwa au kuna tatizo.

Tatizo lillokuwepo Zanzibar katika Visiwa vya Unguja na Pemba, hiyo kupatikana kwa ZND, kutotoa haki kwa watu wanaostahili kupiga kura ambao wamefikia umri na hawapo katika Daftari za ZEC ni suala ambalo kimtaalamo ninavyoona liko katika sehemu kubwa ya Baraza la Wawakilishi, katika uhalisia mnaouona ninyi. Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tuliyonayo hivi sasa na kwa sababu ninyi ndiyo watoaji hoja na kwa sababu Tume mbili zote za NEC na ZEC hasa hapa mikakati ya ziada ya kuona Watanzania hawa na Wazanzibari hawa ambao kuna tatizo linaonekana waziwazi, tatizo ni kubwa kuliko mnavyofikiria ninyi wenyewe. Mikakati gani ya ziada na ni mipango ipi madhubuti inayoonesha kwamba mtakaa na

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. MASOUD ABDALLA SALIM]

kutafakari na kupanga mipango madhubuti kuona basi Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, suala hili linalipatiwa ufumbuzi wa kudumu?

Ninasisitiza kwa kusema kwamba, kila mwenye haki ya kupiga kura kwa mujibu wa Katiba tuliyonayo, Ibara ya 5, apige kura achague, vinginevyo tunatengeneza Katiba mpya lakini Katiba tuliyonayo sasa tayari tunaivunja.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo machache, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kwanza kwa jioni hii na ninamshukuru sana Mheshimiwa Lukuvi, kwa utulivu wake akiwa makini leo. Nashukuru sana. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante, nilisema namwita Mheshimiwa Mkosamali, anaafuatiwa na Mheshimiwa Cecilia Paresso.

MHE. FELIX F. MKOSAMALI: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa fursa ili na mimi niweze kuchangia Muswada huu wa Kura ya Maoni wa Mwaka 2013.

Mheshimiwa Spika, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, kwa hiyo, yale maeneo ambayo sitakubaliana nayo, maana yake ni kwamba, nilikuwa sikubaliani nayo toka huko kwenye Kamati na mpaka hapa sikubaliani nayo.

Kabla ya kujadili hivi vifungu ninapenda kusema mambo machache.

Mheshimiwa Spika, ili tuweze kuumaliza huu mchakato vizuri, lazima kila mmoja wetu atambue kwamba, hakuna mtu ambaye anamiliki zoezi hili la kupatikana kwa Katiba na Katiba ya nchi haitapatikana kwa kundi fulani au watu fulani kuwa washindi zaidi ya wenzao. Kama kuna mtu anafikiri kwamba wao watakuwa washindi, hawatakubali mifumo ibadilike, hawatakubali yale mambo yaliyokuwa yanafanya huko nyuma yabadilike, basi wajue

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. FELIX F. MKOSAMALI]

hiyo Katiba haitapatikana; wafahamu hivyo, Wananchi hawatapitisha Katiba hiyo.

Mheshimiwa Spika, Sheria hii ya Kura ya Maoni ni muhimu sana kwenye mchakato huu. Kwa hiyo, ikikosewa Sheria hii, maana yake sehemu muhimu ya mchakato huu wa Katiba utakuwa na matatizo makubwa sana.

Sasa ngoja nirudi kuanza kupitia vifungu mbalimbali. Kifungu cha 9 kinazungumzia kuhusu madaftari yaliyopo ya wapiga kura ndiyo yatumike kuendeshea kura ya maoni. Madaftari haya yamekuwa yanalamikiwa kila siku kwa upande wa Tanzania Bara na upande wa Tanzania Zanzibar. Nchi zote ambazo wamefanya mchakato wa Katiba, wamekuwa wanaangalia *turn out*, watu wangapi wamepiga kura, asilimia ngapi wameshiriki kupitisha hiyo Katiba. Sasa sisi tunakwenda, watu wameongea hapa matatizo ambayo yanatokea kwenye Madaftari ya ZEC na kadhalika, tumeypuuza tunasema twende tu, hao watajijua watapiga kura!

Mheshimiwa Mwenyekiti, ingekuwa ni uamuzi wangu binafsi ningesema Madaftari yote mawili haya yasitumike kabisa kwenye kura ya maoni, hayafai kwa sababu yameshalalamikiwa na matatizo yaliyopo pale hakuna mtu wa kuya-*solve*. Tumezungumza sana kwamba, kuna Wazanzibari ambao wanaishi Tanzania Bara, sheria inasema tutatafuta zaidi ya 50% ya Watanganyika na zaidi ya 50% ya Wabara. Sasa Wazanzibari wanaoishi Kariakoo wao wanapigia kura wapi? Ni rahisi kuona hilo jambo ni jepesi lakini kama Tanzania Bara tu watu wanaotokea Zanzibar ni zaidi ya 200,000, wana uwezo wa kuathiri matokeo ya kura kwa upande wa Tanzania Bara endapo kura yao itahesabiwa kule, lakini kuna watu hawalioni wanaona haya ni ya kupuuzwa, ni kuacha tu twende hivihivi, badala ya kufikiria namna gani tuwa-*incorporate*!

Nchi ya Zimbabwe kuhakikisha kwamba watu wote wanapiga kura, walitumia vitambulisho vya Utaifa, yaani Vitambulisho vya Uraia vya Zimbabwe ili kila mtu apige kura

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. FELIX F. MKOSAMALI]

mahali alipo. Sisi bado tunakwenda na sheria zenyе vizingiti na zenyе kuweka sifa za ukaazi, yaani watu ambaо hawana sifa za ukaazi wasipige kura na mambo mengine. Sasa haya mambo usipoyarekebisha kwenye mchakato wa Katiba ili uende watu wote wakiwa wameridhika, utakwenda na shida.

Mheshimiwa Spika, tumekutana hapa, kwa taarifa, Ofisi ya Makamu wa Rais iliwaleta baadhi ya Wazanzibari wanaoishi Dar es Salaam wamelalamikia mambo hayo lakini watu wameyapuuza tunaendelea kwamba wao watajijua na kadhalika tuendelee na kazi. Haya Madaftari hayakupaswa kutumika, tulitakiwa tuwe na Madaftari mapya, ambayo yata-*identify* vizuri, kila mtu apate haki yake ya kupiga kura vizuri. (*Makofi*)

Hilo ni moja, lakini wale wanaong'ang'ania basi ng'ang'anieni kwa sababu tulishazoea kupeleka mambo kwa nguvu baadaye ...

SPIKA: Mheshimiwa Mkosamali, tunatunga sheria, wewe tunga sheria tu.

MHE. FELIX F. MKOSAMALI: Mimi nimesema kifungu hiki cha tisa kilipaswa kutoka.

SPIKA: Sasa acha kusema nani anang'ang'ania, wewe tunga sheria tu, unachosema sema na ukitaka *amendment* lete.

MHE. FELIX F. MKOSAMALI: Naomba uwe unanitunzia nafasi hapo unapokuwa unaniingilia niwe nakwenda vizuri.

Kifungu cha 17(3) kinazungumzia Sheria za Gharama za Uchaguzi. Kwamba, kutakuwa na Kamati ya Kura za Maoni, zile Kamati zitaeleza gharama watakazozitumia kufanya kampeni na gharama hizo zitakuwa ni siri mpaka mtu atakapohitaji labda amefungua shauri Mahakamani na kadhalika. Kwanza, tujue ni kwa nini watu waandike gharama halafu iwe siri? Tunataka pia kufahamu uhalali

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. FELIX F. MKOSAMALI]

kwamba, kwenye chaguzi mmekuwa mnasema wagombea waandike gharama za uchaguzi. Sasa hapa tunataka tujue; kwanza, tujue efficiency, ile sheria mmekamata watu wangapi ambao wametumia gharama kubwa au walitumia gharama ndogo kwa uchaguzi uliopita?

Tujue pia kwenye sheria hii adhabu ambazo watazipata hao watu kwenye Kamati hizo za Kura za Maoni ambao hawatawasilisha watapata adhabu gani? Itatokea nini? Mmeweka hapa ili itusaidie nini? Tutahitaji ufanuzi wakati mnajibu jambo hili.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 35 kinasema; matokeo ya kura yataamuliwa kwa zaidi ya 50% huku na zaidi ya 50% ya Bara; ndio kinavyozungumza. Kifungu cha 35(3) kinasema, endapo kura za NDIYO ya swalii la kura za maoni zitakuwa hazijazidi 50% ya kura zote halali zillzopigwa Tanzania Bara au Tanzania Zanzibar, Tume kwa taarifa itakayotangaza katika Gazeti la Serikali, itateua siku nyingine ya kupiga kura ndani ya siku 60. Kwa maana kwamba, endapo upande mmoja wa Muungano haujafikisha hiyo asilimia zaidi ya 50, baada ya siku 60 matokeo yakinangazwa, Tume itaitisha tena kura ya maoni.

Sasa hoja hapa tena inakuja; hizi siku 60 ukisoma hiki kifungu kinavyoendelea, ilitakiwa Bunge la Katiba lije kwanza likutane, likishakutana liangaliwe mambo ambayo yamesababisha vifungu hivyo visipite kwenye huo upande. Sasa hizi siku 60 zinatosha hilo Bunge likutane lijadili hivyo vifungu, kampeni ifanyike ndani ya hizo siku 60 na kura ya maoni ifanyike au mmetumia kigezo gani kupima hizi siku 60?

Cha ajabu zaidi kwenye kifungu hiki hiki cha 35(4) kinasema; "Bila kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (3), Tume pale ambapo mazingira yatahitaji, inaweza (b) kutoa muda unaofaa kwa Rais kwa kukubaliana na Rais wa Zanzibar kuitisha upya Bunge la Katiba kwa madhumuni ya kuangalia upya vifungu.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. FELIX F. MKOSAMALI]

Mheshimiwa Spika, sasa hapa ni Tume ndiyo inamwagiza Rais kuitisha tena Bunge la Katiba; lakini soma Kifungu cha 4, kinampa Rais mamlaka ya kuitisha kura za maoni. Sasa kwa nini Tume ndiyo iamue, *im-direct* Rais na ye ye asifanye hii kazi kama ambavyo amekuwa anafanya mwanzoni. Mwanzoni anayeitisha Bunge la Katiba siyo Tume; kwa nini Tume ndiyo imwagize Rais tena Rais kuitisha kura ya maoni?

Kifungu kidogo cha (5) kilipaswa kufutwa kabisa, kinachosema kwamba, endapo kura itakuwa ya HAPANA, Katiba iliyopo itaendelea kutumika. Hiyo kwanza ni *obvious*, whether hiyo Katiba imepita au haijapita, ile Katiba itaendelea kutumika, lakini hiki kifungu kinataka kuleta vitisho. Kwa nini tuwalazimishe watu wapige kura ya NDIYO kwenye hiyo Katiba itakayokuwa imependekenzwa? Kuna sababu gani? Kama Katiba ni mbovu watapiga kura ya HAPANA na ndiyo maamuzi, ndiyo maana tumewaambia hii inapaswa kuitwa kura ya maamuzi siyo kura ya maoni. Huna haja ya kuwaita watu, huna haja ya kuwalazimisha watu wapige kura ya NDIYO, wakiona haifai hiyo Katiba acha wapige kura ya HAPANA na mchakato uendelee, siyo kuweka kifungu cha kusema msipopiga NDIYO, Katiba hii inaendelea. Weka kifungu, hakuna nchi ambayo mchakato wa Katiba una mwisho. Ukipema mchakato utaishia hapa unakosea. Wewe sema mchakato wa kutafuta Katiba utaendelea, lakini hii Katiba iliyopo *is obvious* itaendelea kuwepo.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 37 kinasema, Tume itaweka utaratibu wa watu walioko nje ya nchi kupiga kura. Huu utaratibu lazima ufahamike, haiwezekani Tume ikakaa yenye we pekee yake ikaamua bila sisi kujuu. Kenya kuna Watanzania wangapi, Rwanda wako wangapi, Uingereza wako wangapi na wanapiga kura kwa utaratibu gani? Hapa mmewe ka kuna Kamati ya Kura Maoni, nazo zinahusika vipi kwa Watanzania walioko nje ya nchi?

Kwa hiyo, hiki kifungu cha kusema kwamba watu walioko nje ya nchi watapiga kura, bado kilitakiwa

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. FELIX F. MKOSAMALI]

kifafanuliwe, utaratibu huo ujulikane; watu hao ni wangapi, wanaandikishwa vipi, kwa muda upi, wapo wangapi, wadau wanashiriki vipi kuwatambua? Huwezi ukaacha tu hivi hivi kwamba, tuiachie Tume iende kuwasajili watu hao walioko nchi za nje wapige kura ya maoni; huwezi kuacha wazi kitu kama hiki.

Mheshimiwa Spika, Tume ambayo tumekuwa sisi wengine hatuiamini na ndiyo maana nchi zingine zilizofanikiwa hata Tume yenyewe ilipaswa iwe Tume Huru, siyo Tume ambayo imekuwa inalalamikiwa. Sasa tumeeleza hizi hoja, wadau wametoa maoni, lakini watu hawabadiliki, kwa sababu wanafikiri kwamba hiyo Tume ikija kuwa huru labda Katiba ambayo wao wanaifikiria ndiyo itapatikana au haitapatikana. Hayo ni mawazo ambayo siyo sahihi.

Mheshimiwa Spika, ninachowenza kuwashauri kwenye kifungu hiki cha 37, kama utaratibu wa watu walioko nje ya nchi haufahamiki vizuri, kifungu hiki bora kiondoke. Tupige kura watu ambao tunafahamiana kwa utaratibu huu uliopo kwa sababu Sheria nzima hajjaweka utaratibu wa namna ambavyo watu walioko nje ya nchi watapiga kura.

Mwisho, ningependa kuchangia kuhusu Kifungu cha 22. Kifungu cha 22 kinazungumza juu ya Msimamizi wa Uchaguzi kwenye kituo anavyoweza kuahirisha zoezi baada ya kuona kuna matatizo.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

SPIKA: Okay, ahsante. Mheshimiwa Paresso, atafuatiwa na Mheshimiwa Anne Malecela.

MHE. CECILIA D. PARESSO: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia katika Muswada huu wa Kura ya Maoni, ambao utaenda kupitisha Katiba Mpya tukielekea katika hatua za mwisho kupata Katiba, ambayo naamini Vijana wa Kitanzania, Akina Mama wa Kitanzania na Wananchi wote wa Tanzania,

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. CECILIA D. PARESSO]

wanatamani kuiona Katiba hiyo. Niseme kwamba, ninaunga mkono Maoni ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani wa Wizara hii. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, matarajio haya yatafikiwa endapo Vijana na Akina Mama wa Kitanzania watapewa haki yao ya kupiga kura kuweza kuidhinisha ama kutokuidhinisha Katiba hiyo. Wanapigaje kura ni kama ambavyo Muswada huu leo tunaujadili. Nami nina maoni machache kuhusiana na uboreshaji wa Madaftari ya Kupigia Kura.

Waheshimiwa Wabunge wenzangu, wametoa maoni kuhusiana suala hili. Ni muhimu sana kwa sababu uzoefu umeonesha kulivyo na matatizo katika Madaftari ya Kupigia Kura, jinsi ambavyo Wananchi wanajiandikisha katika Madaftari hayo, mwisho wa siku anaenda pale kupiga kura jina halionekani, ana kadi jina halipo; hizi kasoro zitaondolowaje? Kila Mtanzania ambaye ametimiza umri wa kupiga kura, aliyejiandikisha, ana haki hiyo na ana wajibu wa kuidhinisha Katiba hii kwa kupiga kura.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeeleza hapa kwamba, suala la uboreshaji wa Daftari la Kupigia Kura kwa Tanzania Bara litaanza, lakini hawajatuambia litadumu kwa muda gani. Tunahitaji tupate muda wa kutosha kwa wale ambao hawajajiandikisha wapate nafasi ya kujiandikisha, Daftari hili liboreshwe, watuambie ni muda gani. Muswada huu haujaonesha mtatumia muda gani katika kuboresha Daftari hili kwa upande wa Tanzania Bara, ni muhimu sana, kuna vijana wengi sana wamefikisha miaka 18 hawajajiandikisha, wanahitaji kujiandikisha na wanahitaji kushiriki katika mchakato huu.

Kwa hiyo, nataka nishauri kwamba, ni vyema kuwepo na muda wa kutosha tunapoenda kuboresha Daftari la Wapiga Kura kwa upande wa Tanzania Bara.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Zanzibar, tumesikia Waheshimiwa Wabunge wa Zanzibar wameeleza

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. CECILIA D. PARESSOJ]

malalamiko hapa kwamba, kuna malalamiko ya muda mrefu kuhusiana na Daftari lao la Zanzibar, kuna unyanyasaji, kuna ubaguzi unaofanywa na hao Masheha wanaondikisha; tunaomba haya yaboreshwe upya. Tunapoelekea katika kuidhinisha Katiba hii tunatarajia kila mtu atashiriki, yule ambaye amefikisha miaka 18 ambaye amejiandikisha. Tunahitaji kuona tunapata Katiba hii kwa amani siyo kwa ubaguzi kwa sababu ya labda wewe ni *CUF*, si kwa ubaguzi labda kwa sababu wewe ni *CHADEMA*, si kwa ubaguzi kwa sababu wewe ni *NCCR* au chama kingine chochote cha Upinzani. Tunatarajia kuona Watanzania wote wallotimiza umri wa kuandikisha waandikishiwe na washiriki katika suala hili. (*Makofj*)

Mheshimiwa Spika, ni muhimu sana kwamba, kasoro zilizopo kwa upande wa Zanzibar na kwa upande wa Bara ziondoke.

Aya ya 9 ya Muswada huu imeonesha haki ya kupiga kura. Naomba ninukuu Kifungu cha (9)(3) kinasema: "Afisa wa kura ya maoni atamtaka mtu anayeomba kura ya kupigia kura kutoa kadi ya mpigia kura iliyotolewa na Tume kwa uthibitisho wa mtu anayedaiwa kuwa anaruhusiwa kupiga kura." Uzoefu unatuonesha katika chaguzi mbalimbali, watu wanaenda hawana kadi, jina lipo, hapa Muswada huu unaeleza kwamba watapewa fomu watajaza au kitambulisho kingine chochote. Tunaelewa hali za wakulima wetu wa kule vijijini, anaweza kweli jina lipo, hana kitambulisho kimepotea, atatakiwa atoe kitambulisho kingine ana kujaza fomu. Tunaweka sharti la kisheria kwamba, mtu huyo atatakiwa na Afisa wa Kura atoe kitambulisho kingine; hapa tutawanyima haki wale ambaeo hawana vitambulisho vingine vyaa ziada.

Mheshimiwa Spika, napendekeza kwamba ni vyema mtu ye yeyote ambaye jina lake lipo lakini hana kadi, ajaze fomu bila sharti la kuambiwa alete kitambulisho kingine cha ziada. Kwa watu waliopo vijijini hawataweza, kwa watu wa mijini angalau wanaweza kuwa na kadi za Benki na wanaweza kuwa na kadi nyingine za

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. CECILIA D. PARESSO]

kuwatambulisha, lakini kwa mtu wa kijiji hataweza kuwa na kadi hii. Ni vyema tusiweke sharti hili la kisheria kwamba atoe kitambulisho kingine kama hana kitambulisho cha kupigia kura. Tuweke wigo mpana kwa kila mtu ambaye ni Mtanzania aweze kushiriki bila kuwa na masharti yoyote ambayo yanawekwa na Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, hivyo hivyo Kifungu cha 4 pia kinalezea masharti hayo hayo. Tunaomba haya masharti ya kumlazimisha kama ni Mtanzania, jina lipo kwenye Daftari la Kupigia Kura lakini hana kitambulisho, aruhusiwe kupiga kura bila kuwekewa masharti.

Mheshimiwa Spika, tumeona katika chaguzi mbalimbali kuna utaratibu wa kujaza fomu, lakini Wasimamizi wa Vituo bado wanaendelea kuweka urasimu usiokuwa na maana. Anaingia mtu kupiga kura kitambulisho hana, anaambiwa ajaze fomu au anaambiwa atoke nje arudi tena. Tunataka urasimu huo uondoke, tunataka Watanzania wapate fursa ya kupiga kura katika kupidisha Katiba ambayo wanatamani kuiona. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, nimalizie kuhusu Tume ya Uchaguzi. Hotuba ya Msemaji wa Kambi ya Upinzani imeeleza vizuri sana, tumeona Tume hii haijawahi kuwa huru, siyo huru kabisa, inafanya kazi zake wakati mwingine kwa kuingiliwa. Leo tunaenda kupata Katiba, Tume hii hii ndiyo itakayosimamia kupata maoni ya Watanzania. Hapa kuna shaka, sijui mnatuhakikishia vipi kwamba Tume hii kweli itakuwa huru, haitaingiliwa, itafanya kazi zake na Mtanzania aliyetimiza umri wa miaka 18 aliyedandikishwa aweze kupata haki na wajibu wake wa kuidhinisha Katiba hiyo?

Nilitaka nipendekeze kwamba, tupate Tume huru itakayosimamia mchakato wa kura ya maoni tunapoelekea kupata Katiba mpya. Kama tunaenda na Tume hii hii ambayo siku zote kwenye chaguzi tumeona ina upungufu, tumeona ina ubaguzi wa hali ya juu, ukiwa Mpinzani basi unaonekana kama huna haki katika nchi hii, tunataka kuona haya mambo yanarekebishika na haki ya

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. CECILIA D. PARESSO]

Watanzania wote bila kujali vyama vyao isikilizwe na kutekelezeka.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Nilisema Mheshimiwa Anne Malecela, atafuatiwa na Mheshimiwa John Mnyika.

MHE. ANNE K. MALECELÀ: Mheshimiwa Spika, nianze kukushukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia hoja hii ya Sheria ya Kura ya Maoni ya Mwaka 2013.

Mheshimiwa Spika, Serikali imetuletea huu Muswada, sisi ni watunga Sheria, lakini Serikali haijasema lazima kila kilichopo hapa tuseme ndiyo. Serikali imeleta hapa ili na sisi tupate nafasi ya kutoa hoja, tuboreshe, tupate Sheria nzuri, ambayo itatufanya tupate Katiba ya Watanzania wote. Kwa hiyo, hapa tuna ruhusa ya kutoa kasoro, kuna ruhusa ya kutoa hoja, mimi naona tusilalamike tusimame katika kutoa hoja kuboresha Muswada huu na tupate Katiba ambayo itaweza kutuondoa Watanzania kwenye hali tuliyonayo, itupeleke katika hali nzuri zaidi. Tuelewe kwamba, Katiba ni Dira na ndiyo itatuonesha nchi hii inaongozwaje.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuipongeza Serikali, kwanza, kwa kukubaliana na Maoni ya Kamati na Maoni ya Wadau wengi ambao walikuja mbele Kamati ya Katiba na Sheria kwamba, Sheria hii tuitumie kwa wakati huu wa maoni ya kupiga kura kwenye Katiba na baada ya hapo Sheria hii inakufa. Mwanzoni ilikuja katika sura ambayo haikuwa hii, lakini sasa naipongeza Serikali kwa kukubaliana na maoni yetu. Wale ambao tulikuwa tunakwenda kwenye Kamati ya Katiba na Sheria japokuwa siyo Mjumbe, tuliona Sheria hii twende nayo, lakini baada ya kumaliza mchakato wa kupiga kura za maoni, Sheria hii ife na tuachane nayo. Naipongeza Serikali kwa hilo.

Mheshimiwa Spika, Tanzania kutumia vitambulisho vya kupigia kura, nimemsikia Mheshimiwa aliyemaliza

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. ANNE K. MALECELJA]

kuzungumza. Mimi ninazungumzia Tanzania Bara, maana nisilingie kwenye mambo ya Visiwani. Tanzania Bara, zaidi ya 80 asilimia ya Wananchi wetu wanaishi vijijini, kule vijijini Wananchi wana vitambulisho vya kupigia kura, kule vijijini kutakuwa na Daftari la Kupigia Kura.

Mheshimiwa Spika, bahati nzuri mimi nimepigiwa kura muda mrefu na nimekuwa mpiga kura muda mrefu, hizi changamoto zinazozungumzwa ni kweli ninaziona zinakuwepo; utamkuta mtu mwingine ana kitambulisho jina lake halipo au amepoteza kitambulisho pale kwenye daftari jina lake lipo. Hapa ninaiomba Serikali kwanza muelewe kwamba, Watanzania Bara zaidi ya kitambulisho cha kupigia kura, zaidi ya jina kuwa kwenye daftari, afadhali wenzetu wa Tanzania Visiwani, sisi hatuna vitambulisho wa uraia. Asilimia ndogo sana huku Bara ambao wana vitambulisho vya uraia, kwa hiyo, hatuwezi kuizungumzla hii, labda Viongozi na Wakazi wa Dar es Salaam kiasi kidogo.

Mheshimiwa Spika, ninaomba wakati wa kupiga kura, Serikali tuwe makini, tutakuwa tunatumia kitambulisho cha kupigia kura na majina yatakuwa kwenye daftari na ninategemea kwamba Serikali sasa mtakuwa katika mpangilio wa kuanza kuboresha lile daftari kama hamjaanza. Ninavyoelewa, kuna sehemu daftari hili limeanza kuboreshwa ili kusije kukatokea yale matatizo. Jamani tuelewe na tukubali kwamba, wakati wa kupigia kura wote siyo nchi yetu tu, kunatokea vitu vidogo vidogo ambavyo lazima Tume zitatakiwa kuchukua yale matatizo na kuyatatua kwenye vituo. Tusianze kuwa na picha kwamba lazima Serikali itatuonea, hapana; lazima kuwe na haki, lazima kila kitu kiangaliwe vizuri, kwa sababu hiki kitu tunachokitafuta ni Katiba ya Watanzania. Katiba mpya ni kitu muhimu sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nije Ibara ya 11, Kifungu cha kwanza na cha pili. Mimi nakwenda kwenye Jimbo langu; Jimbo langu lina jiografia mbaya sana, ni mfano tu na ninategemea na Tanzania nzima sehemu hizi zipo. Kuna Vitongoji kwa mfano, Kitongoji kama Kalungoyo kwenye

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. ANNE K. MALECEL]

Kata ya Vujo, Kwaseijungu Kata ya Bombo, wao kule hawana Taasisi za Serikali. Niipongeze Serikali na nimefurahia sana Ibara ya 11, kifungu cha kwanza na cha pili.

Mheshimiwa Spika, naomba kunukuu: "Kifungu cha kwanza; Tume inaweza bila malipo yoyote kutumia eneo lolote la umma kama kituo cha kupigia kura. Mbili, Tume inaweza pale ambapo kutakuwa na haja, kutumia jengo au eneo binafsi baada ya kupata ridhaa ya mmiliki wa eneo au jengo hili."

Mheshimiwa Spika, naomba hapa niseme Serikali imeangalia vizuri hiki kifungu. Wapiga kura wa vitongoji vyangu kama hivyo nilivyovitaja, wanakwenda mbali mno kufuata vituo vya kupigia kura, kwa sababu labda kwenye vile vitongoji hakuna Taasisi ya Serikali. Kwa kuweka sura hili ambayo imewekwa kwenye Ibara ya 11, kifungu cha kwanza na cha pili, tayari Serikali sasa imepanua wigo, imesogeza vituo kwa Wananchi, itakwenda kutafuta sehemu zingine hata kama siyo Taasisi za Serikali na kuweka kituo cha kupigia kura. Ina maana vituo vya kupigia kura vitakuwa vimesogezwa sana karibu na Wananchi. Jamani kwa nini Serikali inapozungumza mazuri tusiipongeze! Mimi naomba kuipongeza Serikali kwa Ibara ya 11 ambayo sasa imeweka hali nzuri ya kuwafanya Watanzania walioko kwenye milima, mabondeni na walioko sehemu ambazo ni mbali sana, basi wote watapata nafasi ya kupiga kura. Naomba niseme hapa nawaunga mkono asilimia mia moja Serikali mmekuja na jambo zuri sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hapa nina mashaka kidogo, haki ya Raia wa Tanzania waishio nje ya Jamhuri ya Muungano kwamba, eti nao wapige kura. Mimi kidogo hapa nina matatizo; tuelewe na Tume ielewé na Serikali ielewé kwamba, Watanzania wapo kila mahali ulimwenguni; ukienda Korea wapo, ukienda China wapo, ukienda Afghanistan wapo, kila mahali Watanzania wapo; hivi tutafanyaje hawa wapige kura ya maoni jamani? Hapa mahali ni pagumu na tusipoangalia kwa urahisi rahisi maana naona kama tuangalie London tu. Tukisema Watanzania

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. ANNE K. MALECELA]

waishio nje ya nchi iwe ni wote, ulimwengu mzima jamani, tutayaweza hayo? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hebu tuangalie ukurasa wa 43, katika huo mkakati wa kura za maoni, kutakuwa na uanzishwaji wa Kamati za Kura za Maoni; kule Afghanistan utaananza hiki? Kule Dubai haya, huko China haya, ukienda Congo haya; tutaananza hili?

Pili, usajili wa Kamati za Kura za Maoni; tutaweza ulimwengu mzima kwenda kuyafanya haya? Siyo rahisi, kutakuwa na uteuzi wa Maafisa wengi, kutakuwa na Mawakala; hapana, Serikali hapa tupaangalie vizuri, tupaangalie kwa kina, tunatafuta Katiba ambayo itatuboreshea nchi; hawa Watanzania tutawafikia kama tutasema Watanzania ni wote? Wote tunaangalia London tu hapa, London inaweza ikawa ni rahisi lakini Syria wapo, kila mahali Watanzania wapo. Mimi ninaishi Serikali, ninaishi Tume, hili nina mashaka nalo tungeweza kuliachilia mbali. Sisi tunajitahidi tushikamane, tuboreshe, tuhakikishe Watanzania waliopo kwenye nchi yetu wanapiga kura huru na asibaki mtu ambaye hatapiga kura. (*Makofii*)

Sheria hii ya Kura za Maoni ndiyo inayotupa Katiba hii, ndiyo itakayokwenda kuwaambia Wananchi waseme ndiyo au waseme hapana; ni Sheria muhimu hii. Baada ya hapo tukishapata waliosema ndio huku theluthi mbili, kule theluthi mbili, Katiba imepita. Sasa hii kura ya maoni, hii Sheria hii tujitetahidi kuondoa kila kasoro ambayo itatukwamisha.

Baada ya kutoa maoni yangu na mimi kama mtunga Sheria, naomba niseme kwamba, naunga mkono hoja, naomba hoja zangu zichukuliwe. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa John Mnyika, atafuatiwa na Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed. Mheshimiwa John Mnyika!

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru. Katiba ya nchi ni msingi siyo tu wa uchumi wa nchi, ni msingi vilevile wa ustawi wa Wananchi. Kwa hiyo, tunapotunga Sheria kama hii, ambayo imeitwa kimakosa Sheria ya Kura ya Maoni, lakini kimsingi ni Sheria ya Wananchi kwenda kufanya maamuzi juu ya Katiba mpya, ni muhimu Wabunge wa pande zote, wa upande za Chama kinachotawala na wa Upinzani, sote tukakubaliana kwa pamoja kwamba, tunakwenda kutunga Sheria ya Wananchi. Tukubaliane kutengeneza Sheria ambayo itakwenda kuwawezesha Wananchi wenyewe kuandika Katiba yao wanayoitaka.

Mheshimiwa Spika, tumekutana leo kujadili hii Sheria, ikiwa ni jaribio lingine la kuitisha Sheria baada ya kukwama kwenye jaribio la mwaka 2011 wakati Sheria ya Mabadiliko ya Katiba ilipotungwa kwa mara ya kwanza. Tafsiri yake ni nini?

Mheshimiwa Spika, kama mwaka 2011 mwezi Novemba, tungetunga Sheria ni bora, sasa hivi tusingekutana kujadili tena Sheria ya Kura ya Maoni, Sheria ya Kura ya Maamuzi juu ya Katiba mpya, tungeelekeza nguvu kwenye kufanikisha mchakato.

Mheshimiwa Spika, jambo hili litupe tahadhari kwamba, tukikosea hivi sasa kuitunga Sheria hii, tutakwenda kuuweka mchakato wa Katiba mashakani, kwa sababu muda mfupi umebaki kuelekea kuukamilisha huu mchakato. Katika hili ni vizuri Serikali kwenye majumuisho ikawaeleza Wananchi ukweli; Watanzania wametumainishwa kwamba, baada ya kuitishwa kwa Sheria hii ya Kura ya Maoni, kura ya maoni itafanyika na hatimaye Katiba mpya itazinduliwa tarehe 26 Aprili, 2014.

Mheshimiwa Spika, kwa misingi ya idadi ya siku za Bunge la Katiba 70 mpaka 90 na kwa msingi wa idadi za siku zinazotajwa na Mswada huu, siku 60 za elimu peke yake juu ya Katiba na siku 30 za kampeni ya Katiba, ni wazi uwezekano wa Katiba kuzinduliwa tarehe 26 Aprili, 2014

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. JOHN J. MNYIKA]

haupo na ni vizuri Serikali kwenye majumuisho ikawaeleza ukweli Watanzania.

Mheshimiwa Spika, jambo kubwa ambalo linahitaji tafakari ya kina ya Bunge hili na maamuzi ya dhati ni juu ya mamlaka ipi hasa na chombo kipi kisimamie mchakato wa Katiba.

Mheshimiwa Spika, nimeleta Jedwali la Marekebisho kwenye jumla ya vifungu na vipengele 12. Muswada huu una vifungu 52, kutokana na ufinyu wa muda, imewezezana kuleta marekebisho kwenye vifungu hivyo 12.

Mheshimiwa Spika, ukweli kama Wabunge kwa umoja wetu kwa kila upande tungepata nafasi ya kutosha ya kuandaa Majedwali ukweli ni kwamba, sehemu kubwa ya vifungu hivi 52 vinahitaji marekebisho makubwa sana ili kuiwezesha nchi yetu kuwa na mchakato wa Katiba ulio bora.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 4 cha Sheria hii kimetoa mamlaka makubwa sana kwa Mheshimiwa Rais, juu ya kutangaza kipindi cha kura ya maoni ya maamuzi na juu ya kutangaza kipindi cha kampeni ya kura hii ya maamuzi.

Mheshimiwa Spika, mamlaka makubwa haya ya Rais yangeishia yale mamlaka iliyotajwa na Kifungu cha 4(1) peke yake, cha kuielekeza Tume baada ya Rasimu kuwa imetangazwa, Tume kuitisha mchakato wa kura ya maoni. Mamlaka makubwa ya kuamua mpaka kampeni ziwe siku ngapi na ya kuamua kipindi chote cha kampeni, yakitumiwa vibaya yatakwenda kuathiri mchakato mzima wa Katiba huko mbele tunapokwenda.

Mheshimiwa Spika, ili kujenga kuaminiana na Mwafaka wa Kitaifa kwenye mchakato wa Katiba, mamlaka haya ya Rais yaliyopo kwenye Kifungu cha 4(2) ambayo yanakinzana vilevile na Jedwali lilitotajwa, Jedwali

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. JOHN J. MNYIKA]

Ia Kwanza kwenye Fomu Namba Moja, yanahitaji kupunguzwa na yanahitaji kurekebishwa.

Mheshimiwa Spika, mamlaka mengine mabovu ya Muswada huu ni mamlaka ya chombo kipi kisimamie uchaguzi huu. Kwa mujibu wa Sheria hii, kama ilivyokuwa Sheria iliyopingwa ya Novemba 2011 na marekebisho yake yaliyofuatia baada ya hapo, mamlaka ya kusimamia uchaguzi yapo chini ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, Tume hii yenyele ilipokwenda mbele ya Tume ya Mabadiliko ya Katiba kutoa maoni, ilisema haipo huru, inataka ipate uhuru katika Katiba mpya. Tume ilisema haya. Sasa Tume hii ambayo ilisema haipo huru kwenye kusimamia uchaguzi, ndiyo ambayo leo inapewa dhamana ya kusimamia kura muhimu sana itakayoamua hatima ya Taifa letu kwa muda mrefu, kura ya maamuzi juu ya mustakabali wa Katiba mpya ya nchi yetu!

Mheshimiwa Spika, jambo hili halikubaliki kwa tafsiri yoyote ile na halipaswi kukubalika. Tungefanya nini na marekebisho gani ambayo yangepaswa kufanyika? Nakubaliana na Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani, tukikubali kuipitisha hii Sheria kama ilivyo, Bunge hili litakwenda kutunga Sheria inayokinzana na Katiba ya nchi. Mheshimiwa Rais, baada ya Bunge hili kuitisha huu Muswada, akiisaini hii Sheria kuwa Sheria, atasaini Sheria inayokinzana na Katiba ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 98 ya Katiba ya Nchi, imeweka utaratibu juu ya marekebisho ya Katiba ya nchi yetu na juu ya mabadiliko ya Katiba ya nchi yetu. Imeweka vifungu kwa mambo ya Muungano na yasiyo ya Muungano. Ibara hii ya 98 ya Katiba ya nchi yetu, haijaweka kabisa mfumo wa kuandika Katiba mpya ya nchi. Katiba na Sheria hii itakayopitishwa kama haitazingatia matakwa ya marekebisho ya Ibara ya 98 ya Katiba, ni wazi jambo hili litakwenda kutunga Sheria ambayo inakwenda kukinzana na Katiba ya nchi.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. JOHN J. MNYIKAJ]

Mheshimiwa Spika, jambo hili tumelizungumza kwa miaka mingi sana. Mwaka 2011, baada ya Mheshimiwa Rais kutangaza kwamba, sasa tunakwenda kuanza mchakato wa Katiba mpya, wengine tulisema kabla ya Rais kuunda Tume, kwanza, tuitishe Mkutano wa Kikatiba na pili, itungwe Sheria. Wakati ule tunapendekeza haya na tukaleta Taarifa ya kuleta hoja binafsi Bungeni, kati ya mambo ambayo yangetanyika kwa wakati toka mwaka 2011 ni kuanza mchakato wa marekebisho ya Ibara ya 98 ya Katiba ya nchi yetu. Jambo hili halijafanyika, jambo hili linawezekana kabisa kufanyika, jambo hili ni muhimu likafanyika ili kuiepusha nchi yetu na utata tunapokwenda mbele ya safari.

Mheshimiwa Spika, naelewa upande wa Serikali utakuja kutoa utetezi wa kutumia Ibara ya 21 ya Katiba ya nchi, juu ya mamlaka ya Wananchi kushiriki kwenye maamuzi ya nchi yao iwe moja kwa moja au kutumia wawakilishi wao. Ibara ya 21 haijaweka utaratibu huo wa kura ya maoni ya Wananchi au kura ya maamuzi na wala haijatoa mwanya. Ingeweka masharti ya kusema kwamba, Bunge litatunga Sheria ya kuwezesha Wananchi kushiriki moja kwa moja kwenye maamuzi yao, kifungu hicho cha Kikatiba kingetumika kama mwanya wa kutunga Sheria ya Kura ya Maoni. Jambo hilo halijafanyika na kwa vyovoyote vile utetezi wa Serikali hauwezi kuhalalisha uvunjaji huu wa Katiba ambaeo utatokea iwapo Muswada huu utapitishwa kama ulivyo.

Mheshimiwa Spika, wapo wanaolazimisha kusema ni lazima Tume ya sasa kama ilivyo ndiyo isimamie kura ya maoni. Kazi za Tume ya Maoni, kazi za Tume ya Uchaguzi na mamlaka ya Tume ya Uchaguzi, yametajwa kwa mujibu wa Katiba ya nchi, Ibara ya 74. Kwenye kazi za Tume yetu ya Uchaguzi kama ilivyo sasa hakuna mahali popote ambapo Tume imepewa kazi ya kusimamia kura ya maoni. Tafsiri yake ni kwamba, iwapo Bunge lako litaamua leo kutunga Sheria ya kuunda Tume huru kabisa ya kusimamia kura ya maoni peke yake, Bunge hili litakuwa halijavunja Katiba ya nchi na litakuwa limefanya jambo sahihi kabisa.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. JOHN J. MNYIKA]

Mheshimiwa Spika, iwapo Serikali inataka kulazimisha kwamba, ni lazima mifumo yetu ya Kisheria na Kikatiba ndiyo itumike kwenye usimamizi wa kura ya maoni, basi kwanza Serikali ileté hapa Muswada kwa Hati ya Dharura wa kurekebisha Ibara ya 74 ya Katiba ya nchi, ili kuipa Tume kwanza iwe huru. Pili, kuipa kazi ya kusimamia kura hii ya maamuzi, kura hii ya *referendum*.

Mheshimiwa Spika, bila ya kufanya hivyo, tunakwenda kutengeneza mfumo wa kisheria wa kuendesha kura ya maoni ambao malalamiko yanayotolewa juu ya Madaftari ya Wakazi, uhuru wa Wazanzibari kwenye kupiga kura, malalamiko yanayotolewa upande wa Tanzania Bara juu ya uchaguzi, ni malamiko halisi ambayo yatafanya leo zoezi hili katikati ya lindi na kutoaminiana juu ya mchakato wa Katiba katii ya mitazamo tofauti juu ya muundo wa Muungano, katikati ya mitazamo tofauti juu ya masuala ya msingi ya nchi yetu, ya rasilimali za nchi, ya haki za binadamu na mambo mengine. Tuone kabisa kwamba, dhamira ya Watawala kulazimisha Tume hii ndiyo isimamie Uchaguzi, ni dhamira ya kwamba, tukishindwana kwenye Bunge la Katiba, Watawala waende kutumia hatua ya kura ya maoni, kura ya maamuzi, kwenda kuhalalisha maamuzi ambayo hayatakiwi na Wananchi.

Mheshimiwa Spika, kama Watawala walioleta Muswada huu wa Sheria hawana dhamira hiyo, waoneshe kwa vitendo kwa kuwaachia Wananchi, kwa kuruhusu hapa itungwe Sheria ambayo itawezesha Mfumo Huru wa Uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, mimi sina imani kabisa na Tume hii ya Uchaguzi, hata baada ya mabadiliko ya Mwenyekiti wa Tume na Mkurugenzi wa Tume. Mimi binafsi ni mhanga, nitangaze masilah; Ubungo pale tulikesha kwa siku kadhaa ili kumshinikiza mtu mmoja tu atangaze kura halisi ambazo Wananchi walipiga kwenye vituo na wakatangaza kwenye vituo kura halali kabisa. Hali hii hajatokea Ubungo peke yake, imetokea maeneo mbalimbali katika nchi yetu, Bara na Visiwani. Tishio la namna hii ndiyo ambalo Watanzania

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. JOHN J. MNYIKA]

tunakwenda kukutana nalo kwenye kura ya maoni ya Katiba mpya.

Mheshimiwa Spika, wakati wa Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2010, pamoja na kuwa Mgombea, nilikuwa Kaimu Katibu Mkuu wa Chama na Katibu wa Timu ya Taifa ya Kampeni za Chama. Tulishuhudia kupitia Wataalamu wetu wa *IT*, namna ambavyo Daftari la Kudumu la Wapiga Kura lina wapiga kura hewa, lina matatizo makubwa, lina udhaiifu mkubwa. Katika mazingira haya haiwezekani. Tumeshuhudia namna ambavyo matokeo ya kura yanayotoka kwenye Majimbo, iwe ni ya Urais, iwe ni ya Ubunge, ukilinganisha na matokeo yanayokuja kutangazwa Tume Makao Makuu, yana utofauti mkubwa kwenye ngazi ya Urais na ngazi nydingine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, halwezekani katika mazingira kama haya, tukatunga Sheria ambayo tunawateua watu wale wale, kwa mfumo ule ule, wasimamie uchaguzi tena tukiamini kwamba, tutapata matokeo tofauti; jambo hili halikubaliki. Jambo hili linahitaji jambo moja; ridhaa ya upande wa pili. Kwa sababu haya tunayoyazungumza leo, tumekwishayazungumza. Wadau mbalimbali, Asasi za Kiraia, waliokuja mbele ya Kamati Dar es Salaam kwa nyakati mbalimbali toka hata Muswada huu haujarekebishwa, wameyatoa maoni haya. Tujiulize ni kwa nini Serikali imeleta Muswada ukiwa na misingi ile ile? Serikali ina dhamira gani; inataka kufanya nini na uchaguzi huu? Hili ni swali ambalo kwa vyovyote vile majadiliano kwenye hatua ya Kamati ya kupitisha vifungu kwa vifungu hata baada ya kuleta Majedewali, hayawezi kutufikisha pale ambapo Wananchi wanataka, kuwe na mchakato huru na wa haki wa Wananchi wenyewe kuandika Katiba yao wanayoitaka.

Mheshimiwa Spika, mamlaka yanayotolewa humu...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa
muda wa mzungumzaji)*

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Spika, siungi mkono hoja. Ahsante sana. (*Makof*)

SPIKA: Ahsante. Sasa nilisema ninamwitwa Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, atafuatiwa na Mheshimiwa Tauhida Galos.

MHE. HAMAD RASHID MOHAMED: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia Muswada wa Kura ya Maoni wa mwaka 2013. Kwanza, niseme kuwa, mimi ni mionganini mwa Watanzania tulio wahili kuandamana kudai Katiba Mpya, Tume Huru ya Uchaguzi. Mionganini mwa maandano hayo, baadhi ya watu pia walipoteza maisha. Kwa hiyo, leo sitatumia busara nikiacha huu mchakato usimalizike na ukaenda salama, ili Taifa la Tanzania likabaki salama, amani, utulivu na vilevile kuhakikisha kwamba, rasilimali za nchi hili zinawasaidia Watanzania. Katika process hii yapo mambo mengi ambayo yatatutokea hapa katikati, wapo watu wanaolitakia wema jambo hili na wasiolitakia wema. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, ni vyema kama Tanzania tukawa makini na hilo, kwa sababu ya uzoefu wa nchi mbalimbali tumeona kiasi gani rasilimali za nchi zinaporwa kwa kuwa hakuna utawala wa Sheria katika nchi hizo. Unavurugwa kwa makusudi ili usiwepo, watu waporwe rasilimali za nchi. Kwa hiyo, ningeomba Watanzania tutumie fursa hii vizuri, tuache uvymama, tuache maeneo, tukae makini tutafute Katiba ambayo itatufanya mazuri katika nchi yetu hasa kwa vizazi vinavyokuja. Huo ulikuwa utangulizi wangu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, la pili, haiwezekani sisi kwa mazingira yoyote hayo, tukatunga Sheria yoyote ikawa kamilifu. Anayefanya kazi hiyo ni Mwenyezi Mungu peke yake. Vilevile tunafanya kosa pale tunapoona makosa ya dhahiri na tukayapuuza tusiyafanyie kazi. Kwa hiyo, yote mawili lazima tuyazingatie kwamba, hatuna ukamilifu lakini lile ambalo tunaona lina kasoro ni vyema tukalifanya kazi na tukakubaliana.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. HAMAD RASHID MOHAMED]

Mheshimiwa Spika, baada ya utangulizi huo, niende ukurasa wa 57 wa Sheria hii upande huu wa Kiswahili, suala la kupiga kura katika mazingira maalum, Kifungu cha 37. Kwanza, niseme kwamba, kwa mara ya kwanza kwenye Bunge lako Tukufu niliwahi kushauri kwamba, ni vyema raia wetu walioko nje wapate fursa ya kupiga kura. Wakati huo Serikali ikawa na kigugumizi sana, lakini hata leo liliopotumbukizwa kwa bahati mbaya, halikutumbukizwa vizuri kwa sababu mpaka sasa hata wakati wa Sensa, watu wetu walioko nje hawakuhesabiwa. Kwa hiyo, hatuna *data* ya kutusaidia kusema tuna-*base* na watu wa aina gani walioko nje. Nafikiri hii ni kasoro moja; lazima tuweke misingi kabisa kwamba, tunayo kasoro ya kujuua watu wetu walioko nje. Sasa hili kama hatujalifanya kazi vizuri, yapo mashaka kwamba, inawezekana kabisa likatumika jambo hili vibaya na matokeo yake tusiyapate mazuri kama tunavyohitaji sisi wenyewe. Kwa hiyo, inahitaji uangalifu mkubwa sana katika kuliangalia jambo hili. (*Makof!*)

La pili, ni hiki kifungu cha 9. Ninakumbuka wakati nikiwa Kiongozi wa Upinzani hapa Bungeni, tumewahi kuandaa nyaraka nyingi sana kuelezea matatizo ambayo yapo juu ya Daftari la Kupiga Kura Zanzibar. Sasa nichukue jambo hili katika maeneo matatu. La kwanza, lipo tatizo la msingi wala tusilikatae lipo ila ni nani anayepaswa kulitatua ndiyo jambo lenyewe. Sasa yapo maeneo mawili; la kwanza, ni jambo ambalo linahusiana na Jumuiya moja kwa moja na Baraza la Wawakilishi na Baraza la Mapinduzi.

Kwa hiyo, jambo la kwanza lilitegemewa Baraza la Mapinduzi lifanye marekebisho ya Sheria na hatimaye liende kwenye Baraza la Wawakilishi ili Sheria hiyo itekelezwe ibadilishwe na mfumo mzima wa watu kupiga kura upatikane. Hiyo ilikuwa ni hatua ya kwanza. Tulilifanya kazi sana huko nyuma na hata katika Kamati zile za Mwafaka jambo hili lilijitokeza na likarekodiwa. Kulikuwa na wapiga kura, kwa mfano Konde, zaidi ya 3,000 hawakupata nafasi ya kupiga kura mwaka 2005. Kwa hiyo, ni jambo linaloeleweka na lipo. (*Makof!*)

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. HAMAD RASHID MOHAMED]

Kwa kuwa sasa kuna Serikali ya Umoja wa Kitaifa, ni matumaini yangu kwamba jambo hili wangeli-*address* sasa hivi sawa sawa ili watu wakapata haki ya kupiga kura. Hilo lilikuwa jambo la kwanza.

La pili, ambalo ni tatizo kubwa zaidi, katika uchaguzi huu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Sheria ya Uchaguzi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, raia wanatakiwa kumchagua Rais, Mbunge na Diwani. Kwa Zanzibar, raia wana haki ya kumchagua Rais tu kwa kutumia Sheria ya Muungano, lakini Mbunge anachaguliwa kwa kutumia Sheria ya Uchaguzi wa Zanzibar na Daftari la Zanzibar; ni kinyume. Siyo sahihi, tumelisema hili. Sasa hili njia yake ni hii ifuatayo; kwa kuwa Daftari la Kudumu na la Muungano linataka kurekebishwa hivi sasa, ni vyema basi Wazanzibari ambao hawatapata haki ya kuingia katika Daftari la Kudumu la Zanzibar, waingizwe katika Daftari la Muungano ili wapate haki ya kupiga kura ya maoni. Hiyo itakuwa imetuondoa katika kipindi hiki. Lile la kudumu la Uchaguzi wa Zanzibar litashughulikiwa na Baraza la Wawakilishi na Baraza la Mapinduzi. (*Makofî*)

Nami nawashauri ndugu zangu Wawakilishi, wapeleke hoja binafsi Barazani ili waweze kufanya *amendment* ya Sheria ambayo inakinzana na matakwa ya Kikatiba. Ninafikiri tukichukua utaratibu huo, utatuondolea hili tatizo ambalo sasa hivi lipo na wapo Wazanzibari ambao hawapo kwenye Daftari la Kudumu la Zanzibar, wala hawapo kwenye Daftari la Kudumu la Muungano, lakini kwa sababu Daftari hili la Muungano linaboreshwu hivi sasa na kwa madhumuni ya kura ya maoni, wapewe haki Wazanzibari hawa waweze kupiga kura ya maoni juu ya mustakabali wa Katiba yao ya nchi. Ninajaribu kutoa ufumbuzi wa hilo tatizo lakini tatizo ni kubwa na lipo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, lingine ni suala la visanduku vya kura; bahati mbaya haikutajwa idadi ya kila kisanduku cha kura kutakuwa na kura ngapi. Kwa kawaida tunajua

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. HAMAD RASHID MOHAMED]

kabisa katika Polling Station kuna kura 300 au 500 na kadhalika, lakini mara hii Sheria imekuwa *silent* haikusema jambo lolote katika hili. Ningombaa nalo hilo vilevile lielekezwe.

Lingine ni suala la Tume; ni kweli yapo malalamiko makubwa sana ya Tume ya Uchaguzi. Tume zote mbili zimelalamikiwa katika chaguzi zote wala siyo uongo, lakini kwa kura hii ya maoni ina tofauti kidogo na kura ya uchaguzi; ndiyo mtazamo wangu, inawezekana tunatofautiana na wenzangu. Kwa kura hii ya maoni, ina tofauti kubwa sana siyo ndogo, kubwa sana na kura ya uchaguzi. Kura hii ni ya HAPANA na NDIYO. Sasa wasiwasi uliopo ni namna ya *management* kuhakikisha hizo kura zinazoingia kwenye sanduku zinaingia halali au si halali, ndizo au sivyo. Hayo nasema ni utaratibu kwa sababu watakuwepo Mawakala kutazama, tutasimamia vizuri tuhakikishe *process* inaenda vizuri.

Mimi nafikiri hilo wasiwasi upo na ninasema lazima tukubali kwamba, wasiwasi upo na ni wa msingi. Ipo tofauti ya uchaguzi huu, yaani kura hii na kura ya uchaguzi wa wagombea. Mimi nafikiri kwa hapa kinachotakiwa kufanyika ni kupata watu wanaosema HAPANA na wanaosema NDIYO. Mimi nafikiri hili tunawenza tukali-*manage* kwa sababu pale kuna kifungu kinachoturuhusu sisi kuweza kusimamia.

Mheshimiwa Spika, lingine ni suala la kituo cha kwenye gari, kimesemewa na shemeji yangu, Mheshimiwa Malecela, amesema yeye anafikiri ni vizuri. Ni kweli lakini kwa sababu hatuja-*experience* katika chaguzi zote kutumia gari kama kituo cha kupigia kura, ndiyo maana watu wanapata wasiwasi na kwa sababu huko nyuma tume-*experience* vilevile vituo hewa, inawezekana gari nalo likawa ni sehemu ya vituo hewa. Nafikiri nalo hili lingeangaliwa vizuri, kama kutakuwa na gari maalum limetengenezwa maalum kama kontena badala ya gari, kontena limetengenezwa kama kituo cha kupiga kura ni suala lingine, lakini unapozungumzia gari ni kitu ambacho

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. HAMAD RASHID MOHAMED]

Kinatembea, linaweza lika-move from one station to the other. Sasa nafikiri hiyo ni kasoro, lingetakiwa kuangaliwa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, lingine ni suala la elimu ya wapiga kura. Hapa ningeomba sana, kwa bahati mbaya katika mchakato huu kila chama kimeonesha msimamo wake. Kwa hiyo, ni dhahiri tutakapokwenda kwa Wananchi, kila mmoja atakwenda na msimamo wake. Mimi pale nilipotangulia kusema tuache vyama katika hili suala sasa, tutazame masilahi ya nchi, tusimame tutazame masilahi ya Taifa hili. Mimi naogopa sana likimomonyoka hili Taifa, inawezekana watu wakatumia nafasi hii wakalibomoa Taifa hili. Kuna wengine wanashangilia wanafikiri ni jambo la mchezo! Nataka niwapeni dakika moja, Wazanzibari walioko Bara hivi sasa ni kama familia laki moja na elfu kumi na kila mmoja hapungui ana watoto wanane. Familia zilizoko Zanzibar kutoka Bara hazipungui 15,000 na kila moja ina watoto watano mpaka sita. Tunapovunja, tunapovuruga, jamii hii inaenda wapi? (*Makof!*)

Nataka tuwe *conscious* tutazame ubinadamu tu na tuchukue mfano halisi; juzi tulikuwa na Wanyarwanda hapa wamekaa Tanzania miaka 30. Tumekuja na *operation* yetu ile tukasema rudini nyumbani, siyo raia wameondoka na yatatokea. Mkikatisha vipande yatatokea. Kwa hiyo, tuwe *very conscious*, tuangalie masilahi ya watu wetu, masilahi ya vizazi vyetu na masilahi ya uhai wa Taifa letu. Naomba sana, ukishafika miaka ya kukaribia kufa unayasema yale ambayo unafikiri mbele ya safari yatawasaidia wenzako. (*Kicheko/Makof!*)

Nawaomba sana ndugu zangu tulioko ndani kama Viongozi, nawaomba Watanzania wenzangu wote, Taifa letu libaki kama Taifa. Mataifa mengine yalikuwa na nguvu yako wapi? Iraki iko wapi? Libya iko wapi? Watu wanamaliza kupiga mabomu huku wanagawana mafuta, mabomu yanaendelea watu wanagawana mafufa. Wa-Syria wanapigana na Waleviana baada ya kukamata mafuta ndiyo wanaambiwa sasa tutakulipieni vita vyenu

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. HAMAD RASHID MOHAMED]

tugawane hayo mafuta tuenze kulipa madeni. Vita vinaendelea, watu wanakufa. *Two million refugees* wako pale sasa hivi. (*Makof*)

Mimi nawaomba sana Watanzania, twende na mchakato huu na mimi nasema nampongeza sana Rais amekubali twende na mchakato huu. Makosa yapo, yatatendeka katika Taasisi zetu na katika majumba yetu, yako kila pahala, tuendelee kuyasahihisha, tuweke mustakabali wa Taifa tuplicate Katiba ilio nzuri.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Ninaunga mkono hoja. (*Makof*)

SPIKA: Amenilazimisha kusimama, anachokisema ni kwamba, tujadili Katiba kama Katiba na mimi nasema tunao muda wa kutunga Sheria na sisi ni watungaji wa Sheria. Kinachonishangaza ni wale Wajumbe wa Kamati tulioituma kufanya kazi nao wanaanza kushangaa humu ndani! Jamani, nilitegemea wao watatuambia sisi kule tulitofautiana hivi tukakubaliana hivi ama hatukukubaliana na hiki. Mkilalamika tena inakuwa hatutungi Sheria. Bunge lake tatizo lake kila kitu mnakifanya kivyama, hatufanyi hivyo; wenzeni tumekaa miaka yote, tulipofika tunatunga Katiba ilikuwa ya nchi. Tuseme kukosoa tukosoe kwa nguvu zetu zote, lakini sema tufanye nini, unapokosoa sema tufanye nini kusudi tufike mahali Wananchi watusikilize. Sisi nyumba hii tukianza kulalamika, hao walioko nje ambao hawana uwezo hata wa kuingia humu ndani watafanyaje? (*Makof*)

Bahati nzuri, kuna wasomi ndani ya Bunge hili na Wanasheria, watumie *profession* yao kutusaidia na si vinginevyo. Nawaombeni sana Waheshimiwa Wabunge, kumbukeni hili ni Taifa, siyo vyama vyenu, vyama vyenu vyote kama mtakuwa na Katiba ya hovyo, havitaishi. Kwa hiyo, nawaombeni sana mliobaki jaribuni kuleta Utaifa zaidi kuliko nani kasema, nani kasema, wewe unasema nini! Kwa hiyo, ndiyo naiomba. Sasa namwita Mheshimiwa Tauhidha Galos, atafuatiwa na Mheshimiwa Tundu Lissu.

MHE. TAUHIDA CASSIAN GALOS NYIMBO: Ahsante Mheshimiwa Spika, kwa kunipa fursa ya kuchangia. Nianze kwa kuwapongeza na kuwashukuru Mwanasheria Mkuu, Waziri na Naibu Waziri wa Sheria, kweli hapa walipotufikisha wametufikisha sehemu nzuri siyo pabaya, mchakato unaendelea vizuri, wanastahili pongezi, maana kazi siyo ndogo, kila mmoja ana mtazamo wake na fikra zake. Katika nia ya kuwasaidia Watanzania, wameleta kitu kizuri na tunaendelea vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumuunga mkono Mzee Hamad Rashid, aliyekaa kitako sasa hivi. Bado sisi kama vijana tunajifunza siasa, kweli tumegundua kwamba Upinzani siyo chuki, Upinzani ni uzalendo. Mzalendo yejote atakuwa na maneno ya kizalendo. Namshukuru mzee wangu kwa maneno yake mazuri aliyoyazungumza na kweli analitakia Taifa hilli mema. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niende moja kwa moja kwenye masuala mawili, matatu. Kwanza, kabla ya yote nashindwa kuelewa kuna kitu hiki nimekishika mkononi kimeandikwa maoni ya Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni. Toka nilipoisoma hii karatasi kila ninapotafuta nashindwa kuielewa, kwa sababu imejikita kwenye lawama toka mwanzo wa *page* mpaka mwisho wa *page*. Umefika wakati nauliza hivi kweli kama Wazalendo wa Tanzania mnaitakia nini Tanzania? Hivi mnashindwa kuwasaidia Watanzania, mmeshindwa kweli kuwa na vitu vyatya msingi vyta kuviardika humu mkaenda kujitika kwenye lawama, tena lawama zenyewe kinachonisikitisha zaidi kana kwamba kuna mtu alitumwa aizungumzie Zanzibar? Zanzibar ina wasemaji wake na ina watu wake. (*Makofi*)

Upo msemo unaosema; wenyewe tunajuana kwa vilemba. Sasa katika hicho kilemba hatutoani macho mwenzetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna mambo mawili, matatu katika suala zima la Zanzibar, yamekuja mazungumzo kuhusu Masheha. Sina sababu ya kuwalaumu Masheha. Umefika

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. TAUHIDA CASSIAN GALOS NYIMBO]

wakati haya mazungumzo ya leo na mchakato wa leo, niwapongeze Masheha. Kumbe kilichokuwepo hapa, *CUF* wanalamikia Masheha na sisi CCM tunalamikia Masheha; sasa jibu nililolipata mimi kama kijana, Masheha wanatenda haki maana hawasimamii vyama. Tukizingatia Masheha hao hao wapo mpaka Pemba na ichunguzeni jinsi Pemba ilivyo, tunavyokwenda nayo kwenye mchakato, tuje Unguja, tutazame ilivyo, Masheha hawa hawa ndiyo wanasmamia. Leo ndiyo nimepata majibu kumbe Masheha wanatenda haki. Nawaambia Masheha endeleeni na kazi mnayoifanya ni nzuri. Vyama vyote vilivyokuwepo Zanzibar wanawatambua Masheha maana sisi kama CCM tumelalamikia na nimewasikia wenzangu wa *CUF* wanalamikia Masheha. Masheha wanafanya kazi nzuri na tunachokitaka Daftari kwa mfumo huu huu, tumeridhika nao.

Mheshimiwa Spika, nina kila sababu ya kuyazungumza haya, nayazungumza haya kwa sababu tuliingia katika upigaji wa kura za maoni katika suala la Serikali Shirikishi; tulikwenda kwenye Daftari gani mbona halikuwa na hoja iweje sasa hivi iibuke hoja mna kitu gani wenzetu? Tuambizane ukweli, nini tatizo au kipi kinachokuwepo, tumeingia kwenye Shirikishi na tumeridhiana ndiyo maana ninasema sisi Waarabu wa Pemba tunajuana wenyewe, sasa hivi taratibu tunashughulika na mambo yetu. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tulitumia *ZEC*, tulitumia Daftari na hakuna tatizo lilitokea mpaka leo tumekwenda vizuri. Naunga mkono na nina kila sababu za kuunga mkono, sikuona mpaka sasa hivi pa kutoa kasoro leo na kama tunataka kusema Daftari lile halina haki na mimi kama kijana nazungumza hapa, haki imekosekana toka tulipoanza mchakato wa Serikali Shirikishi ndipo ilipokosekana haki. Kama haki ipo, basi tuendelee na Daftari letu lile lile, Wazanzibari wenyewe tumelitengeneza tumeliweka, tumetafuta watu wetu, iweje sasa hivi; kuna kitu gani? Jamani, Warabu wenzangu tunajuana tuendelee na Daftari letu. (*Makofi*)

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. TAUHIDA CASSIAN GALOS NYIMBO]

Mheshimiwa Spika, niliskia malalamiko, kunazungumzwa kwamba, wenzetu, ndugu zetu, mimi mashemeji zangu, wanasema watagoma Pemba. Msigome, kwa nini mgome? Hivi kweli kuna Jimbo Pemba liliolofika watu 10,000; lipo? Sisi kule Unguja ndiyo tukasema tusichanganyane, kaka yangu mwenye Hotuba hii ya Upinzani, ya kwetu tuachie wenyewe huyu hawezি. Bwana nikwambie, sisi kule wanaume huwa wanaoa wake wanne; Pemba ana wawili, Unguja ana wawili na kote anataka apewe haki ya kupiga kura, ndiyo maana nikasema wenyewe tunajuana kwa vilemba tuachieni. Tunachotaka tukizungumze hapa, twende kwenye utaratibu tuwatendee haki Watanzania. Tunataka kuingia kwenye mchakato wa Katiba, Watanzania wanataka Katiba mpya iliyokuwa bora, haya mengine ya kwetu mkifika hapa mkiyazungumza yatawashinda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, muda hautoshi, lakini pamoja na kuwa hautoshi, niseme kwamba, ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja, mchakato uendelee na Madaftari yatumike ya NEC na ZEC ndiyo tunayataka. Utaratibu wetu sisi wengine tutajuana wenyewe kwetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ahsante. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Tundu Lissu, atafuatiwa na Mheshimiwa Simbachawene.

MHE. TUNDU A. M. LISSU: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata fursa ya kuchangia Muswada. Naomba niweke wazi kabisa kwamba, mimi siyo Mzanzibari, siyo Mpemba na wala siyo Mtunguu, mimi ni Mtanganyika. Nazungumza habari ya Zanzibar kwa sababu moja tu, hii ni Jamhuri ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar. Kama tusingekuwa Jamhuri ya Muungano, nisingekuwa; na sababu ya kuzungumza chochote juu ya uchaguzi wa Zanzibar na kwa sababu ni Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayojumuisha Zanzibar tutayazungumza sana ya Zanzibar hatutayaacha. (*Makofi*)

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. TUNDU A. M. LISSU]

Mheshimiwa Spika, hakuna uchaguzi mmoja unaoendeshwa kwa Sheria mbili. Unapochagua Rais unachagua kwa kutumia Sheria moja. Unapochagua Wabunge ni Sheria moja. Unapochagua Madiwani ni Sheria moja. Uchaguzi wowote lazima uendeshwe kwa kutumia *standard* moja, kwa kutumia kipimo kimoja na kwa kutumia sheria moja. Sisi tutakuwa wa kwanza katika dunia hii na tutakuwa kichekesho kufanya uchaguzi kwa kutumia vipimo viwili vinavyotofautiana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tutakuwa kichekesho cha dunia kufanya uchaguzi, kama nilivyosema *Referendum*, kura ya maoni ni uchaguzi; tutakuwa kichekesho kufanya Uchaguzi huu kwa kutumia Sheria mbili zinazotofautiana. Kwa kutumia Taasisi mbili, Tume mbili, zenyе mamlaka tofauti. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Muswada unapendekeza kwamba, kuwe na haki ya kupinga matokeo ya hii kura ya maoni. Unapopinga matokeo unalalamikia ukiukwaji wa sheria na taratibu za Uchaguzi zilizoko kwenye Sheria. Sasa utakapopinga matokeo ya kura ya maoni utatumia sheria ipi; ziko mbili? Sheria moja inasema una haki ya kupiga kura *regardless of ukaazi*. Sheria nyingine inasema kama hujakaa miaka mitatu huwezi ukapiga kura. Utakapoenda kushitaki utasema sheria ipi katika hizi mbili ndiyo imekiukwa wakati moja inasema una haki ya kupiga hivi na nyingine inasema huna haki ya kupiga hivyo hivyo? (*Makofi*)

Pili, utapimaje uhuru wa uchaguzi; siku zote tunasema uchaguzi unatakiwa uwe huru na wa haki; utapimaje uhuru wa uchaguzi na uhaki wa uchaguzi kwa kutumia vipimo viwili vinavyotofautiana?

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana tumependekeza katika maoni yetu kwamba, badala ya kutumia Sheria mbili, badala ya kutumia Tume mbili, tutumie Sheria moja kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tutumie Tume moja kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa sababu katika kura hii ya maoni, tunahitaji kupata msimamo wa pande zote za Muungano, Tume inatakiwa iwe na

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. TUNDU A. M. LISSU]

Madaftari mawili; mawili kwa maana ipi? Kuwe na Daftari kwa ajili ya Wanzanzibari wanaoishi Tanzania Bara, wanaoishi Mombasa na mahali popote pale. Kuwe na Daftari la Wazanzibari na Daftari la pili la Wabara, lakini Tume iwe moja na Sheria iwe moja. Tukifanya hivyo, tutaondokana na masharti ya ukaazi. Masharti ya ukaazi ni namna ya kunyang'anya watu haki ya kupiga kura. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, haya siyo maneno yangu ni maneno ya Mheshimiwa Mahadhi Maalim, kama nilivyosema asubuhi, kwenye andiko lake la miaka mingapi iliyopita. Siyo hoja ya CHADEMA hii, ni hoja ya Wana-CCM ambao wanaona, kuna wengi hawaoni. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ninaomba nizungumzie utaratibu wa kupinga kura ya maoni kwa mujibu wa Muswada huu. Ninaomba nipendekeze badala ya kudanganya Watanzania, ni afadhali kabisa tufute vifungu vyote vinavyohusu kupinga matokeo ya kura ya maoni, kwa sababu tukiviweka katika sheria kama ilivyo, tutakuwa tunadanganya watu. Tutakuwa tunadanganya watu kwamba una haki ya kupinga matokeo ya kura ya maoni, wakati kivitendo hiyo haki haitekelezeki.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Muswada, Kamati ya Kura ya Maoni inayo haki ya kushitaki, kupinga matokeo ya kura ya maoni ndani ya siku 14 baada ya kutangazwa kwa kura ya maoni. Kwenye uchaguzi wa kawaida huu wa Wabunge, sheria imetupa siku 30 za kushitaki, kwenye kura ya maoni unaambiwa siku 14.

Mheshimiwa Spika, katika hizo siku 14, Muswada unapendekeza ukusanye saini za asilimia kumi ya Wapiga Kura waliojiandikisha katika Majimbo matano ya kila upande wa Jamhuri ya Muungano. Jimbo la Mheshimiwa John Mnyika peke yake la Ubungo, lina wapiga kura zaidi ya 400,000. Ukusanye asilimia kumi tu za Ubungo uende Vikokotoni; kuna Jimbo linaitwa Vikokotoni huko au Bumbwini, Mji Mkongwe, utafute asilimia kumi ya Wapiga

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. TUNDU A. M. LISSU]

Kura waliojandikisha katika Majimbo matano ya Bara, Majimbo matano ya Tanzania Visiwani na ufanye hivyo ndani ya siku 14. Ndani ya siku 14 hizo hizo utafute Wanasheria, uwatafutie hela uwalipe wapate muda wa kuandaa Hati za Mashitaka waziwasilishe Mahakamani. Katika siku hizo hizo 14, utafute shilingi 5,000,000 za dhamana ya gharama za kesi.

Mheshimiwa Spika, Sheria kama nilivyosema, Sheria za Uchaguzi za sasa hivi zimetupa siku thelathini. Wengi wetu tunaofahaumu haya mambo tunajua hizo siku 30 ni kidogo sana. Siku 14 haitawezekana. (*Makofi*)

Assuming imewezezeka; Muswada unasema baada ya kesi kufunguliwa, inatakiwa iamuliwe ndani ya siku 14 na Mahakama Kuu yenyeye jopo la Majaji watano. Sasa kwa kawaida ukishtaki upande wa pili unajibu; je, mara hii hao wanaoshtakiwa hawatajibu?

Mheshimiwa Spika, kuna kitu Wanasheria wanaita-rejoinder. Hakutakuwa na *rejoinder*? Huwa kuna utaratibu wa kuita mashahidi watoe ushahidi, wakahojiwa na pande zote. Mashahidi hawataitwa? Kama yote haya yatafanyika, yanawezekana ndani ya siku 14. Mahakama Kuu ya Majaji watano, baada ya kusikiliza mashahidi na kuangalia nyaraka na mambo kadha wa kadha, iandike hukumu ndani ya hizo siku 14; inawezekana jaman? Hapa siyo kudanganya watu kuna haki ya kushitaki wakati kivitendo hakuna haki? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, twende kwenye rufaa. Muswada unapendekeza kwamba, ukishindwa Mahakama Kuu, hukupendezwa, unakata rufaa. Sheria inasema unakata rufaa ndani ya siku saba baada ya kupata nakala ya hukumu na mwenendo.

Kwa utaratibu wa sasa wa Mahakama ya Rufani ya Tanzania, ukitaka kukata rufaa una siku 60 za kuandaa rufaa yako baada ya kupewa nakala ya hukumu na mwenendo. Kwenye hili tunaambiwa unapewa siku saba.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. TUNDU A. M. LISSU]

Kwa mwenendo wa kawaida wa sasa wa Mahakama ya Rufaa, ukishaandaa sababu za rufaa unapewa siku zingine 60 za kuandaa *submissions*, za kuandaa hoja za kisheria. Sheria hii inasema siku saba, baada ya siku saba Mahakama ya Rufani isikilize pande zote, iwasikilize warufani, iwasikilize warufaniwa na itoe hukumu ndani ya siku saba. Kwa nini tunadanganya watu? Kama hatuwezi tukaishi bila uongo, tuseme. Utaratibu huu unadanganya watu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, unapozungumzia kesi za Uchaguzi; kesi za Uchaguzi zina Sheria zake. Mwanasheria Mkuu anafahamu na wengine wanaozifahamu. Kuna *Election Petition Rules*, zinazosema utaratibu utakaofanyika kwa ajili ya kesi za uchaguzi tu. Je, kwenye kesi za kupinga kura ya maoni tutatumia utaratibu gani; tutatumia Sheria ya Mwenendo wa Madai ya Kawaida? Imeandikwa wapi? Tutatumia *Election Petition Rules*, kwa utaratibu upi na imeandikwa wapi? Mambo madogo, mambo ya kawaida kabisa, ambayo yalitakiwa yafanyiwe kazi, hayajafanyiwa kazi na ndiyo maana tunasema tunahitaji muda, Sheria hii ni muhimu sana na muda tulio baki nao ni mchache hatuwezi tukakosea. *We can not afford to make a mistake.* Sisemi hatuwezi tukakosea, hatutaweza kubeba gharama za kukosea. (*Makofii*)

Tukienda na sheria mbovu kwenye kura ya maoni, itatuletea matatizo. Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, amesema haya mambo yanaweza yakavunja nchi, ni kweli. Kenya walijaribu hivi hivi mwaka 2006, walikataa Katiba kwenye kura ya maoni, Watawala wakasema hamtaki siyo tunaendelea na utaratibu huu kama ulivyo. Kulitokea kitu gani Desemba 2007? Leo Rais yuko Mahakamani, Makamu yuko Mahakamani. Hatuhitaji kufuata nyayo za Wakenya, tunahitaji kufanya mambo yetu vizuri zaidi. Namna ya kufanya mambo vizuri zaidi ni kujipa muda wa kutosha kutengeneza utaratibu mzuri wa kisheria utakaohakikisha hatufanyi makosa ya wazi yatakayotupeleka kwenye balaa.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. TUNDU A. M. LISSU]

Mheshimiwa Spika, sijui nina muda kiasi gani, lakini ninaomba niseme la mwisho ambalo ni suala la haki ya kupiga kura. Suala la haki ya kupiga kura ndiyo kiini cha demokrasia mahali popote pale. (*Makof!*)

Waheshimiwa Wabunge, tuna wajibu wa kuhakikisha kila Mtanzania mwenye miaka 18, mwenye akili timamu, anapata haki yake ya kupiga kura. Tukiendekeza masharti, hizi *artificial requirements*, ukaazi, sijui nini, tutanyima watu wetu haki ya kupiga kura. Watu wa Zanzibar ninyi mnafahamu, sababu mojawapo ya Mapinduzi ya Mwaka 1964 ilikuwa ni mchezo kwenye uchaguzi.

SPIKA: Jamani niambie mimi aah!

MHE. TUNDU A. M. LISSU: Ulikuwa ni mchezo kwenye uchaguzi. Mmetengenezewa sheria hamuwezi mkashinda kwa sababu sheria imetengenezwa kwa namna ambayo hamuwezi mkapata haki. Mlichukua silaha, sasa leo hii mnataka miaka 50 baadaye mtutengenezee masharti hayo hayo ya Sultan Jamshid. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana. (*Makof!*)

SPIKA: Ahsante. Namwita Mheshimiwa Simbachawene, atafuatiwa na Mheshimiwa Fakharia Shomar!

MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE - NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia Muswada uliopo mbele yetu, ambao unataka kuelezea utaratibu na masharti ya upigaji Kura ya Maoni ya Katiba hiyo mpya tunayotarajia kuikamilisha.

Mheshimiwa Spika, sina hakika sana kama kweli ipo dhamira ya dhati kwa watu wote kuipata Katiba hii na kama kweli uvyma haupo. Ninachokiona hapa ni siasa, ingawa watu wengi wanakataa siasa wakiisukumia upande wa pili, lakini siasa ipo kubwa. (*Makof!*)

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE]

Mheshimiwa Spika, kura yenyewe ni ya NDIYO na HAPANA, *box* ni moja, Mawakala wamesemwa; hofu hapa iko wapi? Kama kweli Serikali ya Chama cha Mapinduzi inafinya Demokrasia, hawa wasingelikuwepo. Kwa hiyo, niwatoe wasiwasi; rafiki yangu asubuhi alisema hofu ni maradhi. Hii hofu si jambo jema katika jambo *sensitive* kama hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Katiba yenyewe tunayoitunga hapa ni zaidi ya maisha yetu, pengine mpaka mwisho wa Katiba hii wengine wengi hatutakuwepo. Leo hii unaweza ukaitunga kwa *scenario* fulani wakati huo huo ikawa kinyume chake. Kwa hiyo, nichukue nafasi hii kuwaomba sana wenzetu watoe hofu kabisa ya jambo hili na wasiwatie hofu Watanzania juu ya jambo hili jema lilioamuliwa na Serikali na dhamira ya dhati aliyonayo Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi ninapata matatizo tena makubwa; Hotuba ya Kambi ya Upinzani, iliyosomwa na Mwanasheria, inatoa maoni yake ya kurekebisha baadhi ya vifungu na mwishoni tena inasema sheria hii itakuwa *unconstitutional* ikitungwa, kwa maana ya kwamba, haina msingi wa Katiba iliyopo na leo hii Katiba iliyopo imeonekana nzuri na imetetewa sana kwamba isivunjwe na maneno mengi karibu kurasa tano. Katiba hii ambayo siku zote ilikuwa inasemwa haifai! Unajua moja ya sifa ya msomi ni kuwa *consistent*. Hiyo ndiyo sifa ya kwanza ya mtu msomi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, labda niwakumbushe Watanzania, kwa nini leo tuko hapa tunazungumzia Sheria hii ya Kupiga Kura ya Maoni. Tuko hapa kutohana na Ibara ya 98, ambayo Mheshimiwa John Mnyika anasema, Ibara ya 98 hii ndiyo inayotoa mamlaka ya mabadiliko ya Katiba.

Kifungu cha 98cha Katiba kimetoa mamlaka na utaratibu wa utungaji au kufanya marekebisho yote yaliyoko kwenye Katiba hii. Kupitia hiyo tukaja na Sheria ya

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE]

Mabadiliko ya Katiba tulioitunga kwenye Bunge hili na wenzetu wakaikataa baadaye wakaikubali.

Leo tunapokuja Sheria ile ya Mabadiliko ya Katiba, ndio ambayo sasa ikataja huko ndani habari ya upigaji wa kura za maoni. Kwa hiyo, mpaka sasa Sheria ile wanaikubali, lakini hii inayotokana na Sheria inayosema namna ya upigaji wa kura za maoni, inaonekana hii ni *unconstitutional*. Sasa sheria yoyote *jurisprudence* na wasomi wako nje hata ya Bunge hili, wanaweza wakaangalia Hotuba ya Kambi ya Upinzani, wakaangalia kinachofanyika na kwamba ni *un-constitutional* kutokea wapi!

Ninasema hapa habari ya *professional* tuiweke pembedi. Mimi ninataka niwapitishe Watanzania kwenye kifungu kinachoruhusu uhalali wa Sheria tunayoitunga leo na kuwafanya Watanzania, waweze kutoa maoni yao, ambapo inaonekana Kifungu hicho eti hakina maana. Ninataka mwone jinsi ambavyo wanasema hakina maana na kilivyo na maana.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 21(2) cha Katiba yetu, ambacho kinaonekana hakina maana na hakitoi nafasi kwa Watanzania na hili linalofanyika linaharamishwa eti kinasema hivi: "Kila raia anayo haki na uhuru wa kushiriki kwa ukamilifu katika kufikia uamuzi juu ya mambo yanayohusu yeye, maisha yake au yanayolihusu Taifa." Sasa niambieni kupiga kura ya maoni hakumhusu mtu binafsi? Hakumhusu yeye? Hakuhusu maisha yake? Hakulihu Taifa? (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, unajua tafsiri za Sheria, tutawachanyeni sisi Wanasheria, sisi tumezoea kubisha. Tutawachanganya kwa sababu mtu anaweza akataka kuvutia anavyotaka yeye, lakini huko nje ikaonekana jambo *very sensitive* hivi, ambalo lina mantiki sana, lakini kwa tafsiri hii hapa inahitaji uwe wewe Mwanasheria? Katika tafsiri hii, kunahitaji uwe Mwanasheria wala hakuhitajiki. (*Makof*)

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE]

Mheshimiwa Spika, ninarudia tena, inasema hivi: "Kila raia anayo haki na uhuru wa kushiriki kwa ukamilifu katika kufikia uamuzi juu ya mambo yanayohusu yeye, maisha yake na yanayolihusu Taifa. Ninauliza; kupiga kura ya maoni ya Katiba mpya hiyo inayokuja hayamhusu mtu na maisha yake na je, hayahusu Taifa lake? Mimi ninasema hii ni tafsiri mbaya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kama kweli sheria ipo, kwa nini msichukue nafasi kusema? Bahati nzuri katika utaratibu wa uendeshaji wa Bunge lako umeunda Kamati na baadhi ya Wabunge na hata msomaji wa Hotuba hii ya Kambi ya Upinzani ni Mjumbe wa Kamati hiyo. (*Makofii*)

Anavyosema hapa mengi anatu-*take by surprise* tuingie kwenye mgogoro mkubwa, lakini mimi nasema tutumie taaluma zetu vizuri, tuwasaidie Watanzania. Ninaendelea kusema kwamba, umesema vizuri tuwasaidie vizuri Watanzania. Taaluma zetu zisiwe kwa ajili ya ku-*create* hofu na kuwajengea hofu Watanzania ili wadhani kuna jambo *sensitive* wakati tayari yeye mwenyewe amesahihisha, ametoa maoni yake na hata katika mchango ametoa maoni, ambayo kwa hakika angepaswa kuyatoa akiwa kwenye Kamati angetusaidia sana maana angetenda haki kwake, angetenda haki kwa Bunge, lakini angetenda haki kwa chama chake na angetenda haki kwa Watanzania. (*Makofii*)

Kutuchukua hivi ukatuletea mzigo mkubwa, maana tungesikia hata walipigia kura kule wakatofautiana tungesema pengine ni jambo *sensitive* limekuja kwenye *floor* hapa kwa ajili ya kujadiliwa maana lina utata. Huku hawajawahi kubishana, hawajawahi kupiga kura ya kutofautiana, lakini leo tunaingizwa kwenye hili.

Mimi nichukue nafasi hii kuwaomba sana Watanzania watuelewe, mwanasiasa ni mwanasiasa hata umfanyaje atarudi kwenye siasa tu. Kwa hiyo, nichukue nafasi hii kuwaomba kwamba, tunapokwenda kwenye zoezi

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE]

hili tuondoke kwenye misingi ya vyama vyetu, tukifanya hivyo tutawatendea haki Watanzania na tutajitendea haki na sisi wenyewe.

Mheshimiwa Spika, yamesemwa mambo mengi hapa, yapo yaliyosemwa kwamba leo hii upigaji wa kura ya maoni kwa Zanzibar uliopitisha msimamo mzima wa Serikali ya Mseto, Serikali ya Pamoja Zanzibar, leo hii mfumo uleule haufai katika jambo hili. *It is a contradiction* na hata Kanuni ya *precedent* haiwezi kukubali. Huwezi kulifanya jambo wakati huohuo na muda mchache ujao unasema siyo lenyewe. Hili jambo nalo waliangalie, kama kuna hoja nyingine, zipo fursa nyingine, lakini wasiikosee hii sheria nzuri ambayo ina dhamira njema kabisa ya kuwataka Watanzania watoe maoni yao. (*Makofî*)

Amesaitiwa hapa rafiki yangu Mahadhi kwamba, ye ye aliandika andiko. Mahadhi anaweza akawa aliandika andiko na pengine msomi mwingine angefanya andiko lake angepingana na mawazo yake. Leo hii ananukuliwa hapa kama ndiyo msahafu wa haya yanayosemwa leo! Unajua usomi ni kuwa na *strong authority, that is not a strong authority* kwa sababu hilo ni andiko halijawekewa hata jury ya kuifanya *analysis* ili liweze kuwa andiko linaloweza kuwa na hadhi, sisi wengine hata hatulijui. Kwa hiyo, leo haliwezi kuwa ndiyo misingi wa maamuzi ndani ya Bunge hili. (*Makofî*)

Kwa hiyo, mimi nasema kama kweli ipo nia ya dhati, tuna dhati kutoka kwenye miyo yetu juu ya jambo hili, haya madogo madogo yasingekuwepo. Tuwe watu *serious*, jambo hili la Katiba ni *serious* na ambalo Watanzania wanalisubiri sana. Sina hakika kama kuna watu wanataka hili jambo lifike mwisho, maana hata wakati ambapo unataka ku-*accelerate* liende, mtu anashika kamba. Leo unasema lirudi itungwe Sheria Maalum ya Mabadiliko ya Katiba ambayo sasa itazungumzia habari ya upigaji kura. Jamani, utaratibu huo ni mrefu mno. Kwa hiyo, maana yake ni kwamba, hatutakuwa na hiyo Katiba mpya, itakuwa ni

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE]

vikwazo, mikwara na kila siku kutafuta sifa ya kuanzisha mambo ambayo hata hayapo na wala hayalisadii Bunge.

Mheshimiwa Spika, niliona niseme haya na nimeongea kama Mbunge zaidi, kwa sababu nilitaka kutumia haki yangu na mimi ya kutoa maoni kuawakilisha watu wa Kibakwe. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante. Nilisema nitamwita Mheshimiwa Fakharia Shomar, atafuatia Mheshimiwa Mnyaa!

MHE. FAKHARIA KHAMIS SHOMAR: Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza, ninampongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kupitisha Sheria ya Mabadiliko ya Katiba na sasa kuwa sheria kamili ambayo tayari itatuongoza kupata Katiba mpya.

Pili, sina budi leo kuuzungumzia Muswada huu wa Kura ya Maoni ambao najua baadaye itakuwa Sheria na baada ya kuwa Sheria ndiyo itakayotuvusha Watanzania kupata Katiba mpya.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 32(2) inazungumzia upigaji wa kura ya maoni. Mimi nakubaliana na Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, kwa mapendekezo waliyoyatoa. Ninakubaliana na Wizara kwa maelezo waliyoyatoa kwamba, Zanzibar itasimamiwa na ZEC na Bara itasimamiwa na NEC. Kwa sababu, kwanza, ZEC ina uzoefu, ilishafanya kura ya maoni, mchakato umeonekana, Serikali ya Umoja imepatikana. Tatizo lipo wapi leo hapa uwanjani tunaikana? Sheria itakayotungwa kwa sehemu hizi mbili, yaani Zanzibar kushughulikiwa na ZEC na Bara kushughulikiwa na NEC ni sahihi, hakuna tatizo wala hakuna ulakini; kwa sababu tumeweza kufanya tukapata na Serikali ya Umoja na Serikali ya Umoja inaongoza Zanzibar na ukizungumza Zanzibar ni Unguja na Pemba; tatizo lipo wapi? (*Makofii*)

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. FAKHARIA KHAMIS SHOMAR]

Tatizo bado sijalionia, naona kama tunataka kuleta tatizo. Tukisema ZEC isisimamie mchakato wa Zanzibar, itabidi Katiba ya Zanzibar ibadilike, muda huo upo na uwezo huo upo? Kwa sababu hivi vitu ni tofauti, tuingie kwenye sheria tuliyokuwa nayo na tusimamie sheria, itatupa mwongozo na inajulikana ZEC haina matatizo, kama ina matatizo mbona Serikali tunayo na inafanya kazi na tupo sote tunafanya kazi inakuwa leo ZEC ipo hapa tu? ZEC tatizo lao lipo hapa kwa kutoka kwenye kura ya maoni ambayo tunakwenda kwenye Katiba mpya. Tatizo hilo naona halipo na wala halitakuwepo. (*Makofi*)

Nakubaliana na mchakato na ZEC ndiyo isimame na NEC Bara isimamie. Wazanzibari wapo Bara, Watanzania Bara wapo Zanzibar na wanapiga kura, si NEC ipo na haina matatizo. Wanapiga kura, zinahesabiwa na hakuna matatizo. Mchakato wa kura unapatikana, jawabu linatoka na mtu anakamata madaraka yake, sasa matatizo yapo wapi? Mimi sijaona tatizo!

Sasa hivi tunavyokwenda tunazunguka hatutaki tufike tunakokwenda na *Inshallah*, Mwenyezi Mungu atajaalia tutafika, Katiba mpya itapatikana na hakuna kitakachozuia. ZEC itafanya kazi kwa Zanzibar na NEC itafanya kazi kwa Bara na mchakato tutaumaliza.

Mheshimiwa Spika, naomba kuzungumzia kuhusu Masheha. Naona tunataka kujichanganya, kwa sababu Masheha wanafanya kazi kwenye Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, sasa Masheha hao tunakuja kuwazungumzia humu ndani wanafanya kazi gani? Masheha wanafanya kazi zao Zanzibar na wanafanya kazi vizuri, kwa sababu mtu ukiona unamlalamikia sana ni mfanyakazi mzuri, lakini mtu ukimsifu hafanyi kazi vizuri. Vilevile nataka kushangaa, Masheha haohao wawe wabaya kwa Unguja na haohao wawe wazuri kwa Pemba, tunazungumza nini? Kwa sababu Masheha wako kote na wamekaa kwa sheria sawasawa, wamekaa kimchakato sawasawa.

Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)

[MHE. FAKHARIA KHAMIS SHOMAR]

Tuangalie kama tunasema kumeharibika, kuliharibika nini? Kama kuharibika hapo mwanzo tulivyoambiwa tukaandikishe Utaifa wa Uzanzibari, kuna wenzetu waligoma, sasa faida yake wanaiona ndiyo hii, waligoma wakawa hawakwenda, wanasema aah, alikuwa mtu mzima hakuweza kuandika. Mama yangu mtu mzima, ana miaka 80 anakwenda 90 mbona anayo Mzanzibari? Kwa sababu wakati wa kuandikisha Mzanzibari ilikuwa watu wazima hawakuulizwa cheti cha kuzaliwa wala hawakuulizwa chochote, lakini watu wakakataa kwenda. Tuliokuwa tunaipenda nchi na Taifa letu tukaenda na matokeo yake ndiyo haya tunayaona na sasa hivi mtoto ye yote akizaliwa na cheti chake cha kuzaliwa anakwenda. Watu wazima wa miaka ya nyuma kweli hawana lakini ni kosa lake mtu mwenyewe, kama kweli wewe ni Mzanzibari ni kwa nini ulikataa kwenda kujandikisha? (*Makof*)

Sasa hivi unapiga kelele kwamba mimi sina kitambulisho, kama Mzanzibari utakuwa nacho na kama hutakuwa nacho ndiyo utajiandikisha kwenye ZEC na ukijijandikisha kwenye ZEC unapiga kura, hakuna tatizo na kama huna ndiyo huna NEC ipo utaandikisha hukatazwi na utapiga kura. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nataka kuzungumzia Ibara ya 36 kuhusu kura ya maoni ya Watanzania walioopo nje.

Mheshimiwa Spika, bado ni mapema, hatujafanya utafiti, hatujapanga, hatujazungumza, imeingia tu kwenye Muswada. Leo tuitishe sheria hapa utafiti tumefanya saa ngapi? Tunataka kuingiza mamluki bure, kwanza, itabidi ni lazima, ndiyo yale maneno yetu ya nyumbani huwa tunazungumza kwamba tusifukue makaburi yaliyozikwa maiti wa zamani. Kuna kitu unataka kukileta dakika ya mwisho unakiingiza na hicho kitu unajua hakitaleta faida ndani yake kitaleta mkanganiko, hatumjui nani kaandika, hatumjui nani kapiga kura, hatujui nani kama kweli ni Mtanzania, una uhakika kama kweli ni Mtanzania?

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. FAKHARIA KHAMIS SHOMARJ]

Ameondoka miaka 20 au 30 na kuna wengine toka mwaka 1964, kaondoka kashaukana uraia na sheria zetu kwenye ZEC zinazungumzwa. Kuna muda maalum ukiwa kwenye kituo chako hata kama unayo kadi ya Uzanzibari au kitambulisho, huwezi kupiga kura. Tatizo lipo wapi? Tunakana leo? Madhali tumeweza kuitumia ZEC tukapata Serikali ya Umoja na hiyo hiyo itaendelea.

Mheshimiwa Spika, kwa haya machache, naunga mkono hoja mia kwa mia. (*Makofî*)

SPIKA: Ahsante. Nilisema nitamwita Mheshimiwa Mohamed Habib Mnyaa, atafuatiwa na Mheshimiwa Chiku Abwao.

MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA: Mheshimiwa Spika, nashukuru na mimi kwa kunipatia nafasi ya kuchanglia hoja iliyopo Mezani.

Mheshimiwa Spika, kwanza, napenda kusema kwamba, mchakato huu wa kutunga Sheria hapa Bungeni kwa mujibu wa Kanuni ya ku-move *Schedule of Amendment* na pia haya maoni tunayochangia, Serikali ina wajibu wa kupima lile ambalo lina hoja na kubadilisha Sheria wao walioleta hoja, kwa sababu kama tuta-move *Schedule of Amendment* sote humu sijui itakuwa namna gani na leo muda umekuwa mchache kuonana na Kamati ya Katiba na Sheria tukapeleke *Schedule of Amendment*.

Mheshimiwa Spika, nataka kwanza ieleweke kwamba, kura ya maoni haina tofauti na kura nyingine yoyote ya Uchaguzi Mkuu, tofauti inakuja pale tu ambapo siyo watu, ni hapana au ndiyo. Sasa yale mambo yote ambayo ni muhimu katika Uchaguzi Mkuu pia ni muhimu katika kura za maoni.

Kipengele cha kwanza katika hii Ibara, kwenye *definition* kuna kituo cha kupiga kura ambapo wengi wameshazungumza, imetajwa hapa kwamba gari linaweza kuwa kituo cha kupigia kura. Hilo suala ni gumu katika

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAAJ

utaratibu tuliozoea na *cheating* au kura zilizozungumzwa na Waheshimiwa Wabunge wengi, linaweza likatokea. Kwa hiyo, kituo cha gari kisihusike kabisa kuwa kituo cha kupiga kura.

Mheshimiwa Spika, katika *definition* ametajwa Rais na Rais anatajwa wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Katika mchakato wa Sheria ya Mabadiliko ya Katiba na hii kura ya maoni, anapotajwa Waziri wa Sheria na Katiba wa Jamhuri ya Muungano anahusika vilevile na Waziri wa Zanzibar. Inapotajwa Tume ya Taifa ya Uchaguzi inahusika na Tume ya Zanzibar. Kwa hiyo, na hapa pia Rais wa Zanzibar ni lazima ahusike kwa sababu mara nyingi sana Rais wa Jamhuri ya Muungano anashauriana na Rais wa Zanzibar, katika *process* zote kuanzia mabadiliko ya Katiba na kura ya maoni pasiwe na tofauti.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 5(4) inazungumza kwamba; bila ya kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (3), Tume inaweza kutoa ruhusa kwa asasi za kiraia na asasi zisizo za Kiserikali, zinazopendelea kutoa elimu ya uraia na kuendesha uhamasishaji juu ya Katiba inayopendekezwa. Kutoa elimu na kuhamasisha juu ya Katiba hiyo kwa kipindi kisichozidi siku 30 kabla ya upigaji kura.

Sasa hapa zinatajwa hizo asasi na *NGO*, lakini katika suala hili la kura ya maoni, Vyama vya Siasa navyo vinahusika katika kutoa elimu na kushawishi, aidha vile vitakavyoshawishi ndiyo na vile vitakavyoshawishi hapana na hapa haipo. Kwa hiyo, hapa kipengele hiki cha Vyama vya Siasa ni lazima umuhimu wake uwepo, isiwe asasi za kiraia na *NGOs* tu.

Mheshimiwa Spika, Kipengele cha 37(2) kimezua hoja nyingi sana hapa Bungeni. Kwanza, nakipongeza kipengele kinachozungumza kwamba, Raia wa Tanzania waliopo nchi za nje wanaweza wakapiga kura. Naomba ninukuu: "Tume, kwa madhumuni ya kura ya maoni, itaweka utaratibu wa kuandikisha Raia wa Jamhuri ya Muungano ambao wanaishi

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA]

nje ya Jamhuri ya Muungano na ambao hawajasajiliwa kama wapiga kura katika Daftari la Kupiga Kura."

Mheshimiwa Spika, kipengele hiki ndicho ambacho kina mzozo. Kwanza, naipongeza Serikali kuingiza kipengele hiki kujua haki za Raia wa Tanzania ambao wapo nje ya Tanzania, waliokwenda kiuchumi, kimasilahi, kikazi na kwa namna yoyote, lakini wanaipenda Jamhuri yao ya Tanzania. Jambo hili tumelipigania kwa miaka mingi, leo Serikali imekubali, tuipongeze Serikali kwa jambo hili. Tatizo moja linakuja kwamba, hapa sasa ndipo penye matatizo na hili ni tatizo kubwa. Sheria Namba 7 ya Mwaka 2005 ya Zanzibar ndiyo inayoleta tatizo kwamba, hata yule Mzanzibari aliyekuwepo Tanzania Bara kibiashara, anakwenda Zanzibar kila siku lakini anaishi huku, haruhuswi kupiga kura kule. Sasa leo ikiwa huyu mtu anaishi nje ya Tanzania na Daftari litakalotumika ni la Zanzibar na huku la Tanzania Bara, hapa ndipo penye maneno pasiangaliwe kirahisirahisi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, haya uliyozungumza kwamba tuisitunge sheria kwa misimamo ya kivyma, hapa ndipo pana maneno. Mimi napenda nitoe maelezo machache kuhusu suala hili. Katika vitu vilivyozungumzwa katika zile *protocol* za *SADC* za *Political Tolerance*, Chama cha Wananchi *CUF* kimefanya jambo hili kwa miaka mingi sana. Napenda kuwaeleza kwamba, suala hili aliyekuwa Kiongozi wa Upinzani Bungeni, tarehe 24 Juni, 2009 wakati huo ni Mheshimiwa Hamad Rashid, alimwandikia Waziri Mkuu na nakala ninayo, kuhusu tatizo la uandikishaji Daftari la Kupiga Kura Zanzibar na Sheria zinavyoikiukwa na inakiukwa Katiba ya Zanzibar, Ibara ya 7(2)(d) na Ibara ya 4 na Katiba ya Jamhuri ya Muungano Ibara ya 5(2)(d). Sijui kama alipata jibu au hakupata jibu, *Allahu A'alam!*

Tarehe 9 Julai, 2009, Kiongozi wa Kambi ya Upinzani katika Baraza la Wawakilishi, Mheshimiwa Abubakar, alimwandikia Mheshimiwa Waziri Kiongozi wakati huo alikuwa Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha na bahati nzuri yupo Bungeni leo, alimwandikia kulalamika kuhusu suala hilohilo

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA]

Ia uandikishaji wa kupiga kura. Tarehe 27 Julai, 2009, Mheshimiwa Waziri Kiongozi wa wakati huo, akamjibu Mheshimiwa Abubakar, akamwambia atahakikisha kila mwenye haki ya kuandikishwa na kupiga kura, ataandikishwa na atapiga kura. Hilo ndiyo lilikuwa jibu la Mheshimiwa Waziri Kiongozi wakati huo na yupo pale. Bahati mbaya, hayakutendeka kama jibu lilivyotolewa.

Mheshimiwa Spika, tarehe 20 Agosti, 2009, Wabunge wote wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Chama cha Wananchi na Wawakilishi wote, waliandaa kongamano kubwa Karimjee Dar es Salaam. Kongamano hilo walioalikwa uniruhusu niwataje uone kwamba, *CUF* tuliliona hili tatizo kwa muda mrefu kwa ukubwa wake.

Walioalikwa kwenye Kongamano hilo walikuwa Mawaziri Wakuu Wastaafu wote, Maspika wa Bunge na Baraza la Wawakilishi, Katibu wa Bunge na Katibu wa Baraza la Wawakilishi, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Kiongozi Zanzibar, Mkurugenzi wa Vitambulisho vya Ukaazi Zanzibar, Wahadhiri wa Vyuo Vikuu, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera na Bunge), Mkuu wa Jeshi la Polisi, Msajili wa Vyama vya Siasa, Wenyevit wa Vyama vya Siasa, Chama cha Wanasheria Tanzania, Asasi za Kiraia, *Nyerere Foundation*, Wabunge, Wawakilishi na Viongozi wa Dini. Kuzungumzia suala hilo hilo na uvunjifu wa athari za uandikishaji unaoendelea.

Bahati mbaya katika orodha hiyo yote, wapo ambao hawakuhuduria. Mawaziri Wakuu wastaafu walikuja Mheshimiwa Joseph Warioba alikuja, Mheshimiwa Salim Ahmed Salim alikuja, Spika hukuja bahati mbaya, hata aliyekuwa Spika wakati huo. Hili suala lilizungumziwa, lilionesha namna Katiba ya Jamhuri ya Muungano na Katiba ya Zanzibar zilivyovunjwa na aliyesajili vitambulisho aliyeuwepo pale alishindwa kutetea hizo hoja.

Hilo kama halitoshi, Tanzania ilipoanzisha *SADC* mwaka 1992, katika ile *Charter ya Democratic Election*, Tanzania imesaini, ndiyo mle utakuta vipengele kwamba,

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA]

kama mtu ni Mbotswana, kama mtu ni Mtanzania, kama mtu ni Msouth Africa, anaishi nje ya South Africa, lakini katika uchaguzi akipenda arudi aje apige kura nchini mwake. Vinginevyo, maandalizi yanaweza kufanya katika Ubalozi wake. Sasa haya ni mambo ambayo Tanzania imesaini.

Mheshimiwa Spika, ukumbuke kwamba, watu wengi wanatabiri, mchakato huu wa Katiba utakapofanikiwa vizuri, tunakwenda vizuri na *Inshallah* Mwenyezi Mungu ajalie ufanikiwe vizuri, basi tunategemea Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano ataikwaa zawadi ya Mo Ibrahim, lakini yapo mambo ikiwa hatutarekebisha yatamchafulia likiwemo hili la uandikishaji. *Human Right Charter, Article* ya Haki za Binadamu ya Mwaka 1948 na Haki za Watu 1991, zinavunjwa katika hali hii. Kwa maana hiyo, hili suala ni zito.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu suala hili allyekuwa Waziri Kiongozi yumo ndani ya Bunge, Mheshimiwa Makamu wa Rais yule pale yumo ndani ya Bunge na Katiba yoyote tunayoipitisha inayohusiana na Jamhuri ya Muungano, kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar, Ibara 132 ni kwamba, Waziri wa Jamhuri aliwasilishe kule kwa Baraza la Wawakilishi na Baraza la Wawakilishi waridhie. Ili kuondoa mgongano, basi Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais, uchukue hili jukumu la kwamba suala hili likarekebishwe kule Zanzibar kwenye Baraza la Wawakilishi. (*Makofii*)

Sisi hapa tunalizungumza siyo kwamba Bunge hili lina uwezo wa kurekebisha suala hili. Tunalizungumza dunia ijue matatizo yaliyopo Zanzibar, dunia ijue namna tunavyowatetea Wazanzibari na Wazanzibari hivi sasa wameshaamka hawana tena u-vyama katika suala hili la Katiba Mpya, Wazanzibari ninaamini litumike Daftari la ZEC tutashinda, litumike Daftari la Jamhuri ya Muungano tutashinda kwa sababu Wazanzibari wapo *united* katika suala hili.

Kuweka mambo sawa, Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais uchukue jukumu hili, tatizo la kimsingi linalovunja Haki za Binadamu, linalovunja *Charter* ya *SADC* ambayo

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAAJ]

Tanzania imesaini, linalovunja *Human Rights* za *United Nations*, kulinyamazia kimya ni aibu, ni dosari ya kumtia Rais Kikwete. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, túsitunge Sheria kwa malengo fulani. Mimi nataka nilihakikishie Bunge hili kwamba, hii Sheria imemwathiri mpaka Rais wa Zanzibar. Sheria hii ya Ukaazi wa miaka mitatu, ni Rais pekee duniani ambaye haku-vote Zanzibar, amepigiwa kura lakini ye ye hakupiga kura, llimwathiri ye ye pia. Sasa tunaendelea kuliacha. Hivi leo tunatunga Sheria kwa kulenga jambo fulani; ni Rais pekee ndani ya Dunia hii ambaye hakujipigia kura, kapigiwa kura na watu wengine. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, tutaendelea kwa kiasi gani kuiacha dosari iendelee? Busara zinahitajika kwa viongozi wetu hawa. Mwanasheria Mkuu sisi kwa kuwa ni Serikali ya Umoja wa Kitaifa na kwa sababu ile ile ya *politically tolerance*, hatuna sababu kwa nini tuukatae Muswada huu. Litumike Daftari la ZEC tutaukubali, itumike Tume moja tu ya Jamhuri ya Muungano ya Uchaguzi pia tutakubali na Zanzibar malengo yetu tuliyokusudia tutashinda. (*Makof*)

Mapendekezo ya Mheshimiwa Tundu Lissu, sisi hili tuko tayari lakini heshima tu ya kibinadamu, heshima ya ukubwa na dhamana tuliyopewa na Tanzania, Mheshimiwa Makamu wa Pili, suala hili ulichukue likawasilishwe katika Baraza la Wawakilishi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru. (*Makof*)

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Chiku Abwao, atafuatiwa na Mheshimiwa Jafo.

MHE. CHIKU A. ABWAO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi. Naungana na wewe kwa angalizo ulilotoa kwamba, tuache mambo ya Vyama, suala la Katiba liwe ni suala ambalo lina Utanzania bila kujali itikadi zetu; kwa kweli hilo ni jambo la msingi.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. CHIKU A. ABWAO]

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Rais, ameonesha nia ya dhati kabisa kwamba, anataka kutuachia Katiba na alitamka akiwa Iringa nikiwepo katika Mkutano, Siku ya Baba wa Taifa kwamba, kitu atakacho jivunia kwa Watanzania ambacho anaamini atatuachia kama zawadi ni kuhakikisha anatuachia Katiba ilio nzuri, ambayo imetungwa na Watanzania, bila matatizo ya aina yoyote. Hili ni suala la msingi sana na hasa tukianza katika Sheria hii ya Kura za Maoni.

Mheshimiwa Spika, ni jambo ambalo halina utata kwa hii Sheria kwamba ni muda mwafaka inatakiwa irekebishwe, iangaliwe ili tuweze kupata utaratibu mzuri wa kupiga kura hii ya maoni.

Mheshimiwa Spika, vilevile hofu haitakosekana, siku zote mtu analisifia mvua illyomnyeshea. Hakuna Mpinzani hapa ndani ambaye atapinga kwamba Mbunge ye yote aliyeingia katika Bunge hili kutoka katika Vyama vya Upinzani ilikuwa ni patashika nguo kuchanika. Hakuna eneo ambalo uchaguzi ulifanyika hakukutokea purukushani yoyote mpaka ukatangazwa ushindi wa Mpinzani aliyeshinda. Hii ilitokana na Tume ya Uchaguzi. Tume hii ya Uchaguzi ambayo ilituletea shida sana, wengine tulinusurika kufa kutetea Majimbo yetu yasije yakaporwa baada ya kufanya kazi ngumu na kubwa ya kupata ushindi. Tulisimama kweli kweli, vinginevyo hakuna Mpinzani ambaye angeingia ndani ya Bunge hili kwa kuchaguliwa. (*Makofii*)

Sasa Tume hii ndiyo ambayo inatarajiwa isimamie tena kwenye kura ya maoni, ndiyo maana tunapata hofu. Tunapopata hofu msituone wajinga, mthamini yale tunayoyazungumza kwa sababu tulishapata matatizo, tunayajua machungu yake. Kwa hiyo, msitudharau juu ya hilo. Labda ifike mahali na ninyi mtafakari kwa nini ilikuwa hivi, kwa nini wakati wa uchaguzi Mpinzani akishinda inakuwa shida, CCM ikishinda atangazwa mara moja hakuna mikingamo! Mjue kabisa kwamba, sisi Wapinzani ndiyo watu ambao tunatunza amani katika nchi hii. Kwa sababu hakuna wakati ambapo tunajiridhisha kama mtu

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. CHIKU A. ABWAO]

wa Chama cha Mapinduzi ameshinda tukaleta ubishi, haitoeki hiyo, ndiyo maana inakuwa amani pale anaposhinda wa CCM, tabu inakuwa anaposhinda wa Upinzani. (*Makof*)

Kwa hiyo, haya lazima tuyazungumze, hatutayaonea haya wala hatutayaonea hofu. Nchi hii amani ipo na itaendelea kuwepo pale haki itakapozingatiwa. Kinachovuruga amani katika nchi yetu ni pale ninyi CCM mnapotaka ushindi wa lazima, mnapotaka kuua Upinzani, mnaposhabikia mambo ambayo hamtaki kuleta haki ndipo shida ya Upinzani, ndipo shida ya vurugu, shida na matatizo, ugomvi, ghasia zote zinatokea pale haki inapodaiwa na Wapinzani. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hili siyo jambo la kulipuuza, kama alivyosema umedhamiria mama yangu, nafikiri usimamie pia haki kuhakikisha inatendeke ndani ya Bunge hili ili tupate kura za maoni itakapofikia kura za maoni haki itendeke. Kuanzia katika mchakato wa Katiba toka mwanzo tumekuwa na tatizo, tumetoka humu Bungeni bila maelewano, kama siyo Mheshimiwa Rais kuingilia kati hili suala kila wakati kuliweka sawa, leo tusingekuwa tunazungumza haya hapa. Hiyo inaeleweka na inatokea pale tu wenzetu mnapotumia wingi wenu kudharau hoja zetu sisi wachache. Kama kweli tutaachana na mambo ya vyama, tuhakikishe kweli wote tunakuwa kitu kimoja, tunapigania haki, hakuna vurugu itakayotokea katika nchi hii. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kazi unayo wewe kama Kiongozi wetu ndani ya Bunge, kuhakikisha hakuna ukiritimba wowote unaofanyika au mizengwe ya aina yoyote inayofanyika kutupelekea katika vurugu. Wewe ndiyo umeshikilia amani, kama ukitenda haki, haki ikitendeke, hakuna shida.

Mheshimiwa Spika, bado katika hofu hiyo hiyo yanapotokea mazingira ambayo yanasaababisha hofu pia ni tatizo. Kwa mfano, nimeshasema hapa kwamba, hakuna

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. CHIKU A. ABWAO]

eneo lolote ambalo Mpinzani alishinda akatangazwa kwa amani. Wakati huo huo tunaambiwa tena kutakuwa na vituo vya kupigia kura kwenye gari, gari nalo litathaminika na katika nchi ambayo imejaa ukiritimba mwingi sana katika chaguzi, haya magari yatasimamiwa na nani?

Tumekuwa na matatizo sana sisi na Usalama wa Taifa. Usalama wa Taifa umeonesha wazi kabisa katika chaguzi unashirikishwa sana na usimamia sana ushindi wa Chama cha Mapinduzi; tutaamini vipi? Hili suala la kusema gari nalo pia litahesabika ni kama kituo cha kupigia kura lifutwe na litoke kwa sababu ndilo linaloleta hofu. Mwenye gari atakimbiza gari na huwa wanakimbiza masanduku tunayakamata yanakimbizwa, yanabadilishwa mengine, itakuwa gari! Tubariki kabisa dhuluma ya wazi ambayo itafanyika kutusaliti sisi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, hili naomba sana tuliangalie litaleta vurugu na ndilo litakalotuharibia. Kama kweli tuna dhamira nzuri tuache kutunga Sheria za mitego, hii ni mitego.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine muhimu ambalo wengi pia wamelizungumzia, sasa hivi Daftari la Kura tangu limeboreshwa mwaka 2010 kabl ya uchaguzi na tumeona wazi katika chaguzi ndogo ndogo zilizokwisharudiwa, asilimia inayopiga kura ni watu wachache sana. Hii inaonesha wengi hawajajiandikisha na waliojiandikisha wengi wamepoteza vitambulisho vyao vya kupigia kura. Kwa hiyo, hakuna watu wa kutosha wa kupiga kura. Kama kweli tuna dhamira ya kweli, kitu cha kwanza ni kuhakikisha tunaboresha Daftari ili kila Mtanzania ambaye ana sifa ya kupiga kura apige kura katika kura za maoni. Hapa ndipo tutapata Katiba ya Wananchi.

Mheshimiwa Spika, mtu ye yole yule anakiheshimu kitu alichokitengeneza. Tulishuhudia hapa baadhi ya Viongozi wa Vyama fulani waliflikia mahali wakasigina Katiba kwa sababu waliona ni kitu ambacho hakina thamani kwao, kwa sababu hakitendi haki, waliona ni kitu kinachomkandamiza na kinachomwumiza. Ili twende vizuri

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. CHIKU A. ABWAO]

katika huu mchakato wa Katiba, tupate Katiba ambayo kila Mwananchi atai-feel ni yake, atakuwa na machungu nayo kwa sababu ameshiriki na ameona haki ikitendea waziwazi kwamba, kila kilichokusudiwa na Mwananchi anayeitakia mema nchi hii, kimewekwa vizuri bila tabu yoyote, Katiba yetu itaheshimika sana.

Sasa hivi kuna watu tunaapa kulinda na kuitetea Katiba, lakini hatuna moyo nayo, ukiangalia mambo mengi yamewekwa kimtego mtego humu ndani, ambayo yanapelekea kutukandamiza kwa namna fulani. Katiba hii inatupa kigugumizi sana, tunafanya tu kutekeleza hali halisi ya uendeshaji wa shughuli za nchi yetu kwamba Katiba ndiyo Sheria mama ambayo tunatakiwa kuilinda na kuitetea; lakini ili Katiba ilindwe na kutetewa kwa dhati na ipate heshima ambayo kila Mtanzania ataipa ni pale tutakapokuta haki ikitendeka na haki itendeke toka mwanzo wa kura za maoni. Tusibezane hapa.

Mheshimiwa Spika, pia huwezi kukataa leo Mtanganyika akisema suala la Zanzibar, tunaposema suala Zanzibar, tunasema kama Watanzania. Tunawajibika kuhakikisha Zanzibar inatendewa haki kama sisi wengine tunavyotendewa haki upande wa Bara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, bahati mbaya na hili kidogo huwa ninapata majonzi sana, wenzetu wa Zanzibar inafikia hata kujenga ile hali kwamba wa Bara tujione kama hatuhusiki na Zanzibari. Mzanzibari anapoinuka atasema kwa kujivuna kabisa, kujivunia Uzanzibari wake, atatamba na Uzanzibari wake kwa kila namna, lakini sisi Watanganyika imekuwa ni haramu kusema Mtanganyika. Imekuwa ni shida mpaka sasa Mzanzibari anakuwa ndiyo Mtanzania halisi ambaye anaweza kutetea sana masilahi ya Zanzibar, halafu Mtanganyika anajiona hastahili tena kuwatetea Wazanzibari kana kwamba wale siyo ndugu zake na wala hawamhusu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani tunaposisitiza masuala ya Zanzibar, tunasisitiza kama Watanzania ambao

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. CHIKU A. ABWAO]

tumepata machungu sana kuona wenzetu wakuuawa, wenzetu wakipata matatizo makubwa katika chaguzi, wenzetu wakidhulumiwa haki zao za kupiga kura, wakidhulumiwa hata ushindi wao; ni mambo ambayo yanatuma sisi kama Wapinzani. Tunaona wenzetu wanaumizwa na hatutaweza kunyamaza. Pale anaposimama Mtanzania mwenzetu akajitenga ama akatoa onyo eti hatujawatuma; mtutume ninyi ni akina nani? Tunajituma sisi wenyewe kama Watanzania kuona wenzetu hawa amba ni damu yetu, ni wenzetu, ndugu zetu wananyanyasika, wanateseka, lazima tuwalinde, lazima tuwatetee na kuutetea Utanzania wetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, siku zote kumezuka hoja hapa zinajengwa jengwa kana kwamba sisi Wapinzani hatutaki Muungano; siyo kweli. Sisi Wapinzani tunataka Muungano wenyе haki sawa, Muungano amba Zanzibar inapozungumziwa na kusifiwa na Mtanganyika naye asimame vilevile ajisifie, aongee kwa kujidai na nchi yake. Haya ndiyo mambo ambayo kwa ninyi kung'angania kuweka Tanganyika isitambulike, tutafika wakati tutakataa Muungano. Kwa kung'ang'ania, naomba ieleteweke hiyo, kwamba, haya ni mambo ya msingi kabisa, Utanganyika hautakufa na Uzanzibari hautakufa na ndipo Tanzania inakuwa imara. Kwa hiyo, tusinyong'onyezwe pale tunapotetea suala la Zanzibar. Nimeona kila tunapopitia Muswada wa Sheria inayohusika Tanzania nzima Zanzibar na Tanganyika, imekuwa kama kuna utengano fulani na kuna masimango kwamba sisi wengine tukisimama kuitetea Zanzibar inaonekana kama tuna ajenda fulani; hatuna ajenda, tunachotaka ni umoja, usawa na haki. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, hayo yote yakizingatiwa itakuwa ni vizuri. Ameongea jambo la msingi hapa, Rais anakwenda kwenye uchaguzi anashindwa kupiga kura kwa ukiritimba tu; ni mambo ya aibu siyo ya kuyashangilia hata kidogo. Kwa ukiritimba tu, hata mtu mwingine ukikaa ukitafakari, hivi jamani hawa watu wakati mwingine huwa wanawaza mambo gani mbona inakuwa haieleweki, inaleta ukwasi. Tunapotaka Tanzania iwe imara, kama kweli tunaupenda

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. CHIKU A. ABWAO]

Muungano huu udumu, tuache mambo ya ubaguzi, tuache mambo ya vikwazo visivyokuwa vya lazima, tuache mambo ya kuzunguka zunguka katika kutunga Sheria ambazo tuna imani kwamba, zitakuwa ndiyo *source* ya kuweka Muungano ulio imara.

Mheshimiwa Spika, jambo linalotakiwa lieleweke kwa makini sana na hasa ndugu zetu wa CCM ambao mpo wengi na hasa kutimiza hata hii hoja ambayo Mheshimiwa Spika, umeizungumza hapa, tuache mambo ya Vyama, tuangalie hasa uhalisia wa kutupelekea kupata Katiba iliyo nzuri, msitumie wingi wenu vibaya.

Mheshimiwa Spika, kutumia wingi vibaya madhara yake ndiyo yale, toka tumeanza mchakato wa Katiba tunakwenda mbele tunarudi nyuma, tunakwenda mbele tunarudi nyuma; hivi kama Rais naye angekuwa mambo ya ajabu ajabu hayo ya U-chama U-chama hivi leo hata hili suala lisingezungumzwa hapa? Kwa nini tunamuweka Mheshimiwa Rais wetu katika mazingira magumu? Mimi najua hata huko aliko sasa hivi hana amani, anasema Mungu wangu sijui leo watatoka vipi huko ndani. Kwa sababu kila tunapofikia suala linalopelekea kwenye Katiba ambayo yeye amesema anataka iwe zawadi ya Watanzania kuhakikisha kwamba Katiba inatokana na Watanzania wenyewe, itakayopatikana kwa uhuru na haki na uwazi na bila vikwazo vya aina yoyote; anapata shida. Naomba hili nalo muwe mnalifikiria.

Mimi naangalia, shida zote zinatokana na wingi wenu. Pale wengine tunapoona tunanyanyasiaka hata tuseme nini hakuna kitakachobadilika hapa, hatuwezi kusikilizwa, hoja zetu hazitathaminiwa, ndipo tunapoamua kuondoka kwa sababu tunajiuliza tupoteze muda kukaa hapa wakati hata tuseme nini tunaonekana wajinga tunazomewa tu, tunatukanwa tu. Haki ikitendeka wote tukaheshimiana na wote tukawa na dhamira moja kwa vitendo na siyo kwa maneno, hakuna kitakachoshindikana.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Nilisema nitamwita Mheshimiwa Jafo.

MHE. SELEMANI S. JAFO: Mheshimiwa Spika, ahsante. Awali ya yote, napenda kumshukuru sana Mwenyezi Mungu, nami nimepata muda huu mchache kwa ajili ya kuchangia kwa uchache hasa katika ajenda yetu au Muswada ulioko mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu kwa leo utakuwa mfupi sana, kwa sababu kwangu ninashuhudia safari tulioanza kwa muda mrefu, safari muhimu ya Taifa letu hilli, tumeaita sehemu mbalimbali zenyehu changamoto kubwa, leo hii safari yetu tupo katika hali nzuri. Kwa hiyo, nina kila sababu ya kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwamba tunakwenda; ndiyo maana nimesema leo nitazungumza kwa ufupi sana. (*Makofii*)

Jambo kubwa ambalo nataka nilizungumzie hapa ni suala zima la sisi Wabunge tulioomo humu ndani. Jambo la kwanza, mimi huwa ninanyong'onyea sana Wabunge tunaponyoosheana vidole. Naomba niwaambie ndugu zangu hata upande wa Upinzani, mnajua mnaposema kila mara hawa Wabunge wa CCM, sisi wengine tunakasirika sana, kwa sababu mwisho wa siku unakuwa hujengi jambo moja la kujenga Taifa, mara nyingi tunanyoosheana vidole. Wakati mwingine tunajadili mawazo mapana ya mustakabali wa Taifa hilli. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, haya mambo mara nyingi yanakuwa siyo sahihi. Mimi naomba niseme kwa kifupi zaidi na hasa nazungumzia maudhui mazima ya mchakato wa Katiba. Bahati nzuri mzee wangu Mheshimiwa Hamad Rashid, amezungumza maneno mazito sana katika Bunge hili leo. Ndugu zangu, mimi naomba nizungumze kwamba, wakati mwingine unaweza ukazungumza jambo ukatamani kwa ajili ya nafsi yako, lakini hufikirii jambo hilo litakuwa na madhara gani siku za usoni. Kwa bahati mbaya zaidi, nawaomba ndugu zangu, michango yetu hii ijaribu kulijenga Taifa letu liwe pamoja. Wakati mwingine inaonekana kama Wabunge tunajadili nani atashinda na nani atashindwa.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. SELEMANI S. JAFO]

Mimi leo nimepata shida kwa sababu inaonekana wengine wanasema tutashinda na wengine nani atashida hapa. Uelewa wangu ni kwamba, tunakwenda kwenye mchakato wa kujenga Taifa letu hili kupata Katiba mpya. (*Makof*)

Hii ni huzuni kwa sababu tunawachanganya Watanzania wengi waliokuwa nje. Badala Wabunge tuwaweke pamoja Watanzania, inawezekana matamshi yetu yakaleta hofu kwa Watanzania; hili ni jambo baya sana. Mimi naamini Muswada unapokuwa hapa, lengo letu ni kuuboresha, lipi linaonekana lina upungufu tuliweke vizuri. Tujue tunalitengeneza hapa tunaenda kuwaambia Watanzania baadaye waweze kuliamini na kuweza kuhakikisha tunafanya vizuri katika Taifa letu hili.

Mheshimiwa Spika, tunapata shida sana, tunaisifia Kenya katika maeneo mengine, halafu tunalponda Kenya katika maeneo mengine. Nimeona michango yetu hii, lazima wakati mwininge tuangalie jinsi gani tunafanya vizuri, lengo letu lijenge Taifa na lisijenge kutengeneza utengano wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, kiukweli ndiyo maana nimesema hapa leo nitakuwa nazungumza kiufupi zaidi, mimi sitashabikia jambo lolote ambalo linaenda kulisambaratisha Taifa letu hili. Naomba sana, Mbunge yeote ndani ya nafsi yake kuna jambo ambalo mbele lina shari, naomba ndugu zangu tuliepushe jambo hilo. Utaitengeneza shari kwa mikono yako, lakini Mwenyezi Mungu atakwenda kulipa hiyo shari mbele. (*Makof*)

Inawezekana tuna ajenda nyingine ambazo tumezibeba ndani ya Bunge hili, inawezekana kuna ajenda za kulisambaratisha Taifa letu hili kabisa. Nawasihi sana Watanzania, kama tuna ajenda hizo tumezibeba naomba tuziache. Lengo kubwa ni kuhakikisha tunatengeneza nchi yetu kwa kuititia michakato hii ya Katiba. Kuna mmoja anasema ongea Sheria hapa.

SPIKA: Naomba usimsikilize hata kidogo! (*Kicheko*)

MHE. SELEMANI SAIDI JAFO: Mheshimiwa Spika, ndiyo maana nasema hawa watu wanaozungumza mara nyingi zaidi hawajali Taifa letu, hawana uchungu na Taifa letu hili, hawaguswi na matatizo ambayo Watanzania wanaweza kuyapata kutokana na matizo yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kubwa zaidi nataka nigusie kipengele kimoja cha suala zima la upigaji kura. Katika suala la upigaji kura ...

(Hapa Wabunge Wallimba CCM, CCM)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, naomba tunyamaze. Tabia za namna hii hazipendezwi zinakuwa za kitoto, msikilizeni mmoja na mwingine asikilizwe.

Mheshimiwa Jafo, naomba uendelee!

MHE. SELEMANI SAIDI JAFO: Mheshimiwa Spika, suala zima la upigaji kura, kuna maoni mengi yametolewa hapa na mimi naomba sana Serikali ituhakikishie jinsi gani tunavyokwenda kwenye mchakato huu, tutaweka wigo mpana wa watu wengi wakapiga kura. Watu wengi wakipata fursa ya kupiga kura, maana yake tutawashirikisha Watanzania wote. Ndio maana nimeomba sana kwamba, mawazo ya kila mtu yaweze kuchukuliwa kuangalia jinsi gani tutalifikisha Taifa letu likiwa salama. (*Makofii*)

Yamezungumzwa masuala mazima ya uboreshaji wa madaftari. Tuhakikishe madaftari yanabobereshwa, lakini yampe uhuru kila Mtanzania aweze kupiga kura. Tusije tukaongopeana hata kidogo tutaenda kutengeneza Katiba ya Watanzania na kila mtu awe na fursa kubwa ya kupiga kura kwa ajili ya Taifa lake. (*Makofii*)

Ndio maana nimesema katika suala zima la uboreshaji wa madaftari ya wapiga kura, tuangalie kitu gani kitakachowakwaza Watanzania kuwanyima haki yao ya kupiga kura. Kama hilo jambo lipo, naomba tuliweke

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. SELEMANI S. JAFO]

sawa na tuweke uhuru jinsi gani tutafanya Watanzania kwa ujumla wao waweze kupiga kura. Hapo ndiyo tutatengeneza Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambayo ina upana wa kuwagusa Watanzania. (Makof)

Mheshimiwa Spika, naomba yachukuliwe mawazo yote yaliyokuwa *positive* kwa ajili ya kujenga nchi yetu. Ndiyo maana nikasema tusizungumze mtu akagusa katika nafsi ya Chama, tuangalie mustakabali wa Taifa letu unasemaje. Kwa mfano, kama kuna kikwazo chochote kinawanyima Watanzania haki wasipige kura katika kura ya maoni, tuangalie Bunge letu hili litafanya vipi ilimradi Sheria hii itupe maelekezo mazuri, Watanzania wote wawe na fursa ya kupiga kura katika kura ya maoni. Hili ndiyo jambo kubwa sana la kutengeneza nchi yetu. (Makof)

Tukiacha mtu maana yake tutaanza kutengeneza migogoro. Imani yangu ni kwamba, jambo la Katiba lihakikishe kila mtu anaenda kupata fursa. Bahati nzuri tumesema Katiba yetu imepita katika madaraja mengi, Wananchi wametoa mawazo yao, Bunge la Katiba litakaa, hali kadhalika Wananchi watatoa maoni yao. Sasa naomba sana msiwanyime Watanzania haki ya kupiga kura katika kuipitisha Katiba. (Makof)

Naiomba sana Serikali kupitia maoni mbalimbali ya jinsi gani tutaboresha, hasa katika uboreshaji wa daftari la wapiga kura na kuhakikisha kwamba, kila Mtanzania anapata fursa hiyo basi tuweze kutumia nafasi hiyo. Nafasi hii mwisho wa siku tutakuja kutengeneza Taifa ambalo kila Mtanzania atajivunia hakika ametengeneza Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Katika hili, naomba sana katika suala zima la elimu tutoe elimu ya kutosha, isije ikatokea kama uchaguzi tuliofanya, karibu asilimia 40 peke yake ya Watanzania ndiyo waliopiga kura.

Tukiweka wigo mpana, kwa mfano, kuna wazo la mpaka kutumia magari japokuwa lina changamoto yake, lakini nina imani kwamba, zoezi likiboreshw zaidi,

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. SELEMANI S. JAFO]

inawezekana litawasaidia Watanzania ambao wako mbali na vituo vya kupiga kura wakaenda kupiga kura. Tutumie utaratibu wa hayo magari yafanyiwe vipi, lazima tuweke utaratibu mzuri ambao utakuwa huru na kila mtu atakuwa na imani nao. Hii itawasaidia Watanzania waliokuwa maeneo mengine, unakuta watu wazima wanashindwa kufika maeneo ya kupigia kura. Tukilifanya hilo vizuri zaidi, tutahakikisha tumetengeneza Taifa la Watanzania ambao kila mtu amepata uhuru na fursa yake ya kupigia kura.

Mheshimiwa Spika, yangu yalikuwa ni hayo hasa ya kujenga Taifa moja ambalo Watanzania wote tutakuwa na nafasi pana katika suala zima la kura ya maoni. Mwisho wa siku Watanzania tutasimama kwa pamoja kujidai kwamba Watanzania tumeweza, tumetengeneza Katiba yetu katika mchakato mgumu lakini mwishoni tunakuwa na furaha tunagonga glasi kwa pamoja kwamba Watanzania tumeweza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, naunga mkono hoja hii. Ahsante sana. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Assumpter Mshama, ndio msemaji wa mwisho jioni hii.

MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi, nami niweze kuchangia katika hoja hii. Ninayo shukrani mbele za Mungu na mbele ya Bunge lako Tukufu kwamba na mimi leo nitakuwa mmoja wa wachangiaji.

Jambo la kwanza, napenda niipongeze Wizara ya Sheria na Katiba. Nawapongeza sana pia Mawaziri na naipongeza Kamati hasa Mwenyekiti na Kamati nzima, kwa kweli Mungu awabariki sana kwa kazi kubwa mliyoifanya.

Mheshimiwa Spika, kabla sijachangia, naomba niongee na wenzetu upande wa Chama cha CHADEMA. Suala la kwanza nakumbuka walipokuwa wanapiga mbio ili kuingia Ikulu, kitu ambacho walituambia ni kwamba,

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA]

watachukua siku 100 watakuwa wametupatia Katiba. Leo ninachoshangaa hizi siku zote mchakato tuliotumia, bado wanaendelea kuona kwamba tunafanya haraka, turudi nyuma, twende mbele, lakini nataka kusema kwamba, *speed* ni ileile na tutahakikisha Chama cha Mapinduzi kinatekeleza na kuleta Katiba inayoelewaka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tunaloliona mbele yetu nilikuwa nategemea kabisa wote tuje na neno moja la kwamba, tunahitaji Katiba badala ya kuonesha kuna Chama kinataka kurudi nyuma na Chama kingine kinataka kukamata Chama kingine kisisonge mbele. Nataka niwatie moyo Watanzania wote kwamba, wasitegemee jambo lolote kutoka kwa Mpinzani, hata tukifanya vizuri namna gani, hawataona kama tumefanya, wataturudisha nyuma maana kazi yao kubwa ni kupinga. Kwa hiyo, jina lake linaitwa Mpinzani kwa maana yoyote ile hawezi kusema tumefanya. Kwa hiyo, Watanzania msiwe na wasiwasi, maoni mtatoa yatachukuliwa kama ambavyo mtakuwa mmetaka.

Mheshimiwa Spika, nataka nimpongeze Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, lakini ninahisi ile safari walioenda wenzetu itakuwa ya mwisho, tukiongea hapa wakatoka nje, nimwombe mara hii asirudie tena kwa sababu ataona ni mazoea. Kila wakimaliza wanatoka nje halafu wanakwenda Ikulu wanapata soda wakirudi tunairudia. Kwa hiyo, niombe tu kwamba, sasa tumefika mahali pa kuendelea mbele.

Mheshimiwa Spika, nataka niongelee vitu viwili; tuliangalia kwenye kitabu hiki Ibara ya 6 ambayo inaongelea Tume kuwa na wajibu wake. Ujisoma katika kifungu (b) kinasema; kuhamasisha na kusimamia elimu ya mpiga kura kwa ajili ya kura ya maoni. Mimi naomba kuuliza; hiki kipindi kitakuwa ni cha muda gani? Tunapenda kujua itachukua muda gani na ni lini itaanza kufanyika ili watu wajue au muda kama hautoshi au unatosha tungeweza *ku-discuss*, lakini ukiangalia hapa anasema kuhamasisha

Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)

[MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA]

na kusimamia elimu ya mpiga kura kwa ajili ya kura ya maoni. Tunapenda kujua hilo zoezi litachukua muda gani.

Mheshimiwa Spika, ukienda katika Ibara ya 9(3) inasema; Afisa wa Kura ya Maoni atamtaka mtu anayeomba karatasi ya kupiga kura kutoa kadi ya mpiga kura. Mimi sijaona hapa kwa nini tunaona tatizo; hivi kweli tuseme tu kusiwepo kitu chochote cha mtu kuonesha wakati anaenda kupiga kura? Nina uhakika kila Mtanzania aliyepiga kura uchaguzi uliopita anacho kitambulisho, sawa kitambulisho hicho kinaweza kuwa kimepotea lakini tuweke utaratibu mwingle. Katika utaratibu tulionao kuna Wenye viti wa Vijiji na pia Viongozi wa Serikali ambao wapo kwenye vijijiji, basi mtu kama hana kitambulisho alete kitambulisho au alete barua inayotoka kwa Mtendaji kwamba huyu kweli ni mkazi wa hapa na kweli anajulikana. Tukisema mradi yuko kwenye kitabu, anaweza kuwa kwenye vitabu zaidi ya kimoja. Kwa hiyo, naomba kuwepo namna yoyote ya mtu kujulikana kweli ni mpiga kura wa mahali pale.

Ukienda katika Ibara ya 15, Viongozi wote wa kura za maoni watateua Mawakala wasiozidi wawili wa kura ya maoni watakaokuwepo mahali ambapo kura zinapigwa katika kila eneo la kupiga kura.

Mheshimiwa Spika, ninawaza jambo moja; tumeongea kwamba, hata watu walio nje ya Tanzania wanaweza wakapiga kura. Je, na nchi nyingine nyingine ambazo wapo kama Ukraine na dunia nzima, tunao uwezo huo wa kuweka watu wawili wa kuhakikisha kwamba wale watu wamepiga kura? Jambo hili ni lazima kila mtu ambaye yupo nje ya nchi na uwezo wa Tanzania tulionao na mahitaji tuliyonayo; tuna uwezo wa kuhakikisha kila Mtanzania popote alipo tumemfikia?

Ushauri wangu ni kwamba, naomba kama Mtanzania anajisikia anapenda kuhusika katika zoezi hili; kwa nini tuseweke utaratibu wa kwamba, kwenye Ubalozi au Balozi ye yoyote tuliyenaye kama mtu anaweza kufika sawa

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA]

au tunaweza kuamua kwamba jamani wewe uko nje, katika zoezi hili acha tukuwakilishe. Ninavyoangalia uchumi wetu, ukienda kila nchi na kuhakkisha, maana ukifanya mahali pengine na pengine ukipaacha, wengine watajisikia vibaya. Sasa naomba tuangalie namna ambayo kama wanakosa walio nje basi wakose wote na kama wanapata basi tuwe na uwezo wa kuhakkisha wanapata wote, kitu ambacho naona kinaweza kikawa kigumu.

Naomba nitoe ushauri kwa Watanzania wote kwamba, tunaposema Kamati yetu au *NEC* haifanyi vizuri, nadhani hatuwatendei haki. Kila Mbunge aliyepo mahali hapa amepitia katika jambo hilo, wote tuliochaguliwa hapa tumeingia kupitia watu wale, lakini leo tunaona hawafai, tunaona hawawezi, tunaona watoke, hivi kweli hata kama tunasema kwamba kulikuwepo na ubishano ni ubinadamu, hata nyumbani kwetu na waume zetu au watoto wetu kuna mahali wakati mwingine tunapishana. Sasa ile ya kung'ang'ania kwamba hawafai tuwaondoe, naona siyo sawa, kama kuna vitu vya kurekebisha turekebishe lakini hiyo *NEC* imetuleta vizuri na waliotoka Zanzibar mmeingia humu vizuri na walio na kesi, hizo kesi zimeamuliwa yamkini zilikuwa wana matatizo. Naomba tuwaheshimu, tuwapongeze na tuwatie moyo kwamba, kipindi kinachokuja waweze kufanya vizuri zaidi, lakini leo kusema tena tutunge kitu kipyra nadhani tutakuwa hatuwatendei haki.

Wameshutumiwa muda mrefu lakini nawapongeza kwa kazi nzuri, mimi niliingia vizuri tu hapa na haki yangu ilionekana. Wale wenzetu wanaolalamika hata wao tabia kubwa walijonayo ni kwamba, lazima washinde kwa kila kitu. Wakiambiwa wameshindwa inakuwa nongwa, lakini kwenye kushinda wanaona ni sawa. Kwa hiyo, wakubali wanaposhindwa wameshindwa na wanaposhinda wameshinda na tuheshimu hicho chombo kinachotuleta ndani ya Bunge.

Katika haya machache, Mwenyezi Mungu awabariki. (*Makofii*)

SPIKA: Naona muda uliobakia hautoshi, lakini kama nilivyosema, ndugu zangu hii ni Katiba ya nchi na siyo kitabu cha chama chochote kile; kwa hiyo, ni vizuri tukajadili mawazo. Nami sina matatizo pale mtu anapotoa mawazo yake hata kama mazito kwa kiasi gani, lakini yawe na lengo la kusema sasa tunatokea wapi. Isiwe tunajaza tu maneno halafu inakuwa haitusaidii sisi na vizuri zaidi Watanzania wanatuangalia na ni vizuri tusiwe watu wa kuwafanya Watanzania watuelewe kama tunavyotakiwa kufanya. Jamani, tuseme ukweli, hapa tunatunga sheria. Kwa misingi hiyo basi, kuna marudio mengi sana katika mjadala huu, mimi nataka muda zaidi utumike kwenye Kamati ya Bunge Zima.

Kwa hiyo, hawa nillionao wanatosha kusudi tuweze kupata muda mwangi kwenye Kamati na ninaamini wale watakaokuwa wameleta *amendment* zao, unapoleta *amendment*, kwanza, nawasihi, Bunge hili nalionna hivi, lakini Mabunge mengine Mbunge akileta *amendment* yake anafanya mjadala na wote bila kujali chama anachohusika. Katika *amendment* wenzako wanaweza kukuongzeza maneno mazuri ama wakakwambia hii punguza, lakini hapa kila mtu akichukua *ki-amendment* chake anakileta na anataka sisi wote tukubali tu. Sasa hii siyo Bunge, kutunga sheria ni pamoja na *ku-network*, hivyo ndivyo tulivyozoea sisi wote, unakwenda kwa wote kwa sababu lengo ni kutunga sheria na wenzako wakikwambia hii haifai na wewe ukubali na mtu mwininge akisema kitu kinachofaa pia tukubali.

Sasa tunachokifanya mwenye *amendment* kesho ikikosekana basi ni inakuwa ni tatizo, sasa hiyo sivyo na katika Muswada wa namna hiyo, tungependa mashauriano zaidi kuliko kupiga kura. Kwa hiyo, naomba Mbunge ye yote mwenye jambo lake analofikiri ni kubwa, atuite tukae lakini siyo tukitoka hapa tunatoka tena tunarudi kwenda kukata rufaa kwa Rais, tusifanye hivyo kwa sababu haina maana yoyote, kwani kama kuna jambo kubwa tukae kwa pamoja hapahapa na watunga Sheria wa mwisho ni sisi hayupo

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[SPIKAJ]

mwagine. Hili ndiyo ombi langu na tumwogope Mungu katika kutenda hayo yote, nawaomba sana.

Kuna vitabu vitakatifu, sipendi kuvitaja lakini kitabu kitakatifu cha nchi ni Katiba, hicho ndiyo kitabu kitakatifu cha nchi. Kwa hiyo, tuitunge Katiba itakayomsaidia Mtanzania yejite, uwe wewe mtawala leo au mtawala kesho, iwe ni Katiba ambayo sisi wote tunasema hiki ndiyo kitabu chetu cha Tanzania. Tuache ushabiki usiokuwa na faida yoyote kwa mtu. Kwa hiyo, tutunge sheria na siyo vinginevyo.

Baada ya kusema hivyo, hao niliosema watazungumza kesho niwataje; yupo Mheshimiwa Kheri Ameir, Mheshimiwa Abdallah Sharia Ameir, Mheshimiwa Sylvester Mabumba, Mheshimiwa Jaddy Simai Jaddy, Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha, Mheshimiwa Livingstone Lusinde na Mheshimiwa David Silinde; hawa jamaa wananchanganya kila siku. Yupo Mheshimiwa Christine Mughwai na Mheshimiwa John Shibuda na baada ya hapo watajibu wenye hoja halafu tutaingia kwenye Kamati ya Bunge Zima ambapo tutafanya kazi ya kutunga sheria.

Kwa kuwa sina matangazo mengine, naomba niahirishe kikao cha Bunge hadi kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 1.40 usiku Bunge lillahirishwa hadi Siku ya Alhamisi,
Tarehe 5 Desemba, 2013 Saa Tatu Asubuhi)*